Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NANE

## Kikao cha Arobaini na Saba – Tarehe 14 Agosti , 2012

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

Spika (*Mhe. Anne S. Makinda*) Alisoma Dua

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae, Katibu.

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa Fedha 2012/2013.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 370

### Gari la Kubebea Wagonjwa

**MHE. DONALD K. MAX (K.n.y. MHE. FAITH M. MITAMBO)** aliuliza:-

Tatizo la magari ya kubebea wagonjwa liko kwenye Wilaya nyingi ikiwemo Wilaya ya Liwale ambayo vijiji vyake vya Ndapata, Nambinda, Mlembwe, Mpengele, Kigwema, Mkundi, Barikiwa na vitongoji vyake, vimo pembezoni mwa pori la Hifadhi ya *Seleous.*

Pia vipo mbali na hospitali ya Wilaya na hakuna Kituo cha Afya karibu:-

(a) Je, Serikali inaweza kutoa gari la kubebea wagonjwa kwa wananchi wa vijiji hivyo?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuiongezea hospitali ya Wilaya ya Liwale ili liweze kuhudumia vijiji vingine vilivyo mbali na hospitali hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo, Mbunge wa Liwale, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba lipo tatizo la uhaba wa magari ya kubebea wagonjwa katika Wilaya ya Liwale katika maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge. Halmashauri ya Wilaya ya Liwale inayo magari mawili (2) ya kubebea wagonjwa ambayo ni *DFP 6393* lililotolewa na Serikali mwaka 2009, na SM 4997 lililotolewa na Serikali mwaka 2007/2008. Magari haya yapo katika Hospitali ya Wilaya yakihudumia Tarafa mbili za Liwale na Makata.

Hata hivyo, gari Na. 4997 halifanyi kazi kutokana na kuharibika. Aidha, Kituo cha Afya Kibutuka kinahudumiwa na Gari Na. 3961 lililonunuliwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Liwale katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 ilipata mgao wa pikipiki nne (4) za miguu mitatu (Bajaji) kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Pikipiki hizo tayari zimepokelewa na kupelekwa katika vijiji vya Mpengere, Mirui, Kimambi, na Ngongowele ili kupunguza adha ya kusafirisha wagonjwa wanaohitaji kuletwa katika Hospitali ya Wilaya.

**MHE. DONALD K. MAX:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Naomba nimwulize Naibu Waziri kwamba tatizo la magari ya kubebea wagongwa lipo katika maeneo mengi sana. Kwa hiyo, kisera kusema kweli Wilaya zote tunakabiliwa na tatizo kama hilo, kwa sababu upande wa Mkoa wa Geita sasa hivi ukitazama kule Busanda kuna tatizo kubwa kama Jimbo la Geita

vilevile. Sijui haya magari kama yamekwishafika kama Mkoa wetu wa Geita utafikiriwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, anachosema Mheshimiwa Max ni sahihi. Ni kweli kwamba kuna maeneo mengi sana ambayo yana matatizo makubwa ya magari haya. Hata mnapoisikia Serikali hapa inatamka hapa habari ya Bajaji na Pikipiki ni katika kuonesha jinsi ambavyo Serikali inaona kwamba kuna tatizo.

Mheshimiwa Spika, mara ya mwisho uliagiza kwamba tukupe orodha ya yale magari ambayo tulikuwa tumepeleka katika Wilaya na tukafanya hivyo. Katika orodha ile tulionesha kwamba ni magari 43 kwa kipindi kile yalikuwa yametolewa ili *push up* lile tatizo ambalo liko pale.

Mheshimiwa Spika, suala la msingi hapa tunachofanya ni kwamba tunaitaka Halmashauri yenyewe iingize katika mipango yake. Wengine wanaingiza katika elimu, wengine wanaingiza katika afya. Tunachoweza kusema hapa sasa hivi ni kwamba Halmshauri yenyewe ndiyo inatakiwa iweke katika kipaumbele iseme sisi *Ambulance* kwetu hapa sasa ni kipaumbele na kwa msingi huo tuweze kupitisha katika Bajeti.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Waziri Mkuu imeshapita na hapa siwezi kuahidi kitu chochote sisi tunakwenda kwa *Cash Budget*, naweza nikamhurumia tu kwamaba kuna tatizo pale na watu wa Geita

wananisikia nikizungumza lakini hatuna ujanja hapa katika jambo hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kabati, sasa usianze kuuliza kule kwetu hakuna gari, hapana, hayo siyo maswali.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Japokuwa lazima niulize kule kwetu kwa sababu hospitali iliyopo katika Jimbo la Iringa Mjini ambayo ni Mpya ya Wilaya, nayo ina tatizo la gari la wagonjwa. Vile vile hospitali kwa sababu haina *OPD* mara nyingi imekuwa ikipeleka wagonjwa kutoka kwenye hospitali ile ya Wilaya kupeleka kwenye Hospitali Kuu. Naomba Naibu Waziri Mwanri kama alivyotusaidia basi aendelee kutoa kipaumbele kwa hospitali ile ili wagonjwa waweze kupelekwa katika hospitali kuu ya Mkoa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, tunachokisema ni kwamba, swali la msingi linakuwa na eneo na Waziri amejiandaa, ukitaka tu tuseme kila mtu Jimboni kwake haiwezekani. (*Makofi*)

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika ahsante kwa kuniona. Gari la kubebea wagonjwa lililokuwa limekabidhiwa katika kituo kidogo cha Mbuguni Wilayani Arumeru ni zaidi ya mwaka sasa halijulikani gari hilo liko wapi;

Je, ni Serikali ilihamisha gari hilo?

**SPIKA:** Hilo swali ni jipya kabisa, tunaendelea. Nilijua utashindwa tu. Tunaenda Ofisi ya Rais na Utawala Bora.

Na. 371

**Taasisi Zinazoundwa na Wake za Marais Kuwa chini ya Serikali**

**MHE. LETICIA M. NYERERE (K.n.y. MHE. NAOMI M. KAIHULA)** aliuliza:-

Kumekuwepo na tabia ya Wake za Marais hapa nchini kuunda *NGO'S* na kuzisajili kama taasisi zao binafsi wakati zinatumia rasilimali za Serikali:-

Je, Serikali itaweka lini utaratibu wa kufanya Taasisi hizo ziwe za kisheria ili hata Wake za Marais wanapomaliza muda wao wapokezane vijiti kama Urais unavyofanywa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Naomi Mwakyoma Kaihula, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba zipo Taasisi zinazoendeshwa na Wake za Marais. Taasisi hizi hufanya shughuli zake kama zilivyo taasisi nyingine za hiari na zisizokuwa za Serikali.

Ipo taasisi ya Wanawake na Maendeleo (WAMA) iliyoanzishwa na Mama Salma Kikwete, mke wa Rais wa awamu ya Nne Mhehsimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Taasisi nyingine ni Mfuko wa Fursa Sawa Kwa Wote (*Equal Opportunity for all Trust Fund(EOTF)* iliyoanzishwa na Mama Anna Mkapa, Mke wa Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa.

Mheshimiwa Spika, kama zilivyo taasisi zingine za hiari na zisizo za kiserikali *NGO'S* taasisi hizi ziliundwa kutegemea na jinsi Mke wa Rais anavyopenda kujishughulisha na shughuli za kijamii. WAMA na *EOTF* zilianzishwa na kuandikishwa kwa mujibu wa sheria inayotawala taasisi hizo na wala hazitumii rasilimali za Serikali.

Inawezekana kabisa akatokea Mke au Mume wa Rais ambaye hana utashi au mapenzi ya kujishughulisha na shughuli za kijamii. Kutokana na mazingira hayo, Serikali haioni sababu za kuweka utaratibu wa kufanya taasisi hizo ziwe za kisheria ili wake/waume za Marais wanapomaliza muda wao wapokezane vijiti maana kwa kufanya hivyo tutakuwa tunawalazimisha kufanya shughuli wasizo na utashi nazo.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Kwa kuwa, taasisi hizi ziko chini ya Mfumo wa Vyama vingi, na kwa kuwa, zote zinafanikiwa kwa kiwango cha juu kwa sababu ya kuegemea kofia ya Marais, naiomba Serikali itoe maelezo ni jinsi gani

Watanzania wa Vyama vyote wananufaika na taasisi hizi na inatumia vigezo gani kuwanufaisha Watanzania wote bila kujali itikadi zao za Vyama vya Siasa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ametaka kujua kwamba wao wanaegemea upande wa Rais, hawa ni wake za Rais. Lakini swali la Msingi ametaka kujua Watanzania wananufaika vipi bila kujali itikadi zao.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie kwamba Wake za Marais wote wawili hawa, hakuna anayefanyakazi kwa kubagua itikadi za Vyama. Nitapenda kutoa mifano hapa kumdhihirishia hilo analosema. Kwa mfano *EOTF* ya Mama Anna Mkapa yeye anashughulika na akina Mama wajasiriamali tangu imeanza mpaka leo amewafikia akina Mama elfu ishirini na mbili ambao amewapa mafunzo ya ujasiriamali, kuwatafutia masoko, amewasaidia kushiriki katika maonesho na katika kufanya hivyo haulizi kama wewe ni CCM, CUF au CHADEMA au unatoka Mwanza au Sumbawanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa WAMA ya Mama Salma Kikwete, mpaka sasa ametoa misaada kwa wanafunzi 933. Amejenga sekondari Nyamisati karibu na *Delta Rufiji* ambayo inapokea watoto yatima na watoto wasiojiweza nchi nzima kutoka Bara na Visiwani bila kujali kama yeye anatoka Chama gani.

Amechangia shilingi milioni mia mbili kwa ajili ya kujenga Hospitali ya akina Mama kwa chama cha

Madaktari wanawake (MEWATA), nina uhakika utakapoenda kutibiwa pale hutaulizwa kama wewe ni *CUF,* CHADEMA au *NCCR.* Lakini pia ameanzisha kampeni inayosema tuwakinge watoto na UKIMWI ya Mtoto wa Mwenzio ni Mwanao Mkinge na UKIMWI.

Katika kufanya hilo haulizi umetoka Chama gani. Sasa hivi anasaidia pia kutoa misaada mbalimbali katika hospitali kutoa vifaa, ambayo imefikia dola za kimarekani milioni tatu ambazo amezipata kutoka kwa wahisani *Project Care* wa Marekani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka niwahakikishie Watanzania kwamba taasisi hizi zinahudumia Watanzania wote hazina ubaguzi wa Mikoa, rangi wala itikadi. (*Makofi*)

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kupata nafasi.

Kwa kuwa, kwa sasa hivi katika kipindi cha miaka ya hivi karibuni, kumekuwepo na kusajiliwa kwa *NGO's* nyingi sana nchini na kwa kuwa, katika kipindi hiki tumeona ni namna gani baadhi ya *NGO* wanavyoshiriki katika kuchochea vurugu nchini na baadhi yake wameonekana kabisa kufurahia migomo mbalimbali iliyopo nchini.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wanafuatilia *NGO'S* hizi na kuona malengo yake, lakini siyo hivyo tu na kuhakikisha kwmaba *NGO's* hizi hazitumiki na mataifa mengine ya nchi za nje ili kuleta vurugu nchini?

**SPIKA:** Halina uhusiano na swali la msingi, Mheshimiwa Jitu Soni.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika ahsante sana. Nilikuwa naomba kuiuliza Serikali.

Je, itakuwa tayari katika hizi *NGO's* nyingi mara nyingi huwa zinashughulika Mijini tu, Je, Serikali itakuwa tayari kusaidia kuratibu na kuhakikisha kwamba zinafanya kazi pia Vijijini ikiwemo mifuko ya Wake za Marais waende hasa vijijini.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, sera na sheria za nchi yetu zinataka ukiandikisha *NGO's* kwanza una-*declare*, unaeleza maeneo gani wewe utafanyakazi. Kwa hiyo, zipo *NGO's* zilizosajiliwa zinafanyakazi vijijini na Mijini.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema hapa ni kwamba anaiuliza Serikali itakuwa tayari kuhakikisha kwamba na wao wanakwenda Vijijini. Nataka kusema kwamba kazi hii ni ya wanasiasa wote sisi, Wabunge, Vyama vya Siasa kataika maeneo yetu tuhakikishe kwamba tunawahamasisha watu mbalimbali kuanzisha taasisi hizi na *NGO's* ili tuwe na *NGO'S* maeneo ya Mijini na Vijijini.

Lakini nataka nikuhakikishie kwa hizi *NGO'S* za hawa akina mama wawili ambao mimi napenda nichukue nafasi hii mbele ya Bunge hili Tukufu kuwapongeza sana kwa kazi nzuri wanayoifanya wao, taasisi zao zinakwenda Mijini na Vijijini kama nilivyosema wanafunzi kwa mfano wanaokwenda

Nyamisati wanatoka Mikoa yote nakuwa-*identified.* Wanatambuliwa watoto yatima na watoto wasiojiweza kutoka Mikoa yote Mijini na Vijijini. *(Makofi)*

Na. 372

**Uingizaji Nchini Bidhaa Zisizo na Viwango**

**MHE. RAMADHAN HAJI SALEHE** aliuliza:-

Kumekuwa na hali ya uingizaji nchini bidhaa zisizo na viwango na baadhi ya bidhaa hizo zimekuwa zikiwadhuru watumiaji:-

Je, ni hatua gani za maksudi zinachukuliwa dhidi ya tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhani Haji Salehe Mbunge wa Bumbwini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *TBS* kwa kushirikiana na wadau wengine kama vile Tume ya Ushindani (*FCC*) na Mamlaka ya Chakula na Dawa (*TFDA)* zimekuwa zikishirikiana katika kusimamia ubora wa viwango vya bidhaa kwa lengo la kumlinda mlaji.

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti uingizaji wa bidhaa zisizo na viwango nchini, Serikali imeweka vituo vya

udhibiti, bandari ya Tanga na Dar es Salaam, ikiwemo kituo cha kupokea mafuta cha Kurasini *Oil Jetty (KOJ)* na vituo vya ndani vya kuhifadhia makontena *Inland Container Depot*, Maeneo ya Namanga, Horohoro, Holili na Sirari na baadaye Tunduma kwa lengo la kuimarisha kwa bidhaa zinazoingia toka nje.

Mheshimiwa Spika, Mwezi Februari 2012, *TBS i*meanza kutekeleza mfumo wa kukagua bidhaa nje ya nchi kabla hazijasafirishwa kuja nchini kwa kutumia viwango vya Tanzania *(Pre-shipment Verification of Conformity to Standards* (*PIVOC*).

Mheshimiwa Spika, cheti cha ubora hutolewa kwa bidhaa zinazokidhi hitaji la ubora wa viwango vya kitaifa au kimataifa. Aidha, mfumo huo wa ukaguzi utatumika sambamba na mfumo uliopo wa kukagua bidhaa wakati zimefika katika bandari zetu kwa bidhaa ambazo zitakuwa hazina vyeti hivyo. Pamoja na hayo, *TBS* imejiwekea utaratibu wa kufanya ukaguzi wa kushtukiza wa mara kwa mara katika maduka yanayouza bidhaa zinaingia toka nje ya nchi, na mara bidhaa hizo zinapobainika na kukamatwa hatua za kisheria huchukuliwa ikiwa ni pamoja na kuteketeza bidhaa hizo.

**MHE. RAMADHAN HAJI SALEHE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, bidhaa hizo zinakaguliwa na *TBS* na bado baadhi ya maduka yanaendelea kuuza bidhaa zilizo chini ya kiwango. Je, Waziri unatuambia kwamba *TBS* siyo waaminifu?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, bidhaa zozote nchini ambazo hazina viwango ambazo zimeingizwa kinyemela na zinauzwa katika mitaa au maduka mbalimbali ni kinyume cha sheria na kwa vyovyote vile, Serikali inaendeleza mkakati wake wa kuzikamata na kuzichukulia hatua zinazostahili ikiwemo kuziteketeza.

Mheshimiwa Spika, naomba kusisitiza kwamba bidhaa hizi kama zimeingia kwa njia za panya, zimeingia kwa njia zozote zile au kupitia watumishi wa Serikali ambao siyo waaminifu, sisi tutazichukulia hatua na tunaendelea kuongeza uwezo wa kufanya hiyo.

**MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa moja kati ya sababu ambazo zinasababisha nchi yetu isinufaike vya kutosha kwenye sekta ya madini ni kwamba makampuni mengi ya madini yananunua bidhaa nje ya nchi na badala ya kutumia bidhaa za ndani kwa kusingizia kukosekana kwa ubora wa bidhaa hizo.

Je, Mheshimiwa Waziri atakiri kwamba *TBS* imejiridhisha kwamba bidhaa zinazozalishwa nchini hazijakidhi viwango?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Masauni kama ifuatavyo:-

Ni kweli baadhi ya makampuni ya madini kama anavyosema yamekuwa yakiagiza bidhaa kutoka nje, bidhaa ambazo kwa kweli zinaweza zikatengenezwa hapa Tanzania na hili suala halijawa suala la viwango. Wakati mwingine wamesingizia suala la wingi wa bidhaa husika.

Serikali katika mipango yake na kwa kutumia mashirika yake mengine yote, tumeyaagiza mashirika yote na makampuni yote ya madini yanayofanya kazi hapa nchini, jambo la kwanza; manunuzi yote yanayopatikana hapa nchini yanunuliwe hapa nchini kwanza kabla hawajaagiza hizo bidhaa nje ili kuweza kuongeza ajira kwa wananchi wetu na kuweza kuchochea ukuaji wa viwanda vyetu vya ndani na ni jambo ambalo Serikali inaahidi kuendelea kulifuatilia kwa nguvu zote. *(Makofi)*

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa kuna magari yaliingia nchini bila kukaguliwa na *TBS* walichaji asilimia 10 ya thamanai ya gari au shilingi laki saba.

Je, Serikali iko tayari kuyatafuta magari hayo na kuyafanyia ukaguzi?

**SPIKA**: Wewe itabidi uyaonyeshe yako wapi. Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara naomba

nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vincent Nyerere, kama ifuatavyo:-

(a) Kwanza ni kweli kwamba utaratibu mzima wa ukaguzi wa magari nje ya nchi, uliingiwa na dosari kubwa na kama mnafahamu kulikuwa na makampuni 8 ambayo yalikuwa yanafanya kazi hiyo ya ukaguzi na Kamati yako ya Bunge iliweza kwenda huko nchi za nje pamoja na kushirikiana na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali na kugundua kwamba makampuni 5 kati ya 8 yalikuwa yanafanya kazi kinyume kabisa na viwango na hayakuwa yakitenda haki. Serikali imeyafuta makampuni 5 kati 8 yaliyokuwa yanafanya kazi hiyo na hii ilitokana na agizo ambalo lilitoka humu ndani Bungeni.

(b) La pili, kwa kuwa katika mchanganyiko huo inawezekana kuna magari ambayo hayakukaguliwa nchini na kwa sababu ya tishio la uwezekano wa kuwepo na vimeo kama vile vya kemikali ambavyo ni hatari sana kwa maisha ya watu. Serikali inapogundua kwamba kuna aina yeyote ya magari hayakaguliwa, tutafanya kazi hiyo kwa uaminifu na ningemwomba Mheshimiwa Vincent Nyerere na Waheshimiwa Wabunge wengine wote kama unafahamu gari lolote nchini halikukaguliwa tafadhali utuambie na Serikali kupitia *TBS* itafanya kazi hiyo.

Na. 373

## Kusaidia Ukuaji wa Viwanda Nchini

**MHE. ZARINA S. MADABIDA (K.n.y. MHE. RITA L. MLAKI)** aliuliza:-

Serikali imeweka wazi kuwa katika Sera zake itasimamia ukuaji wa viwanda nchini na kuhakikisha kuwa bidhaa za kilimo zinaongezwa thamani kabla ya kuuzwa nje ya nchi.

(a) Je, Serikali imesaidia uanzishwaji wa viwanda vingapi nchini katika kipindi cha miaka mitano?

(b) Je, ni mazao gani yaliyosindikwa ambayo yaliuzwa nje ya nchi katika kipindi cha miaka mitano?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA)** alijibu**:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rita Louise Mlaki, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC)* na Mamlaka ya maeneo Huru ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje *(EPZA)* imesaidia uanzishwaji wa viwanda 174 kupitia Sera na mikakati ya kuvutia uwekezaji nchini kati ya mwaka 2007/2011.

Aidha, jumla ya miradi mipya ya viwanda 988 ilisajiliwa TIC na miradi 446 ilipewa leseni za kuanzisha viwanda na Wakala wa Usajili wa Biashara *(BRELA),* wakati *EPZA i*litoa leseni 54 kwa kipindi hicho na kufanya jumla ya miradi ya viwanda iliyopewa leseni kufikia 500.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa ya Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* ya mwaka 2007/2011 inaonyesha kuwa, mazao ya aina tofauti tofauti 41 yalisindikwa na kuuzwa nje ya nchi. Aidha, jumla ya uzito wa kilogramu trilioni 10.5 ya bidhaa zilisindikwa na kuuzwa nje na kuliingizia Taifa shilingi trilioni 6.6.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hiyo. Kwa kuwa Serikali imekuwa na Sera ya kusaidia kuanzisha viwanda na vile vile Sera ya kulinda viwanda hivyo. Lakini Sera hizo utekelezaji wake inategemea ni nani yuko juu ya meza na utashi wake:-

(a) Je, Serikali haioni sasa Sheria itungwe ili kusudi iweze kuweka mashiko katika Sera hizi ambazo sasa hivi hazitekelezwi?

(b) Je, Serikali iko tayari kuileta hiyo Sheria haraka iwezekanavyo ili kusudi basi tulinde viwanda vyetu vya nchini kama inavyosema kwenye Sera hizo? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika,

kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zarina Madabida, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwanza katika hali ya kawaida sasa hivi, Serikali inazo Sera tayari za kulinda viwanda vya ndani na nia yetu hasa ni kuhakikisha kwamba viwanda hivi vya ndani vinaweza vikakuwa na kuongeza ajira. Hilo la kwanza.

Lakini la pili tunaongezea uwezo nchi ya kuweza kutengeneza bidhaa zenye viwango vya Kimataifa na hivyo kuweza kumudi ushindani wa bidhaa ambazo zinatoka nchi zingine na sasa hivi, hususani katika soko letu la pamoja la nchi za Afrika Mashariki. Kulinda viwanda vyetu vya ndani sasa hivi itaendana moja kwa moja na Sheria inayotawala Jumuiya za Afrika Mashariki kwa sababu tayari tumekuwa soko moja.

(b) Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kuendelea mwaka hadi mwaka Serikali itakuwa tayari kuzipitia Sheria zake, Sera zake ili kuhakikisha zinaendana na wakati na tunaendelea kuvilinda viwanda vyetu kama nilivyosema katika jibu langu la msingi.

Na. 374

## Changamoto ya Mahitaji Makubwa ya Umeme

**MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza:-

Jiji la Dar es Salaam linakuwa kwa kasi sana ikiwa ni pamoja na kujengwa kwa majumba makubwa ya ghorofa yanayohitaji matumizi makubwa ya umeme:-

Je, Serikali imejipanga vipi kukabiliana na changamoto za maendeleo ya maji na tatizo la umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE**) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini kwa kupitia *TANESCO* imeandaa mipango kabambe ya kukarabati, kuboresha na kujenga miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme katika Jiji la Dar es Salaam inayofadhiliwa na Serikali pamoja na washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, miradi inayotekelezwa katika Jiji la Dar es Salaam ni pamoja na mradi unaofadhiliwa na Serikali ya Finland na Tanzania ambao unaokadiriwa kugharimu *Euro* milioni 26.5 katika

maeneo ya *City Centre*, Sokoine na Kariakoo; mradi unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AFDB)* ambao utakarabati vituo vya kupoozea umeme vilivyopo katika maeneo ya Sokoine na Ilala unaogharimu Dola za Marekani milioni 7.6.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine ni mradi ujulikanao kama *TEDAP* unaofadhiliwa na Benki ya dunia kwa gharama za Dola za Marekani milioni 15.6 unaohusisha kazi za ufungaji wa *transfoma* mpya 10 maeneo ya Chan'gombe na Kariakoo, *transfoma 6* katika maeneo ya *City Centre*, *Factory Zone I&II,* Mburahati, Mikocheni na *Oyster Bay* ; na miradi inayofadhiliwa na Serikali kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 0.584, miradi hii ipo katika hatua mbali mbali za utekelezaji katika maeneo mengi ya Jiji la Dar es Salaam ambapo inatarajiwa kukamilika mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, pamoja na miradi hii, Serikali itaendelea kuweka mikakati mbalimbali ili kuhakikisha kuwa inakabiliana na changamoto za ukuaji wa Miji kwa kuwa na umeme wa uhakika muda wote.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za Serikali katika kuboresha umeme katika Jiji la Dar es Salaam ambazo nazipongeza sana, ninayo maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Je, Serikali lini itakamilisha kazi ya kufunga *transfoma* ya Mburahati na Mikocheni pia *Oyster Bay* ili wananchi wa Kijitonyama, Sinza, Mbezi, Kimara na

Wilaya nzima ya Kinondoni nao waweze kupata umeme wa uhakika?

(b) Je, Serikali itakamilisha lini ujenzi wa *sub-station* ya Kurasini na Mbagala ili wananchi wa maeneo haya pia waweze kupata umeme mkubwa na wenye kutosheleza mahitaji yao?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mariam Kisangi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru napokea pongezi kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge, lakini pia ameuliza ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa transfoma katika maeneo ya Mburahati na Mikocheni.

Kwenye jibu la msingi nimeeleza miradi hii yote iko katika hatua za utekelezaji na kazi hizi zinaendelea na inakusudiwa kukamilika ndani ya mwaka huu 2012 kwa miradi yote ya transfoma na maeneo uliyoyataja pamoja na *sub-station* ambazo umezitaja maeneo ya *City Center.*

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Waziri kwa kuwa sasa hivi Wizara yako kupitia *TANESCO* imeanzisha zoezi la kukagua wizi wa umeme unaofanyika katika majengo au mitaa ya Miji ya Dar es Salaam.

Je, ni ipi tathmini ya zoezi hili ili hao wafadhili ambao umewataja hapa, wasije wakaingia roho nyonge wakaanza kuondoa misaada yao?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE)**: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mhehsimiwa Rajab Mbarouk kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Wizara ya Nishati na Madini kwa kushirikiana na *TANESCO* tunaendesha operation kabambe katika Jiji la Dar es Salaam, kukagua majengo pamoja na viwanda na nyumba mbalimbali ambazo watu wamejiunganishia umeme kwa njia za wizi na udanganyifu na zoezi hili litakuwa ni endelevu ili kuhakikisha kwamba Wizara pamoja na Shirika la umeme *TANESCO* halipotezi mapato ambayo mengi yanapotea kutokana na wizi na zoezi hili litaendelea na Mikoa mingine ili kuhakikisha kwamba tunasimamia vizuri rasilimali na Shirika linaweza kukuwa kiuchumi na kuweza kujiendesha kwa faida.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa kumekuwa na tatizo la *transfoma* huko Dar es Salaam kulipuka lipuka, na hili linasemekana linatokana na watu wabaya ambao wanaiba mafuta ya transfoma na wanapikia sijui *chips* kuhatarisha afya za watu.

Je, sasa Serikali inafunga *transfoma* mpya, ina mkakati gani kuhakikisha sasa wizi huo haupo tena?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE)**: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Diana Chilolo analouliza kuhusu *tranfoma* kulipuka lipuka katika Jiji la Dar es Salaam na maeneo mengine nchini:-

Ni kweli kwamba matatizo mengi yanayotokea ya kulipuka kwa *transfoma,* mengine ni ya kiufundi lakini mengine yanachangiwa na wizi wa mafuta katika *transfoma* maeneo mbalimbali mchini. Serikali tunapenda kutoa wito kwa wananchi wote kwa sababu *transfoma* hizi ziko kwenye maeneo mbalimbali ya nchi na maeneo mengine ni ya mitaani ama Vijijini na si rahisi kwa Serikali ama *TANESCO* kuweka walinzi kila *transfoma* kuhakikisha kwamba hazihujumiwi.

Niombe kutoa wito kwa Wabunge, wananchi wote ambao wana mapenzi mema na Taifa lao wawe walinzi wa kushirikiana na Serikali katika kuhakikisha kwamba transfoma hizi hazihujumiwi na sisi kwa upande wa kiufundi tutaendelea kuzikarabati na kufunga transfoma mpya maeneo ambayo transfoma zimechoka ili kupunguza milipuko na kupunguza ajali zozote zinazoweza kutokana na milipuko hii ya *transfoma. (Makofi)*

Na. 375

**Tatizo la Maji - Lushoto**

**MHE. HENRY D. SHEKIFU** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuondoa tatizo la maji japo kwa kuchimba na kutengeneza visima vifupi vilivyoharibika katika Kata za Kwekanga, Malibwi, Ngwelo, Mlola, Kilole na Makanya?

(b) Kwa kuwa mpango wa Benki ya duni wa kusambaza maji Vijiji 10 kila Wilaya unaonekana kushindwa. Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya miradi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Henry Daffa Shekifu, Mbunge wa Lushoto lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto inaendelea kuvifanyia matengenezo visima vilivyoharibika katika Kata za Kwekanga, Malibwi, Ngwelo, Mlola, Kilole na Makanya kwa kufunga pampu mpya kama ifuatavyo:-

Kata ya Kwekanga; visima vinne (4) kati ya vinane (8) katika Kijiji cha Kwekanga; Kata ya Ngwelo kisima kimoja (1) kati ya viwili (2) eneo la Zahanati; Kata ya Mlola kisima kimoja (1) kati ya tatu katika Kijiji cha Lwandai na Kata ya Malibwi visima vitano (5) katika Kijiji cha Malibwi.

Ukarabati wa miradi katika Kata nilizozitaja ulifanyika kupitia programu ya maji wakati wa kutekeleza miradi midogo midogo yenye kuleta matokeo ya haraka (*quick wins*).

Aidha, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto itaendelea na kazi ya kukarabati visima vifupi vilivyoharibika na kuchimba visima katika Kata zilizobaki kwa kadiri fedha zitakavyopatikana.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa Vijiji 10 katika kila Halmashauri. Hadi sasa Halmashauri 67 zimepata vibali vya kuanza ujenzi wa miundombinu ya maji. Kati ya hizo, Halmashauri 50 tayari zimeanza ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji. Nachukua fursa hii kuhimiza Halmashauri 17 zilizobaki zianze utekelezaji wa miradi mara moja. Halmashauri ya Lushoto inatarajia kusaini mikataba na wakandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya maji katika Vijiji vitatu (3) vya Kweminyasa, Bumbuli na Irente Juu kwa gharama ya shilingi milioni 827.7.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya maji ya Vijiji 10 kulingana na kasi ya Halmashauri katika kufanya tathmini ya taarifa mbalimbali kwa ajili ya kupata vibali vya kuanza ujenzi wa miundombinu ya maji. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge katika Majimbo yenu kuhamasisha kasi ya utekelezaji wa mradi huo ili ulete matokeo mapema.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nina maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(a) Kwanza niishukuru Serikali kwa hizi juhudi baada ya kubanana sana, lakini katika visima 24 ambavyo vilikuwa vimeharibika ni visima 11 tu vimetengenezwa katika Kata nilizotaja. Bado viko visima karibu 13.

Je, Serikali inatamka nini na hakuna dalili zozote za kuonyesha kwamba kuna uchimbaji wa visima vipya. Serikali inatamka nini juu ya kumalizia visima hivi?

(b) Katika suala la visima 10 katika kila Wilaya ni kweli kwamba mradi huu umeanza karibu miaka 9 iliyopita. Kwa Wilaya ya Lushoto ni visima 3 tu na ahata hivyo vitatu ambavyo vimesemewa kwamba wanasubiri kuanza, wamesubiri no *objection* kutoka Benki ya Dunia mpaka leo kuanzia mwezi wa tisa, *no objection* haijatoka.

Sasa Serikali inatamka nini katika ucheleweshaji huu ambao saa nyingine tunasingizia Halmashauri, lakini ni vikwazo vinavyotokana na Benki ya Dunia?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo lakini kwanza nimpongeze sana kwa kufuatilia suala la maji katika Wilaya yake ya Lushoto, kwani maswali haya ameyauliza kuanzia miaka 2003/2004 mpaka 2009 yamekuwa yakiulizwa.

Mheshimiwa Spika, nianze na sehemu (b) kwamba, miradi hii imechukua muda mrefu na ni karibu miaka 9 bado haijaanza. Sasa nichukue mfano wa Wilaya yake ya Lushoto, ni nini kilichotokea:-

Mheshimiwa Spika, cha kwanza, ni kwamba, kigezo kikubwa ambacho kimechukua muda mrefu ni kwamba, miradi hii inapitia ngazi mbalimbali, ngazi ya Halmashauri, ngazi ya Wizara na baadaye kupata *No Objection* kwenye ngazi ya Benki ya Dunia.

Kwa hiyo, katika ngazi ya Wilaya, kuna mambo ambayo wanatakiwa wayatekeleze. Sasa kwa mfano, Lushoto walipopata yule Mkandarasi Msanifu ambaye ni *Col. Consult,* alipewa kazi mwaka 2009, kazi ile alitakiwa aifanye kwa miezi 9, lakini ilipofika 2010 akawa hakumaliza ile kazi, kwa maana hiyo akaomba kuongezewa muda.

Mheshimiwa Spika, alipoomba muda akaongezewa, lakini ilipofika 2011 akawa tena hakumaliza ile kazi. Akaomba kuongezewa mara ya tatu na mara ya tatu ndio Halmashauri, ikakataa baada ya kuona kwamba, anasuasua.

Kwa hiyo, tatizo kubwa linaloonekana vilevile hapa, ni kwenye utendaji, utekelezaji wa wale Wakandarasi ambao tunakuwa tumewapata kwenye Halmashauri zetu, wanakuwa ni watu ambao wanasuasua.

Mheshimiwa Spika, na nichukue nafasi hii kumpongeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Lushoto,

kwa kuamua kumsimamisha huyu na kutafuta watu wengine, ili waweze kufanya kazi iweze kwenda vizuri. Nmhakikishie tu Mheshimiwa Shekifu kwamba, katika Vijiji vyake vile vitatu, tayari vimetengewa milioni 827 kama nilivyosema. Kwa hiyo, kama hizo taarifa zitafika Wizarani, watapewa *No Objection* na itaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili, kwamba, visima vilivyobaki vitafanyiwa nini?

Mheshimiwa Spika, la msingi ni kwamba, utekelezaji umeanza. Viko visima ambavyo vimeshakarabatiwa kwa hiyo, ukarabati utaendelea kulingana na fedha zitakavyoendelea kupatikana na jinsi na wao pia wanavyoweka vipaumbele vyao bila kutegemea tu fungu kutoka Wizarani.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ili na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, Sera ya Taifa ni kuhakikisha kwamba, watu wanapata maji safi na salama. Vijiji vingi vya Tanzania, kwa kweli, hasa vijijini, wana tatizo kubwa la maji na hasa kwa mfano kule Mkoani kwetu Geita pamoja na Jimbo langu la Busanda, kwa kweli, changamoto ni kubwa sana, hasa Vijijini. Ningependa kujua sasa ni nini hasa mpango wa Serikali, wa kuleta maji na kupeleka maji safi na salama, hasa Vijijini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la

nyongeza la Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunao mpango na mpango huu tumesema kwamba, ulianza mwaka 2006 wa miaka mitano mitano, lakini unalenga kufikia mwaka 2025 kuona kwamba, maji Vijijini tutakuwa tumefikisha 95% na maji Mijini 100%. Ili kuutekeleza, tulianza kwa miaka mitano mitano.

Sasa ni kweli, yametokea matatizo hapa katikati, awamu ya kwanza ya miaka mitano imechukua muda mrefu na hivyo, kulazimika kuongeza muda mwingine. Katika hiyo awamu ya kwanza, ndio hivyo vijiji vitatu ambavyo tumeviainisha kwamba, kila Halmashauri inavyo; na baada ya ongezeko la fedha Mheshimiwa Waziri, alipotangaza hapa ndani, kuna Vijiji vingine viwili vinafanya nini, Vinaongezeka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme tu kwamba, kama nilivyosema, ni kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, wahamasishe utekelezaji wa harakaharaka kwenye Halmashauri zao, ili taarifa zifike Wizarani na Benki ya Dunia inapozipata hizo taarifa, inatoa *No Objection,* na ile miradi inaendelea kutekelezwa. Lakini azma ya Serikali, kuona kwamba, Vijini ifikapo 2015 wanapata maji angalao kwa 65%.

**MHE. MWIGULU L. M. MADELU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Hili tatizo la visima kuharibika pamoja na mabomba, liko nchini kote. Suluhisho lake, ilikuwa ni Serikali, kuwa na Mfuko wa Maji, kama ilivyo kwenye barabara, ili iweze kusaidia mabomba yaliyoharibika.

Kwa kuwa Serikali, inatengeneza Programu ya Vijiji vipya. Sheria, tayari ilishapitishwa tangu mwaka 2009 ya kuwa na Mfuko wa Maji.

Je, ni kitu gani kimecheleweshwa kuwa na Mfuko wa Maji, ili kusaidia mabomba yaliyoharibika Majimboni?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la nyongeza, la Mheshimiwa Madelu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru kwa kuuliza swali ambalo ni zuri, linagusa sehemu moja muhimu ya uharakishaji wa utekelezaji miradi ya maji. Nikiri kwamba, ni kweli, kuna mapungufu baada ya Sheria kutungwa mwaka 2009, hadi leo 2012 bado *regulations* zilikuwa hazijaandaliwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuliona hili Mheshimiwa Waziri, ameshaagiza; Watendaji wetu na wao wameisikia sasa hivi ninavyoongea ni kwamba wamepewa muda hadi mwezi wa 12 wawe wameshakamilisha kuandaa *regulations* na vilevile *regulations* hizo, zitaambatana na namna ya kuusimamia huo mfuko na kuonesha vyanzo vya kupata fedha kwenye huo Mfuko.

Kwa hiyo, tunataka tuwaahidi Watanzania, kwamba, tunalifanyia kazi na ifikapo Mwezi wa 12, litakuwa liko tayari.

Na. 376

## Mradi wa Maji wa Kiburubutu

**MHE. RACHEL M. ROBERT (K.n.y. MHE. SUZAN L. KIWANGA)** aliuliza:-

Mji wa Ifakara wenye wakazi takribani 100,000 sasa umepeleka maombi ya kupatiwa Shilingi 500,000,000/= kwa ajili ya upembuzi wa mradi wa maji ulioko Kiburubutu:-

Je, ni lini Serikali, itapeleka fedha, ili kazi hiyo iweze kuendelea?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suzan Limbweni Kiwanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunakiri kupokea barua ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero, kuhusu maombi ya shilingi milioni 500, kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa mradi wa maji ulioko Kiburubutu, ili kuboresha huduma ya maji katika mji wa Ifakara, ambao ni Mji Mkuu wa Wilaya ya Kilombero. Kutokana na Ufinyu wa Bajeti, Serikali, inatekeleza miradi ya maji katika Mkoa wa Morogoro kwa awamu. Katika awamu ya kwanza, miradi inatekelezwa katika Mji wa Kilosa, Gairo, Mvomero na Turiani. Kazi zinazoendelea sasa ni ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Spika, wakati miradi iliyotajwa inaendelea, Miji ya Ifakara, Mahenge na Mikumi, itafanyiwa upembuzi yakinifu, usanifu na kuandaa makabrasha ya zabuni, kulingana na upatikanaji wa fedha. Kwa Mwaka huu wa Fedha, Wizara itashirikiana na Mamlaka ya Maji safi na Maji taka Morogoro, kuandaa hadidu rejea kwa ajili, ya kumpata Mtaalamu Mwelekezi wa kufanya kazi zilizotajwa, ukiwemo mradi wa maji uliko Kiburubutu.

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nilikuwa naomba kumwuliza Naibu Waziri wa Maji, japokuwa miradi hiyo ya awamu ya kwanza imeshaanza katika Miji ya Kilosa, Gairo na Mvomero. Nilikuwa nataka kujua imefikia hatua gani na lini itakamilika?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba, katika miradi hii ya vijiji 10, Mkoa wa Morogoro. Mkoa wa Morogoro uko nyuma sana katika utekelezaji na Wilaya hii ya Kilosa, ndio sasa inatakiwa iwasilishe zile taarifa kwenye Wizara na baadaye zipate *No Objectionm,* ili ujenzi uanze. Kwa hiyo, tunataka kuwahimiza kwamba, zile taarifa waziwasilishe haraka kwa sababu, usanifu ulishafanyika, ili sasa mpewe kibali cha kuanza ujenzi wa miundombinu kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi.

**MHE. MUSSA Z. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Milioni 500 kwa suala la upembuzi ni pesa nyingi sana. Na maeneo mengi sana katika Halmashauri nchini mwetu, ni pesa nyingi sana zinatolewa kwa upembuzi. Matokeo yake, visima vinachimbwa na maji kunakuwa hakuna.

Mheshimiwa Spika, ni hatua zipi sasa zitachukuliwa kwa wale wanaofanya upembuzi huu na baadaye maji kutokupatikana?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli, yako maeneo ambayo upembuzi yakinifu ulifanyika, visima vikachimbwa, lakini maji hayakupatikana. Na hili sio la ajabu kwa sababu, tulivyosema huko nyuma ni kwamba, teknolojia ya utafiti wa maji chini ya ardhi, bado haitoi 100%; utafiti unatuashiria kupata maji kati ya 50% mpaka 70%.

Sasa ni nini kinafanyika; ni kwamba yale maeneo yote ambayo hayakupata maji, tutarudia kwenye maeneo yaliyo karibu nayo na ikishindikana, tutachukua hatua nyingine, ikiwa ni pamoja na Vijiji vya karibu au teknolojia nyingine kama za uvunaji wa maji, mabwawa na kadhalika.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, Mungu akubariki kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri, ni kwa sababu, mradi wa maji ambao umejengwa katika Kata ya Mwankoko, kwa ajili, ya kusambaza maji kwenye Mji wa Singida, umeshakamilika. Tatizo lake kubwa ilikuwa ni *TANESCO* kupeleka umeme. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hapa nilimwandikia Mheshimiwa Waziri, barua ya kumwomba aiambie *TANESCO* Singida, kupeleka umeme Mwankoko na akakubali.

Je, Wizara yako iko tayari sasa kuawagiza wahusika ili waweze kuwasiliana na *TANESCO,* kupeleka mradi kule Singida, iondokane na shida ya maji? Ahsante sana.

**SPIKA:** Kweli, Mungu kanipa, lakini mbona hili Swali la Singida hili, lilikuwa la nani hii wewe? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Vita Rashid Mfaume Kawawa?

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, hili tatizo la maji la Mji wa Ifakara, linafanana kabisa na matatizo ya maji katika Mji wetu wa Namtumbo. Ambapo Mji huo, Mamlaka ya Maji ilishafanya utafiti kwa kupitia Mhandisi Mshauri, ambaye alifanya kazi yake na ripoti yake ilishakwenda Wizarani. Wizara inasemekana ilishapeleka kwa sababu, mradi wenyewe unafadhiliwa na *World Bank,* ilishapelekwa Benki ya Dunia na kila ninapouliza, tunaambiwa tunasubiri *No Objection.*

Mheshimiwa Spika, sasa wananchi wa Namtumbo wananiuliza, huyu *No Objection* atarudi lini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Kawawa, ni yale yale matatizo. Uliza swali la Kisera, umeona jirani yako pale alivyouliza swali lile, la kiujumla; sio tena unauliza tena habari ya Namtumbo, habari hiyo haiwezekani, huyu hakujiandaa hivyo kwa saula la Namtumbo.

Kwa hiyo, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Dkt. Festus Bulugu Limbu.

Na. 377

**Hitaji la Kivuko – Kisiwa cha Ijinga Wilayani Magu**

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU** aliuliza:-

Wananchi wa Kisiwa vha Ijinga, Kata ya Kahangara, wamekuwa wakipata kero kubwa sana wakati wa kusafiri kwenda na kutoka Kisiwa hicho:-

(a) Je, Serikali, ina mpango gani wa kuwajengea gati wananchi hao kwa pande zote mbili, ili nao wafaidi uhuru na maendeleo?

(b) Je, ni lini Serikali, itajenga kivuko (Pantoni) kwenda katika Kisiwa hicho, ili kiwakomboe wananchi wa Kisiwa hicho, kutoka kwenye lindi la umasikini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Festus Bulugu Limbu, Mbunge wa Magu, lenye vipengele (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kabla ya Wizara, kuweka mpango wa kujenga gati, kununua Kivuko kwa ajili ya Shinembo na Kisiwa cha Ijinga, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, itatuma Wataalam, ili kutafiti uwezekano wa kuweka kivuko hicho pamoja maegesho ya pande zote mbili.

Utafiti huo utawezesha kujua kama kuna kina cha maji cha kutosha, pamoja na usalama wa njia ambayo kivuko kinaweza kutumia. Matokeo ya utafiti huo ndio yataiwezesha Serikali, kupanga kununua kivuko na kujenga maegesho/gati au kutokununua kivuko.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa msingi wa maelezo haya serikali itaweza kununua kivuko kipya kwa ajili ya Shinembo na Kisiwa cha Ijinga, baada ya kupata matokeo ya utafiti wa kitaalam na kuwa na uwezo wa kifedha. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Magu, italazimika kuimarisha barabara itakayoenda eneo la kivuko.

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Napenda kuipongeza sana Serikali, kwa majibu yake yenye matumaini kwa wananchi wa Kisiwa cha Ijinga, ambao

wamehangaika sana siku nyingi, kusafirisha mazao yao na kupata huduma mbalimbali. Kwa sababu, pale kuna Zahanati, kuna Kituo, kuna Shule ya Msingi na kuna wanafunzi wanaosoma Sekondari pale Shinembo.

Mheshimiwa Spika, sasa nina maswali mawili ya nyongeza; Mheshimiwa Waziri, amesema watatuma Wataalam, ningependa kujua hawa wataalam watatumwa lini? Kwa sababu, hii sio mara ya kwanza kuwasilisha kero hii ya wananchi wa Ijinga. Napenda nijue ni lini, Waziri ama Wizara, itatuma wataalam hao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa sababu, hali ni mbaya na wananchi wanalalamika muda mrefu. Je, Waziri, hawezi kutenga fedha kuanza kujenga maegesho ama gati hivi sasa wakati utaalamu wa kujua kama kivuko kitaweza kupita, njia iko salama, na kadhalika?

Watenge fedha kwa ajili ya kujenga maegesho pande zote mbili, ili kuondoa kero ya wananchi wanaposafirisha mazao yao, wanayaweka kwanza kwenye maji ndio wayavushe. Kwa hiyo, yanapungua thamani.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, yuko tayari kuangalia uwezekano huo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba, Mwaka huu wa Fedha, tutatuma Wataalam. Naomba nikuahidi kwamba Wataalam hao watatumwa mapema iwezekanvyo, baada ya kumaliza Kikao cha Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sehemu ya pili kwamba, tungetenga fedha za ma-gati. Haitawezekana kutenga fedha za magati kwa sababu, kwanza ni lazima tufanye utafiti, tuone kina cha maji, kinatosha kwa pantoni tena ni kwa pantoni aina gani inatakiwa kujengwa. Ndio tutafanya *design* tuweze kuona hayo magati yajengwe ya kiwango au *size* gani.

Kwa hiyo, ni lazima tufanye kwanza utafiti wa kina cha maji, halafu tuta-*determine* ni aina gani ya gati inatakiwa ijengwe.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Sehemu ya barabara ya Shelui kwenda Singida Mjini, eneo la Mlima Sekenke, imeharibika sana na ni hatari sana kwa mabasi na malori makubwa yanapopita eneo hili.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, atakubali nami kwamba, barabara hii ilijengwa chini ya kiwango?

Kwani ni takribani miaka mitatu tu tangu ianze kutumika na imeharibika?

**SPIKA:** Swali zuri sana, lakini sio mahali penyewe. Maana ilikuwa habari ya kivuko na barabara, tena barabara ya Sekenke, inaingiaje hapo? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Vicent Nyerere, swali jingine linalofuata.

Na. 378

**Kuanza Kazi Kwa Kivuko Kati ya Musoma Mjini na Rorya**

**MHE. VICENT J. NYERERE** aliuliza:-

Maegesho ya kivuko kati ya Musoma Mjini (Mwigobero) na Rorya (Kinesi), yameshakamilika:-

Je, ni lini kivuko hicho kitaanza kufanya kazi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vicent Josephat Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli ujenzi wa maegesho ya Kivuko kati nya Musoma Mjini na Rorya, uliokuwa ukitekelezwa na *Cooperation Sole* kwa kushirikiana na Kampuni ya *Best Tanzania Limited* umekamilika.

Mheshimiwa Spika, kazi ya ujenzi wa kivuko kipya cha *MV. Musoma* cha kuhudumia kati ya Musima (Mwigobero) na Rorya (Kinesi), chenye uwezo wa kubeba tani 85, ilikamilika Mkoani Mwanza, tarehe 12 mei, 2012 na kilisafirishwa kwenda Musoma na kufika tarehe 14 Mei, 2012. Kivuko hiki, kilianza kufanya kazi tarehe 16 Juni, 2012. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Vicent Nyerere, swali la nyongeza.

**MHE. VICENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya swali la myongeza. Swali lilikuwa la zamani kweli mpaka kivuko kimeanza kazi. Kwa kuwa, kivuko tayari kimeanza kazi na hakuna kibanda cha wasafiri kusubiri kujikinga na mvua au jua, pia vyoo.

Je, Serikali, iko tayari kukamilisha mapungufu hayo?

Mheshimiwa Spika, Swali la pili. Barabara itokayo kivukoni Kinesi, kuelekea Kuruye, ni mbaya, haipitiki kwa muda wote wa mwaka.

Je, Serikali, iko tayari kuweka lami kuelekea kivukoni?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikubaliane na yeye kwamba, tutaangalia hilo suala la kujenga kibanda kwa ajili ya wasafiri wanaosubiri kupanda hicho kivuko.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu barabara. Suala la barabara tutaliangalia kama ni lazima tujenge, tunaweza kuikarabati hata kwa changarawe, sio lazima tujenge kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa wakazi wa Mkoa wa Mara, hususan wafanyabiashara, wanafaidika sana na huduma hii ya kivuko.

Je, ni kwa nini Serikali, isijenge nyumba za watumishi upande wa Kinesi, Rorya, ili kuweza kurahisisha ratiba ya kivuko hiki kuanzia Rorya, asubuhi na sio Musoma Mjini, kurahisisha huduma za kiuchumi na kijamii?

Kwa maana sasa hivi, kinawajibika kurudi Musoma Mjini jioni, hata kama hakina abiria kwa sababu, wafanyakazi wale, hawana nyumba kule Kinesi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la kujenga nyumba za watumishi kwa pande zote mbili tutaliangalia katika kuboresha utendaji kazi wa kivuko kile. *(Makofi)*

Na. 379

## Mwongozo wa Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake

**MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza:-

Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake (*WDF*) ulianzishwa mwaka 1993 ka Azimio la Bunge kwa Mujibu wa *Exchequer and Audit Ordinance* ya 1961 kwa lengo la kutoa mikopo kwa wanawake na vijana, kiwango cha mkopo cha 500,000/= zinazotolewa na Halmashauri zote hapa nchini kwa vikundi vya akina Mama hazikidhi haja kutokana na mfumuko wa bei hali inayowasaabishia kushindwa kurejesha mikopo hiyo.

(a) Je, Serikali haioni kuna haja ya kubadilisha mwongozo ambao umepitwa na wakati na hauendani na uhalisia wa maisha ya sasa?

(b) Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya kuongeza kiasi ili kuendana na thamani halisi ya shilingi?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELAO YA JAMII, JINSI NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana naMheshimiwa Mbunge kuwa mwongozo wa

uendeshaji wa mfuko wa Maendeleo ya Wanawake hauendani na uhalisia wa maisha ya sasa. Mwongozo huo ulioandaliwa mwaka 2000, kwa maelekezo ya Wizara ya Fedha, ili kuhakikisha kuwa kunakuwepo na utaratibu mzuri wa uendshaji wa mfuko huu.

Aidha, mwaka 2006, Wizara yangu ilifanya tathmini ya mfuko ambapo pamoja na mambo mengine ilipendekezwa kuwa mwongozo wa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake unahitaji kudurusiwa. Hivyo, kwa mwaka huu wa fedha Wizara yangu imejipanga kuanza kuudurusu ili uweze kukidhi mahitaji ya sasa na kuendeshwa kwa ufanisi zaidi kwa manufaa ya walengwa.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamnisha Mheshimiwa Mbunge kuwa kiasi cha mikopo inayotolewa kwa wanawake kupitiavikundi vyao hutofautiana kati ya Halmashauri moja na nyingine na kati ya kikundi kimoja na kingine kutokana na uhalisia wa raslimali zilizopo katika Halmashauri na aina ya mradi wa kikundi husika.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa kiasi cha mikopo inayotolewa kwa walengwa kinaongezeka ili kuendana na thamani ya shilingi, Wizara itaendelea kuhamasisha Halmashauri ziendelee kutenga fedha kwa ajili ya mfuko huu. Naomba Waheshimiwa Wabunge ambao sote ni Madiwani tuzihimize Halmashauri zetu kutenga 5% ya Mapato yake ya ndani ili kuimarisha mfuko huu na kuufanya kuwa endelevu.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, tathmini hiyo imefanyika miaka sita iliyopita na kama tathmini hiyo itatumika kuandaa mwongozo huo. Je, Serikali haioni kwamba tathmini hiyo imepitwa na wakati?

Pili, tunatambua kwamba Halmashauri nyingi nchini zina mapato kidogo kutokana na vyanzo vyake vya ndani hivyo kushindwa kutenga fedha katika mifuko hiyo.

Je, kwa nini sasa fedha hizo zisitokane na Serikali kuu?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, kama ifuatavyo:-

Suala la tathmini kufanyika mwaka 2006 ni kweli lakini tumechelewa kudurusu mwongozo kutokana na kwamba tathmini mojawapo ya mapendekezo ambayo walitoa ni kwamba fedha hizi sasa zipitishiwe *SACCOS* badala ya Halmashauri. Lakini tulipofanya *consultation* na wadau mbalimbali ikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na ya Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wizara ya Kilimo na Chakula bado wadau wengine wanapendekeza fedha hizo ziendelee kutolewa katika Halmashauri kwani ukizitoa kwenye Halmashauri riba itakuwa ndogo.

Kwa hiyo, hapo kidogo palitupa changamoto kwa sababu ya kuhakikisha tunapata mawazo mengine ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ya Mheshimiwa Jenista Mhagama. Kwa hiyo, nakuthibitishia kwamba haitakuwa *outdated* hiyo tathmini kwa sababu tutakuwa tume-*take into consideration issues* zote ambazo wadau wamezielekeza na ninakuthibitishia tu kwamba mwakani tutakapopitisha Bajeti yetu mwongozo utakuwa umekamilika.

Suala la pili la kuhusu mapato kidogo Serikali kuu itoe. Kwanza nikuthibitishie kwamba tayari kuna mifuko mbalimbali ambapo wanawake na wenyewe wanafaidika. Kwa mfano Benki ya Wanawake, kuna mfuko wa uwezeshwaji ambao uko chini ya Dkt. Mary Nagu.

Lakini hili naomba nilisisitize kwa kutumia Bunge hili kwamba Halmashauri zinatakiwa kuchangia asilimia tano ya mapato yao ya ndani kwa ajili ya mfuko wa maendeleo ya wanawake hata kama umepata shilingi mia mbili unachotakiwa kufanya ni ku-*make sure 5%* inatengwa kwa ajili ya mfuko wa maendeleo ya wanawake.

Kwa hiyo, tukisema Halmashauri hazina vyanzo vingi vya mapato, sidhani kama ni utetezi ambao utawasaidia.

Mheshimiwa Spika, uwezeshaji wa wanawake wa kweli ambao utabadilisha maisha yao ni uwezeshaji wa kiuchumi na elimu. Hayo masuala mengine tunapiga tu siasa ya kutaka *fifty- fifty,* lakini kama tuta *focus* katika elimu na katika kuwawezesha kiuchumi tutaweza kufanikiwa.

Kwa hiyo, naomba Bunge lako Tukufu kuhakikisha kwamba Halmashauri zote zinatenga 5% ya mapato yao ya ndani kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake.

**MHE. ZAHRA ALLLY HAMAD:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, licha ya uchache wa fedha ambazo hupelekea mfuko huu kutokuwa endelevu lakini Mheshimiwa Waziri haoni kama sababu kubwa ambayo inakosekana ni kukosa elimu ya ujasiria mali ambayo hupelekea mfuko wa wakopaji kushindwa kuendeleza biashara zao na kubakia fedha ile kutumika labda kwa kutolea mwali ndani au kufanyia harusi?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zahra Hamad Mbunge Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nikubaliane na Mheshimiwa Zahra kwamba mojawapo ya mapendekezo ya tathmini ambayo tuliifanya ni kwamba *issue* kubwa

kwa nini mfuko unalegalega ni kwamba wanawake wengi walikuwa pia hawapewi elimu ya ujasiriamali.

Kwa hiyo, hiyo kweli ni mojawapo ya *observation* ambayo imeonekana. Lakini sasa tunapokuja katika kudurusu huu mwongozo wa kuhakikisha mwongozo unafanya kazi kitu kikubwa ambacho kitapewa kipaumbele sasa hivi itakuwa ni lazima vikundi vile vipewe mafunzo ya ujasiriamali.

Hilo tunalisisitiza sana na nitumie Bunge lako Tukufu tena kuziomba Halmashauri hasa Mkurugenzi wa Halmashauri ambaye ndiye Mwenyekiti wa Mfuko huu wa Maendeleo ya Wanawake, Katibu wake ni Afisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya, kuhakikisha kwamba kabla hawajatoa fedha hizi kwa vikundi vya akina Mama wanawapa mafunzo ya ujasiriamali. Hivyo badala ya mwanamke kukimbilia kwenda kununua *gold.* Kwetu sisi Tanga ukimpa mtu fedha anafikiria kwenda kununua *gold* na Khanga mpya. Kwa hiyo, ni kweli kama hatutawaelekeza vizuri jinsi ya kutumia fedha hizi za maendeleo hatutafika tunakotaka kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na siku ya leo tuna shughuli nyingi sana. Kwa hiyo naomba nitambue kwanza wageni waliopo Bungeni nao ni wengi.

Kwanza kabisa naomba nimtambue Balozi wa Tanzania nchini China, Mheshimiwa Balozi Philip Sanka

Marmo, ambaye pia alikuwa Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. Lakini Mheshimiwa Rais alimpa heshima sana ya kumteua kuwa Balozi wetu nchini China. Tunakukaribisha sana nyumbani Mheshimiwa Balozi wetu nchini China. Tunakukaribisha sana Mheshimiwa Balozi kwani hapa ni nyumbani kwako. Aidha amekuwa hayumo humu ndani Bungeni kama miaka miwili tu iliyopita. Kwa hiyo, alikuwa hapa hapa Bungeni. Karibu sana Mheshimiwa Balozi. (*Makofi*)

Kuna wageni watano wa Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan, Mwenyekiti wa Kamati ya Utendaji ya *Jumuiya ya Madola (Commonwealth Parliamentary Association (CPA)* Tawi la Tanzania ambao wamekuja kuhudhuria Mkutano wa *CPA* wa Wabunge wote ambao wanatoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa sababu *CPA* na wenzetu wana *CPA Branch Zanzibar* na Tanzania Bara. Sasa *CPA Branch* ya Tanzania imeamua kuwakaribisha wenzetu katika mkutano huu tutakaoufanya leo mchana waweze kushiriki.

Kwa hiyo, wako hapa nao ni Mheshimiwa Mahmoud Mohamed Musa Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi, yupo Ndugu Yahya Kassim Hamadi, Katibu wa Baraza la Wawakilishi na wengine ni Mheshimiwa Ally Salim Haji, Mheshimiwa Mtumwa Kheri Baraka na Mheshimiwa Abdallah Mohamed Ally. Sasa haswa ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tumewakaribisha kwenye mkutano utakaofanyika leo. Karibuni sana. (*Makofi*)

Pia tuna wageni ambao ni wanafunzi 20 waliofanya vizuri katika Mtihani wa kidato cha Sita, hawa kuna shughuli yao tutakayofanya hapa. Kwa hiyo, tutakuwa nao baadaye.

Pia kuna wakuu wa shule kumi zilizofanya vizuri nao tutawaona baadaye, na kuna wazazi 20 na wanafunzi 20 waliofanya vizuri katika mitihani ya Kidato cha sita mwaka 2012. Wazazi hawa naomba wasimame walipo na wanafunzi wataingi ndani ya Bunge. Ahsanteni sana na Hongereni sana kwa kazi nzuri. Karibuni sana. (*Makofi*)

Pia naomba niwatambue Walimu wa shule 10 zilizofanya vizuri, maana yake hapaninguvu ya wazazi na Walimu ndiyo imezalisha matunda bora. Ahsanteni sana na tunashukuru sana. (*Makofi*)

Lakini pia tuna Mheshimiwa Mbunge Mstaafu Chrisant Mzindakaya, ambaye sasa hivi ni Mwenyekiti wa *NDC*, karibu sana. (*Makofi*)

Pia tuna wadau wa elimu kutoka Mashirika ya Kimataifa yaani *Development Partners* wakiongozwa na Ndugu Beatrice Omar, mshauri wa elimu kutoka *SIDA* na wadau wengine wote karibuni sana *or the other Development Partners.* Ahsanteni sana na karibuni sana. Hawa wanatoka *SIDA Canada.* (*Makofi*)

Lakini tuna wageni waliofika kwa ajili ya mafunzo, nao ni wanafunzi 63 na Walimu wao kutoka Shule ya Msingi *Martin Luther Dodoma,* karibuni sana na msome

vizuri, Waheshimiwa Wabunge wengi watoto wenu wako huko nadhani wengine watakuwa wamefika hapa. Karibuni sana watoto. (*Makofi*)

Lakini pia tuna wanafunzi 40 pamoja na Walimu wao kutoka Chuo Cha *VETA Dodoma* ambao ni majirani zetu, kama wamekosa nafasi basi wataingia Ukumbini baadaye.

Kuna wanafunzi 100 pamoja na Walimu wao kutoka Shule ya Sekondari Mlimwa, Dodoma. Someni vizuri kwani elimu ndiyo msingi wa maisha. Karibuni sana. (*Makofi*)

Pia kuna wanafunzi 35 kutoka Shule ya Sekondari ya Baobao iliyopo Mapinga na Mkuu wa Shule Ndugu Venance Pongoa. Naomba wasimame na karibuni sana. Waheshimiwa Wabunge hii ni moja ya shule nzuri zilizopo katika nchi yetu na tunawatakia mafanikio mema nyie wasichana na msome vizuri, tunawategemea na ukombozi upo shuleni na siyo kwingineko. *(Makofi)*

Pia tuna wanafunzi 28 wanaofanya mafunzo kwa vitendo hapa Bungeni katika idara ya Utawala. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mtakuwa mnakutana nao na ninadhani Mila na Desturi zetu hapa Bungeni mnazifahamu na karibuni sana. (*Makofi*)

Pia tuna watoto 20 wanaoratibiwa na Shirika la *Save the Children* ambao ni wageni wa kikundi cha Wabunge wa Lishe Salama na Chakula na Haki ya Watoto. Hawa watoto wamekuja kuwasilisha Azimio la

Haki za watoto, elimu na kuboresha masuala ya huduma za afya kwa watoto. Naomba wasimame. Karibuni sana na ahsanteni sana lakini sijui mnawasilisha wapi hilo Azimio lenu, mimi sijui. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Pia tuna wageni 12 wa Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga, kutoka Asasi ya *VICOBA Program of Dar es Salaam* wakiongozwa na Mratibu Mtendaji wao Ndugu Aldo Mfinde. Hawa ni wana Kamati wa Maadhimisho ya miaka kumi ya *VICOBA* Tanzania. Nadhani hawajapata nafasi na Mkurugenzi wa *VICOBA* Mama Likokola, naona watapata nafasi baadaye.

Lakini vilevile kuna wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, ambao ni Ndugu Cliff Disonoko na Joseph Mangara ambao ni viongozi wa harambee ya Hospitali ya Temeke na Vijibweni na ninaunganisha hivyo kwamba wanasema niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba Kamati ya Harambee ya ujenzi wa Hospitali ya Temeke na Vijibweni inawakumbusha kurejesha fomu za michango walizowapatia kwa ajili ya kuchangia ujenzi wa hospitali hizo. Michango hiyo inaweza kuwasilishwa kwa wafuatao:-

Bwana Cliff Sonoko Mwenyekiti, Mheshimiwa Abbas Mtemvu na Mheshimiwa Faustine Ndugulile.

Kwa hiyo, mliochukua fomu mnachukua huko na siyo mnarudisha bure bali mnarudisha na *something.* (*Makofi/Kicheko*)

Pia tuna mgeni wa Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI Bwana John Lema, ambaye ni mlezi wa Jumuiya ya Wazee wa CCM Mkoa wa Mwanza. Karibu sana. (*Makofi*)

Lakini pia tuna wageni watano wa Mheshimiwa Felisther A. Bura, ambao ni Viongozi wa Dini wakiongozwa na Dkt. Godwin Lekundayo, Askofu Mkuu wa Kanisa la Waadventista Wasabato Tanzania. Karibuni sana na tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Pia tuna wageni 50 wa Mheshimiwa Dkt. David M. Malole, Mbunge wa Dodoma Mjini ambao ni Wazee kutoka Kata ya Chang'ombe Dodoma, jana tuliwatamka lakini hawakupata nafasi. Tunawakaribisha na ahsanteni sana kwani ninyi ndiyo wenyeji wetu, tunawashukuru sana. (*Makofi*)

Vilevile kuna wageni 24 wa Mheshimiwa Betty E. Machangu, a mbao ni Serikali ya Wanafunzi wa Chuo cha Ualimu Mandaka, kilichopo Mkoani Kilimanjaro wakiongozwa na Wakufunzi wanne ambao ni Bi. Leyla Hoza. Nafikiri wamekosa nafasi lakini jana walikuwepo.

Pia tuna wageni wa Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, ambao ni Nabii Hibro ambaye ameambatana na Mkewe Nancy pamoja na Wachungaji wengine wawili kutoka Afrika. Ahsanteni sana na karibuni sana. (*Makofi*)

Lakini pia tuna wageni sita wa Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda, ambao ni Wajumbe wa Bodi ya Shule ya Baobao, *High School* wakiaongozwa na Mwenyekiti wa Bodi Dkt. Cleo Ngirwa, hao ndiyo Wajumbe wa Bodi. Tunawatakia mafanikio mema kwa kutulelea mabinti zetu. (*Makofi*)

Vilevile tuna wageni 11 wa Mheshimiwa Rahel Mashishanga Robert, ambao ni Kamati ya Utendaji ya Wilaya ya Shinyanga, wakiongozwa na Katibu wa CHADEMA Wilaya ya Shinyanga ambao ni Ndugu Daud Rwechungura, karibuni sana katika Ukumbi wetu huu wa Bunge. (*Makofi*)

Pia tuna wageni wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ambao ni Walimu Wakuu kumi (10) kutoka Mkoa wa Mwanza, karibuni sana. (*Makofi*)

Pia tuna wageni wa Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, hawa ni Wawakilishi wa Chama cha Wazee Wastaafu Mkoa wa Tanga Karingo wakiongozwa na Mama Halima Seif na Mzee Dismas Mhando. Ahsanteni sana sijawaona! (*Makofi*)

Vilevile tuna wageni wa Mwenyekiti wa Chama cha Wanawake Wabunge *TWPG* Mama Anne Abdallah ambao ni Anna Matinde na Sarah Mlela kutoka *Tanzania Women Chamber of Commerce, where are they?* Wako wapi?

Hawa wanaandaa mkutano mmoja mkubwa sana wa wanawake Tanzania pamojana Waheshimiwa

Wabunge mtahudhuria lakini tunajaribu kuona kwamba huo mkutano mkubwa kabisa utakaofanyika utakuwa karibu na vikao vya Bunge. Kwa hiyo, wako hapa kwa madhumuni hayo ya kuandaa mkutano huo na hivyo basi mkisikia taarifa ndiyo hizo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Andrew Chenge anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba asubuhi hii saa tano kutakuwa na kikao katika ukumbi Namba 231. Hawa wanamalizia ile *Finance Bill* ambayo inatakiwa kuja Bungeni na kujadiliwa katika muda wa siku moja ijayo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa James Lembeli anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.15 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati. Kikao hiki kitafanyika katika Ukumbi Namba 231 jengo la utawala ghorofa ya pili.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.15 mchana kutakuwa na kikao katika ukumbi wa Msekwa. Naamini kuna mkutano mkubwa sana wa *CPA* mle Ukumbini wakati huo huo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba saa 7.15 mchana kutakuwa na

Kikao cha Kamati yake katika Ukumbi wa Msekwa B. Haya matangazo yatapata matatizo karibuni! *(Makofi)*

**SPIKA:** Wabunge wote ni wajumbe wa *CPA* na Rais wa tawi hilo ni Mheshimiwa Spika na ndiye atakayefungua mkutano huo. Katika mkutano huo tunawaalika pia wenzetu kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar, hawa niliowatambulisha ambao wamekuja kushiriki. Tunaomba Waheshimiwa Wabunge wote wahudhurie ili kujifunza mambo muhimu kuhusu *CPA.* Nilikuwa na wasiwasi kwamba hii mikutano mingine ya saa 7.15 kwani tuna huu mkutano mmoja tu wa mwaka.

*CPA Tanzania Branch* sisi wote ni wanachama. Sasa mara nyingi habari zetu wenyewe hatuzifahamu. Unaweza kwenda mahali mtu akakwambia habari ya *CPA* wewe mwenyewe usijue. Kwa hiyo, tuna huo mkutano mkubwa kwa wote. Naomba sana mzingatie hilo saa 7.15 tutajitahidi tumalize kabla ya kuanza kikao cha Saa. 10.00.

Kwa maana hiyo pia leo hii mimi sasa Mheshimiwa Spika, nawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, leo baada ya kuahirisha Bunge Saa 12.15 kama Spika na pia kama Rais wa *CPA* tumejumuisha pamoja, tutakuwa na futari kwa Wabunge wote. (*Makofi*)

Aidha, katika futari hiyo Mheshimiwa Spika, pia amewaalika wafuatao kuungana naye: Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote lakini hao wote ni Wabunge, viongozi wa dini ngazi ya mkoa tumepeleka

kadi, viongozi wa Serikali ngazi ya mkoa pamoja na Wilaya ya Dodoma Mjini tumepeleka kadi, baadhi ya wawakilishi wa wazee wa Dodoma, hawa tuliowaona hapa. Maafisa wa Bunge wa Wizara mbalimbali walioko hapa Bungeni na Waandishi wa Habari za Bungeni waliopo hapa Bungeni.

Kwa hiyo, futari hiyo itatolewa leo tarehe 14 Saa 12.30 jioni. Naomba kusisitiza kwamba kuhudhuria kwenu ili tujumuike pamoja na wenzetu wa dini ya kiislam katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani, itakuwa ni fahari kwetu sisi wote. (*Makofi*)

Kwa hiyo, wote mnaalikwa saa kumi na mbili..

**WABUNGE:** Wapi?

**SPIKA:** Katika viwanja vya Bunge hapo. Eenh, katika viwanja vya Bunge hapa. Tunajaribu kupata eneo kubwa, ama tutakuwa pale nje au *basement*, lakini inaelekea kama *basement* itakuwa ndogo. Kwa hiyo ni hapa hapa Bungeni.

Nina matangazo mengine ambayo naomba myasikilize na mtaona kama inavyofaa. Kwanza kabisa huyu Mheshimiwa Sulemani Jafo nafikiri kwa niaba ya Mheshimiwa Alhaji Mohammed Missanga, anaomba niwatangazie Wabunge wote waislam waliofunga kufika katika kikao kifupi leo saa 7.00 mchana baada ya kipindi cha Bunge katika ukumbi wa Msekwa. Ukumbi huo ndiyo ambao wote tutakuwa huko kwenye kikao cha *CPA.* Sasa naona mtagongana pale.

Halafu tangazo lingine, huyu ni Sulemani Jafo ambaye ni Katibu wa *TAPAFE* (*Parliamentarians friends of environments*) anaomba niwatangazie Wajumbe waliopata barua ya kikao kwamba leo Saa. 7.00 mchana baada ya kipindi cha Bunge kutakuwa na mkutano Ukumbi wa Msekwa. Ukumbi wa Msekwa uko *occupied* sasa sijui, mtaenda ku- *synchronize* nyie wenyewe kwa kadri mtakavyoona inafaa.

Kwa hiyo, kikubwa naomba mkumbuke Saa 7.15 tuna mkutano wa *CPA* na Wabunge wote mnahusika, jioni Saa 12.30 tutakuwa na futari ya Wabunge wote na wageni niliowasema, wengine wamepewa kadi na wote mnakaribishwa.

Waheshimiwa Wabunge tuendelee na hatua inayofuata. Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge.

**KUTENGUA KANUNI**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maelezo ya hoja ya kutengua Kanuni chini ya kifungu cha 150(1) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007.

Kwa kuwa, moja ya shughuli zilizopangwa katika orodha yetu ya shughuli za leo ni kuwatambua, kuwaenzi na kuwapongeza wanafunzi waliofanya vizuri katika mitihani yao ya Kidato cha Sita mwaka 2012 na kwa kuwa, kwa mujibu wa Kanuni ya 140 (e) Spika ameweka utaratibu maalum wa wageni kutengewa

sehemu maalum ya kukaa, na kwa kuwa, Kanuni ya 139(2)(c) inatoa fursa kwa wageni waliotoa mchango unaohitaji kuenziwa kutambulishwa Bungeni, ili kuliwezesha Bunge kutekeleza shughuli hii kikamilifu inabidi Bunge litengue Kanuni ya 140 (e) kwa mujibu wa Kanuni ya 150(1). Hivyo basi Bunge linaazimia kwamba kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa shughuli hii katika Mkutano huuu wa Nane, Kanuni ya 140 (e) itenguliwe kama ifuatavyo:-

Kanuni ya 140(e) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba wageni walioko Bungeni wakae sehemu maalum waliyotengewa, itenguliwe na badala yake Wanafunzi hawa waruhusiwe kuingia ndani ya Ukumbi wa Bunge ili Bunge liwatambue, liwaenzi na kuwapongeza kwa kufanya vizuri katika mitihani yao ya kidato cha Sita mwaka 2012 kama ambavyo tumewahi kufanya katika siku za nyuma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja lliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge liliafiki kutengua Kanuni za Bunge Zilizotajwa)*

**SPIKA:** Vipi hamuwataki watoto wenu! (*Makofi/Kicheko*)

Jamani tuna ndugu Nathan Mpangala Kiongozi wa Kitaifa wa Chama cha Wachora Katuni na mchora

Vibonzo katika kituo cha ITV. Yuko wapi huyu? Aah, yuko pale. Vile vibonzo mnavyoviona ni yeye. (*Kicheko/Makofi*)

Halafu tuna afisa Mifugo kutoka Wilaya ya Mbulu, Ndugu Edwin Kileo. Ahsante sana. Huyu ni mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani. (*Makofi*)

Katibu wa caucus ya CCM, Mheshimiwa Jenista Mhagama anaomba niwatangazie kwamba Kamati ya Uongozi ya CCM watakutana saa 7.15 mchana. Kuna mgongano wa vikao leo, nadhani mta- *sort out* vizuri. Katibu!

## HOJA ZA SERIKALI

Hoja ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi

**SPIKA:** *No, no, no* kuna ile Hoja nyingine.

### Bunge Kutambua, Kuwaenzi na Kuwapongeza Wanafunzi waliofanya Vizuri katika Mitihani ya Kidato cha Sita Mwaka 2012

**SPIKA:** *Sergeant at Arms* awaingize watoto. Waziri wa Elimu utatoa maelezo wakati ukifika. (*Makofi*)

*(Hapa Wanafunzi waliofanya vizuri zaidi Mtihani wa Kidato cha Sita Mwaka 2012 waliingia Ukumbini)*

**SPIKA:** Ahsante mnakaribishwa. Waziri wa Elimu. Haiwezekani mkasimama *in a small circle? In a small circle* wa huku waende hivi na wa huku waende hivi, *just in a numbers. I mean a semi circle! Okay*, au wamewa – *block* watu wengine! *Okay*, Waziri wa Elimu.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge, Walimu, Wazazi, na Wanafunzi, Mabibi na Mabwana.

Mheshimiwa Spika, nina furaha kubwa kupata fursa hii ya kushiriki katika halfa hii ya kuwapongeza wanafunzi waliofanya vizuri zaidi katika mtihani wa Kidato wa Sita mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, katika mtihani wa kidato cha SIta uliofanyika *February* mwaka 2012 na matokeo yake kutangazwa na Baraza la Mitihani la Tanzania tarehe 1 mwezi Mei, mwaka 2012 jumla ya wanafunzi 44,190 waliofanya mtihani kama watahiniwa wa shule. Kati yao jumla ya wanafunzi 40,775 walifaulu mtihani sawa na asilimia 92.2 kati ya hao waliofaulu kwa kiwango cha daraja la kwanza hadi la tatu walikuwa 35,201 sawa na asilimia 79.66. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhanti kwa Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitahani Tanzania, pamoja na wafanyakazi wote wa Baraza hilo kwa kazi nzuri waliyoifanya ya uendeshaji wa mitihani ya taifa. Tumeweza kuwa na hafla hii ya kuwapongeza wanafunzi waliofanya vizuri zaidi kutokana na kazi

kubwa iliyofanywa na Baraza la Mitihani katika utunzi, usahihishaji na usimamizi wa mtihani.

Mheshimiwa Spika, katika hafla hii nimewaleta mbele yako vijana 20 wakiwemo wavulana 10 na wasichana 10 waliofanya vizuri zaidi katika mtihani wa kidato cha sita mwaka 2012. Vijana hawa wote 20 walipata ufaulu wa daraja la kwanza. *(Makofi)*

Wanafunzi hawa wametoka katika shule 10 zikiwemo shule za Serikali Nane, na za zisizo za Serikali mbili.

Naomba nizitaje shule hizo: Shule ya Sekondari ya Wasichana Marian, kwetu kule Bagamoyo wanafunzi saba (7), shule ya Sekondari Mzumbe wanafunzi watatu (3), shule ya Sekondari Feza wanafunzi wawili (2), shule ya Sekondari Kibaha wanafunzi wawili (2), shule ya Sekondari Kilakala mwanafunzi mmoja (1), shule ya Sekondari ya Ufundi Ifunda mwanafunzi mmoja (1), shule ya Sekondari ya Wasichana Tabora mwanafunzi mmoja (1), shule ya Sekondari ya Wavulana Tabora mwanafunzi mmoja (1), shule ya Sekondari Minaki mwanafunzi mmoja (1) na shule ya Sekondari Mpwapwa mwanafunzi mmoja (1). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunawapongeza vijana hawa ili kuwatia moyo na kutoa hamasa kwa vijana wengine waliopo shuleni. Katika hafla hii kila mwanafunzi atazawadiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu cheti, kompyuta pakato (*lap top computer*) moja, na fedha taslimu shilingi 200,000/=. *(Makofi)*

Aidha, kila shule iliyotoa mwanafunzi au wanafunzi bora itazawadiwa shilingi 1,000,000/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hafla hii mwenye jukumu la kuwapongeza vijana hawa na kuwakabidhi zawadi ni Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima ninawasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu orodha ya Wanafunzi ishirini pamoja na shule walizosoma na kufanya mtihani wa kidato cha sita kwa ajili ya kupongezwa na kukabidhiwa zawadi na Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ifuatavyo:-

Briton Lema shule ya Sekondari ya Wavulana Tabora. (*Makofi*)

**SPIKA:** Asogee mbele. Lema sogea mbele huku. Mmh! (*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Simama hapa, simama nyuma kidogo halafu atakayefuata atakuja mbele yako.

**SPIKA:** Mmh!

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Julius Ruvanga, shule ya Sekondari Kibaha, Alex Isidori shule ya Sekondari Kibaha, Farida Abdallah, shule ya Sekondari Mpwapwa, Benson Maruchu, shule ya Sekondari Mzumbe, Nickson Mwamsojo, shule ya Sekondari Mzumbe, Gwamaka Njobelo, shule ya

Sekondari Mzumbe, Belinadino Mgimba, shule ya Sekondari Minaki, Jamal Juma, shule ya Sekondari ya Wavulana Feza, natambua kwamba Jamal Juma yuko nje ya nchi, kwa hivyo hakuhudhuria hapa leo. (*Makofi*)

**SPIKA:** *Okay*!

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Zawadi Mdoe, shule ya Sekondari ya Wavulana Feza.

**SPIKA:** Nyie wanafunzi, anza mstari mwingine.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Prisca Longo, shule ya Sekondari ya Wasichana Tabora, Esther Marcel, shule ya Sekondari ya Ufundi Ifunda, Neema Kiula shule ya Sekondari ya Wasichana Kilakala, Neema Munuo, shule ya Sekondari ya Wasichana Marian, Evelyn Mapunda, shule ya Sekondari ya Wasichana Marian, Nashivai Kivuyo, shule ya Sekondari ya Wasichana Marian, Mary Kiangi, shule ya Sekondari ya Wasichana Marian, Rachel Sigwejo, shule ya Sekondari ya Wasichana Marian, Immaculate Mosha, shule ya Sekondari ya Wasichana Marian na Faith Asenga, shule ya Sekondari ya Wasichana Marian. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawasilisha pia orodha ya shule 10 zilizotoa wanafunzi bora kwa ajili ya kukabidhi zawadi za shule kwa wakuu wa shule hizo. Orodha hiyo ni kama ifuatavyo:-

1. Shule ya Sekondari ya Wasichani Marian;
2. Shule ya Sekondari ya Wasichana Kilakala;

3. Shule ya Sekondari ya Ufundi Ifunda;
4. Shule ya Sekondari ya Wasichana Tabora;
5. Shule ya Sekondari ya Wavulana Feza;
6. Shule ya Sekondari Mzumbe;
7. Shule ya Sekondari Mpwapwa;
8. Shule ya Sekondari Kibaha;
9. Shule ya Sekondari Minaki; na
10. Shule ya Sekondari ya Wavulana Tabora.

Mheshimiwa Spika, zawadi za shule hizi zitakabidhiwa kwa wakuu wa shule hizo na zoezi hilo litafanywa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, baada ya utambulisho huo ninaomba sasa kwa heshima kubwa na taadhima nimkaribishe Mheshimiwa Waziri Mkuu aweze kuongea na kuwakabidhi zawadi wanafunzi na wakuu wa shule husika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana! Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, wageni waalikwa, mabibi na mabwana!

Mheshimiwa Spika, tarehe 1 Julai, 2011 ulituruhusu kuwepo ndani ya Bunge lako Tukufu kuwapongeza vijana wetu waliofanya vizuri katika mtihani wa kidato cha Sita mwaka 2011. Leo kwa mara nyingine tena na kwa heshima kubwa umetupatia nafasi ya pekee kushiriki katika hafla kama ile ya mwaka jana ya

kuwatambua na kuwapongeza vijana wetu ambao wamefanya vizuri katika kuhitimu kidato cha sita mwaka huu 2012.

Naomba nikushukuru sana wewe Mheshimiwa Spika pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kukubali kutengua Kanuni za Bunge na kuruhusu vijana wetu pamoja na wageni waalikwa kuingia ndani ya ukumbi huu ili kuwapongeza.

Mheshimiwa Spika, ninakumbuka katika matokeo ya mwaka jana kiwango cha ufaulu wa mtihani wa Kidato cha Sita kilikuwa asilimia 92.03. Mwaka huu ufaulu umeongezeka na kufikia asilimia 92.2. Aidha, ni jambo la kutia moyo ambapo wanafunzi waliendelea kufanya vizuri katika masomo ya Sayandi yaani Kemia, Fizikia, Hisabati, Baiolojia na Kilimo.

Orodha tuliyonayo inaonesha vijana 16 ni wa mchepuo wa *PCM,* mmoja ni *PGM,* mmoja ni *CBA,* mmoja ni *ECA* na mmoja *HKL.* Hili ni jambo zuri na ni la kujivunia sana. (*Makofi*)

Lakini nimebaini pia kwamba, kati ya wanafunzi 20 walioko mbele yetu wanafunzi wawili waliingia kidato cha Tano wakitokea katika shule za Kata. Wanafunzi hao ni Esther T. Marcel, msichana kutoka shule ya Sekondari Olele Kilimanjaro na Briton H. Lema mvulana kutoka shule ya Sekondari Kitangiri, Mwanza.

Mheshimiwa Spika, napenda niwape pongezi za kipekee wanafunzi hawa kwa juhudi kubwa walizozionesha. Kufaulu kwao kunadhihirisha kwamba, shule hizi za Kata tukiweka bidii kwa kuziwezesha zaidi zitafanya vizuri zaidi kama ilivyo katika shule nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niwapongeze pia kwa namna ya kipekee Walimu wa shule hizi ambao kazi yao nzuri imejidhihirisha kwetu siku ya leo. Naelewa kuwa Serikali ina jukumu za kuziboresha shule hizo za Kata kwa matarajio kwamba, wanafunzi wengi zaidi wataweza kupata nafasi ya kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nitumie nafasi hii kuzipongeza shule ambazo zimefanya vizuri katika kutoa wanafunzi 20 walioko mbele yetu siku ya leo. Tumesikia hapa kwamba Shule ya Sekondari ya Wasichana Marian pekee ina wanafunzi saba kati ya wanafunzi 20 walioko hapa. Niruhusu niwapongeze kwa namna ya kipekee Walimu na uongozi wa shule hii ya Marian kwa kazi nzuri. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze wazazi na walezi na wanafunzi hao 20 kwa kuwawezesha kufikia malengo yao. Michango ya wazazi na walezi ni kichocheo muhimu katika mafanikio ya maisha ya watoto. Aidha, ni ishara ya kwamba wazazi wametimiza wajibu wao vizuri kuhusu watoto wao. Lakini pia niwapongeze Walimu ambao ndio hasa wamehakikisha wanawalea na kuwasimamia vizuri watoto hawa hadi kufikia hatua hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwahakikishia Walimu wote kwamba Serikali inatambua mchango wao na inathamini na kufurahia matunda ya kazi nzuri wanayoifanya. Naomba Walimu wote nchini kushirikiana na wazazi na Serikali kwa pamoja kufundisha watoto wetu kwa bidii ili waweze kufanya vizuri katika masomo yao kama tunavyoshuhudia katika hafla hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya vijana hawa yametokana na juhudi kubwa za wanafunzi wenyewe kujiwekea malengo na kufanya bidii katika kuyatimiza kwa nidhamu. Huu ni mfano mzuri kwa vijana wetu kutumia fursa waliyopewa na Serikali na wazazi wao pamoja na Walimu wao kutimiza malengo yao. Ni mfano mzuri unaofaa kuigwa na wanafunzi wengine kote nchini. Nidhamu ndiyo siri ya mafanikio hususan katika kujituma na kufuata vizuri maelekezo ya Walimu. Hii ni pamoja na kuepuka makundi mabaya yanayoweza kuwa kikwazo katika kupata mafanikio hayo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi tunao hapa vijana wetu, leo nitumie fursa hii kuwaeleza kwamba sasa wanatarajia kujiunga na Vyuo vya Elimu ya Juu. Huko vyuoni kuna masomo lakini pia kuna changamoto. Maisha ya Vyuo vya Elimu ya Juu ni tofauti na yale ya Shule za Sekondari, badala ya kuitwa wanafunzi wengine sasa watakuita mwanachuo.

Kule chuoni kuna uhuru zaidi wa maamuzi yako mwenyewe na utawala ni binafsi. Wewe kama mwanachuo hakuna wa kukusukuma tena ili uweze

kusoma, ni wewe mwenyewe mwanangu kujipangia muda wako wa kusoma, muda wa kulala au muda wa kwenda kwenye mambo mengine ambayo hayahusiani na malengo ya shule. Unao uhuru wa kujiamulia wewe mwenyewe.

Sisi kama Serikali na kama wazazi na walezi tutakachofanya ni kuwawezesha na kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu awasaidie muweze kufanya vizuri zaidi na kumaliza masomo yenu. Ninawaomba mtumie vizuri uhuru mtakaopata bila kurudi nyuma katika maendeleo ya masomo. Tunataka ufaulu wenu uwe mzuri zaidi kwa vile sasa ninyi mnakwenda kujenga weledi, mnakuwa wataalam wa fani fulani, tumieni muda wenu kujifunza zaidi, kutafuta maarifa zaidi na kuvumbua mambo makubwa zaidi yatakayowasadieni ninyi wenyewe na jamii kwa ujumla ili kujiletea maendelelo. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijamaliza, naomba nirejee niliyoyasema mwaka jana ndani ya ukumbi huu kwamba ni vizuri utaratibu huu wa kuwatambua wanafunzi bora uwe endelevu na ikiwezekana wanafunzi hawa wapewe fursa zaidi ya kuendelezwa katika Vyuo Vikuu vya kipekee nje ya nchi. Vyuo ambavyo vinafanya vizuri zaidi hasa katika fani ambazo tunadhani zitatujengea uwezo kama Taifa letu siku zijazo.

Mheshimiwa Spika, nimeambiwa hapa kwamba, ili kuwatia moyo vijana hawa na kutoa hamasa kwa vijana wengine waliopo shuleni wafanye vizuri zaidi pamoja na pongezi hizi kila mwanafunzi atazawadiwa

cheti na kompyuta pakato pamoja na shilingi laki mbili. Aidha, kila shule iliyotoa mwanafunzi bora itazawadiwa shilingi milioni moja. Mimi nasema kwa kuanzia tukubali kupokea zawadi hizo na nawashukuru wote waliochangia kufanikisha jambo hili.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe wito kwa wadau wa elimu kujitolea kwa hali na mali kuchangia masuala ya elimu ikiwa ni pamoja na kuwatunuku wanafunzi ambao wanafanya vizuri. Nimedhamiria kwamba katika siku zijazo tutajaribu vile vile kushirikisha sekta binafsi kuona ni namna gani wanaweza kuwa nao wanachangia katika kutoa tuzo kwa wanafunzi hawa na hasa kama zitakuwa zile zinazohusu ufadhili katika Vyuo Vikuu. Matumaini yangu ni kwamba wako wenye moyo mzuri ambao watakuwa tayari hasa kwa mafunzo au masomo yale ya sayansi.

Mheshimiwa Spika, pili, tunatarajia kuanzia mwaka kesho tutakapokuwa tunapata fursa kama hii, tutoe taarifa vile vile juu ya wanafunzi waliokwishatangulia ili muweze kujua wanaendeleaje huko waliko pamoja na wale ambao watakuwa wamepewa vyeti leo. Tumeamua kufanya hafla hii kwa lengo la kuwapa moyo vijana wetu walioko mbele yetu. Watanzania wote wanawaona, wanasikia na naamini wanawapongeza kwa sababu ni haki yenu kupongezwa. Mmefanya vizuri mnastahili, hongereni sana wanangu kwa kufanya vizuri. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa niko tayari kuwakabidhi zawadi. Nirejee tena

kukushukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kutupa fursa hii kwa mara nyingine tena ahsanteni sana. (*Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Utaratibu unakuwaje Waziri. Ndio Mheshimiwa Waziri eleza.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Nitasoma majina.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niwaite majina wanafunzi hawa ili mmoja mmoja aweze kupokea zawadi zao za cheti pamoja na zawadi. *Laptop* hatukuchukua.

*(Hapa wanafunzi walikabidhiwa vyeti na zawadi zao)*

**SPIKA:** *Laptop* zinatoka wapi?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**: Mheshimiwa Spika, samahani kwa sababu zile zawadi zingine *bulk* na tuna hafla leo jioni, huko ndiko ambapo watakabidhiwa zawadi zile za *Laptop* pamoja na fedha taslimu na Wakuu wa Shule watakabidhiwa fedha taslimu katika hafla ya jioni leo ambayo ni chakula rasmi ambacho Waziri Mkuu atakula na vijana hawa. Kwa hivyo, hapa tutawapatia vyeti tu.

**SPIKA:** Ahsante.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naomba niwataje majina kama ifuatavyo:-

Briton Lema, Shule ya Sekondari ya Wavulana Tabora. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hata makofi peke yake ni motisha.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Julius Luvanga, Shule ya Sekondari Kibaha; Alex Isidori, Shule ya Sekondari Kibaha; Faridi Abdallah, Shule ya Sekondari Mpwapwa; Benson Maruchu, Shule ya Sekondari Mzumbe; Nickson Mwamsojo, Shule ya Sekondari Mzumbe; Gwamaka Njobelo, Shule ya Sekondari Mzumbe na Belinadino Mgimba, Shule ya Sekondari Minaki.

Mheshimiwa Spika, Jamal Juma amesafiri kwa hivyo cheti chake tutakihifadhi. Anayefuatia ni Zawadi Mdoe, Shule ya Sekondari ya Wavulana Feza; Twisca Longo, Shule ya Sekondari ya Wasichana Tabora; Esther Marcel, Shule ya Sekondari ya Ufundi Ifunda; Neema Kiula, Shule ya Sekondari ya Wasichana Kilakala; Neema Munuo, Shule ya Sekondari ya Wasichana Marian; Evelyn Mapunda, Shule ya Sekondari ya Wasichana Marian; Nashivai Kivuyo, Shule ya Sekondari ya Wasichana Marian; Mary Kiangi, Shule ya Sekondari ya Wasichana Marian; Rachel Sigwejo, Shule ya Sekondari ya Wasichana Marian; Imaculata Mosha, Shule ya Sekondari ya Wasichana Marian na mwisho Faith Assenga, Shule ya Sekondari ya Wasichana, Marian. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**SPIKA:** Ahsante kwa niaba yenu Waheshimiwa Wabunge, tunaomba tuchukue nafasi hii pia kuwapongeza watoto wetu kwa kazi nzuri waliyoifanya. Kama alivyosema Waziri Mkuu huo ndio mwanzo wa safari. Safari iliyoko mbele ina mawimbi makubwa kweli kweli. Wengine wanakwenda nayo wengine wanaweza kuyamudu.

Lakini naamini kwa busara na vipaji mlivyopewa na Mwenyezi Mungu mtayamudu maisha ya huko mbele. Kikubwa ni kuangalia makundi yasiyokuhusu kwa yatakupeleka kwingine. Wewe sikiliza, tumia akili yako, fanya maamuzi, sio unasikiliza tu na kwenda nayo aah! Sivyo wanavyofanya katika maisha. Sikiliza, pima, amua cha kwako kwa sababu mwisho wa siku *you are going to be alone. Nobody else will be there except you and yourself. (Makofi)*

Kwa hiyo, hilo ndio kubwa sana, tunawapongeza sana na ahsante Walimu na shule zilizofanya kazi nzuri hii na ahsante wazazi kwa malezi bora na watoto wangu wengine wale wa *Baobab* pale siku nyingine nataka kuwaona hapa. Nanyi watoto wetu wa Baobab nataka tuwaone hapa na mko jirani sana na Marian, sio? Mko jirani, kwa hiyo tunawatakia mafanikio mema. Sasa namwomba *Serjeant-at-arms* awachukue muweze kutoka nje. (*Makofi)*

*(Hapa wanafunzi waliondoka Ukumbini)*

**SPIKA:** Mnageuka kwa msitari kama mlivyokuja.

## MWONGOZO WA SPIKA

**SPIKA:** Kanuni inasema tunamaliza kazi moja kwanza tunaingia ya pili, hatuwezi kuingiliana. Mheshimiwa Dkt. Kikwembe.

**MHE. DKT. PUDENSIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante nasimama kwa kanuni ya 68 fasili ya saba (7) kuomba Mwongozo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tukio hili lililotokea hapa ni kubwa sana na naliunga mkono kwa maana kwamba tumewapongeza vijana wetu pamoja na shule walizotoka na walimu wao

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako kwamba je, Serikali haioni kwamba ni muhimu pia hata wakapongezwa Walimu wale mmoja mmoja waliofundisha masomo hayo mpaka kufanikisha wanafunzi walipofikia? Naomba Mwongozo wako?

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako Kanuni ya 68(7). Mwaka jana niliomba Mwongozo wako na naomba na leo nirudie tena. Baada ya tukio kubwa hili lililotokea la kuwapongeza vijana wetu mwaka jana nilisema kwamba, ingefika wakati sasa Serikali ifikirie kama sehemu ya kuwapa zawadi. Ni kweli zawadi ya kompyuta ni nzuri, zawadi ya pesa na cheti.

Mheshimiwa Spika, hivi si umefika wakati sasa kama nchi angalau hawa watoto 20 Serikali ingewapa *scholarship* kwenda kwenye vyuo bora duniani ili

angalau tupate watoto ambao na sisi wanasoma *Harvard,* Yel, na *Oxford Universities,* iwe sehemu kama ya kuwafanya watoto wetu huko shuleni wasome kwa bidii, kwa kujua kwamba, tukifanya vizuri tunakwenda kwenye Vyuo Vikuu bora duniani? (*Makofi)*

Narudia kama nilivyosema mwaka jana, naomba na leo Serikali waendelee kulitafakari kama sehemu ya zawadi.

**SPIKA:** Nimemwita Dkt. Kigwangalla umeshamaliza au hukusimama kama hukusimama sio lazima useme.

**MHE. DKT. HAMIS A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, nilisimama lakini nimeahirisha.

**MHE. DAVID E. SILLINDE:** Mheshimiwa Spika, nataka tu kutoa rai kwa maana ya pongezi kwa niaba ya Kambi ya Upinzani Bungeni kwa wanafunzi wote ambao wamefanya vizuri katika mitihani yao. Kwa hiyo, sio tu Serikali peke yake inawapongeza hata Kambi ya Upinzani Bungeni tunawapongeza sana na kwa namna hiyo ni kwamba tunawafikishia salamu zetu ila tu tutaendelea kutoa rai kwa Serikali iwekeze na kuboresha zaidi katika Shule za Sekondari za Kata ili mwaka unaokuja tuone angalau wanafunzi wanaongezeka zaidi. Maana yake asilimia 90 ya wanafunzi waliofaulu hapa kwetu ni wanafunzi wa vipaji maalum. Kwa hiyo, tungependa mwaka kesho wanafunzi wa Shule za Sekondari za Kata idadi iongezeke.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**SPIKA:** Nina muda mfupi. Mheshimiwa Mng'ong'o wa mwisho, nawaomba.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa Mwongozo huo wa kipengele namba 67. Nataka kufahamu na napenda nitoe ushauri wale wanafunzi ambao wamekuwa wa vipaji na mara nyingi wamekuja hapa Bungeni kupongezwa. Je, Serikali inajua wote wameajiriwa wapi kwa sababu ilitakiwa hawa watoto ambao wana vipaji basi wawe wakimaliza mafunzo yao wafuatiliwe na wapate ajira Serikalini ili kuendelea kupata wataalam. Sina uhakika kama watoto wote ambao tumekwishawapongeza hapa Serikali inajua baada ya mafunzo yao wameajiriwa wapi au wamepata ajira za uhakika.

**SPIKA:** Waheshimiwa hakuna Mwongozo wowote, nyie leo mmeona Wizara ya Elimu mmeamua kujadili. Kwa hiyo, nikiona majina yenu hapa hampati nafasi mmeshajadili. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa Waheshimiwa Wabunge kwa utaratibu wa Mwongozo, hakuna Mwongozo hata mmoja. Haya yalikuwa mawaidha yenu tu basi. Kwa hiyo tunaendelea Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

## Makadirio na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013 - Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kama mnavyojua leo ndio siku yetu ya mwisho, tutaanza na wale ambao hawajazungumza hata mara moja; yuko Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Sylvester Mabumba na Mheshimiwa Christowaja Mtinda ajiandae na Mheshimiwa Rachel Masishanga Robert pia ajiandae.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipatia nafasi hii nami kuwa mmoja katika wachangiaji katika hoja ya Wizara iliyo mbele yetu. Nasema ni bahati nzuri kupata nafasi kwa sababu kama Wizara mbili zilizopita ikiwa hii ya tatu nimeomba, sikupata nafasi.

Mheshimiwa Spika, kwanza nikupongeze wewe kwa kunipa nafasi hii, lakini vilev ile niwatakie kheri za mwisho wa mfungo wa Ramadhani Waislamu wote pamoja na Watanzania wote tuliomo ndani na waliomo nje.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema kwamba, hii ni mara ya kwanza sijapata kuona Bunge hili lilivyokuwa na mshikamano katika miezi yote ya Ramadhani tunapokuwepo hapa kama walivyokuwa wameshikamana safari hii. Tumeshikamana kweli

kama Watanzania, lakini tumeshikamana kweli kama jamii ambayo tuko katika kijiji kimoja cha Bunge la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, huo ni ushahidi tosha kwamba hata wewe leo unafuturisha katika futari ya jioni. Tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna wale walioniuliza hapa tulipokuwepo jamani hii ni wapi nawaambia kwamba sisi tuko katika kumi la mwisho tunasema ni kumi la *maghfira.* Tumepita makumi yote; la kwanza, la pili na hili la mwisho la *maghfira*. Kwa hivyo, *Inshallah* tuombeane dua na sisi tuwe tumepita katika *maghufira* haya.

Mheshimiwa Spika, pili, nataka kuwapa pole wale ndugu zetu waliokuwa wamepata maafa katika meli yaliyotokea hivi karibuni, lakini vile vile katika ajali Mheshimiwa Idd Azzan pamoja na Dkt. Abdullah tunawapa pole na *Inshallah* Mwenyezi Mungu awavue hili na lingine.

Mheshimiwa Spika, lingine napenda kumpa hongera sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu, kielelezo kilichofika hapa ni kuhakikisha kuwa kwamba Wizara ya Elimu inajitahidi na inafanya kweli. Tofauti na wale wengine waliokuwa wamesimama jana wakasema kuwa Tanzania mika 50 iliyopita inafanya nini.

Mheshimiwa Spika, hiki ni kielelezo na hata wao hawajijui kuwa miaka 50 iliyopita, Dada yangu Lyimo nisamehe kidogo, nakupenda sana lakini na wao wamesomeshwa na CCM hiyo hiyo ya miaka 50

ambayo wao ndiyo wao wako hapa na zaidi ya 75% ya walioko hapa wamekuwepo katika miaka hiyo 50 ambayo CCM imekuwa ikitawala, kwa hiyo nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ya kuzingatia pamoja na sifa tulizotoa kwa Wizara ya Elimu kwa mnasaba huu tulionao sasa hivi naungana na wale waliosema kuwa suala hili la mgogoro wa Walimu Wizara isiache kama lilivyo.

Mheshimiwa Spika, ni lazima tukae chini Walimu ni watoto wetu na Walimu ni moja ya watu katika jamii yetu na nchi ambayo haina Walimu bora na hapa imethibitika kwamba hatuwezi kuwa na *product* nzuri kwa viongozi waliofuata na jamii tuliyonayo. Kwa hiyo, mgogoro uliopo sasa hivi tunaomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu pamoja na Wizara ya Elimu na Serikali kwa ujumla, ni vizuri wakakaa chini kuweza kutafakari na tuweze kuyaamua yale ambayo yanawezekana kuamulika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Walimu ni watu muhimu katika nchi yetu na ni muhimu wao wamepewa kazi huwezi kusema kati ya wao na sisi kuwa hukupita katika migongo ya Walimu, walikuwa wanafunzi jana na leo ndiyo Walimu na walisomeshwa na Walimu ambao hapa hawapo na wao wanasomesha wanafunzi ambao kesho na keshokutwa watakuwa viongozi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Walimu nao wachukue nafasi yao ya ualimu ni wito na huwezi

kumlipa Mwalimu kiasi kile ambacho anastahili kulipwa.Wanafanya kazi ambayo ni muhimu, nao waelewe kuwa Serikali wanayoifanyia kazi nayo ni Serikali maskini.

Mheshimiwa Spika, kuna Wabunge waliotangulia wamenukuu hapa kuwa kuna wasomi wazuri akina Shakespeare na Mandela, lakini naomba kununukuu moja katika *verse* za *Quran* ambayo Mwenyezi Mungu anasema *Iqra bisimi-rabika ladhi kharaka.*

Mheshimiwa Spika, lakini kama hilo halitoshi Bwana Mtume (*Swala-llah Alayh Wasalaam - S.A.W)* anasema: "*Kuna alim au mutaalim* au *mustamia wala takun rabia fataulika".* Anasema kuwa Mwalimu ambayo umeelimika ambao ni Walimu ambao wanasomesha watotoa wetu siku hizi. *Amutahlima* au mwenye kujifunza kwa maana kwamba sote tunajifunza au mstahama au unasikia kama hivi sasa tulivyo tunavyosikia *walaatatun rabia fataulika* usiwe katika kundi la nne utaangamia.

Mheshimiwa Spika, sasa tunawaomba Walimu wasitupeleke huko kwenye kuangamia watusaidie kusomesha watoto wetu na tunaomba Wizara nayo kwa upande wao wakae na Walimu tuone kuwa tatizo lilipo linatatuliwa. Katika suala hili tunaomba Wizara ya elimu vile vile kama inawezekana katika mitaala ya elimu sasa hivi liwekwe somo la maadili, maadili kwa maana ya uzalendo kwani uzalendo umepotea. Tuliposoma sisi Walimu waliotufundisha ni tofauti na sasa kwani sasa uzalendo hakuna.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile tunaomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu kufikiria suala la lugha ya Kiswahili kutiliwa mkazo. Kama tulivyopata taarifa katika Wizara mbalimbali zilizopita ni kwamba, Walimu wengi wa lugha ya Kiswahili wanahitajika. Kwa hiyo, soko la lugha ya Kiswahili lipo. Tunaomba hilo pia liweze kufikiriwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. SILYVESTER M. MABUMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima, lakini pia niipongeze Serikali kupitia Wizara ya Elimu kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kufundisha vijana wetu na tumeona hivi punde kazi njema inayofanywa na Walimu wetu. Walimu wetu wanafanya kazi nzuri ya kufundisha vijana wetu na wale wanaozingatia mafunzo matokeo yake tumeona kuwa wanafanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kuhusu ubora wa elimu katika shule zetu za sekondari na shule za msingi na baadaye nitazungumzia elimu ya juu ya vyuo vikuu. Katika shule za msingi na sekondari ubora wa elimu umeshuka sana kutokana na kutokuwepo kwa vifaa vya kufundishia, vifaa vya maabara lakini pia motisha ya Walimu kwa maana ya mishahara yao na mazingira mazuri ya kufundishia. Kwa walimu wetu mazingira ni magumu sana.

Mheshimiwa Spika, tunapotaka kuona vijana wanaofanya vizuri ni lazima tuhakikishe kuwa shule zetu zinakuwa na vifaa muhimu, vitabu na vifaa vya maabara, kundi la watoto 20 kwa sekondari tulizonazo nchini ni kuwa bado tuna safari ndefu ya kuonysha kuwa watoto wetu wanafundishwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba kupitia Bunge lako Tukufu Serikali ione umuhimu wa kuboresha miundombinu katika shule zetu za sekondari na za msingi ambazo zinatoa vijana hawa kwenda sekondari na baadaye kuingia Vyuo Vikuu bila kuwa na maabara. Vijana wetu hawawezi kujifunza kwa vitendo watabaki na *theory* ambazo wakati wa mitihani wanapo *practice* hawawezi kufanya vizuri kwa sababu ni vitu vipya kwao. Naomba Serikali itoe vifaa hivi na pia sekta binafsi iunge mkono juhudi za Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba mchango wangu uelekee katika Vyuo Vikuu, naomba ku- *declare interest* kuwa mimi ni Mjumbe wa Baraza la Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Serikali imepunguza *OC* katika Vyuo Vikuu vya umma hapa nchini. Suala hili limeathiri sana utendaji katika utendaji katika vyuo vikuu vyetu vya umma.

Mheshimiwa Spika, Vyuo Vikuu vya Umma vilikuwa vikipewa bilioni moja kwa mwaka kama *OC* imeshushwa mpaka milioni 100, vyuo hivi vimeshindwa kupata vitabu, kulipia gharama za umeme, maji na vyuo vingine kama *Open University* ambayo ina

majengo ya kukodi inakuwa tabu sana kugharamia gharama za pango kwa sababu *OC* imepunguzwa.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri wa Elimu atakapokuja kufanya majumuisho atuambie ni vigezo gani wamevitumia kupunguza *OC* kutoka bilioni moja hadi milioni 100 kitu ambacho kimeathiri sana vyuo hivi vya umma.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuwa vyuo vikuu vinadai Serikali *arrears* ya bilioni 57, haya ni malimbikizo ambayo Serikali ilishindwa kulipa kwa wakati watumishi wa Vyuo Vikuu na wafanyakazi mbalimbali katika Vyuo Vikuu. Hii imevunja morali ya Wahadhiri wetu kwa kuwa wanaidai Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu atuambie ni kwa nini mpaka sasa hivi ama ni yeye au Wizara ya Fedha haijatoa fedha hizi ambazo ni muhimu sana kwa kuwatia moyo Walimu wetu wa Vyuo Vikuu tunaposema tunahitaji wataalam, tutawapata vipi kama Wahadhiri bado wao wanafanya kazi katika mazingira magumu na Serikali inashindwa kuwalipa mahitaji yao. Naomba Waziri wa Elimu atuambie kwamba ni lini deni hili la bilioni 57 Serikali italipa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine uajiri katika Vyuo Vikuu hufanywa na Mabaraza ya Vyuo Vikuu husika katika siku za karibuni, Serikali kupitia Tume ya Utumishi ya Ajira imekuwa ikifanya kazi ambayo imekuwa ikifanywa na vyuo vikuu ku-*recruit* wafanyakazi, Wahadhiri na wataalam mbalimbali katika vyuo vikuu

vya umma. Hii imekwaza sana utaratibu kwa sababu siyo wote wana taaluma sahihi ya kuweza kuwa-*interview* hawa ambao wanafanya kazi vyuo vikuu, Wahadhiri na wataalam mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kibaya zaidi *interview* hizi za ku-*recruit* watumishi katika vyuo vikuu imekuwa ikifanywa na Tume ya Utumishi ya Ajira lakini baadaye hupeleka *bill* katika chuo husika, *bill* ambazo ni kubwa na kama hapa tulivyosema kuwa *OC* imepunguzwa kutoka bilioni moja kwa milioni 100. Vyuo hivi vitatoa wapi fedha kulipia hizi bills ambazo zinadaiwa na Tume ya Ajira kuwa ime- *conduct interview* ya ku- r*ecruit* wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, naomba utaratibu huu kwa sababu uko kinyume na Sheria ya Ajira ya Vyuo vikuu Serikali izingatie na iangalie kwa makini utaratibu huu siyo mzuri kuendelea nao. Vyuo vikuu viachiwe uhuru wa ku-*recruit* wafanyakazi ambao Vyuo Vikuu vitakuwa vinawahitaji.

Mheshimiwa Spika, lingine ni fedha za maendeleo ambayo Serikali ilikuwa ikivipelekea vyuo vikuu hivi vya umma, fedha hii imekuwa haitolewi kwa wakati. Kwa maana nyingine ni kuwa Vyuo Vikuu mikakati na mipango yao ya kupanua huduma imeathirika sana. Tunaposema Vyuo Vikuu vyetu viwe na vifaa muhimu ambavyo wanafunzi au wanachuo kwa jina watavihitaji vitapatikana vipi wakati fedha ya maendeleo haipelekwi na Serikali.

Mheshimiwa Spika, jana mchangiaji mmoja alizungumza kuwa pengine ni Wizara ya Fedha ambayo inashindwa kupeleka hizi fedha ambazo zinapitishwa na Bunge lako Tukufu. Naomba sana Serikali yetu iangalie haya, hatutarajii kuona baadaye hata Wahadhiri nao wakaingia kwenye migomo kama wanafunzi wanavyogoma kutokana na kutokupelekewa fedha zao za mikopo ya elimu ya juu, tutakuwa tumelipeleka Taifa kubaya.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Waziri wa Fedha wayaangalie haya, ni muhimu sana kuhakikisha kuwa kile ambacho Bunge lako Tukufu linapitisha, Wizara ya Fedha na Wizara ya Elimu visimamie kuhakikisha kuwa hivi vinatekelezwa, vinginevyo tutakuja kujikuta tunaanzisha matatizo ambayo hayastahiki.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nisisitize tu kuwa Waziri wa Elimu ni mzalendo sana na namwelewa Mheshimiwa Kawambwa na Msaidizi wake Naibu Waziri, Mheshimiwa Philipo Mulugo wahakikishe haya ambayo tumeyasema wanayafuatilia na Wizara ya Elimu. Nawaunga mkono kwa sababu nia yao njema, lakini bila kupewa pesa na Wizara ya Fedha wataishia kuwa na mipango ambayo utekelezaji wake ni mgumu sana.

Mheshimiwa Spika, Serikali nzima ipo hapa, naamini wamenisikia, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu. Kabla sijaanza mchango wangu kama Mwalimu, naomba niungane na wenzangu kuwapongeza vijana waliopata ushindi mkubwa katika kidato chao cha sita.

Mheshimiwa Spika, kwa upendeleo maalum naomba nimpongeze binti aliyetoka shule ya Sekondari Kilakala kwa kuwa nami nimesoma huko *form five* na *six.* Pia nisimsahau mama yangu mpendwa Mheshimiwa Magreth Mkanga, ni mwalimu wangu wa *form five* na *form six* Kilakala. Kwa hiyo, yote ninayoongea hapa ni matunda yake nampongeza sana Mheshimiwa Mkanga.

**SPIKA:** Mbona Anna Tibaijuka amesoma huko na mimi nimesoma huko, sasa vipi?

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi, naomba sasa nijikite katika mchango wangu tarehe 19 Aprili, 2012, wakati nachangia ripoti ya *CAG* kuhusu kulipa mishahara hewa kwa watumishi kadhaa hususani wa elimu ya juu nili- *findout* kwamba hata mimi mwenyewe niliingizwa kwenye *pay roll* ya Chuo Kikuu Huria kwenye *Annual reports* za Chuo Kikuu Huria kwa miaka mitatu mfululizo.

Mheshimiwa Spika, sasa sijui kama nilikuwa kwenye *pay roll* ama vipi, lakini nilikuwa kwenye *annual report* kuanzia mwaka 2007/2008/2009/ 2010. Nilihoji ni kwa nini nimeingizwa kwenye *Annual Reports* za Chuo Kikuu

Huria wakati mimi sikuwahi kuomba kazi wala sikuwahi kuandika barua yoyote.

Mheshimiwa Spika, kwa mshangao mkubwa nikitegemea kuwa Wizara na Chuo Kikuu Huria kitajibu vizuri, nililetewa majibu na nadhani Wizara inayo, nikiambiwa kuwa, mimi mwaka 2006 niliomba kazi kupitia anwani ya Chuo Kikuu cha Mkwawa, nilikuwa *Lecture* pale, sikuomba kazi kama *part time lecture* wa Chuo Kikuu Huria.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi na nimeambiwa kuwa Chuo kinaamini na naomba ninukuu kwa heshima yako: "Ni vizuri yeye mwenyewe Mheshimiwa Christowaja Mtinda apatapo nafasi Bungeni awaeleze Waheshimiwa Wabunge uhalisia wa jambo hili ili kusaidia kuboresha yaliyoandikwa katika *Hansard* tarehe 19 Aprili, 2012".

Mheshimiwa Spika, ukweli uliopo ni kwamba, sikuwahi na narudia tena kuwa, sikuwahi kuomba kazi Chuo Kikuu Huria kwa namna yoyote ile na wao wamekiri kuwa barua ya kuniajiri pale haipo. Sasa Chuo Kikuu Huria kuwa na *poor record keeping* hii inatoka wapi.

Mheshimiwa Spika, huu ni uwongo na uwongo huu unajidhihirisha katika maelezo yao waliyojibu Wizarani kuwa wame-*quote* kuwa 2006 niliomba kazi. Lakini kikao namba 45 cha Wakuu wa Vitivo na namba 46 kilichokaa tarehe 2/11/2005 na kikao kingine cha tarehe 8/11/2005, kilipitisha jina langu na wakati

wanasema 2006, mimi nimeomba kazi, sasa ni mwaka upi unatangulia 2005 au 2006?

Mheshimiwa Spika, watendaji wetu wamekuwa ni wadanganyifu wakubwa, wanapeleka ripoti za uongo kwa wakubwa halafu matokeo yake viongozi wa Wizara wanafanya vitu ambavyo siyo sawasawa. Sasa mimi leo hii ni Mbunge nimepata nafasi ya kuongea hapa kwamba, Chuo Kikuu Huria chini ya Dkt. Francis Charles ambaye alikuwa ni Mkurugenzi wa Kituo cha *Open University* Iringa ndiye aliyepeleka jina hili.

Waheshimiwa Waziri na Naibu Waziri nawaombeni sana huyu Francis Charles ni Mtanzania yuko hapa nchini, mtafuteni awapeni *details* za uhakika, ni kwa nini ameingiza jina langu wakati siyo sawasawa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, kama nilivyosema nilikuwa Mhadhiri Chuo Kikuu Mkwawa, naomba nizungumzie kidogo kuhusu hicho chuo, Mwaka huu Serikali ilfanya mabadiliko makubwa ya kuitoa *top management* ya Mkwawa kufuatia *scandle* ambayo ilijitokeza ya matumizi mabaya ya fedha za mikopo na fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, kuna kitengo ambacho kimesahaulika cha Manunuzi. Kwa habari ambazo ninazo kimeonekana kina udhaifu mkubwa sana. Naomba kwa heshima yako na ruhusa yako nimtaje Mkuu wa Kitengo anaitwa Mrs. Jane Swalo Mpuya huyu ni *Head of Department*.

**SPIKA:** Sisi tungependa sana uzungumzie *theory* kuliko kutaja majina, maana majina yanaweza kukupeleka pabaya, wewe zungumza tu hoja yako bila kutaja majina.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Huyu Mkuu wa Idara, kuna jengo linajengwa pale la *lecture theaters consultant* alikadiria kwamba lijengwe kwa shilingi bilioni 5.6, lakini yule aliyetenda, alitenda kwa bilioni 2.6 *variation* inayoonekana ni shilingi bilioni 1.2, maana yake jengo lile halitamalizika.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Mkwawa kwa ambao wamekwenda hilo ndiyo Jengo la kwanza kujengwa tangu Chuo kile kibadilishwe kuwa Chuo Kikuu. Wanafunzi wanataabika, wanasoma kwenye *cafeteria*, Wahadhiri wanarudia *topic* moja kuwafundisha wanafunzi kwa sababu wanafunzi wanatakiwa wagawanywe katika vikundi.

Mheshimiwa Spika, kama Benki ya Dunia imetoa fedha kujenga *Lecture theaters* na kama haitamalizika kama ilivyokadiriwa maana ilikuwa imalizike tarehe 30 Septemba, mwaka jana, mpaka sasa hivi haijamalizika. Maana yake ni kuwapa usumbufu mkubwa wanafunzi na kuwapa usumbufu mkubwa sana Wahadhiri kwa kufanya kazi kupita kiwango. Naomba jambo hilo liangaliwe ili *lecture theater* imalizike.

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye suala lingine kuhusu mihula ya shule. Kumekuwa na mabadiliko ya mihula ya shule hasa muhula wa kidato

cha tano na kidato cha sita. Sasa hivi wanafunzi wa kidato cha sita wanamaliza muhula mwezi wa Pili, kuna matatizo makubwa sana ya mgawanyiko wa Walimu kwenda kusahihisha mitihani.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wa kidato cha sita wanapomaliza mtihani mwezi wa pili wanafunzi wengine wanakuwa bado wapo shule wakiendelea na masomo, *O-Level* na wengine *A-Level,* kidato cha tano. Walimu ni wale wale wachache, wanachukuliwa kwenda kusahihisha mitihani labda mwezi mzima, huku wanafunzi wanabaki bila Walimu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara iangalie utaratibu wa kurudisha ule muhula wa mwanzo ambapo wanafunzi walikuwa wanaanza kidato cha tano mwezi wa saba ili mihula iende sambamba. Walimu wanaposahihisha mitihani hapo wanafunzi wanakuwa wamefunga shule, ili tuwatendee haki wale wanafunzi ambao wamebaki darasani. Ikumbukwe wazi kwamba wasahihishaji wakubwa wa mitihani ni Walimu wanaofundisha shule za Serikali, ni wachache sana kwa asilimia ndogo wanatoka shule za *private*.

Mheshimiwa Spika, tumeona hapa wanafunzi wa Saint Marian wapo sijui nane au wangapi ambao wamefanya vizuri. Hiyo ni *private school*, lakini *Government schools* Walimu wanakimbia kwenda kusahihisha mitihani, *at the same time* wanawaza kumaliza *syllabus*. Wakirudi hawawezi kumaliza *syllabus,* wanaingia njia za mkato wanafundisha kwa maswali na majibu vitabu vya Mheshimiwa Nyangwine

tunavijua. Naiomba sana Wizara iliangalie jambo hilo, ikiwezekana mihula ya zamani irudishwe.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kuhusu Kitengo cha Ukaguzi, tumeshuhudia bajeti ya Kitengo hiki, kimekuwa kikitengewa hela ndogo sana, inavyoonekana ukaguzi haufanyiki vizuri. Tuna shule nyingi sana za *primary* na sekondari na Vyuo vya Serikali. Kitengo hiki kwa kutokutengewa fedha za kutosha ukaguzi haufanyiki, shule hazifanyi vizuri.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa masikitiko makubwa hata kama hatusemi, mimi ni Mwalimu, Walimu wana mgomo baridi, tumejionea hapa. Mwalimu akikufundisha moja jumlisha tatu ni kumi na tatu, kama ni darasa la kwanza utashika hivyo hivyo, hutabadilika. Matokeo yake tutajenga Taifa la aina gani?

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri na Wizara kwa ujumla mliangalie suala hilo kwa dhati ili ukaguzi uendelee kufanyika katika shule zetu ili elimu yetu iwe bora.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nisipoteze wakati, naomba nikushukuru na naomba Wizara iyafanyie kazi haya niliyoyazungumza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Spika ahsante. Naomba moja kwa moja nijikite kwenye mchango wangu kwa sababu Kanuni haziruhusu pongezi zilishatolewa kwako naomba niendelee moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na suala la Bodi ya Mikopo. Wabunge wengi jana walichangia kuhusu ucheleweshaji wa mikopo kwa wanafunzi kutoka kwenye bodi ambayo inasababisha migomo ambayo tunaiona kila mara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kucheleweshwa kwa mikopo, nataka kuihoji Serikali, fedha zimekuwa zinaanza tayari kukusanywa kwa wale ambao walipewa mikopo...

*(Hapa Kengele ililia)*

**SPIKA:** Siyo kengele yako hiyo.

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Fedha hizi hazionekani zinafanya nini baada ya kukatwa kwa wale watu hasa Walimu ambao wanakatwa kila mwisho wa mwezi zinaingia wapi? Nataka kujua fedha hizo zinaingia kwenye mfuko gani. Toka bodi ya mikopo imeanza kukata hela kwa Walimu, ni kiasi gani kimeshakatwa na kimefanya kazi gani na kiko kwenye akaunti gani. Nnataka kujua kuhusu hilo.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni kutokuwa na uwiano kwa marejesho ya mikopo kwa Walimu. Kuna Walimu wanaokatwa sh. 52,000, kuna Walimu wanaokatwa sh. 42,000, kuna Walimu wanaokatwa sh. 20,000 , kuna Walimu wanaokatwa sh. 10,000, lakini pia kuna Walimu ambao hawakatwi kitu chochote wakati wapo watu ambao wamesoma nao kozi hizo na

wameanza nao kazi, lakini bado hawakatwi hata senti tano. Nataka kujua usawa upo wapi kwa Walimu. Ni kwa nini hakuna uwiano katika urejeshwaji wa mikopo.

Mheshimiwa Spika, naomba pia mikopo hii waangaliwe wanaochukua kozi kwa ngazi ya cheti. Hawa nao ni walimu tunawategemea katika shule zetu, ni kwa nini wanabaguliwa? Naiomba Serikali kwamba Walimu wanaochukua kozi za cheti na wenyewe waangaliwe kwenye mikopo na itolewe kwa haki. Kuna watoto ambao wanapata mikopo asilimia mia moja ambao hawahusiki. Wanaopata asilimia hamsini ndiyo wale wanaohusika kupata mikopo asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, ni nani anayefanya hivi na kuwaacha watoto hawa wa wakulima wanaotakiwa kupata asilimia mia moja hawapati na watoto wa Mashishanga na watoto wa Viongozi wanapata asilimia mia moja kwa nini? Wale ambao wana maisha duni na wanatakiwa wasaidiwe, yatima lakini hawapati hii mikopo wanapata asilimia hamsini. Naomba majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye suala la kufanya kazi katika mazingira magumu. Walimu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, wakati wa kipindi cha Mheshimiwa Rais Mkapa kulikuwa kuna posho ya kufundisha, naomba kuuliza posho hii aliyeitoa alikuwa na maana gani?

Mheshimiwa Spika, leo hii Walimu waliopo Mikoa ya pembezoni kwa mfano Mkoa wa Shinyanga, Simiyu

wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Mnawatolea posho ya kujikimu ya kufundishia, hamuwapi posho ya usafiri, hamuwapi posho ya nyumba, wataishi katika mazingira gani na watakuwa na moyo gani wa kufundisha kama hawana hata posho moja wanayoifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, mbali na hilo bado wanafuata mshahara katika Halmashauri za Miji katikati, mtu yupo porini ataendaje na anautegemea huo mshahara kama nauli? Naiomba Wizara iangalie hili suala la posho ya kufundishia irudi na Walimu wapate hizi posho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Walimu wa Vijijini na waliopo pembezoni ni tofauti na waliopo Dar es Salaam. Walimu waliopo Dar es Salaam nimewahi kushuhudia, Mwalimu anaingia darasani anauza ubuyu, anasema kopeni kwanza ubuyu, ndiyo nitawafundisha. Wanafunzi wanakopa ubuyu kwanza, halafu ndiyo anafundisha, sasa huko kijijini Mwalimu atafanya kitu gani.

Mheshimiwa Spika, Mwalimu wa Kijijini hawezi kuuza ubuyu kwa sababu watoto hawana hela, hata ile senti kumi hawana, lakini watoto wa mjini wanapewa hela kidogo ndiyo maana Walimu wa Mjini kidogo maisha wanayaweza. Hawa waliopo Vijijini mnawafanya nini? Naomba hiyo posho ya kufundishia irudishwe.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana kumeanzishwa mfumo wa kuweka *multiple choice* kwa somo la

hisabati kwa shule za msingi, tunatengeneza kizazi kipi? Wale mbumbumbu wale ndiyo huwa mabingwa wa ku-*guess*, yaani anafumba tu linakuwa jibu la ukweli, mwisho wa siku huyo ndiye anayefaulu na anakwenda Sekondari na kule anakuwa hajui kusoma na kuandika kwa sababu ya *multiple choice* kwenye hesabu.

Mheshimiwa Spika, nashindwa kuelewa kwa kweli na nasikitika sana na inaniuma, tunatengeneza kizazi kipi? Tunataka kuwa na *mathematician* kweli nchi hii? Hatuko *serious*! Naomba hesabu zirudi, mtoto afanye hesabu kwa kuonesha njia na hatimaye apate jibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ukimwekea *multiple choice* anaweza kukosea jibu lakini amekaribia kupata mbili na mbili iko hapa anajua ndiyo jibu, kumbe siyo. Lakini kwa *multiple choice* kwa kweli tutakuwa tunawajengea watoto kitu ambacho siyo tena hakifai. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala la shule. Tumekuwa tukijenga shule nyingi sana, tumejenga shule nyingi za msingi, tumejenga shule za sekondari kwa wingi sana na vyuo tumevifungua vingi sana. Lakini tusitilie mkazo kufungua shule za msingi na kuongeza sekondari na vyuo. Tuangalie hiyo elimu inayotolewa ni bora? Wingi wa shule za sekondari na wingi wa shule za msingi na vyuo kama hakuna ubora ni afadhali kuacha, kwa sababu tunatengeneza Taifa la vijana mambumbumbu, vijana ambao hawawezi kuuzika, hawawezi kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo kubwa ambalo sasa hivi lipo, tusiegemee kutilia mkazo elimu ya msingi na sekondari kwa kujenga shule kwa kweli tutakuwa hatuwasaidii watoto kama elimu itakuwa bado hairidhishi. Hatutawasaidia kwa chochote kile.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo nimeliona kila Waziri anayeingia katika Wizara hii anakuwa na *policy* zake. Kwa nini hakuna mwendelezo wa Waziri aliyeanzisha nyuma na huyu anayefuata akiendeleze. Matokeo yake kila anayekuja anakuja na kitu chake. Sasa hii elimu kweli itatufikisha wapi kwa sababu kila anayeteuliwa analeta ya kwake na aliyetoka yanabaki pale pale na anayekuja anaanzisha mambo yake. Hapa hatutafika, tutaendelea kucheza danadana na watoto wetu watakuwa hawafanyi vizuri na watakuwa wanaonekana mambumbumbu kila siku.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na kozi nyingi sana katika Taifa letu na katika Vyuo vyetu. Naomba Wizara ianzishe kitengo maalum ambacho kitaweza kuwaandaa wanafunzi kuchagua ni kozi gani zinaweza kuwafanya wakapata kazi kuliko kuwasukumia tu kwa sababu vyuo vipo, mnawasukuma tu, lakini kazi zinakuja kuwa za shida.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara iandae kitengo ambacho kitasaidia kuwashauri wanafunzi kwamba kozi hii mkiisoma itawasaidia kuna ajira. Lakini kuwasukumia wanaenda vyuo vya ualimu ajira hakuna, miundombinu hamtengenezi, hakuna madarasa, vurugu tu. Inatia uchungu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwenye suala la Maafisa Elimu Taaluma, Takwimu na Walimu. Kama Maafisa Elimu Takwimu hawajajiendeleza waende wakajiendeleze wasiwaonee wivu Walimu ambao wamejiendeleza. Kwa sababu wamekuwa wanawafanyia vikwazo, hawashirikiani nao vizuri kwa sababu tu Walimu wanajiendeleza. Kama wenyewe ni Maafisa Elimu basi na wenyewe watoke wakajiendeleze, lakini siyo kuwafanyia vikwazo Walimu ambao wanajiendeleza. Suala hilo limenisikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, kuna fedha za MMEM, nikiangalia katika ripoti ya hali ya utekelezaji wa mpango wa MMEM II, kwa kweli ni jambo la kusikitisha sana. Sasa hivi kuna MMEM III, hii MMEM III inakuja kufanya nini wakati MMEM II imefanya asilimia 15 tu mwaka jana. Madarasa 6,843 tu ambayo ni asilimia 15 ndiyo yamejengwa, nyumba za Walimu asilimia tano tu ndiyo zimejengwa, vyoo asilimia 2.5.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunakwenda kwenye MMEM III kufanya nini, tunakwenda wapi? Kwa kweli hivi ni vitu vya kusikitisha sana. Naiomba Serikali, bila elimu kwa kweli nchi hii hatutaendelea popote, tutashindwa kuepeleka vijana wetu nje ya nchi kupata ajira kwa sababu ya elimu ambayo tunaanza nayo toka msingi.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie na suala la *TCU*. Naiomba *TCU* wabaki kama kupitisha mwanafunzi kama amemaliza *form six* unastahili kwenda Chuo, lakini isimpangie chuo mwanafunzi, ipitishe tu kwamba pointi zako zinatosha kwenda chuo, basi ukatafute

chuo mwenyewe. Lakini hili suala la kutafutiana vyuo na *TCU* unampeleka mwanafunzi Chuo ambacho hakitaki, sioni kama ni jambo muhimu. Nafikiri kuna haja ya *TCU* sasa kumpa mtu *go ahead* kwamba wewe unaweza kwenda kwenye chuo chochote lakini siyo kumpangia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale atafuatiwa na Mheshimiwa Jasson Rweikiza.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia katika Wizara hii. Kabla sijaanza kuchangia ningeomba nijaribu kueleza labda Waziri anaweza kunisaidia.

Mheshimiwa Spika, tunapokea simu nyingi ambazo zinalalamika kwamba inaelekea kuna mpango wa mitihani ya vijana wetu kusahihishwa kwa njia ya kompyuta na kwa maana hiyo kompyuta iko *sensitive* sana, inaweza ikasababisha baadhi ya vijana wengine hasa wale ambao wanatoka vijijini sana wakawa *disqualified* kwa sababu ya karatasi zile zimekuwa chafu na mnafahamu shule nyingi za vijijini wengine wanasomea kwenye vumbi, wanafanya mtihani halafu karatasi inakwenda kwenye kompyuta inawezekana kwamba akawa *disqualified*.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri anieleze kwamba kuna usahihi gani au umakini gani katika kusahihisha mtihani kama kompyuta itatumika katika kusahihisha mitihani hii.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ambalo nataka kuliongelea ni kwamba, katika ukurasa wa saba katika hotuba ya Waziri, ameeleza sana kuhusu elimu ya awali na kwamba mpango mkubwa ni kuhakikisha kuwa kila shule ya msingi ina darasa la elimu ya awali lenye madawati yanayolingana na hali ya watoto wa elimu hiyo.

Mheshimiwa Spika, hapa nina wasiwasi kidogo. Shule nyingi zilizoko vijijini kama mnavyofahamu zina Walimu wachache sana, unaweza ukakuta shule moja ina wanafunzi 500 hadi 600 lakini kuna Walimu wawili au watatu na Mwalimu huyu anatakiwa afundishe watoto wa elimu ya awali. Sijui mpango huo utatekelezwa vipi, naona kwamba ni mgumu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba katika sera ya elimu ijaribu kuangalia sana kwa shule ambazo zipo pembezoni kabisa mwa nchi, maana yake wale watu ambao wanaishi vijijini iwasaidie zaidi. Kwa sababu mijini inakutwa *ratio* ya Mwalimu moja kwa thelathini (1:30) au moja kwa ishirini na tano (1:25), lakini vijijini *ratio* ya Mwalimu kwa mwanafunzi ni moja kwa sitini (1:60) au moja kwa sabini (1:70) au moja kwa mia moja (1:100).

Mheshimiwa Spika, sijui mpango huu utatekelezwa vipi na ni vipi hao wanafunzi wanaotoka katika shule za pembezoni wanaweza kufaidi mpango huu. Lakini kwa sababu hapa chini umeelezea kuhusu mpango mwingine tena wa MMEM III, ningeomba mpango huu ungelenga zaidi kwa shule ambazo zipo vijijini. Kwa sababu mijini wenzetu wanafaidi, lakini kwa vijijini jamani hatuwatendei haki kabisa watu hawa, kwa sababu wanakosa mambo mengi.

Mheshimiwa Spika, tunazungumza mambo ya sekondari, shule za msingi unakuta shule zenyewe hata mazingira yake ni mabaya sana, zimejaa vumbi. Naomba mpango huu wa MMEM III basi ulenge zaidi kwa shule zilizopo pembezoni ili nao wafaidi isiwe upande mmoja tu. Kwa hiyo, naomba sana Waziri ahakikishe kwamba suala hilo linazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ambalo naomba kulizungumzia ni kuhusu migomo ya Walimu. Nashangaa kwa sababu mimi na-*declare interest* kidogo kwa sababu niko kwenye Kamati ya Huduma za Jamii. Wakati tumekutana na Walimu tumeongea lakini baada ya mwezi mmoja, miwili mbele wanagoma.

Mheshimiwa Spika, lakini hatukuambiwa sana mambo hayo kwamba yatakuwepo na tulifikiri kwamba kwa sababu kulikuwa na malimbikizo ya mishahara yao, bila shaka hiyo itakuwa imeshakwisha, hata kabla hatujaingia Bungeni. Lakini matokeo yake hawa Walimu tena wameanza kugoma.

Mheshimiwa Spika, nafikiri hivi, migomo hii ya Walimu haiwezi kutatuliwa kwa njia ya Mahakama, haitawezekana. Kwa sababu kwa Mahakama labda mtu ameiba, lakini huyu mtu anadai haki yake, ukipeleka Mahakamani *of,course* ni kwamba mlitumia hatua ya juu kabisa kuhakikisha kwamba huu mgomo unasitishwa, lakini sio ufumbuzi ambao umepatikana.

Mheshimiwa Spika, naomba kama ingewezekana basi nafikiri Wizara ya Elimu ina wataalam wengi, tukae na vyombo hivi, tukae na Walimu tuzungumze kwa sababu hapa hatapatikana mshindi. Labda lugha ya kichungaji niseme hapa wote tumeanguka au tumepata au tumeshindwa.

Mheshimiwa Spika, kuna kushindwa wote au kushinda wote. Kwa hiyo, naomba kwamba njia pekee ambayo itasababisha tuweze kumaliza mgogoro huu ni kwa njia ya kuzungumza tu. Tukiongea tutamaliza mambo hayo, lakini kwa njia ya Mahakama wala haitatokea kwamba ukashinda au wakashinda, la! Wote mtakuwa mmeshindwa au mmeshinda wote.

Mheshimiwa Spika, la pili, nataka niongelee kuhusu wanachuo ambao tumeshuhudia wenyewe siku chache zilizopita au miezi michache iliyopita wakati Serikali imetangaza nafasi za ajira, wanafunzi wengi walipokuja hapa Dodoma walikwama kwa sababu eti walikuwa hawaja-*sign* mkataba na kwa maana hiyo walinyimwa kupewa vyeti wapeleke huko kunakohusika Wizarani.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kwa kweli adhabu waliyopewa wanafunzi ya kuwaambia kwamba wakalipe ada kwa wakati huu wameshamaliza wako nyumbani, ni adhabu kubwa sana na nafikiri Serikali pia inaweza kuwa makini kwa nini itokee mtu asi-*sign*? Kwa nini kusiwe na elimu?

Mheshimiwa Spika, itolewee elimu kwa wanafunzi hawa, mpaka inafikia hatua anakwenda kuchukua vyeti wananyimwa. Kumnyima cheti chake maana yake umemuua maana hawezi kupata kazi, hawezi kufanya chochote kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kutolewe elimu ya hali ya juu katika vyuo vyote. Hawa wanafunzi wasigome ku-*sign* na hatima yake kwa sababu anayepata adhabu hiyo sasa ni mzazi sio mtoto tena, sio mwanafunzi hata kama yeye anahusika, lakini atakayelipa hela zile ni mzazi. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie suala hili. Hawa wanafunzi ambao wamenyimwa vyeti vyao kwa ajili ya kwenda kuombea kazi huko, naomba ikiwezekana wapewe, wakati huo tunatafakari nini kifanyike mbali ya hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ambalo naomba niongelee katika mchango wangu ni kuhusu Walimu hasa Walimu wa masomo ya sayansi. Tumeshuhudia wenyewe hapa Ndugu zangu, wanafunzi wakija hapa wakipata zawadi lakini ukiangalia shule ambazo wanatoka, ni shule ambazo zimekuwa *equipped* kila kitu wanacho.

Mheshimiwa Spika, ni shule ambazo wana Walimu wazuri wa masomo ya sayansi, wana Walimu wazuri wa masomo yote, wana vifaa, wana maabara maana nimezisikiliza sana shule hizi, ni shule nzuri. Sasa ni lini shule zilizoko pembezoni au zingine za Serikali, za Kata zitapewa uwezo huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina hakika kwamba kuna wanafunzi wengi sana wenye vipaji vizuri sana huko tunakotoka, lakini kwa sababu ya Walimu hawapo, halafu vifaa havipo, unategemea huyu mwanafunzi hata kama alikuwa na kipaji atafanya nini? Si kumnyima haki yake huyu? Nani alaumike hapa?

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iliangalie suala hili. Ni suala gumu, zito lakini tuliangalie kwa makini zaidi kwa sababu Walimu wengi wanaokuja unakuta wanaishia kwenye shule zilizoko Mjini, lakini huku pembezoni hakuna kwa sababu hapa Mjini, Mwalimu wa masomo ya sayansi ana soko kubwa. Anapata *tuition* hapo, kwa hiyo akienda Vijijini huko hapati kitu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba jamani kuwe na mazingira mazuri ya shule za Kata. Walimu wakipatikana wa sayansi wapelekwe huko pia nako kuna watoto wenye vipaji maalum huko. Hivyo, naiomba sana Serikali iliangalie kwa makini kwa sababu wanafunzi wako wengi sana ambao wana uwezo, lakini tunawakosesha haki yao kwa sababu hatuna Walimu wa kutosha, hatuna vifaa vya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafikiri kwamba, hata hizi hela za rada zilikuwa zimepatikana, labda hata zingepelekwa huko kuboresha shule zilizoko pembezoni kuliko tuanze kugawanya Mjini, Mjini wana nafasi kubwa. Wote hapa tunajua tunatoka Vijijini, wachache sana ambao wamezaliwa Mjini, lakini huko tulikotoka jamani tunakufanyizia nini?

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iliangalie suala hili ili kuhakikisha kwamba shule zilizoko Vijijini huko zinaboreshwa, nazo zinakuwa na vifaa vyote vinavyohitajika kwa ajili ya kumsomesha mwanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia naishukuru Serikali kwa tangazo la Waziri kwamba shule sasa ziboreshwe, badala ya kufungua shule nyingi za sekondari, sasa hizi zilizopo ziboreshwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa sijui hii kengele ya kwanza ya pili?

**SPIKA:** Mheshimiwa, hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii muhimu sana ya Wizara ya Elimu, ambayo naamini kabisa ndiyo nguzo ya mafanikio ya Taifa lolote lile.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi na wa upande wa Upinzani, wameweza kueleza changamoto ambazo zinaikabili sekta hii ya elimu. Nawashukuru sana kwa kuona kwamba elimu ndiyo njia pekee ya kuweza kulikomboa Taifa letu. Mengi yameongelewa, lakini niseme tu kimsingi bado Serikali haijaipa kipaumbele elimu na ndiyo sababu tunaona kwamba uwekezaji katika elimu Tanzania bado ni mdogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha wazi katika mitandao mbalimbali na hata katika vitabu kwamba kwa *standard* ya Kimataifa angalau kila nchi inapaswa kuweka asilimia sita ya pato lake la Taifa katika elimu. Lakini Tanzania bado tumeweka asilimia 1.4 wakati wenzetu wa Kenya wana asilimia saba, wenzetu wa Rwanda wana asilimia tano na nchi ndogo kama Burundi wana asilimia 3.2. Kwa hiyo, nadhani bado hatujawekeza vizuri katika suala la elimu na ndiyo sababu tunaona ni jinsi gani elimu ya Tanzania inazidi kuporomoka.

Mheshimiwa Spika, jana wakati naongea nimeongea na Wabunge wengi wanakubaliana na mimi kwamba elimu ni Mwalimu, lakini ukiangalia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, suala la Walimu bado, ambalo ndiyo hasa nyenzo muhimu ya kuweza kuboresha elimu katika nchi yetu, bado halijachambuliwa kiyakinifu na kupatiwa suluhisho la kudumu.

Mheshimiwa Spika, sisi tukisema tunaonekana kwamba tunaonea gere Serikali ya Chama cha

Mapinduzi, lakini kusema ule ukweli, hatuwezi kuwaonea gere au hatumwezi kuonea gere jambo ambalo ni la msingi kama suala la elimu wakati elimu yetu iko *ICU*. Hatuwezi kumwonea gere mtu alie *ICU,* sana sana tutakuwa tunamhurumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi tunajitahidi kueleza yale ambayo tunaona wazi kwamba, Serikali imeshindwa kwa hiyo lazima yafanyiwe upembuzi wa kina na kuhakikisha kwamba elimu yetu inakuwa nzuri na wanafunzi wetu wanaweza kusoma, kuandika na kuhesabu.

Mheshimiwa Spika, sitaki kurudia yale ya jana, lakini nataka niseme tu, Mheshimiwa Waziri aliwahi kusema kwamba mgomo wa Walimu hauhusiani na madai yao ya nyuma isipokuwa ni madai mapya. Lakini ni wazi kwamba bado madai ya Walimu ya nyuma yako pale pale.

Mheshimiwa Spika, kuna Walimu wengi wanadai, kwa mfano, jana nimetoa mifano na mingine inaendelea, naendelea kupata *messages* nyingi na simu kutoka kwa Walimu wa maeneo mbalimbali, katika Halmashauri ya Mkuranga wanadai fedha nyingi sana, lakini vile vile kule Mwanza.

Mheshimiwa Spika, leo nilikuwa namsikiliza Katibu wa CWT anasema Walimu wa sekondari wanadai zaidi ya shilingi milioni 500 kule Mwanza. Sasa tunashindwa kujua kwa nini msitupe takwimu sahihi ili tuone kweli nani anayesema kweli; ni Walimu au ni Serikali, ili tuweze kuondoa huu mkanganyiko.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hapa Serikali inatuambia Walimu hawadai huko nyuma, madai yamekwisha na kama yapo ni kidogo sana, lakini Walimu bado wanasema wana madai ya msingi. Kwa hiyo, tunaomba mtupe takwimu sahihi, yupi yuko sahihi ili tuweze kuondoa huu mkanganyiko.

Mheshimiwa Spika, naomba vile vile niongelee suala la ukaimu. Kwanza niipongeze sana Serikali kwa kuhakikisha kwamba suala la ukaimu katika Wizara sasa limefikia ukomo na nimpongeze sana *Professor* Balalusesa kwa kuwa Kamishna mpya wa elimu. Naamini kabisa Balalusesa amepitia mfumo wa elimu kuanzia elimu ya msingi kama Mwalimu mpaka kuwa Mwalimu wa Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ana uelewa mkubwa wa suala zima la elimu hapa nchini. Kwa hiyo, naamini kabisa na nitashangaa sana kama bajeti ya mwaka ujao bado hakutakuwa na mabadiliko makubwa kwa sababu naamini Kamishna ni mtu muhimu sana katika kuboresha au kuleta mabadiliko katika elimu hapa nchini. Kwa hiyo, hilo nalipongeza.

Mheshimiwa Spika, lakini niende kwenye suala la ukaguzi, limeongelewa na Wabunge, hamna Mbunge aliyesimama hapa bila kuongelea suala la Kitengo au Idara ya Ukaguzi. Kama nilivyosema na naendelea kusisitiza kwamba ukaguzi ndiyo nyenzo pekee au ndiyo Idara pekee ambayo inaweza ikaonesha ubora wa elimu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nilitegemea kabisa baada ya kuwa na *D by D,* elimu ya shule ya msingi na sekondari kupelekwa TAMISEMI, Kitengo hiki cha Ukaguzi sasa kingeboreshwa kwa sababu kimebaki pale Wizarani. Matokeo yake Kitengo hiki kimeendelea kukanyagwa, hakipewi fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, naomba Wabunge wote kwa sababu tuko hapa Dodoma twende tu katika Kitengo cha Ukaguzi Wilaya ya Dodoma Mjini, huwezi ukaamini Kitengo hiki kiko katika Idara au jengo la zimamoto na toka tarehe 1 Julai, wamepewa *notice* ya kuondoka.

Mheshimiwa Spika, lakini kama haitoshi, kitengo hiki katika mwaka wa fedha 2011/2012 hapa Mjini pekee yake waliomba milioni 49, wamepewa shilingi laki nne. Shilingi laki nne kwa ajili ya Wilaya nzima kwa mwaka, shilingi laki mbili unusu zikiwa ni kwa ajili ya *per diem* na shilingi laki moja na nusu kwa ajili ya *ground travel*. Je, kama hapa Mjini hali iko hivyo, huko Mikoani hali ikoje?

Mheshimiwa Spika, lakini nizungumzie pia katika Kanda, najua kwamba kaguzi hizi ziko Kikanda, Kanda yenye Mkoa zaidi ya mmoja na natambua kwamba kuna Kanda yenye Mikoa mitatu, kwa kipindi cha miaka miwili na nusu wamepewa shilingi milioni mbili na laki tano.  Hii ina maana kwamba kwa Mkoa mmoja kwa mwaka ni shilingi laki tatu na nusu, hivi kweli tunaipeleka wapi elimu yetu?

Mheshimiwa Spika, halafu tukisema mmeshindwa, mnasema hapana. Sasa kama mnaupa Mkoa shilingi laki tatu na nusu kwa mwaka afanye ukaguzi, anaufanya kwa misingi ipi? Yaani na kwa uwezo gani? Jana nimemsikia Mbunge mmoja akisema kwamba wanategemea hata matairi kutoka kwa Ma- *DC* matairi ambayo yamekwisha ndiyo wanapewa waweke kwenye magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sio hivyo tu, watu hawa wanategemea ada ya wanafunzi ya shilingi mia tano, mia tano kwa kila ada ya mwanafunzi wa sekondari na wa *primary*. Lakini tujue kwamba sasa hivi Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeondoa ada kwa shule za msingi, sasa hawa Wakaguzi wanatoaje hiyo shilingi mia tano katika shule za *primary* wakati hamna ada. Kwa hiyo, naamini hili ni tatizo kubwa sana na ni lazima tulifanyie maboresho mpende, msipende. Naomba sana hili lishughuulikiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la Chama cha *Scout* Tanzania, naomba nilirudie na niliseme kwa uhakika kwamba Chama hiki pamoja na majukumu yake ya msingi kimeacha majukumu yake na kufanya biashara ambazo ni haramu kwa nchi yetu. Nitaomba nikuletee barua nilizonazo na vielelezo vinavyoonesha kwamba Viongozi wamekuwa wakijihusisha na biashara ya madawa ya kulevya. Wamekuwa wakipeleka nje watu ambao sio wanachama na matokeo yake watu hao wanabaki katika nchi hizo.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni la hatari sana na hata mwaka jana wakati wa *Jubilee* ya Malikia walipelekwa watu ambao sio wanachama wa chama. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze kama anajua matatizo haya na ni hatua gani zimechukuliwa kwa sababu wamekuwa wakitapeli.

Kuna Mama mmoja ambaye ni Mkurugenzi wa shule ametoa shilingi milioni 45 kwa ajili ya wanafunzi wake kupelekwa, hawakupelekwa na mpaka leo hii Chama kile kimemlipa shilingi milioni 21 kuanzia mwaka 2008 mpaka leo bado anadai. Hii ni hatari sana naomba Chama hiki Viongozi wake wachunguzwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia suala la *TEA*. *TEA* imeundwa kwa Sheria Na. 8 na *TEA* inafanya kazi nzuri sana. Naomba niwapongeze sana, lakini bado lile tengeo la bajeti haliwafikii asilimia mbili na sasa hivi wana mpango maalum wa kujenga *hostels* za wasichana.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana kwa sababu siku zote tumekuwa tukisema kwamba idadi ya wasichana au wanawake huku katika ngazi za maamuzi hawapo kutokana na kukosa elimu na tunaambiwa katika kipindi cha miaka miwili tu, zaidi ya wasichana 16,000 wamekatishwa masomo kwa sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naamini pamoja na mpango huu kabambe wa *TEA* wa kujenga hizi hosteli. Naamini kabisa Waheshimiwa Wabunge tutasaidiana nao ili kuhakikisha kwamba tunajenga mabweni.

Mheshimiwa Spika nakuomba sana katika kuacha *legacy,* sisi kama Wabunge wa kipindi hiki, naomba hasa kwa sababu Bunge hili linaongozwa na Spika Mwanamke, tuhakikishe kwamba *at least* tunajenga hosteli moja na iwe imeandikwa majina ya Wabunge wote wa mwaka huo ili tuweze kuweka *legacy* wasichana wawe na hosteli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile ombi langu naamini pia kwamba watoto wa kiume pia wana matatizo makubwa hata labda kuliko wasichana. Kwa hiyo, naomba pamoja na kujenga *hostels* za wasichana, huko baadaye pia *TEA* ihakikishe kwamba inajenga hosteli za wavulana.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni suala zima la kustaafu kwa Viongozi katika Vyuo vya Elimu ya Juu. Ni wazi kwamba Sheria ya kustaafu ni miaka sitini, lakini Viongozi hususani *VC's* na wale wasaidizi wao sasa hivi bado kuna ambao wameshamaliza miaka sitini lakini wako kwenye madaraka na wengine watafikisha miaka sitini wakiwa bado kwenye madaraka.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aondoe hiki kitendawili, kwa nini Sheria inasema kustaafu ni miaka sitini, lakini wale watawala katika vyuo ambao *majority* pia ni Wahadhiri bado

wameendelea kuwepo katika madaraka. Hili lilikuwa pia kwenye *speech* yangu, lakini nililiruka.

Mheshimiwa Spika, naomba hayo niliyoyazungumza, Mheshimiwa Waziri atakapokuja aweze kutusaidia. Ahsante nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Napenda kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Elimu. Kwanza niseme kabisa kwamba kama tunavyofahamu, elimu ndiyo msingi ya maendeleo ya Taifa lolote na jamii yoyote. Kwa hivyo, niipongeze Serikali ya CCM kwa juhudi kubwa wanazozifanya katika kuboresha elimu. Vyuo tunaviona vingi sana, Vyuo Vikuu, Vyuo mbalimbali vya Ufundi na Stadi mbalimbali, shule za msingi na sekondari zinajengwa, niseme CCM inafanya vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niongezee kusema kwamba, CCM yenyewe kama chama kina shule, ndiyo maana kina uzoefu mkubwa na tunaposisitiza kwa Serikali kwamba ifanye vipi kwenye elimu ina uzoefu huo. Jumuiya ya wazazi ambayo ni ya CCM inamiliki shule nyingi nchi nzima. Mimi nipo kwenye Uongozi wa Jumuiya hii kwa ngazi za juu na mwaka huu tuna uchaguzi ndani ya Chama cha Mapinduzi. Sio kama vyama vingine ambavyo akikaa pale kiongozi anakaa maisha yake yote.

Mheshimiwa Spika, CCM kila miaka mitano tuna uchaguzi, CCM yenyewe na Jumuiya na mwaka huu tuna uchaguzi na tumeomba nafasi mbalimbali kwenye Jumuiya. Lakini uamuzi uliopo ni kwamba,

shule hizi za wazazi tutaziboresha. Tutaboresha usimamizi, tutazikarabati, tuboreshe muundo wa uongozi wa shule hizi ili huduma ya elimu izidi kuwa nzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo na Serikali ya CCM inafanya kwa kujua kwamba elimu ni jambo la muhimu. Ijitahidi sana kuongeza bidii kwenye kutoa huduma hii ya elimu kwa wananchi wa Tanzania. Sasa tumesikia hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni nzuri na inatupa matumaini, lakini niseme kwamba, tuongeze jitihada hasa kwenye vitengo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, shule za sekondari za Kata hizi zilizojengwa kwa bidii kubwa, Serikali na wananchi wamejenga kwa bidii kubwa kwa mchango mkubwa, tuongeze nguvu hasa kwenye maabara na maktaba ili shule ziwe shule kweli. Maana nyingi zipo, zina majengo machache ya madarasa, hakuna nyumba za walimu, vyoo havitoshi, hakuna majengo ya utawala. Kwa hiyo, tuongeze nguvu ili shule hizi zikamilike.

Mheshimiwa Spika, tumeona kwenye randama moja hapa, tulipewa wiki moja iliyopita kwamba, kila Halmashauri, shule mbili zinaboreshwa, zinakamilishwa. Shule mbili ni chache mno, hazitoshi. Pale Bukoba nina shule 31 za Sekondari, kila mwaka shule mbili, ina maana miaka 16; sasa ni muda mrefu sana, vijana wengi watakwenda bila kupata elimu nzuri, bila maabara, bila maktaba. Tuongeze angalau kila mwaka shule tano kila Halmashauri, kusudi shule nyingi ziweze kukamilika vizuri na ziweze kutoa ubora mzuri.

Mheshimiwa Spika, lakini pia suala la maslahi ya Walimu, achilia mbali hii ya wanaogoma na nini, ila nao si wengi ni wachache tu, nimeona kwenye takwimu hapa. Lakini maslahi ya Walimu yaangaliwe vizuri, hasa Walimu wa Vijijini.

Mheshimiwa Spika, Walimu wanapangiwa Vijijini, wengine hawaendi, hakuna nyumba za kuishi, maslahi kule ni duni kidogo. Sasa angalau kuwe na utaratibu mzuri wa kuwahamasisha waweze kupenda kwenda kule vijijini hasa nyumba za kuishi, kama kuna posho kidogo ya kuwaongezea wale wa vijijini, waweze kupenda kazi yao ya ualimu kule vijijini.

Mheshimiwa Spika, niishauri Wizara hii katika Kitengo cha Ufundi, maana ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Sasa katika ufundi, bado mkazo hautoshi, vyuo vya ufundi havitoshi; vijana wengi wanatoka mashuleni, shule za msingi, za sekondari, hawapati stadi za ufundi mbalimbali ambao ni muhimu. Wizara, iweke mkazo kwenye jambo hili, vyuo viongezwe; pale Bukoba, hakuna chuo cha ufundi na bajeti hii haina.

Mheshimiwa Spika, nimesoma bajeti kwa kina, hakuna mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi pale Bukoba, angalau vijana hawa wanatoka mashuleni, waende kwenye Chuo cha Ufundi. Kwa hiyo, hii itiliwe mkazo mkubwa kusudi vijana wapate stadi na ufundi unaostahili. Ni kazi ya Wizara hii na naomba waifanye.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo naomba Wizara hii ilifanye, ni jambo muhimu sana, niliseme leo.

Kuna utaratibu wa siku nyingi sana, wa miaka mingi ambao Baraza la Mitihani *(NECTA)* linao wa kutoa *Division III* kwa Vijana wanaofeli somo la hesabu, daraja la III. Ukifeli somo la hesabu Kidato cha IV, unapewa Daraja la III, hata kama umefaulu masomo mengine vizuri, una A una B una C, umepasi vizuri masomo mengine, ukifeli hesabu unapewa daraja la III. Hii imekuwepo muda mrefu sana.  Nasema huu sio utaratibu sahihi, muda umefika ubadilishwe.

Mheshimiwa Spika, inakuwa kama vile kwamba, Hesabu pekee ndio somo la maana, si kweli. Sio kwamba, hesabu peke yake ndio somo lenye maana sana, je Kiingereza? Ambalo ni somo linalofundishia masomo yote, masomo yote ya Jiografia, Historia, Baiolojia, Kemia na mengine, Lugha ni Kiingereza, lakini akifeli Kiingereza hapewi adhabu hii, ila akifeli hesabu anapewa daraja la III, jambo hili, liangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, zamani ilikuwa ni somo la siasa, baadaye siku hizi limekuwa *Civics,* zamani ilikuwa linaitwa Siasa na Kiswahili, tuliangalia, waliangalia wakaona kwamba, imepitwa na wakati, wakaacha. Limebaki somo la Hesabu peke yake, ukifeli hesabu unapewa Daraja la III.

Mheshimiwa Spika, hii iangaliwe upya, si muafaka kwa sasa hivi, ukizingatia kwamba, hata Walimu wa Hesabu hawapo au kama wapo hawatoshi. Shule inakaa mwaka mzima, miaka miwili, ina Mwalimu mmoja wa Hesabu, badala ya wanne au watatu, au hamna kabisa Mwalimu wa hesabu. Mwanafunzi akifeli Hesabu, anapewa adhabu ambayo hastahili kupewa

adhabu hiyo, sio kosa lake. Hakuna Walimu, hakuna vifaa, nimesema maabara hazipo, maktaba hakuna, sasa kupewa Daraja la III, anaonewa bure huyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna kipindi ilikuwa kwenda kuomba mkopo Bodi ya Mikopo, kama ni Mwanaume uwe na Daraja la I, *Form IV* na *Form VI.* Kama ni Mwanamke, uwe na Daraja la I au la II, *Form IV* na *Form VI,* kama hauna hiyo hau-*qualify* kupata mkopo.

Mheshimiwa Spika, sasa hawa vijana wanaonewa tu kwa sababu ya somo moja la hesabu, anakosa haki za msingi pamoja na Bodi ya Mikopo hawampi mkopo na haki nyingine. Cheti kinakuwa cha Daraja la III, kumbe amepasi vizuri masomo mengine. Kwa hiyo, jambo hili Wizara, naomba iliangalie, iagize Baraza la Mitihani libadilishe, ili liondolewe vijana wote wapewe haki zao kulingana na ufaulu wao ulivyo. *(Makofi*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba niongee mambo mengi lakini kwa kifupikifupi.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na suala la kwanza, niipongeze Wizara, wanafanya kazi nzuri pamoja na mapungufu yaliyopo. Lakini, niwapongeze vijana ambao leo wameonesha umahiri wao wa kufanya vizuri katika Kidato cha VI.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze msichana aliyetoka Shule ya Kata ya Olele, Rombo, Mkoani Kilimanjaro. Naomba niwaambie hao wanaosoma Shule za Kata, *it can be done, play your part;* ukifanya wajibu wako utafaulu na mambo yatakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nijielekeze kwenye mambo ambayo nataka kuchangia; mojawapo ni mitihani ya *multiple choice.* Naomba niiombe Wizara, kwamba, inawezekana kweli *multiple choice* ikawa nzuri, lakini mara nyingi inakuwa nzuri kwa wale ambao wako *level* ya juu zaidi.

Mheshimiwa Spika, ukimpa mwanafunzi wa Kidato cha VI *multiple choice,* ata-*attempt* kufanya hilo swali, ili aone kama anapata majibu yanayokaribiana na yale yaliyoko kwenye *multiple choice.* Lakini ukiwapa hawa watoto wa *primary,* sana sana atapiga bahati nasibu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba hebu tuwape wanafunzi hawa *chance* ya kutumia akili yao. Tuwaache wafanye, hata kama watafanya nusu nusu au robo na robo tatu, yaani robo tatu iwe ndio kufanya, lakini *multiple choice* naomba isiwe nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, naomba niongee kuhusu *Higher Education.* Kuna *Scholarships* ambazo Kamati ya Ulinzi na Usalama, tulikuwa tunawasomea Waheshimiwa Wabunge hapa, kwamba, Serikali ya

China, inakuwa na *Scholarships* kwa Watanzania. Inasema kwamba, tuki-*sponsor* wanafunzi 100 wao wataongeza ufadhili wa wanafunzi wengine 100.

Mheshimiwa Spika, nawaomba Serikali, iliangalie hili, kwamba, kama kweli hizi *scholarship* zinapatikana, kuna haja *Higher Education* itoe *Sponsorship* kwa wanafunzi wetu katika kila fani. Naomba Serikali, isaidie wanafunzi hawa kupata hizo nafasi za *scholarship* nchini China.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, ni ukaguzi. Mwaka jana nilichangia ukaguzi, nikasema jinsi ambavyo ukaguzi wa shule za msingi unakuwa ni wa shida. Wale Wakaguzi, wako kwenye Ofisi za Wakurugenzi au hata ingewezekana wakawa na Ofisi zao pembeni na ya Mkurugenzi, lakini ukweli ni kwamba, hawawezeshwi vya kutosha. Wakati mwingine, kama wengine walivyokuwa wanasema, ni kweli hawana mafuta, wakati mwingine hawana magari, lakini tunategemea waende wakafanye ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, Walimu wana *abscond* sana, yaani wanakwepa sana vipindi. Tusiwaone Walimu wanalalamika hapa, tukafikiri kwamba, wao ni wazuri sana. Ni wazuri ndio wanafundisha watoto wetu, lakini ukweli ni kwamba, wengi pia wanakwepa vipindi, wanahitaji ukaguzi. Lakini licha ya hiyo kuna pia namna wanavyoandaa vipindi vyao na kuandaa somo; haya nayo yanatakiwa yakaguliwe. Naomba Idara ya Ukaguzi, Serikali, iliangalie vizuri, iweze ku-*provide*

*facility* ambazo wanazihitaji kama magari, kama mafuta.

Mheshimiwa Spika, jambo la nne, ni nyumba za Walimu. Kuna kitu kinaitwa *economic impact* au *social impact;* kwamba, kama barabara imejengwa hapa, watu wanajenga vibanda vya biashara wapate pesa kwa sababu, ile barabara imejengwa. Sasa mimi nilikuwa ni kiongozi huko Kanda ya Ziwa, nikawaambia Wasukuma na Wanyamwezi kwamba, shule za sekondari zimejengwa kila Kata na wewe mfugaji una ng'ombe zaidi ya 40,000 au 30,000. Sasa *diversify* biashara yako, uza ng'ombe kidogo, jenga nyumba za kukodisha kuzunguka zile shule za kata, ili Walimu wakija wewe unawakodishia 10,000/=, 15,000/= kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, nikawaambia ukijenga kama vyumba sita kwa 15,000/= kila mwezi una 90,000/=. Ukajenga kwenye Kata mbili au tatu, una pesa nyingi, tena wakati mwingine niseme pengine haina kodi kwa sababu, inawezekana *TRA* wakawa hawajafika, hawajaweza kukufuatilia.

Mheshimiwa Spika, lakini haya mambo hayafanyiki. Maeneo mengi nchini, wanaweza kupata matofali ya kuchoma kwa pumba za mpunga. Wanaweza kupata matofali haya ya *hydroform,* lakini na maeneo mengine matofali ya kuchonga. Naomba hebu tutumie mtindo huu, pengine Serikali, labda inatakiwa ipeleke somo hilo kwamba, Halmashauri za Wilaya, Wakurugenzi, wajaribu kuwahamasisha wafanyabiashara walioko kwenye maeneo yao

wajenge nyumba za Walimu, wakodishe kwa hawa Walimu. Sidhani kama hawa Walimu, wanatarajia kukaa bure moja kwa moja. Inawezekana kabisa wakapata vyumba vya bei nafuu wakakaa, lakini alimradi viwe ni vyumba ambavyo vinakidhi mahitaji.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu mimba za watoto. Naomba niwaambie wazazi wenzangu kwamba, jamani, malezi yanaanza na mzazi. Malezi ya watoto wetu ni lazima yaanzie kule nyumbani kwetu. Haiwezekani, wewe mtoto anasoma shule ya msingi, anatakiwa saa 10.00 saa 11.00 awe amerudi nyumbani, huyu mtoto anakuja saa 1.00, saa 2.00 na mzazi unampokea na huulizi. Anaweza kukwambia ndio mama foleni, magari shida, mahali kama Dar-es-Salaam, lakini kuna maeneo mengine mtoto huyu akitoka shule saa 10.00 lazima *within half an hour* awe nyumbani, lakini mzazi unanyamaza.

Mheshimiwa Spika, naomba wazazi tuliangalie hili. Tutalaumu sana kwamba, wototo wetu wanapata mimba. Mwalimu huyu, hawezi kuwa anafanya mambo yote pamoja, kwa ajili ya mtoto wako. Atamfundisha yale yanayostahili, lakini malezi lazima yaanzie nyumbani. Lazima wazazi, tukae na watoto tuwaambie ubaya wa kukutana na wanaume kwenye umri mdogo. Tuwaambie watoto, kwa nini lazima wasome kwanza na kama ni mambo mengine, ndio yaende baada ya wao kusoma; naomba wazazi, tulichukue hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, pia nashauri, hebu Wakuu wa Shule, watafute *partnerships* na shule nyingine. Kuna nchi ambazo zina shule za msingi ambazo zinaweza kuwa zinapenda *partnerships* na shule za Tanzania. Kwa mfano, niliona *Association* moja inaitwa *Friends of Urambo,* ambapo wanafunzi wale ni wa Uingereza, ni wanafunzi wa shule za msingi, wanakuja kwenye shule kadhaa, wanashirikiana na wenzao, wanawafundisha kujenga, wanapaka rangi nyumba au zahanati.

Mheshimiwa Spika, yaani zile *skills* ambazo mtu mzima anafanya, wale watoto ndio wanafanya na wanafanya na kweli nyumba inakamilika, unaona imependeza. Kwa hiyo, nikasema pengine, sio wazo baya kushirikiana katika mawazo haya kwamba, Walimu, wakatafuta *partnerships* na shule nyingine kwa ajili ya kupeana uzoefu na pengine pia, kusaidiana katika *exchange* ya lugha.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni Baraza la Mitihani. Naomba niwapongeze, pamoja na kuwa ndio, mara chache chache kunatokea kuvuja kwa mitihani, lakini kwa kweli, niseme wanajitahidi. Wanaondoa wale wafanyakazi ambao ni wabaya, wanaoeneza au wanauza mitihani, lakini naomba niseme Baraza la Mitihani, linafanya vizuri na naomba mwendelee kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, ni Bodi za Shule. Kule kwenye maeneo huko Vijijini, *criteria* ya kutafuta Wajumbe wa Bodi, naona labda inawezekana ni ngumu kidogo. Kwa hiyo, Shule nyingi

za Kata, hazina Bodi za Shule na kama hazina Bodi za Shule, maamuzi pia yanakuwa ni magumu.

Mheshimiwa Spika, naomba uangaliwe uwezekano wa kurekebisha na kwamba watu wote walioko kule kwenye maeneo, ambao wana uelewa, ikiwezekana wawe *included* kwenye hizi Bodi za Shule. Sheria moja inasema ni lazima awe Kidato cha IV, sasa lakini wanaweza kuangalia Kidato cha IV ni nani na nani?

Mheshimiwa Spika, yako Makampuni kwenye maeneo yetu yana watu wa Kidato cha IV, yako Makanisa, iko Misikiti, naomba Mheshimiwa Spika, *criteria* hii ya kuchagua Bodi za Shule iangaliwe, kwa ajili shule ziweze kuwa na Wajumbe wa Bodi, ambao watasaidia kwenye kutoa maamuzi kwenye zile mashule.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, nashukuru kwa Serikali, kurudisha mitihani ya Kidato cha pili. Mwanafunzi asipopimwa, hutategemea afanye vizuri, kwa hiyo, naomba niipongeze Serikali, kwa hilo. Lakini niombe, ziko Sekondari ambazo hazifanyi *test* kuanzia Januari mpaka Julai, wanapofanya mtihani wa *Semester.* Mwalimu hafanyi hata *test* moja hata *quiz* moja, huyu mwanafunzi unayempeleka kwa miaezi sita bila *test,* anajiandaa wakati gani? Naomba Serikali, iweke utaratibu wa kuwawezesha wanafunzi kufanya *test,* ikiwezekana *once per two weeks* au mara moja kwa wiki.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi uliyonipa niweze kuchangia mawazo katika Hotuba hii muhimu. Mwaka jana Serikali, ilituletea hapa Bungeni, Mpango wa Miaka Mitatu ya Maendeleo. Tulipokea, tukajadili na kupitisha na nilifarijika kuona kwamba, elimu ni moja ya vipaumbele vitano. Huu ulikuwa ni uamuzi sahihi.

Mheshimiwa Spika, Mataifa ambayo tunasema yameendelea, kilichowafikisha hapo ni elimu; waliwekeza katika elimu, sasa wanavuna maendeleo. Mwaka 1987, nchi zisizofungamana na upande wowote *(Non Aligned Movement Countries)* walikutana Zimbabwe na moja ya ajenda waliyoizungumzia ni kwamba, hizi nchi za Kusini, nyingi zilikuwa zimetawaliwa, lakini zikapata uhuru. Kama tunavyojua nchi nyingi za Kiafrika, zilipata uhuru miaka ya 60, lakini maendeleo yake kisiasa, kiuchumi, kijamii, bado ni duni; wakajiuliza kulikoni?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wazo likawajia kwamba, wamwombe Mwalimu Nyerere, ajaribu kutatua tatizo hilo; akakubali na alichofanya ni kuunda jopo la watu 27 mashuhuri kutoka *Continents* zote, lilikuwa jopo lililohusisha Wanasiasa, Wanazuoni, Wanasayansi, Wafanyabishara, Maprofesa na vile vile kulikuwa na Askofu mmoja.

Mheshimiwa Spika, hiyo Tume, iliitwa Tume ya Kusini *(South Commission)*. Tume hiyo ilizunguka nchi mbalimbali, ikafanya mihadhara, wakachukua mawazo ya watu mbalimbali na kuyaweka katika kitabu kinachoitwa *"Challenge to the South".*

Mheshimiwa Spika, hicho kitabu, upate nafasi ya kukisoma kwa sababu, kina maoni mengi na mapendekezo mengi. Suala ambalo ningependa kulinukuu kutoka katika hicho kitabu, ni kwamba, walitoa angalizo kwamba, tofauti kubwa ambazo waliziona kati ya nchi zilizoendelea na zile za Kusini ni kwamba, wenzetu walio Kaskazini, wameendelea katika sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, sisi wenyewe ni mashahidi kwamba, nchi kama Malaysia au Korea Kusini, tulikuwa na uchumi unaofanana katika miaka ya 50 na 60, lakini wao wakawekeza katika sayansi na teknolojia na vile vile wamejenga viwanda. Sasa hivi, tunaziangalia hizo nchi wanavyotu-*over take* kimaendeleo. Sisi tumebaki tunalalamika na kutafuta wachawi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ilani yetu ya Uchaguzi, imetuelekeza kwamba, tujenge Shule za Sekondari kila Kata, mwitikio umekuwa mzuri na nikichukua Jimbo langu, mwaka 2000 tulikuwa na shule mbili za Sekondari, sasa hivi tunazo 27.

Mheshimiwa Spika, tuwapuuze wanaosema ni shule za yeboyebo, matunda tumeyaona. Lakini changamoto kubwa ambayo tunayo katika matatizo ya kuendesha hizi shule ni uhaba wa Walimu na hasa

Walimu wa sayansi, lakini pia uhaba wa maabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka jana matokeo ya mtihani wa Kidato cha IV yalipotoka, wanafunzi wengi katika Jimbo langu walifaulu somo la Biolojia, lakini cha kushangaza ni kwamba, shule nyingi hazina maabara. Nikauliza, hawa wamefaulu vipi? Nikalezwa kwamba, *marking skim* imekarabatiwa kwa wale ambao hawana *laboratory,* wao wanasahihishiwa tofauti, lakini walikuwa wamefaulu; tunawadanganya wanafunzi, tunadanganya Taifa; huwezi ukafundisha sayansi bila maabara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kutoa ushauri kwa Mheshimiwa Waziri, yeye ni Mwalimu wa Wahandisi, wanafunzi wake wote walikuwa wanapitia katika mikondo ya Sayansi na kwamba miaka mitatu au mitano au kumi atakayokuwa Waziri, ningependa akumbuke kwamba ni Waziri ambaye alisimamia masomo ya Sayansi na kwamba alijenga maabara na pia alitupatia Walimu wa Sayansi. Ujenzi wa maabara ni kitu ambacho hakiwezi kuepukika.

Mheshimiwa Spika, nimezungumzia habari za changamoto ya uhaba wa Walimu, nasema mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. Serikali ningependa kuipongeza kwa juhudi kubwa ambazo imefanya katika kutafuta jawabu la upungufu wa Walimu. Mikakati iko wazi ya kuzalisha Walimu wengi.

Mheshimiwa Spika, hapa tunazungumzia *quantity* lakini nafikiri sasa ni wakati muafaka wa kubuni sera za kujihakikishia kwamba tunataka Walimu walio bora na siyo bora Walimu. Imani ya wananchi wengi ni kwamba, vijana wetu wanajiunga na kozi za ualimu ni wale ambao wameshindwa kupata nafasi kujiunga na kozi nyingine.

Mheshimiwa Spika, busara ya kawaida na hekima ya kawaida yaani *common sense* inatuelekeza kwamba, mtu anayefaa kuwa Mwalimu ni yule ambaye yeye mwenyewe awe mwelewa, awe na taaluma na aweze kufundishika, awe na akili zinazochemka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hapo inabidi nitoe wazo kwamba, tufanye uamuzi wa makusudi kwamba tuweze kuwanasa wahitimu ambao wamedhihirisha kuwa na uwezo kitaaluma, tuwashawishi hao ndiyo wajiunge na vyuo vya elimu ili tupate *cream* ndiyo waende kufundisha.

Mheshimiwa Spika, kama wazo hili litakubalika na ningeomba Serikali ilikubali ni kwamba tutahitaji mageuzi makubwa sana katika sera ya ufundishaji, mazingira ya kuleta huo mchakato wa kuzalisha Walimu inahitaji uamuzi wa kijasiri. Tuangalie maslahi ya kuanzia wanachuo wanaotaka kuwa Walimu, hata mishahara na marupurupu watakapokuwa wamekamilika.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuwe na vivutio mbalimbali kama fursa za kujiendeleza na siwezi kuvitaja vyote. Yaani hivi vivutio viwe wazi na vioneshe upendeleo wa wazi kwa Walimu, vijana wetu wawaonee gere wale waliokwenda kujifunza ualimu, wapigane vikumbo yaani iwe taaluma *competitive*. Hilo ni wazo la pili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naishia kwa kuzungumza habari za *division number four*. Miaka ya nyuma matokeo yakitoka yalikuwa yanapangwa katika madaraja matatu yaani daraja la kwanza, la pili na la tatu, lakini hivi karibuni kuna daraja la nne.

Mheshimiwa Spika, matokeo yanapotokea Mheshimiwa Waziri anatangaza na karibu kila wakati anasema kuna kuongezeka kwa ufaulu, lakini ukiangalia kwa umakini na kwa undani kukiwa na ongezeko la ufaulu maana yake ni ongezeko la idadi ya wanafunzi wanakuwa *division four.*

Mheshimiwa Spika, matokeo yakitangazwa wazazi wanatamba wanakwenda vilabuni wanasema mtoto wangu amepata *division four* ya 29. Mwingine anasema mtoto wangu amepata *division four* ya 31 na yule wa *division four* ya 31 anaona ni kubwa kuliko ya 29.

Mheshimiwa Spika, wanaamini watoto wao wamekubuhu na ni wasomi na kesho yake wanakuwa wa kwanza kufika nyumbani kwa Mbunge kuona tuwatafutie kozi, wanaona wamesona na sasa

matatizo yao yamekwisha, kwa hiyo, tuwatafutie kozi wawe maofisa wakubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama tupo *serious* na kama tunataka maendeleo ya taaluma hapa nchini kusema kweli kigezo cha *division four* kitatupeleka pasipo. Kama tutaikumbatia *division four* kama ni ngazi ya ufaulu sidhani kama tutafika. Nataka kushauri kwamba tunapotathmini maendeleo ya taaluma yetu tuchukue *division one* mpaka three peke yake, ndiyo tuambiwe hii inakwenda vipi.

Mheshimiwa Spika, lakini na hawa wa *division four* na wenyewe tuelezwe, lakini kama kweli tunataka kujipima tuchukue *division one* mpaka *three*, tunaweza kuendelea na kutoa cheti cha *division four* ili kutambua kwamba walikwenda shule, lakini kwamba wamefaulu mimi siamini hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapo kwa kuunga mkono na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante na sasa nimwite Mheshimiwa Ritta Kabati atafuatiwa na Mheshimiwa Zabein Mhita.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Elimu Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa na nimpongeze Naibu Waziri Mheshimiwa Mulugo na Makatibu wa Wizara ya Elimu na watendaji wote wa

Wizara ya Elimu kwa kuwasilisha bajeti yao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nianze na shukrani. Kwanza kabisa niendelee kuwashukuru Mawaziri wa Wizara ya Elimu kwa sababu Iringa kulitokea tatizo kidogo katika Shule ya Sekondari ya Efatha. Kwa kweli kulikuwa na tatizo ambalo lilifanya mpaka watoto walitaka kuandamana, lakini nilipoliwasilisha Wizarani walilitatua kwa busara kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya wanasiasa walitaka wale watoto waandamane na kutokana na busara zao hapakuweza kutokea maandamano yoyote. Kwa hiyo, nawashukuru sana Wizara ya Elimu kwa busara kubwa ambayo walikuwa wameifanya na niwaambie watoto wengine wa shule wasiandamane kabla tatizo lao halijatatuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, niendelee kuwashukuru Waziri na Naibu Waziri kwa kuja kwao kushiriki katika tamasha lililoandaliwa na Masanja kwa ajili ya kuchangisha pesa ya watoto wanaosoma katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Naibu Waziri alikuja tukafanya lile tamasha katika uwanja wa Samora, ni tamasha ambalo lilifana sana na alichangia tukushukuru kwa mchango wako na vilevile ukachangia kwamba utatusaidia kuwasomesha watoto watatu wanaotoka katika Mkoa wa Iringa. Kwa hiyo, niendelee kukushukuru sana na niombe Mawaziri wengine waige mfano huo.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba tu ufafanuzi kutokana na ule mchango ambao alisema kwamba atatuchangia ili kuwasomesha watoto wetu watatu. Kumekuwa na utaratibu wa Serikali kuwasomesha watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu au watoto yatima kuanzia *form one* mpaka *form four,* basi! Lakini wakishafaulu kwenda *form five* na *six* au wakienda Chuo Kikuu wale watoto wanaanza kupata shida na wanaanza kutafuta wapi wasomeshwe.

Mheshimiwa Spika, leo hii ningependa kupewa ufafanuzi kwamba hawa watoto wakishafika *form five* na *form six* au kwenda Chuo Kikuu, je, uyatima unakuwa umeshakwisha au mazingira magumu sasa yanakuwa yamekwisha?

Mheshimiwa Spika, labda watakapokuwa wanajibu watueleze na hata pia Mheshimiwa Waziri pamoja na kuwa alisema kwamba atatusaidia kuwasomesha wale watoto labda atuambie pia na wenyewe wataishia wapi ili tujipange.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine labda niwaombe Wizara hii ijaribu kuangalia mgomo wa Walimu, Walimu kweli wanafanya kazi kwenye mazingira magumu sana. Wanapata mishahara midogo na wamekuwa wakilalamikia vitu vingi siku nyingi. Labda mngetumia busara kuhakikisha kwamba sasa hivi Walimu wetu nao wanatendewa haki ili hii migomo isiendelee kwa sababu inapoendelea hii migomo kikubwa tunaharibu Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, hili Taifa tunalipeleka wapi ambapo kutakuwa hakuna wasomi? Kuna mgomo baridi ambao unaendelea mpaka sasa hivi pamoja na kuwa Mahakama imesema kwamba huu mgomu uishe. Kwa hiyo, naomba pia hili liangaliwe ili Walimu wafanye kazi kwa kujitolea kutokana na kuboreshewa vitu ambavyo wanavitaka.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine labda nizungumzie Idara ya Ukaguzi. Hii Idara kwa kweli inafanya kazi katika mazingira magumu sana. Utakuta idara nyingi ambazo zipo hasa katika Halmashauri zetu wengi hawana vyombo vya usafiri na unakuta kwamba ramani ambazo zipo katika mkoa wetu wa Iringa ni ngumu kidogo kumfanya Mkaguzi aende akakague shule yake wakati hawana vifaa kabisa.

Mheshimiwa Spika, tunaomba pia iangaliwe sana hii idara pengine ikiwezekana wale waliopendekeza kwamba Idara ya Ukaguzi ijitegemee ingekuwa vizuri zaidi, kwamba ikapewa fungu lake nchi nzima ikafanya kazi kwa kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusiana na Shule za Kata. Kwa kweli niipongeze sana Serikali kwa hizi Shule za Kata, katika Mkoa wetu wa Iringa hizi shule zimetuokolea watoto wetu wengi sana. Watoto ambao kuna watu walikuwa wanawachukua baada tu ya kwamba hawana kitu cha kufanya na kuwapeleka kwenda kufanya kazi za ndani.

Mheshimiwa Spika, hiki kitu mimi kimekuwa kikinigusa muda mrefu na niishukuru Serikali kwamba angalau sasa hivi lile wimbi la watoto wa kike wanaotoka Iringa kwenda kufanyishwa kazi za ndani limepungua kwa kiasi kidogo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hiyo niwatangazie wale madalali ambao bado wamekuwa wakija kwenye shule zetu za Iringa na kuwachukua watoto ambao wamefaulu kwa kuwarubuni na kuwapeleka kwenye miji mikubwa kwenda kufanyishwa kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli naomba Serikali pia iwaangalie hawa watu kwa sababu watoto wetu wa Iringa wengi utakuta wanafanyishwa kazi za ndani. Huko wanapata mateso makubwa sana na wengine wanaletwa Iringa wameshapata UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba jambo hili Serikali iliangalie. Wakati mwingine tunapewa hata lugha za kudharaulika kwamba utakuta ukitaka kuaga unakwenda nyumbani, wanakwambia twende ukatutafutie Ma-*tx*, Ma-*tx* wakati hawajasoma? Naiomba Serikali na sasa hivi tuna utaratibu, tunataka tuuzindue Mfuko wa kuwasaidia watoto wa Iringa waweze kusoma.

Mheshimiwa Spika, nitaomba wananchi wote tusaidiane na kushirikiana ili kuhakikisha kwamba watoto wa kike wa Iringa sasa wanasoma, kama walikuwa wanaitwa Ma-*tx* basi wawe Ma-*tx,* kwa ajili ya elimu yao na siyo Ma-*tx* kwa ajili ya kudhaulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, naomba niseme kwamba, niko tayari kutafuta hata sensa kuangalia hawa watoto ambao wametolewa Iringa kwenye shule walikuwa wanasoma, lakini wamekwenda kufanyishwa kazi za ndani, tuone wako wangapi na wako kwa nani na wanafanya kitu gani kuhakikisha kwamba watoto wetu na nguvu kazi yetu sasa inarudi katika Mkoa wetu wa Iringa.

Mheshimiwa Spika, sisi tunapenda lakini, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Spika sisi kama akinamama wa Iringa na Njombe ameweza kuonesha mfano kwamba, akinamama wa Iringa tunaweza, kwa hiyo, hongera sana Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho nataka nipate ufafanuzi kuhusiana na *promotion*. Walimu wengi wamekuwa wakilalamika kwamba *promotion* zinacheleweshwa na wengine wanapata *promotion* lakini hawapati mishahara yao kwa muda unaotakiwa. Labda na hili pia liangaliwe kwani Walimu wengi wamekuwa wakilalamikia sana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kupata ufafanuzi ni kuhusu kufuta udahili Serikalini kwa elimu ya juu kupitia *mature age entry.* Ufutwaji wa huu udahili unawafanya Walimu wengi kukosa kwa sababu Walimu wengi walikuwa wanafundisha kwanza halafu baadaye ndiyo wanakwenda kusoma na utakuta kwamba wengine wanaweka akiba zao wanajisomesha wala

hawategemei mkopo kutoka Serikali wala sehemu yoyote.

Mheshimiwa Spika, labda na hii ingeangaliwa kwa sababu nimekuta Walimu wengi wanalalamikia kuhusu ufutwaji wa hu udahili ambao umefanyika na Serikali kwa mwaka ujao.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine nizungumzee kwamba, shule nyingi zimekuwa hazina vifaa hasa shule za Kata, hakuna vifaa vya kufundishia yaani Walimu hawana vifaa vya kufundishia wala wanafunzi hawana vitabu na vile vile kumekuwa hakuna mabweni kiasi kwamba watoto hasa wa kike ambao wanafaulu wanapata shida sana, wanahangaika wamefaulu lakini wanatoka sehemu za mbali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali ifanye utaratibu. Lakini niwashukuru sana wenzetu ambao wamekuwa wakichangisha pesa kwa ajili ya kujenga mabweni kwenye shule zetu za Kata.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, natoa wito kwamba tutakapochangishwa tuchangishwe sisi wazazi na viongozi tuunge mkono ili kuhakikisha kwamba watoto wetu sasa hivi wanaosoma kwenye Shule za Kata wakae kwenye mabweni ili iwasaidie hata katika ufaulu wao.

Mheshimiwa Spika, pia niipongeze Serikali kwa kurudisha mtihani wa *form two* na wa darasa la nne. Kwa kweli huu utatusaidia sana watoto wetu kujipima kwa sababu tumeona kwamba watoto wengi

wamekuwa wakimaliza shule wanakuwa hawana uwezo wa kusoma wala kuandika, lakini wakati ule ilipokuwepo hii mitihani ilikuwa inasaidia sana kuwezesha watoto kupimwa na wale wasioweza wanarudishwa. Kwa hiyo, nafikiri niipongeze sana Serikali kwa hatua ambayo wameichukua kwa sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Zabein M. Mhita.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii ya Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kondoa Kaskazini, naomba nitoe shukrani zangu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kufanya ziara ya kukagua chanzo cha maji cha mtaro wa Ntomoko na kutoa maelekezo na ahadi. Wananchi kwake yeye Mheshimiwa Waziri Mkuu wanamwambia, *jazakallah khaira*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba nimpongeze kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Kaimu Katibu Mkuu, Kaimu Kamishna wa Elimu, Wakurugenzi na Walimu wenzangu wote ambao wako katika Wizara ya Elimu kwa kutayarisha bajeti yenye matumaini na ya kisayansi. Vile vile naomba niwapongeze Walimu wote nchini kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba basi niombe ombi moja, hawa Makaimu katika Wizara, yaani Kaimu Katibu Mkuu na Kaimu Kamishna wa Elimu, tunaomba basi muwathibitishe kwa sababu hawa wana uwezo mkubwa, nawafahamu ili waweze kufanya kazi kwa kujiamini.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Kondoa Kaskazini kwa kushirikiana na Mbunge wao wameweza kuchangia kwa kiwango kikubwa sana katika ujenzi wa Shule za Sekondari. Mwaka 2006 kulikuwa na shule saba tu za sekondari lakini mpaka kufikia mwaka 2007 kukawa na ongezeko la Shule za Sekondari 25 kufikia shule 32. Juhudi kubwa imefanywa, lakini bado kuna upungufu mkubwa wa Walimu.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mfano, Shule ya Sekondari ya Sakami, mahitaji ni Walimu tisa, lakini waliopo ni wanne na kuna upungufu wa Walimu watano. Shule ya Sekondari Kinyasi; mahitaji tisa, lakini waliopo ni wanne, tuna upungufu wa Walimu watano.

Mheshimiwa Spika, pia Shule ya Sekondari Kikilo; mahitaji ni Walimu tisa, waliopo ni Walimu watano na upungufu ni Walimu wanne. Shule ya Sekondari Changaa; mahitaji ni Walimu tisa, lakini waliopo ni Walimu watano na upungufu ni Walimu wanne.

Mheshimiwa Spika, huo ni mfano tu, lakini sasa naomba nioneshe basi upungufu wa Walimu katika masomo yaani kimasomo hasa katika masomo ya Sayansi.

Shule za Sekondari zifuatazo hazina kabisa Walimu wa *Mathematics*, hakuna! Nazo ni Shule ya Sekondari ya Busi, Kinyasi, Kiteo, Loo, Mto Bubuna, Sakami, hawana kabisa Mwalimu wa *mathematics*.

Mheshimiwa Spika, shule zifuatazo hazina kabisa mwalimu wa *biology* yaani hakuna! Nazo ni Shule ya Sekondari Kikilo, Changaa, Dilai na Kalamba.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye somo la *Chemistry*. Shule zifuatazo hazina kabisa Walimu wa somo hili. Nazo ni: Shule ya Sekondari ya Busi, Changaa, Kalamba, Kikore, Kinyasi, Kisese na Masawi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upungufu huu wa Walimu ambao ni mkubwa na mimi nimesema natoa mfano tu. Iwapo kabisa Walimu wa masomo hayo hawapo tunategemea nini kwa matokeo? Ndiyo maana hata leo wakati vijana wetu wakizawadiwa sikushangaa kuona hakuna mtoto anayetoka Shule ya Sekondari Kondoa kwa sababu kuna upungufu mkubwa wa Walimu.

Mheshimiwa Spika, sasa je, Wizara ina mpango gani wa dharura wa upatikanaji wa Walimu wa masomo niliyoyataja ili wanafunzi basi waweze kunufaika na elimu wanayoipata? Tungependa watoto wetu wakimaliza masomo wanufaike basi na hiyo elimu, lakini kunufaika wakati Walimu hakuna kwa kweli ni ngumu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nioneshe upungufu mkubwa wa vitabu vya kiada katika shule zetu za sekondari na kwa kuwa mimi ni Mwalimu naomba nioneshe kiuwiano sasa kwa masomo. Uwiano wa mwanafunzi kwa kitabu, mfano somo la jiografia, kitabu kimoja wanachangia wanafunzi sita (1:6); *Englis,* kitabu kimoja wanafunzi wanne (1:4); *History*, kitabu kimoja wanafunzi nane (1:8); *Civics,* kitabu kimoja wanafunzi nane (1:8) na Kiswahili, kitabu kimoja wanachangia wanafunzi wanne (1:4).

Mheshimiwa Spika, huo upungufu ni mkubwa. Kwa hiyo, naomba basi Wizara ihakikishe kwamba vitabu vinapopatikana waweze kutuletea na sisi katika Wilaya yetu ya Kondoa ili wanafunzi hawa waweze kupata basi taarifa zilizopo kwenye vitabu hivyo na pia wanapopewa mazoezi na walimu wao waweze kuyafanya kwa kutumia vitabu kwa sababu shule zetu nyingi ni za *day*, baada ya masomo wanafunzi wanakwenda nyumbani, siyo rahisi kuchangia vitabu wakati watoto wanasoma katika shule za kutwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna upungufu mkubwa sana wa nyumba za Walimu pengine ndiyo maana hata hawa Walimu wanapofika katika maeneo hayo, wanaondoka. Lakini hata hivyo, wananchi wanajitahidi sana kuchangia ujenzi wa nyumba za Walimu. Vile vile wanajitahidi sana kutafuta nyumba ambazo Walimu hawa wanaweza wakakaa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuonesha upungufu huo wa Walimu nisiwe mwizi wa fadhila kwa sababu mwaka uliopita upungufu wa Walimu ulikuwa mkubwa sana kuliko ulivyo hivi sasa. Kwa hivyo, nasema tu, naishukuru Wizara kwa kweli walisaidia, lakini basi Mheshimiwa Waziri, mdogo wangu Dkt. Shukuru Kawambwa, naomba watusaidie kutuongezea walimu na nina imani nikiwa Mwalimu mwenzenu mtanisaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikaa pale Wizara ya Elimu miaka kumi.

**SPIKA:** Kama Naibu Waziri wa Elimu. (*Kicheko*)

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, Wizara hiyo mimi nimelelewa hapo kwa miaka mingi nisingependa kutumia muda mrefu. Niwatakie Watanzania Iddi El-fitri njema, *Inshallah*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia machache katika Wizara hii muhimu sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijasahau, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Naibu Waziri wa Elimu kwa kazi nzuri anayoifanya ya kukagua shule zetu. Naiomba Wizara pamoja na Waziri waendelee kumpa nguvu za kutosha na niunganishe hapo

kwamba kile Kitengo cha Ukaguzi kiweze kupewa fedha nyingi ili kazi anayoifanya Naibu Waziri iwe rahisi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu nakumbuka zamani wakati tunasoma kitengo hiki kilikuwa kinafanya kazi vizuri sana. Walikuwa wanakuja madarasani wanasikiliza walimu wanavyofundisha, wanaangalia miandiko yetu tunaandika vipi na kuona jinsi wanafunzi wanavyoendelea kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vizuri kile kitengo kiongezewe fedha kiweze kufanya kazi vizuri na hata huu upungufu mwingine unaojitokeza sasa hivi naamini kitengo hiki kikiwezeshwa na kupewa fedha za kutosha hayatajitokeza na itaweza kuwabana hata wale Walimu ambao hawafuati taratibu zao za kazi na kuweza kuboresha elimu yetu.

Mheshimiwa Spika, tunajua elimu ni ufunguo wa maisha na ndiyo urithi pekee ambao tunaweza kutoa kwa watoto wetu, lakini elimu yetu sasa hivi inakokwenda ni kubaya. Sasa umefika wakati tujadiliane na mwisho tukubaliane tujue ni tatizo gani linaloikumba elimu yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, inawezekana upo upungufu mwingi kuhusiana na kwa nini watoto wetu hawaelewi, *either* ni msongamano wa wanafunzi madarasani au ni uhaba wa Walimu au vitendea kazi ni vichache, nafikiri yapo mambo mengi ambayo yanasababisha elimu yetu inazidi kushuka.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu tukayazungumza, tuache kuwa na majibu rahisi kwa maswali magumu kwa sababu tunatafuta sababu kwa kufikiri kwamba, ni mgomo Walimu wamegoma na kuwalazimisha warudi kazini, mimi sioni kama hili jambo ni muafaka. Ni vizuri tukazungumza, tukawasikiliza Walimu wetu, tukajadiliana nao na tukajua tatizo ni nini na tuweze kulitatua kama nilivyosema hapo mwanzo.

Mheshimiwa Spika, tumewasikia Walimu kwenye vyombo vya habari wakisema wanarudi kazini kwa kinyongo. Sasa sitegemei kama watakwenda kufundisha watoto wetu. Kutakuwa na mgomo baridi unaoendelea na hili litalipeleka Taifa letu kuwa Taifa la wajinga.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri tukazungumza, tukatatua matatizo haya niliyokwishayasema ili watoto wetu waweze kupata elimu bora ambayo itawasaidia katika maisha yao. Kama nilivyosema urithi pekee tunaoweza kutoa kwa watoto wetu kwa sasa ni elimu bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niongelee suala la sensa. Tarehe 25 na 26 mwezi huu zoezi la sensa litafanyika katika nchi yetu. Mwanzo tulijua Walimu watashiriki lakini kwa dhamira njema Serikali inadai kwamba waliamua kuwapa wanafunzi waliomaliza *form four* na kidato cha sita angalau nao waweze kupata fedha za kujikimu.

Mheshimiwa Spika, sina tatizo na hilo, hoja yangu ni kwamba, wanafunzi wamekwenda likizo mwezi wa Sita na sasa hivi ninavyozungumza wanafunzi hao wako likizo tena na tumeambiwa kwamba Walimu siyo wote watakaoshiriki kwenye zoezi hilo.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali itahakikishaje wale waliokosa masomo kwa kipindi cha mwezi mzima wanafidiwa hasa kwa wale wanaomaliza darasa la saba na kidato cha nne hasa ikizingatiwa kwamba watafanya mitihani hivi karibuni ya kumaliza darasa la saba na kidato cha nne? Je, watafidiaje masomo yao?

Mheshimiwa Spika, jana nilisikitika sana kuna Mbunge mmoja alichangia hapa Bungeni akasema mgomo wa Walimu umewasababishia wao kutoshirikishwa kwenye sensa. Sasa naitaka Serikali itwambie hivi aliyoyasema ni kweli au ni masuala yake binafsi. Kwa sababu kama ni kweli mtakuwa hamkuwatendea haki Walimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kumaliza suala la sensa, naomba nizungumzie mimba za wanafunzi kwa shule za msingi na sekondari. Hili limekuwa ni tatizo kubwa katika familia zetu, watoto wengi wa kike wamekuwa wakishindwa kuendelea na masomo yao. Bunge lililopita iliundwa Kamati hapa wakati huo Mama Sitta akiwa Waziri wa Elimu kwa lengo la kupita na kuchukua maoni ya wadau kuhusu kuwaruhusu watoto hawa wa kike waweze kuendelea na masomo.

Mheshimiwa Spika, binafsi ningeona sasa ufike wakati tuwaruhusu watoto hawa wa kike waendelee na masomo kwa sababu tukiendelea kuwaacha huko mitaani kwanza wameshakosa elimu, ameshafunzwa kwa kupata mimba, naamini kwa wale watukutu kama ni tabia yao wataendelea, lakini wale wachache ambao naamini watajutia kosa walilofanya hawatarudia na watajifunza kutokana na makosa.

Mheshimiwa Spika, ningeiomba Serikali ufike wakati sasa tuwahurumie watoto hawa. Pia itapunguza tatizo la utoaji wa mimba, kwa sababu wengi wanapojua kwamba hawataendelea na masomo wanakimbilia kwenda kutoa mimba na matokeo yake anakufa yeye na kile kiumbe hai ambacho hakina makosa hapa duniani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niiombe Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayojiita sikivu, basi isikie na hiki kilio cha watoto wa kike waweze kurudi shuleni.

Mheshimiwa Spika, niongelee suala la matatizo ya Walimu. Toka jana nasikiliza Wabunge wakichangia, wengine wanayasema matatizo lakini wengine wanasema suluhisho la matatizo ya Walimu siyo mgomo. Siungi mkono mgomo, lakini ufike wakati sasa tusikilize matatizo ya Walimu hawa. Leo ukiangalia mshahara wa Mwalimu wa kawaida ni shilingi 200,000/= kwa mwezi. Hivi shilingi 200,000/= kwa mwezi utaifanyia nini?

Mheshimiwa Spika, ada ya watoto wa shule wenyewe tunajua tunavyosomesha watoto. Walimu hawa wanapanga na kodi ya nyumba iko juu kweli kweli, usafiri uko juu, lakini wakilalamika wanaambiwa kwamba kuna *messages* zinatumwa, kuna watu wanawashawishi Walimu wagome.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iangalie matatizo haya ya Walimu wetu, tuyafanyie kazi. Tukae mezani tuzungumze na Walimu hawa na naamini kabisa watafanya kazi kwa dhamira nzuri, waipende kazi yao na wasifanye kazi kwa kinyongo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yamesemwa kwa muda mrefu sana lakini sasa ufike wakati Serikali na Wizara husika wahakikishe kwamba madeni ya Walimu yanalipwa ili tuanze ukurasa mpya. Mheshimiwa Susan Lyimo, amesema hapa kwamba ni vizuri tukajua ni madeni gani yanayodaiwa kwa sasa kwa sababu leo tunasikia Wizara inasema yalishalipwa, Walimu bado wanaendelea kulalamika kwamba hawajalipwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa manung'uniko yote haya ni vizuri tukaja na mahesabu yaliyo sahihi, yaliyohakikiwa na tumalize matatizo haya ya walimu, wana haki ya kudai na kama tunavyojua wote tuliofika hapa tumepita madarasani na Walimu wametufundisha na leo tuko hapa Bungeni. Ni lazima tuwajali Walimu kwani bila Walimu tutakuwa na Taifa la watu wajinga. Kwa hiyo, tusikilize kero zao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Azza Hillal Hamadi, hayupo! Nitamwita Mheshimiwa Said Mtanda, naona hayupo pia. Nitamwita Mheshimiwa Dkt. David Mallole na Mheshimiwa John Mnyika atakuwa wa mwisho.

**MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja ya Wizara ya ELimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, katika nafasi hii naomba nizungumzie hasa kuhusu shule kongwe zilizoko katika Jimbo la Dodoma Mjini ambazo ni shule ya Sekondari ya Msalato pamoja na shule ya Sekondari ya Bihawana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, shule ya Sekondari ya Msalato ilijengwa na Kanisa la Anglikana mwaka 1961 wakati huo ikiitwa Mvumi *Girls Middle School*. Baadaye mwaka 1970 ilitaifishwa ikawa ni shule ya Serikali na shule ya Kitaifa na imekuwa wakati wote ikijitahidi kuchukua watoto wenye vipaji maalum.

Mheshimiwa Spika, mara ya kwanza halikuwa tatizo kubwa sana shule ilipokuwa imeanza, maana idadi ya wanafunzi ilikuwa ni ndogo hakukuweza kujitokeza upungufu wowote mkubwa. Lakini kadri idadi ya wanafunzi ilivyozidi kuongezeka na matatizo

nayo yakaanza kuongezeka. Kumejitokeza upungufu mkubwa sana wa miundombinu kwa maana ya majengo na hasa upande wa vyoo, mashimo ya vyoo yako machache sana ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi iliyopo pale.

Mheshimiwa Spika, matatizo makubwa yafuatayo ningeomba Wizara hii ijaribu kuyaangalia kwa karibu sana:-

Tatizo la kwanza, ni lile la wigo wa shule. Shule ya Sokondari Msalato ina eneo kubwa sana lipatalo kama hekta 29.5. Kujenga wigo wa eneo kama hilo ni kazi moja kubwa sana. Katika makisio ambayo yalifanywa mwezi Mei mwaka 2011 ilionekana kwamba ili wigo huo uweze kujengwa kunahitajika fedha taslimu isiyopungua sh. 267,529,950/= Wigo wa shule ya Sekondari Msalato una umuhimu ambao ni mkubwa sana kwa sasa hivi hasa kwa sababu mji umepanuka na nyumba nyingi sana zimeshasogea karibu na shule.

Mheshimiwa Spika, matatizo makubwa inayoyapata shule ya Sekondari Msalato ni pamoja na kuingiliwa kwenye mabweni yao wakati wa usiku. Mengine ni wizi na utoro. Tunafikiri kwamba hali kama hii ikiendelea haiwezi kuiweka mahali pazuri shule yetu ya Sekondari ya Msalato yenye historia ndefu iliyotukuka, maana kwa kweli imeweza kutoa viongozi wengi sana wa nchi hii ambao wamepitia katika shule hiyo. Ni vizuri tukajitahidi kuisaidia shule hiyo ili iweze kupata wigo.

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba inawezekana bajeti hii ikawa ni *tight* ambayo pengine haikuweza kufikiria masuala ya wigo wa shule hii ya Msalato, lakini kutokana na umuhimu wake naomba sana Wizara iangalie kwa ukaribu sana hata kutafuta njia nyingine ambazo zinaweza zikasaidia wigo huo ukajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wetu sasa hivi wamechoka na michango na fedha hizi ni nyingi mno sh. 267,529,950/=, ni fedha nyingi hata kama tukisema kwamba wachangie wananchi hawataweza. Namwomba Mheshimiwa Waziri, Wizara yake itafute akili yoyote inayowezekana hata kama ni kwa njia ya michango ambayo inaweza ikaongozwa na Waziri Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, akisaidiwa na ndugu yetu pale Naibu Waziri Mheshimiwa Philip Mulugo, waendeshe basi michango hiyo ili fedha hii iweze kupatikana na wigo huo uweze kujengwa kwa ajili ya usalama wa watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, kuna wengine wanakuwa na dhamira ya kufikiri tu kwa sababu tu ni watoto wa kike hata kama ukiingia humo watakufanyaje. Lakini nashukuru siku moja fundisho ambalo mtu mmoja aliwahi kupewa na watoto wa kike, kwa hiyo na wao hata wenyewe si watu wa kuwadharau, ni watu wenye nguvu.

Mheshimiwa Spika, siku moja waliweza kutoa fundisho kwa kijana ambaye alikuwa ameingia hapo na nadhani kwa kiasi fulani waliambizana kwamba hawatarudia tena lakini bado tatizo hili linasonga

mbele siku hadi siku na mwisho litakuwa kubwa sana. Kwa hiyo, naomba sana mliangalie sana suala la wigo wa shule ya Sekondari Msalato tuweze kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, suala lingine la pili linahusiana na maji. Shule imeshakuwa kubwa na kuna matatizo makubwa sana ya maji. Tulifikiri kwamba ujaribu kuangalia uwezekano wowote wa kuwachimbia hata kisima cha maji. Shule inajitahidi kutumia fedha ya matumizi ya kila mwezi isiyopungua sh. 1,600,000/= kwa ajili ya matumizi ya maji tu pale kwenye shule ya Sekondari, kwa matumizi ya kila siku ya wanafunzi pamoja na Walimu.

Mheshimiwa Spika, kama kisima kingeweza kujengwa pale na wameshakiwekea makisio si zaidi ya shilingi milioni 30, nadhani kingekuwa ni ukombozi mkubwa sana na kusingekuwepo tena na sababu ya kurudia rudia kila wakati kuzungumzia habari ya maji pale Msalato kama kisima cha maji kitaweza kuchimbwa kwa ajili yao.

Mheshimiwa Spika, Sekondari ya Msalato ilikuwa na gari la kuwasaidia vijana wakati wanaugua usiku kwa kuwakimbiza hospitali. Pia ile gari iliweza kuwasaidia kwa safari za hapa na pale mjini. Gari limeharibika na matengenezo yake yanahitaji si chini ya shilingi milioni 10. Naomba pia hilo mliangalie ili muweze kuona mtawasaidia vipi.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa upande mwingine lipo tatizo la shule kutokuwa na hatimiliki (*title deed*). Suala hili la kukosa hatimiliki baadaye nina hofu

linaweza likaja kuleta madhara pale shuleni kwa maana ya kwamba ukikutana na watu ambao ni wabishi sana wanaobisha kwamba mpaka wako uko wapi, hebu tuoneshe hati, wanazidi kusogea zaidi kuingilia eneo la shule, kumbe kama Wizara ingesaidia kuwapatia *title deed,* basi shule ingeweza ikajua jinsi ambavyo wangeweza kujitahidi kulinda eneo lao lisiendelee kunyemelewa zaidi na zaidi. Hii ni shule moja ya Sekondari ya Msalato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kuna shule ya pili inaitwa Bihawana Sekondari na yenyewe haiko mbali ukitoka hapa iko upande wa Kusini mwa mji. Shule hii yenyewe ilijengwa mwaka 1961 na ilijengwa na Padri mmoja ambaye sasa ni marehemu Padri Jiovan Vilidi maarufu kwa jina la Padri Yohanne kama wanavyomfahamu kule Bihawana. Hata yenyewe kipindi kile mwaka 1961 idadi ya wanafunzi ilipokuwa bado ni ndogo hakukuweko na matatizo lakini baada ya kutaifishwa kwenye miaka 1970 idadi ya wanafunzi ilizidi kuongezeka na matatizo yako mengi kwa upande wa miundombinu, lakini wameomba niwazungumzie zaidi kuhusu suala la maji.

Mheshimiwa Spika, maji Bihawana Sekondari ina matatizo, wanafunzi wanaweza wakakaa hata muda wa siku tatu bila kuoga na kama mtu haogi maana yake pia hana uwezo hata wa kufua nguo zake na wakati kumbe hizi shule za Kitaifa tunategemea kwamba ndio zinakuwa kitovu cha ustaarabu. Watoto wajifunze ustaarabu hata wanaporudi kijijini wakawahimize wanakijiji namna wanavyoweza kutumia maji, kuweza kuhifadhi afya zao, waoge,

wafue nguo waonekane kwamba ni nadhifu lakini sasa inaanza kuwa ni kinyume chake watu kujifunza kukaa hapa zaidi ya siku bila kuoga. Sasa hatuelewi watakaporudi kijijini watakwenda kuwaelimisha nini wanakijiji iwapo wao wenyewe wamezoea kukaa hapa kwa muda wa siku tatu pasipo kuoga?

Mheshimiwa Spika, zoezi lilitumika kuweza kuigawa ile shule ikaanzishwa Shule ya Mbabala Sekondari angalau kupunguza shehena ya wanafunzi pale lakini hata kule Mbabala Sekondari na kwenyewe taabu ni hiyo hiyo, hakuna maji watu wanakaa muda mrefu sana bila ya kuoga au bila ya kufua nguo. Ninaomba hizi shule hasa hizi kongwe, Msalato, Bihawana pamoja na sasa Mbabala ambayo imechepuka kidogo baada ya wanafunzi kufurika pale Bihawana, zote ziangaliwe kwa ukaribu sana hasa katika matatizo ya maji lakini Msalato Sekondari iangaliwe zaidi kuhusu tatizo la wigo wa shule na shule ambazo hazina *title deeds* pia na zenyewe ziangaliwe ziweze kupewa *title deeds* ili maeneo ya shule yaweze kulindwa vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia, nawashukuruni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa John Mnyika ndio msemaji wetu wa mwisho.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, lakini katika siku hizi za mjadala huu nimekuwa nikipokea ujumbe kutoka Jimboni, Walimu, wanafunzi, wazazi wakisema kwamba nikichangia nisiunge mkono hoja mpaka Serikali iweze kushughulikia

madai ya msingi ya Walimu, wafanyakazi na uboreshaji wa elimu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna jambo moja ambalo mara nyingine huwa inabebeshwa mzigo mkubwa sana Wizara ya Elimu ambayo kwa kweli mzigo huu ulipaswa kubebwa na Wizara nyingine. Tunajadili leo Wizara ya Elimu ikiwa tayari tumekwishapitisha bajeti kuu ya nchi, tayari tumeshapitisha bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo ina TAMISEMI ambayo sehemu kubwa ina mzigo mkubwa wa elimu na tumekwishapitisha vilevile bajeti ya Ofisi ya Rais ambayo ina Menejimenti ya Utumishi wa Umma inayoshughulikia masuala ya wafanyakazi ikiwemo masuala yanayohusu Tume ya Walimu na Utumishi wa Walimu.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu, michango yetu mingi tunayoitoa kwa kweli ni ushauri tu wa Serikali kwa siku zijazo, lakini maamuzi ya msingi yalikwishafanyika. Pengine mjadala huu wa leo na mjadala wa jana uwe fundisho kwetu inapokuja bajeti kuu ya Serikali badala ya kukimbilia kupiga kura ya "Ndio" tuungane pamoja kupiga kura ya "Hapana pale bajeti kuu inapokuwa haijatimiza vipaumbele vya msingi vya kulikomboa Taifa kwenye sekta za msingi za Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siungi mkono bajeti hii iliyoko hapa mbele.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri kwenye majumuisho, kwa kuwa kilio kikubwa cha Wabunge wengi ni kwamba kuna ufinyu wa bajeti kwenye sekta ya elimu kwa kushauriana na Wizara ya Fedha, Serikali ikubali ili kutushawishi kuunga mkono, Serikali ikubali kutoa *commitment* kwa kuwa keshokutwa tunakwenda kujadili Muswada wa Sheria ya Fedha na kwa kuwa kwenye Mkutano huu wa Bunge tumetoa mapendekezo mbalimbali ya kupanua wigo wa vyanzo vya mapato kwa Serikali, tukishapitisha Muswada wa Sheria ya Fedha tukiongeza kiwango cha fedha, Serikali itoe *commitment* leo kwenye majumuisho kwamba iko tayari kuleta bajeti ya nyongeza kwa ajili ya Wizara ya Elimu ili kuboresha maslahi ya Walimu, kuboresha mazingira ya shule zetu ili kuboresha elimu kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wanasayansi wana msemo kwamba, "Palipo na msuguano pana mwendo". "*Where there is a friction there is movement".* Ukitazama historia ya Taifa letu kuliwahi kutokea misuguano na misuguano ikaleta mwendo. Mwaka 1966, wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam waligoma. Wakati huo baada ya uhuru, matarajio ya uhuru yalikuwa yanaelekea kupotea, kukazalishwa kizazi cha wakati huo kilikuwa kinaitwa kizazi cha Mabenz yaani wanatembelea Ma-*benz*.

Mheshimiwa Spika, Wazee hapa wengine waliona, sisi historia tunazisoma, wazee hapa watathibitisha, kizazi cha Mabenz kwamba wale wana maisha mazuri sana, wanatembelea Mabenz, lakini wale waliopigania

uhuru, wakavuja jasho wana hali ngumu. Wanafunzi wakati ule wakaanza msuguano na Mwalimu Nyerere aliitikia msuguano ule kwa kwenda kuzungumza na wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kauli ya mwanzo mwanzo sana Mwalimu Nyerere aliitoa wakati ule akasema, wanafunzi walikuwa wanadai maslahi, wanafunzi walikuwa wanalalamikia waliopo kwenye utawala wanajipendelea.

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Nyerere akasema: "Mnadai mishahara, mnadai maslahi, mnawalalamikia watawala wanavyojipendelea naanza na mimi mwenyewe, nakata mshahara wangu". Mwalimu Nyerere akakata mshahara wake akitaka kujenga msingi wa kujali pengo lililokuwa linajengeka kwenye Taifa na msuguano ule wataalamu wengi wa historia wanakubali kwamba kati ya mambo ambayo yalimgusa Mwalimu wakati anatangaza Azimio la Arusha ni pamoja na yale mazungumzo ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, sasa kizazi cha leo tumefika mahali ambapo matabaka haya yanaongezeka, migogoro imeongezeka, tofauti ya wakati ule waliokuwa wanazungumziwa wanaitwa Ma-*benz* siku hizi wanaitwa Mashangingi, hali ileile imekuja. Mimi naomba Serikali izisome hizi alama za nyakati, unaposikia wanachuo wanagoma, unaposikia Walimu wanagoma, usidhani kwamba hawa ni watu wasiokuwa na akili timamu, hawana mwelekeo lakini Serikali isikilize sauti za wananchi, Serikali ichukue hatua.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa wito kwa Serikali iwarudishe wanafunzi 25 waliosimamishwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mwalimu Nyerere angewafukuza akina Samwel Sitta walipogoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam leo wasingekuwa Mawaziri. Serikali isikie sauti, Rais aisikie sauti, awarudishe hawa wanafunzi wa Kitanzania wamelizie elimu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kidogo kuzungumzia kuhusu mgomo wa Walimu na kauli ya Serikali iliyotolewa Bungeni tarehe 10 Agosti, 2012. Ukipitia hukumu ya Mahakama, sina sababu ya kuingilia uhuru wa Mahakama, utabaini kwamba katika hatua iliyofikia hivi sasa, mgogoro huu na matatizo haya yaliyopo hayataweza kusuluhishwa kwa majadiliano ya pande mbili ambazo tayari zilishasajili kwa Msuluhishi kwamba zimeshindwa kukubaliana bila upande wa tatu kuingilia kati kwenye majadiliano.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu, Ibara ya 63, Bunge ndio chombo kikuu kwa niaba ya wananchi kuishauri na kuisimamia Serikali. Sasa kwa kuwa Mahakama imetamka kwamba majadiliano yanayoendelea yafanyike chini ya Washauri wa Masuala ya Kazi au Wataalamu wa Masuala ya Kazi. Mimi napendekeza Bunge lako Tukufu litumie madaraka yake kwa Ibara ya 63 ili wale washauri wa kwenda kusimamia majadiliano wateuliwe na Bunge au wateuliwe na Kamati husika ya Bunge kwa kuwa Serikali imekwishashindwa kupatana na Walimu na chanzo cha migogoro iliyopo ni bajeti ya Serikali na Bunge ndio lenye wajibu kwa niaba ya wananchi kupanga matumizi ya fedha, kupanga vipaumbele lina

uwezo wa kuamua kuelekeza nguvu kwa masuala haya ya kutatua mgogoro.

Mheshimiwa Spika, napenda vilevile kupata kauli ya Serikali kwa sababu katika kipindi hiki cha mgomo pamoja na masuala yanayohusu CWT, Serikali vilevile nayo watumishi wake, watendaji wake wameelezwa kuwa walikiuka Ibara ya 4 na Ibara 107 katika kipindi cha mgomo. Ningetaka kauli ya Serikali, inachukua hatua gani kwa watumishi wake na watendaji wake waliokiuka Katiba ya nchi katika kipindi cha mgomo.

Mheshimiwa Spika, nimesoma hotuba ya Waziri na naunga mkono na siku zote naunga mkono ujenzi wa Chuo cha Muhimbili maeneo ya Kwembe Mloganzila lakini nasikitika kwamba kiwango cha fedha kilichotengwa ni kidogo, kwa sababu kwa mujibu wa Mpango huu wa Taifa wa Miaka Mitano kwa mwaka huu wa fedha Serikali ilipaswa kutenga shilingi bilioni 10 kwa ajili ya miundombinu ya barabara, maji na miundombinu mingine ikiwemo umeme, pale maeneo ya Kwembe Mloganzila. Kwa hiyo, naomba Serikali itoe kauli kwa nini isiongeze kiwango hiki ili ahadi ile iweze kutekelezwa kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, lakini mwaka jana nilitahadharisha Serikali kuhusu fidia ya ardhi ya wananchi pale Kwembe Mloganzila lakini katika kipindi hiki cha utekelezaji Serikali ambayo Mawaziri wake walikwenda kuwaahidi wananchi kuwa watalipwa fidia ya ardhi huku kukiwa na kesi mbili Mahakamani, Serikali imekwenda kuwavunjia wananchi na sasa hivi ninavyozungumza kuna Wakimbizi wa ndani yaani

*Internal Displaced Person,* wako pale Kwembe, Wakimbizi ndani ya Tanzania. Naomba kauli ya Serikali ambayo Mawaziri wake walikwenda kuwaahidi wale wananchi, ni misaada gani ya kibinadamu ambayo Serikali imeshapeleka mpaka sasa kwa matokeo ya Serikali kutumia Kampuni ya Madalali kesi ikiwa Mahakamani kwenda kuwavunjia wananchi. Mheshimiwa Waziri mimi nisipopata kauli ya Serikali nitakwenda kuwaeleza wale wananchi pengine waje Ofisini kwako ili wawe Wakimbizi kwenye ofisi yako au ofisi za Wizara kwa sababu Serikali ndio imesababisha hali inayoendelea pale Kwembe.

Mheshimiwa Spika, napenda vilevile kupata kauli ya Serikali kuhusiana na mgogoro kwenye Shule ya Sekondari ya Mburahati, sekondari ambayo inasomewa kwenye shule za msingi na kuna mawazo ya aina mbili yanayokinzana na kwa mwaka mzima yanakuwa yanaendelea kukinzana, ama kuigeuza ile shule ya msingi kuwa ya Sekondari au Serikali kwa kushirikiana na Manispaa ya Kinondoni kupata eneo mbadala.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, michango ni mingi sana tu. Kila mtu anasema fedha hazitoshi, hazitoshi, sasa nyie wenyewe mlipitisha makadirio hapa. Sasa inatakiwa Waheshimiwa

Wabunge kama tulivyosema tuangalie utaratibu wetu wa kupitisha bajeti kwa sababu mkiwa mnasema *value* inaonekana *endless* yaani inatakiwa sijui iweje, hakuna Wizara hata moja ambayo hamkusema kwamba fedha haitoshi, hata moja na *priority* mlijenga wenyewe. Kwa hiyo nadhani ile hoja yetu ya kuanza utaratibu mpya, nadhani ni muhimu zaidi sasa kuliko wakati mwingine wowote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, saa hizi tunaomba Wabunge wote waende kwenye Ukumbi wa Msekwa kwa sababu tuna kile kikao cha *CPA*, ni kama kikao maalum kuweza kuelezwa juu ya *CPA* na kama nilivyosema wote ni Wajumbe.

Saa 10.00 jioni tutaendelea na baadaye saa 12.30 tutakuwa na futari hapahapa katika maeneo ya Bunge, tunajaribu kuona kama wageni wamezidi basi tutachukua uwanja mkubwa, kama hawako wa kutosha basi tutakuwa *basement*, lakini mtaona wapi pa kufanya.

Kwa hiyo naomba nisitishe shughuli hizi mpaka saa 10.00 jioni.

*(Saa 7.15 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Mussa Z. Azzan) Alikalia Kiti*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MARGARET A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania sasa imeamua kueneza vyuo vya ufundi vya *VETA* kila Wilaya ya nchi. Sasa kwa vile watoto na wanafunzi wenye mahitaji maalum (wenye ulemavu) wanapata matatizo katika ajira rasmi hata kwa wachache wanaokidhi vigezo, nashaurri kila Wilaya itenge asilimia maalum kwa ajili ya kudahili wanafunzi wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, hii itasaidia kuwapa fani na ujuzi katika aina fulani ya ufundi na hatimaye kuweza kujiajiri wenyewe. Nafahamu kuna vyuo vya wenye ulemavu pekee lakini ni vichache kwa nchi nzima hivyo kuwa mbali kufikiwa na wenye ulemavu tulionao nchini. Kwa msingi huo, Wizara ihakikishe kuna zana za kufundishia na kujifunzia wenye ulemavu, Walimu wenye taalum husika, matumizi ya lugha ya alama kwa viziwi na kadhalika ili hatimaye waweze kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile elimu ya juu sasa inagharamiwa kwa mikopo ya wanafunzi, nashauri wanafunzi wenye ulemavu na wale wanaotoka kwenye familia za wazazi wenye ulemavu, wapewe kipaumbele katika kupata mikopo asilimia mia moja toka Bodi ya Mikopo kutokana na hali ya umaskini inayowazunguka. Wenye ulemavu walio wengi hawamudu gharama hizo kwa kuwa wanafunzi hawa sio wengi katika vyuo vikuu. Naiomba Serikali ione uwezekano wa kuwasomesha bure kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile elimu maalum ina changamoto nyingi hapa nchini, naishauri Idara ya Elimu Maalum iliyo chini ya ofisi ya Kamishna wa Elimu sasa iundiwe kurugenzi ambayo itatengewa kasma yake na kufanya maamuzi ya masuala ya wenye ulemavu kwa wakati muafaka kuliko ilivyo sasa.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Wilaya yangu ya Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Shukuru Kawambwa kwa hotuba nzuri na yenye uchambuzi wa kina ambayo imetolewa asubuhii ya leo. Jitihada zinazofanywa na Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni za hali ya juu na zinastahili pongezi. Ni kwa msingi huu, nachukua fursa hii kutamka kwamba naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, napenda kumpongeza Mheshimiwa Philip Augustino Mulugo, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Mbunge wa Songwe, kwa kazi nzuri ambayo anaifanya katika Wizara jambo ambalo limeleta heshima kwa Wizara na kuimarisha ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue fursa hii kuomba Wizara ikumbuke kwamba tuliwahi kuteua shule mbili katika Halmashauri ili zisaidiwe kukamilisha miundombinu kama vile maabara, madarasa, *library* na kadhalika. Shule hizi ni shule za sekondari za Kishisha na ile ya Sekirari. Ni vyema Wizara ikatufafanulia suala hili kwani wananchi wengi hawajui ni nini kilichotokea

na hivyo kusababisha fedha za kutekeleza mradi huo zisitolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE.AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuchangia maeneo kadhaa ambayo sikuweza kuwasilisha kwa mdomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ione namna ya kurudisha *TSD* ambayo ni Tume ya Utumishi ya Walimu ambapo kwa sasa ni idara chini ya Tume ya Utumishi wa Umma. Zamani ilipokuwa *TSD* ilikuwa inafanya vizuri kuliko ilivyo sasa. Hali hii ya Walimu kutokuwepo kwenye mwamvuli mmoja inasababisha kuwepo kwa mlundikano wa madai ya Walimu kwa mfano *TSD* wanapandisha madaraja Walimu na wanakuwa hawalipwi stahili ya mishahara yao mipya kwa sababu wanaopanga bajeti ya wangapi watalipwa na shilingi ngapi ni Wizara nyingine nje ya *TSD* ambazo ni Wizara ya Elimu na TAMISEMI. Ni vema sasa *TSD* irudishwe Wizara ya Elimu ili mgongano huu usiendelee kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iangalie pia namna ya kurekebisha mihula yetu. Mihula ya Kidato cha Kwanza na Darasa la Kwanza ni vema ianze JanuarI na Kidato cha Tano ianze mwezi Julai kama tulivyokuwa tunafanya zamani. Vyuo vya Ualimu, Cheti na Diploma nao waanze mwezi Julai. Hii itasaidia kutumia muda wao vizuri badala ya ilivyo sasa ambapo Kidato cha IV wanasahihisha Novemba na

Disemba. Kidato cha VI wanasahihisha mwezi Machi, Vyuo, Cheti na Diploma wansahihisha Juni na Julai. Kwa mtitiriko huo unakuta takribani miezi mitatu Walimu wazuri wa sayansi wote wanakuwa wanakwenda kusahihisha mitihani ilihali tunalalamika hatuna Walimu wa kutosha! Ni vema hao tulionao tukawatumia vyema, hivyo mitihani ifanywe kwa kuziangatia mihula na mapumziko ya Julai na Desemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo cha Ukaguzi bado madai yao hayajalipwa, wakiuliza wanajibiwa madai hayakuhakikiwa. Hii inawafanya kuwa wanyonge wanapolinganisha na Walimu wengine. Kwa mwaka 2011/2012 walilipwa fedha za kuendeshea ofisi shilingi 600,000 kwa ajili ya mafuta ya gari na shilingi laki nne kwa ajili ya posho ya kujikimu lakini hawakupelekewa fedha za kufanyia matengenezo magari na vifaaa vya kuandikia. Ni ukweli usiopingika wamekuwa wakiomba matairi ya magari yao baada ya kuvuliwa kwenye magari ya Wakuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakaguzi pia wanalalamikia mishahara yao hawalipwi kwa ngazi ya *TGST I* kama wanavyolipwa maafisa wa ngazi za elimu kwenye Halmashauri za Wilaya. Naamini Idara hii ikiwa mamlaka itaimarisha pia maslahi ya watendaji wake pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mungu kwa vile ananilinda na kunipigania kimwili na kiroho. Pia napenda kumpongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri na jopo lake zima linalomwezesha kufanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii ili niweze kuchangia machache katika Wizara hii nikianzia na kuipongeza Wizara kwa kuongeza Walimu wa Elimu ya Awali. Maana huku awali ndiko anakoandaliwa mtoto kwa kumpa mtiririko thabiti wa kumwezesha kujengeka vizuri kiakili. Cha msingi hapa, ni uwepo wa zana za kufundishia za uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa Elimu ya Msingi Walimu hawatoshi mashuleni na kupelekea wanafunzi kufeli mitihani kwa kukosa baadhi ya masomo. Hivyo naomba wale Walimu, wanafunzi mara wamalizapo mafunzo yao waajiriwe mapema ili wazibe mapengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la madawati katika shule za kata (sekondari). Kitendo cha kuwachangisha madawati kila wanaoanza Kidato cha Kwanza hata kama kuna kaka/dada yake aliyemaliza mwaka uliopita sio kizuri. Kulikuwa na uwezekano wa yeye kurithi dawati la kaka/dada yake. Maana dawati lile linakuwa bado zima na angeweza kulitumia hadi kumaliza Kidato cha Nne na kuliacha. Naiomba Serikali iliangalie hilo kwani ni kero sana kwa wazazi kwani michango ni mingi wanayochangishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgomo wa Walimu, huu unasababishwa na upungufu wa maslahi. Mishahara ni midogo, hawana nyumba kwa makazi, hawana motisha kwa yale mazuri wanayofanya. Pamoja na hayo, napenda kutoa masikitiko yangu ya wale Walimu walioaga dunia kutojaliwa familia zao pale wanapokosa mfuatialiaji wa mirathi kutokana na kukosa uelewa. Walimu hawa familia huwa zinahangaika na wengine hata kukosa wa kuwasomesha. Baadhi ya Walimu hawa walikuwa wanadai Serikali malipo fulani fulani kama mapunjo ya mshahara au posho fulani. Naiomba Serikali ione haja ya kuhakikisha haki inatendeka kwani kumbukumbu zake zinakuwepo kwenye faili laki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la ukaguzi mashuleni, miaka ya nyuma Idara ya Ukaguzi ilikuwa inafanya kazi vizuri na walikuwa wanawaogopa Wakaguzi. Hatua hii ilikuwa inawafanya wafanyakazi wafanye kazi kwa uhakika. Walikuwa wanaandaa maazimio ya kazi na maandalio ya masomo. Yalikuwa yanakaguliwa kwanza na Mwalimu Mkuu kisha Wakaguzi. Siku hizi Walimu wengi wanafundisha bila maandalio na wala maazimio. Kutokana na hali hii inachangia kwa kiasi kikubwa kuanguka kwa wanafunzi au kushuka kwa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nizungumzie suala la mikopo ya elimu ya juu. Mikopo hii naomba iangaliwe ni akina nani wanahitajika kupata mikopo. Maana baadhi yao wanaopewa hawahitaji ila wanachukua kwa vile inapatikana kwani wazazi wao

huwa wana uwezo. Matokeo yake wapatapo huenda kununua magari vilevile baadhi yao baada ya kumaliza mafunzo yao huenda kufanyia kazi maeneo mengine tofauti na makubaliano. Hivyo Wizara iwe makini kuhakikisha mikopo hiyo inatolewa ipasavyo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tuhuma za uwepo wa mishahara hewa inayolipwa katika Chuo Kikuu cha Dodoma katika mazingira yafuatayo:-

(i) Wafanyakazi kuwa na *cheque number* mbili.

(ii) Wafanyakazi kuacha kazi na fedha zao kuendelea kupelekwa pasipo kurejeshwa Wizarani na Utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe Wizara ya Fedha imetangaza hivi majuzi kwamba kila mwezi Serikali inapoteza shilingi bilioni tano kwa ajili ya mishahara hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *capitation grants*, hili ni tatizo. *Capitation grants* hazifiki shuleni kwa wakati na kwa ukamilifu. Napenda kupata taarifa ya *capitation grants* zilizopelekwa Manispaa ya Kinondoni.

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja. Pia ninawapongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika elimu na mafunzo katika kipindi cha mwaka 2011/2012. Aidha, nawapongeza kwa

matayarisho na uwakilishi mzuri wa bajeti ya Wizara 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita zaidi katika mgogoro unaoendelea baina ya Serikali na Walimu kupitia Chama chao (CWT), kisababishi kikubwa ni malipo, madeni na posho. Naiomba Serikali kuongeza kasi katika kutatua kero na changamoto hizi za Walimu ambapo Serikali wasipolipatia kipaumbele suala hili tunaweza kuifikisha pabaya sekta hii ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu unaotumika na Serikali wa utoaji mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu ufanyiwe marekebishio kwani utaratibu uliopo bado haukidhi mahitaji hasa kwa watoto wanaotoka katika familia zenye kipato duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kuishauri Serikali kuweka mkazo katika suala la ukaguzi wa utoaji wa elimu kwani sehemu hii naiona imesahaulika kwa kuwekewa vipingamizi vingi vikiwepo vifaa na fedha. Lakini na muhimu zaidi ni kipaumbele katika mipango ya Wizara hasa katika Halmashauri zetu kwa kidogo wanachopewa Halmashauri wanaweza kutimiza au kutekeleza suala hili la ukaguzi japo kidogo ili kuboresha elimu yetu ya msingi na sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali mbaya ya elimu Kibondo. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na 'Uwezo' mwaka huu inaonesha kuwa Wilaya ya Kibondo ndiyo Wilaya ya mwisho kielimu Tanzania. Hii inasababishwa na upungufu wa Walimu hasa wale wanaopangiwa kutoripoti. Pia mgogoro uliodumu kwa muda mrefu kati ya Afisa Elimu na Walimu Wilayani Kibondo. Hivyo naomba aondolewe Kibondo kwani hata Halmashauri alizotoka kulikuwa na matatizo makubwa. Ahamishwe haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuiomba Wizara itoe '*incentives'* yaani vivutio kwa Wilaya za pembezoni ikiwemo Kibondo, hii itasaidia kupunguza Walimu wanaoripoti na kuondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule ya wasichana Kibondo Sekondari. Shule hii ni miongoni mwa shule ambazo zilifutwa *O level* na kubaki na *A level* pekee. Napenda kupata majibu ya Serikali kwani shule hii ilikuwa inachukua wanafunzi zaidi ya elfu mbili lakini sasa ina wanafunzi wasiofika mia nne. Mabweni yamebaki na popo, je, huku si kutumia shule hii vibaya? Kwani ina majengo ya kutosha lakini hakuna anayeyatumia. Naiomba Serikali ibadilishe matumizi ya shule hii ili itumike vizuri kwani shule za Kata Kibondo hazina mabweni, kwa nini shule hii isichukue watoto wa *O level?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TCU* na Bodi ya Mikopo. Napenda kupata majibu ya Serikali kwani kuna vyuo binafsi ambavyo vinatoza fedha ambazo hazilipiwi na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Kwa nini *TCU* inawapangia watoto maskini kwenye vyuo binafsi bila kuangalia uwezo wao wa kulipa ada na michango ya ziada ambayo hailipiwi na Bodi ya Mikopo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia utaratibu wa sasa wa Bodi ya Mikopo unapaswa kupitiwa upya kwani migomo inazidi kuendelea endapo hatutapitia upya na kwa haraka Sheria ya Bodi ya Mikopo. Utaratibu wa sasa haujaweza kuwapatia mikopo watu maskini hivyo sheria iletwe haraka kwa marekebisho.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nami kupata fursa hii ili nitoe mchango wangu wa mawazo katika bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro katika elimu ya juu inayosababishwa na Bodi ya Mikopo pamoja na Serikali yenyewe, inaanza kuwa tatizo sugu linalozoeleka katika nchi yetu. Hivi kuna tatizo gani kuwapatia wanafunzi wetu wa elimu ya juu mikopo yao kwa wakati na pia kuwapatia fedha za mafunzo kwa vitendo kwa wakati? Wizara au Serikali inaitupia lawama hii Bodi ya Mikopo na Bodi nayo inaitupia lawama Serikali na matokeo yake ni migogoro na migomo katika elimu ya juu na inaathiri muda wao wa kujifunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimba kwa watoto wa kike zinazosababishwa na mazingira duni ya kujifunzia ikiwemo pia uhaba wa hosteli hasa katika shule za sekondari za kata ni tatizo linaloekea kukosa ufumbuzi Serikalini. Naishauri Serikali iboreshe mazingira ya elimu katika shule za kata hasa kwa kuhakikisha kuwa kila shule ya sekondari ina hosteli kwa ajili ya watoto wanaokaa mbali na shule na hasa watoto wa kike. Hosteli zitasaidia watoto wajifunze kwa utulivu bila kupoteza muda wake na pia bila kukutana na vishawishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Wizra ya Elimu imeendelea kuwa siyo kipaumbele cha Serikali na hasa katika Idara muhimu ya Ukaguzi. Ikiwa Idara ya Ukaguzi haipewi umuhimu wowote, haitengewi bajeti ya kuwezesha shughuli zake, tunatarajia vipi elimu inayotolewa iwe bora wakati Walimu pamoja na vifaa na mazingira ya kufundishia havikaguliwi? Naitaka Serikali iipe Idara ya Ukaguzi uzito wake unaostahili kwa kuiwezesha kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mchango wangu juu ya hoja ya makadirio ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na uzoefu. Kazi yoyote huendelea kuimarika kutokana na uzoefu wa ujuzi unaojengwa kadri mtu anavyoendelea na kazi hiyo. Moja ya tatizo linalokabili sekta ya

ufundishaji katika shule zetu ni ukosefu wa Walimu wenye uzoefu, Walimu sasa hivi wafikapo mashuleni, kutokana na mishahara midogo, mazingira mabaya ya kazi, huhamia katika shughuli nyingine au kuacha kazi katika miaka mitano na hivyo shule zetu kupokea Walimu wapya na kufanya zikose Walimu wenye uzoefu wa kufundisha na hasa madarasa ya chini, darasa la kwanza na la pili. Madarasa haya huhitaji Walimu wenye umri mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wingi wa wanafunzi madarasa ni tatizo katika ufundishaji. Hili ni tatizo kwani Mwalimu hawezi kusahihisha daftari 400 kwa siku kwa ukamilifu, usahihishaji unahitaji umakini kama ni hesabu Mwalimu anafutilia njia ya namna ya kupata jibu na kumkosoa mwanafunzi lakini pia Mwalimu kufanya tathmini ya namna watoto walivyopokea somo lake na kupanga namna ya kurudi darasani siku inayofuata kama ni masomo ya kuandika, kujieleza, Insha na kadhalika. Mwalimu anapaswa kusoma kikamilifu kazi ya kila mwanafunzi na kupima uelewa. Sasa kutokana na wingi wa wanafunzi darasani, Walimu husahihisha kwa kuweka *Tick* moja kila ukurasa, Walimu sasa hawapimi uelewa wa watoto mzigo, ni mkubwa, Serikali hailioni hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwango vya Walimu, ninaunga mkono kuchagua wanafunzi wenye *Division III* katika kujiunga na Vyuo vya Walimu. Bado kiwango hiki ni cha chini, Serikali iendelee katika mpango huu na ikibidi wanafunzi wa *Division II* na *Division III* ndio waende kwenye vyuo hivi, aliye na elimu duni hawezi kufundisha kwa kiwango kwa kuwa na yeye hajui.

Walimu walio kwenye ajira tayari wapewe mafunzo ya muda mfupi (mafunzo ya Walimu kazini). Program hizi zilikuwepo zamani, zifufuliwe hasa kwa Walimu wa Kiingereza, Sayansi na Hesabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lugha ya Kiingereza, kwa kuwa nchi yetu haijatoa uamuzi wa kutumia Kiswahili kwa masomo yote na kwa kuwa Kiingereza ni lugha inayotumika Kimataifa, kibiashara, kazi na kadhalika, nchi yetu haiwezi kujitenga, lugha hii ifundishwe kikamilifu ili vijana wetu waweze kujiamini pale wanaposhindana na nchi nyingine kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utulivu Walimu kazini. Serikali isifanye mzaha katika kushughulikia maslahi ya Walimu na hasa mishahara yao. Kumbuka Walimu hawa hutegemea mishahara mwezi mzima kwa kuwa hawana posho. Inawezekana katika mgomo wa majuzi, hoja ya kudai posho mbalimbali ilijitokeza. Kipato kidogo huwafanya Walimu wasitulie kazini na kuchukua muda mwingi kufundisha *tuition*, kufanya biashara na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wenyewe. Mwamko kwa wanafunzi kujisomea uko chini kabisa. Kujisomea imekuwa ni kitu kisichotiliwa mkazo mashuleni. Mbinu za kuwafundisha wanafunzi wazoee na kuona umuhimu wa kutafuta elimu, kuongezea maarifa wanayopewa na Mwalimu, wanafunzi sasa hivi hutegemea kichwa cha Mwalimu hata kama uwezo wake wa maarifa unazidiwa na wanafunzi. Maktaba mashuleni hazina vitabu vya kujisomea, Serikali iweke mkazo na kuweka utaratibu wa kupeleka vitabu

vyenye hadithi ndogondogo *(petty stories)* ili watoto wavisome vya lugha zote, vitabu vya ziada (*supplementary books)* vipelekwe mashuleni ili wanafunzi wavisome kukuza lugha na maarifa. Walimu wawe na rejista, mwanafunzi akimaliza kitabu aweze kueleza maudhui, mwanafunzi anaweza kusoma vitabu 10 kwa muhula na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya watu wazima. Sera ya Elimu ya Watu Wazima ilitekelezwa na kuonyesha mafanikio miaka ya 1970/1980. Baada ya hapo hakuna elimu hii. Hakuna mahali popote utakapokuta darasa kwa watu wazima. Naomba kuuliza, mtaala wa elimu hii uko wapi? Ukiuliza hata katika Halmashauri watakuonyesha MEMKWA wakati mwingine watataja kikundi cha mafundi seremala, hizo *honorarium* zinalipwa kwa Walimu wapi? Wanafundisha nani? Nashauri elimu hii ni ya muhimu, Wizara ijipange upya kuandaa mtaala, vitabu na Walimu. Rudini nyuma kutathmini ni vipi miaka ya nyuma elimu hii ilifanikiwa ili iweze kuendelea.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuendelea kuchangia Wizara hii ya Elimu na Ufundi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya elimu hapa nchini ni ya kibaguzi, watoto wa wakulima na wafugaji hawawezi tena kusoma na watoto wa wafanyabiashara wakubwa au hata na watoto wa viongozi wa Serikali. Mfumo uliopo ndio unaosababisha hayo yote, elimu kuwa ni biashara ndio sababu ya yote hayo. Serikali iangalie kwa upya jinsi ya kuhakikisha

kwamba elimu inapatikana kwa wote na kwa urahisi, ili kuondoa ubaguzi uliopo wa kuwatenga watoto wa wakulima katika kupata elimu bora pamoja na watoto wa watu wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya majengo mengi ya Shule za Msingi vijijini hayaridhishi. Baadhi ya majengo yamejengwa wakati wa kupata uhuru, ni miaka 50 iliyopita. Serikali iangalie jinsi ya kukarabati majengo yaliyochakaa ya baadhi ya Shule za Msingi vijijini. Fedha itengwe ya kutosha kwa ajili ya samani na vifaa vya kufundishia ili elimu itolewe katika mazingira mazuri, ya utulivu na yaliyo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la mimba mashuleni halijapungua, wasichana wengi wanashindwa kumaliza masomo kutokana na mimba. Baadhi yao wanapata mimba kutoka kwa Walimu wao na wengine kutoka kwa wanafunzi wenzao. Wengine wanapata mimba kutoka kwa watu wazima wanaowadanganya kwa zawadi ndogondogo kama *chips* na kipande cha kuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ijenge mabweni kwa shule za kutwa kwa wasichana hasa katika Wilaya ya Handeni, Mkoani Tanga ambako kwa taarifa iliyotolewa na Baraza la Watoto kwa Waheshimiwa Wabunge waliotembelea Wilaya ya Same, Kilwa na Ruangwa katika Kamati za Kudumu za Bunge, kuangalia shughuli za Baraza hilo la Watoto wanaodhaminiwa na Shirika lisilokuwa la Kiserikali *"Save the Children"* taarifa hiyo ilisema kwamba, Wilaya ya Handeni inakabiliwa na tatizo kubwa la

mimba za mashuleni kutokana na ukosefu wa mabweni katika shule nyingi za sekondari. Serikali iangalie jinsi ya kutatua tatizo hilo kwa kujenga mabweni kwa ajili ya wanafunzi wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wote wanaothibitika kuwapa mimba wasichana wa shule na hivyo kuwa sababu ya kukatisha masomo yao, hatua kali za kisheria zichukuliwe lakini pia baada ya kujifungua wasichana wapate nafasi nyingine, waendelee na masomo na wafanye mitihani yao ili maisha yao yasiwe yameharibiwa moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Katibu Mkuu, Wakurungezi wote pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa bejeti hii nzuri. Ninaomba Mwenyezi Mungu awatie nguvu na mshikamano ili Wizara hii izidi kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushuka kwa taaluma ya elimu nchini. Napenda kuikumbusha Serikali kuwa huu utaratibu wa mfumo wa utoaji taaluma kubadilika mara kwa mara, hushusha sana taaluma ya elimu kwa wanafunzi wa Shule za Msingi na sekondari nchini. Wakati ninaanza kusoma mimi darasa la kwanza, masomo yaliyokuwa yanafundishwa kwa darasa la

kwanza ni matatu tu na masomo hayo ni Kuhesabu, Kuandika, Kusoma. Ni ukweli usiopingika wanafunzi tulijengewa msingi mzuri na uelewa ulikuwa wa kiwango cha juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi darasa hilohilo la kwanza linafundishwa masomo saba nayo ni Hisabati, Kiingereza, Kiswahili, Sayansi, Michezo, Stadi za Kazi na TEHAMA. Je, wanafunzi wadogo hawa masomo yote haya wataelewa? Ninaishauri Serikali irudie mfumo wa zamani ili watoto tuwajengee msingi bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kushauri somo la Kiingereza lifundishwe kama somo na masomo mengine yafundishwe kwa lugha ya Kiswahili. Wanafunzi wajue Kiingereza kwa vile ni lugha ya mawasiliano Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maslahi ya Walimu. Inasikitisha sana ninaona Mwalimu anapewa umuhimu mdogo wakati taasisi zingine zinapewa kipaumbele kimaslahi. Hivi ni nani ambaye hakutokea kwa Mwalimu? Kila mmoja wetu tumefundishwa na Walimu ndiyo maana tupo hapa. Sasa ni sababu zipi ambazo zinamfanya Mwalimu apewe mshahara mdogo ambao hauendani kabisa na hali halisi ya maisha ya sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali iache kuwapiga Walimu danadana, iwape mishahara inayoendana na hali halisi ya maisha ya sasa. Ni ukweli usiopingika mshahara wa Mwalimu ni nauli tu ya daladala, bado mara zote amekuwa akifanya kazi

kwa kukopwa yaani malipo baadaye. Tabia hii itakwisha lini? Naomba maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, posho ya kufundishia. Napenda kutoa masikitiko yangu kwa Serikali kuendelea kukataa kuwapa Walimu posho ya kufundishia ambayo zamani ilikuwepo Serikali ikasema inaunganisha kwenye mishahara. Ukweli ni kwamba Serikali haijaunganisha. Sasa lini posho hii Mwalimu atapewa ili aweze kupata moyo wa kufanya kazi kwa bidii na kwa ufanisi wa juu? Nasubiri maelezo ya Serikali tafadhali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuundwa kwa chombo kimoja cha ajira kwa Walimu. Ni ukweli usiokwepeka kuwa Walimu wanafanyakazi kwenye mazingira magumu sana kwani hawana chombo kimoja cha kuwapa huduma hivyo hata kupata huduma ni shida wakati mwingine hata barua zao huweza kupotea bila yeye kujua ataendelea kusubiri kujibiwa kumbe barua yake haikufika. Mwalimu anawajibika Wizara ya Utumishi, Ofisi ya Rais, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI. Ninaomba ombi la Walimu lipatiwe ufumbuzi ili waweze kuwa na chombo kimoja cha kusimamia mambo yao na kuwapatia ufumbuzi. Nasubiri majibu ya Serikali tafadhali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu kupandishwa vyeo. Kuna tatizo sana Walimu kuteuliwa nafasi mbalimbali za uongozi mfano Afisa Elimu wa Wilaya, Afisa Elimu Taaluma, Afisa Elimu EWW, Afisa Elimu Vielelezo na kadhalika. Uteuzi wa nafasi hizi hauko

wazi, suala ambalo linawapa hisia Walimu kuwa ni la kujuana. Napenda kuishauri Serikali kuwa ni vema nafasi hizi ziwe zinatangazwa kisha wanaotaka na wenye sifa watume maombi na usaili utumike kuwapata Maafisa hawa ili kuondoa dukuduku kwa Walimu. Maneno haya nimeyapata kwa Walimu wenyewe hasa wale waliojiendeleza hadi Chuo Kikuu au zaidi. Ninasubiri maelezo ya Serikali ili Walimu wasikie tafadhali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti finyu katika sekta za Walimu. Napenda kukiri kuwa katika sekta za elimu mfano Idara ya Elimu ya Watu Wazima, Idara ya Tume ya Utumishi ya Walimu *(TSD)*, Idara ya Elimu na kadhalika, zinatengewa fedha ndogo sana matokeo yake zinashindwa kujiendesha zikiwemo Idara ya Ukaguzi na Idara ya Takwimu na Vifaa. Ninaiomba sana Serikali kuangalia uzito wa idara hizi ndipo ziangalie kiwango cha kutenga kwa idara zote kwenye Halmashauri zote nchini zikiwemo za Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia mbili ya makato ya mishahara kwa ajili ya CWT. Napenda kupongeza mpango wa Walimu kuwa na chombo chao cha kuwaunganisha na kuwapigania yaani CWT. Ukweli Chama cha Walimu Tanzania kimeandikishwa kisheria na kinatoa huduma nzuri ingawa huduma hizo hazitoshelezi kulingana na kiwango wanachochangia Walimu cha asilimia mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kushauriana na CWT kuhakikisha inafanya mambo haya mawili yafuatayo: Chama cha Walimu Tanzania

kiwe kinampa Mwalimu kifuta jasho anapostaafu na Chama cha Walimu kianzishe *SACCOS* kila Wilaya kwa ajili ya kukopesha Walimu, kuwapa mitaji ya kuendesha miradi mbalimbali ya kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumalizia mchango wangu kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia nikiamini Mheshimiwa Dkt. Kawambwa, Waziri mwenye dhamana na kaka yangu akisaidiana na Mheshimiwa Mulugo, Naibu Waziri watatoa maelezo au ufafanuzi wa mchango wangu. Ninawatakia afya njema na nguvu na mshikamano ili waendelee na ufanisi uleule wa siku zote.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninaunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nanyumbu ina matatizo makubwa katika sekta hii ya elimu na hapa naorodhesha changamoto au matatizo yafuatayo yanayotukabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa Walimu, Wilaya ya Nanyumbu ipo pembezoni mwa nchi hii na ilikuwa uwanja wa mapambano wakati wa harakati za ukombozi wa Msumbiji. Tatizo ni kuwa baadhi ya Walimu wanaopangiwa kwenda huko hawafiki kwenye vituo vyao vya kazi hivyo kuweka pengo kubwa la Walimu wa Shule za Msingi na za Sekondari. Ninaomba Serikali iweke vivutio kwa Walimu wanaopelekwa kwenye Wilaya ya Nanyumbu na zinginezo zenye mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa nyumba za Walimu, ni tatizo kubwa Wilayani Nanyumbu. Shule nyingi za msingi na za sekondari hazina nyumba za Walimu hivyo kupelekea Walimu wengi kuishi kwenye nyumba duni na kuwafanya waishi maisha duni na hivyo kupunguza morali yao ya kufanya kazi. Naomba Serikali iongeze ruzuku kwa Wilaya ya Nanyumbu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa matundu ya choo na madawati. Shule nyingi Wilayani Nanyumbu zina uhaba mkubwa wa matundu ya choo kiasi cha kuwafanya wanafunzi wajisaidie vichakani. Ni hatari kwa watoto kupata magonjwa ya kuambukiza. Sambamba na hilo shule nyingi Wilayani Nanyumbu zina uhaba wa madawati. Wanafunzi wengi hasa wa Shule za Msingi wanakaa chini hivyo kuathiri mwenendo mzima wa elimu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa vyumba vya madarasa. Shule nyingi hasa za msingi zina uhaba mkubwa wa vyumba vya madarasa sambamba na hilo madarasa mengi yamechakaa na mengine yanahatarisha maisha ya wanafunzi kwani kuta zake zimekatika. Kwa hili ni kwa kuwa fedha zinazopelekwa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ni chache hivyo kufanya kasi ya kujenga vyumba vya madarasa kuwa mdogo. Ninamwomba Waziri au Naibu Waziri kutembelea Nanyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugunduzi wa gesi Mtwara una kuja sambamba na changamoto mbalimbali za maendeleo. Teknolojia hii ya uchimbaji wa gesi na

mafuta Mtwara utahitaji wataalam kwenye sekta hii. Je, Wizara inajiandaa vipi kukabiliana na tatizo la wataalam wazalendo ambao watashika nafasi mbalimbali katika sekta hii? Ninaomba wakati wa majumuisho Waziri aeleze Wizara mipango iliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ndio msingi wa maendeleo wa taifa lolote lile duniani. Hapa Tanzania elimu inaporomoka kwa kasi kubwa sana, ni jambo la hatari sana na mbaya zaidi Serikali haioni kama tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ngazi zote kuanzia *primary school, secondary school* hata vyuo vikuu, viwango vya elimu inayotolewa haiwafundishi watoto kukabiliana na changamoto za maisha ya dunia ya leo. Mtoto anamaliza *primary school* hajui kusoma wala kuandika wakati kakaa darasani miaka saba. Mtoto anamaliza *secondary school* hawezi hata kuandika *essay* wala kujieleza, mtoto anamaliza chuo kikuu hawezi kuandika barua ya kuomba kazi, hii ni hatari kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yanayofanya elimu kuporomoka, wote tunayaona wazi na kila leo tunatoa ushauri Serikali inaziba masikio. Shule hazina vitendea kazi, vitabu hakuna, mazingira ya kufundishia watoto ni magumu sana hayampi Mwalimu fursa ya kufundisha vizuri wala mwanafunzi nafasi ya kumwelewa Mwalimu wake. Mtoto anakaa chini kwenye udongo/sakafu, wako zaidi ya mia darasani

(hakuna viwango vya idadi) wanaandikia kwenye magoti, ataelewaje anachofundishwa? Wapo wanafunzi ambao ni *slow,* huyu Mwalimu ataweza kusaidia wangapi kwa kuinama chini? Kwa vyovyote ataendelea na wale wanaoelewa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wamekata tamaa na kazi yao, wanafundisha ili mradi siku zipite asubiri mshahara, Serikali haiwajali wala kuwathamini. Leo ni zaidi ya miaka mitano wanalalamika maslahi yao hawapewi. Serikali inachangia asilimia 100% watoto wetu kukosa elimu nzuri. Ualimu ni moyo na dhamira na siyo kushika chaki na kuingia darasani, wakati Walimu wamevunjika moyo, wako shingo upande, wanalazimishwa kufundisha kwa nguvu kwa amri ya Mahakama, Waziri hapo unategemea matunda gani? Serikali inatamba eti mmetumia rungu, hamwoni aibu! Nyie mngesoma hivyo mngefika mlipo leo? *This is shame*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mwalimu ndiye anayejenga msingi wa mtoto yeyote kwa maana hiyo anatakiwa kuwa *competence*, *intelligent and creative* kujenga msingi imara wa watoto. Nchi nyingine wanachukua wanafunzi waliofaulu vizuri Daraja la I na II wanasomea Ualimu hapa Tanzania wale waliopata Daraja la IV, *point 28, 27,29* ndio wanasomea Ualimu. Hii inaonyesha jinsi gani Serikali isivyoona umuhimu wa elimu bora. Ualimu ni *last option,* wale waliokosa kusomea *course* nyingine kwa sababu ya *pass mark* wanakwenda Ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za watoto walemavu wenye mahitaji maalum zina changamoto nyingi sana. Watoto wale wanahitaji vifaa vyote muhimu ili waweze kusoma. Walimu ni wachache sana wa vipaji maalum kwa sehemu kubwa shule hizi zinategemea misaada na ufadhili wa mashirika mbalimbali. Je, ni kwa nini Serikali haitengi fedha kwa ajili ya shule hizi kukidhi mahitaji ya vifaa vyao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shule ya watoto walemavu wa macho (vipofu) inaitwa Buigiri, iko Chamwino jirani na Ikulu hapa Dodoma. Serikali na viongozi mbalimbali hupita jirani pale kila siku hakuna fedha yoyote inayotengwa kwa ajili ya shule hii. Shule ya Uhuru mchanganyiko, Buguruni ziangaliwe na Serikali, watoto wanashindwa kusoma kwa ajili ya kukosa vifaa vya kufundishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo ya elimu ya juu ina matatizo makubwa kila kukicha. *Criteria* zilizowekwa na Serikali ili mwanafunzi apate mikopo ina upendeleo mkubwa. Kutoa mkopo kwa fani za *Science*, Ualimu na *Technicians* ni kuleta matabaka kwa sababu kila fani hapa nchini inahitajika. Tunahitaji Madaktari, Wanasheria, Mainjinia, Wahasibu na kadhalika. Serikali ikae chini na kuangalia njia na utaratibu bora zaidi, viwango vya ufaulu ndio iwe dira ya kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mchezo unafanywa kati ya Maafisa Mikopo wa Makao Makuu na wale wa Kanda, mikopo ya wanafunzi inatolewa *HQ* inachukua wiki tatu haijaingizwa kwenye akaunti ya chuo,

wanafunzi wa vyuo hivyo wamekuwa wakiteseka huku fedha yao ikifanyiwa biashara. Ninao ushahidi wanafunzi wa Chuo cha Mipango Dodoma zaidi ya 26 fedha yao ilichelewa kufika chuoni, walipofuatilia Dar es Salaam wakaambiwa waende kwa Afisa Mikopo wa Mipango fedha yao ilishatoka muda. Inaonekana kuna makubaliano kati ya Afisa Mikopo wa Bodi (Ndugu Elias) na Afisa Mikopo wa Zone ya Dodoma (Ndugu Chikala). Waziri aeleze Bunge fedha inayochelewa kufika chuoni wiki tatu baada ya kutoka Bodi inakuwa inafanyiwa nini? Kina nani wanahusika na hatua gani zinachukuliwa?

**MHE. GAUDENTIA M. KABAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nawapongezeni sana Waziri, Naibu, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Kamishna na wote kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia kufuatia rai iliyotolewa na Mbunge Ntukamazina kwamba uanzishaji wa shule binafsi ni "biashara haramu. Ukweli ni kwamba uanzishaji na uendeshaji wa shule binafsi kwanza siyo biashara. Ukishaichukua kama biashara basi utashindwa kutimiza malengo ya elimu nchini na malengo ya Serikali ku-*libaralize* elimu nchini ndiyo maana mimi nashauri kuwa wenye shule hizi wawe na *background* ya elimu yaani awe Mwalimu au aliwahi kuwa Mwalimu na kadhalika la sivyo shughuli hii nzuri itachanganywa na biashara na hivyo kuififisha kabisa. Sina haja ya kuelezea mchango wa shule binafsi hapa nchini maana nyie mnafahamu zaidi kuliko mimi hivyo nashauri Serikali (Wizara) iendelee kuzisimamia kwa karibu kwa kuzikagua kabla ya kuanza na wakati

zinaendelea ili kuhakikisha ubora wa elimu unakuwepo na zisigeuzwe biashara kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, ni shule zetu za kata. Naomba wenzetu wanaoziponda warejee miaka miwili ya nyuma ambapo vijana wamekuja hapa Bungeni kupewa zawadi za ufaulu wa juu wa Kidato cha Nne wa shule za kata, waziite jina lolote lile, lakini naomba kwenye majumuisho Waziri asisahau kueleza mambo makuu yaliyotokana na kuwepo shule za kata ambazo sasa ndizo nyingi kama shule za Serikali kuliko zile za *boarding.* Atoe takwimu ya ushindi ikiwezekana *otherwise* hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Prof. Balalusesa kwa uteuzi wake kama Kamishna wa Elimu. Naamini kwa uteuzi huu kwa kweli upele umepata mkunaji. Namwombea kazi njema pamoja na changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba kuchangia hoja ya Wizara ya Elimu kwanza kwa kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza kuchangia katika eneo la Shule za Msingi. Katika Jimbo la Kondoa Kusini katika Wilaya ya Chemba, Mkoani Dodoma, tuna upungufu mkubwa wa Walimu katika shule za Birise, Mengu, Wairo, Mwailasabe na nyingine nyingi, naishauri Wizara kuangalia kwa makini ni namna gani ya kuwapanga Walimu wanapotakiwa kuripoti

kwa mara ya kwanza badala ya kuwapanga bila hata kuangalia mazingira wanayotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, idadi kubwa ya Walimu hasa wasichana wanapangwa katika shule za mijini mfano katika shule za Kondoa Mjini, kuna idadi kubwa ya Walimu ukilinganisha na shule za vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, shule za Sekondari za Kata, shule hizi zimekuwa na faida kubwa kwa vijana wetu wanaomaliza darasa la saba lakini pamoja na nia njema hii ya Serikali shule za Mpendo, Gwandi, Lalta, Mwailanje, Songolo, Jangalo, Makorogo, Soya na Chemba, zina Walimu wachache mno na hawazidi watatu lakini katika shule za kata za Kondoa mjini zina idadi kubwa ya Walimu. Naiomba Serikali kuhakikisha kunakuwa na usawa katika upangaji wa Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, njia sahihi ya kuondoa tatizo la ujauzito katika shule hizi za kata ni kuhakikisha kunakuwa na mabweni ya wasichana ili wasitembee muda mrefu jambo linalowafanya wakutane na vishawishi visivyokuwa na msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. ABDULSALAAM S. AMER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nawapongeza sana kwa kuteuliwa kwao kushika nyadhifa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu ni suala linalomgusa kila binadamu aliyepo katika dunia hii. Katika matatizo yanayotukabili katika masuala ya maendeleo ni Wizara hii ya Elimu. Nashukuru sana Wizara kwa kutupatia vitabu vinavyofafanua juu ya malipo ya Walimu, ni msaada sana kwetu sisi Wabunge kuweza kufuatilia kwenye Halmashauri zetu na kuhakikisha kweli wamelipwa na lazima Walimu wajue haki stahili yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vya *VETA* vilivyopo kwenye Wilaya zinazotegemea kilimo waweze kutoa mafunzo ya udereva na ufundi wa kutumia matrekta kwa kuwafundisha jinsi ya kuendesha matrekta na kulima pia. Vyuo vingi vya ufundi wameelekeza zaidi udereva wa magari tu. Kwenye kauli mbiu ya Kilimo Kwanza kwa kweli kuna uhaba sana wa fani hiyo hapa nchini. Leo utapata madereva wa trekta ambao wenye ujuzi wa mazoea tu hawana leseni na ufundi wa jinsi ya kutumia jembe la aina yoyote. Kutopata elimu juu ya kutumia matrekta na nyenzo zake na kukosa vyeti vya ufundi, huwafanya kupata malipo duni na kutoweza kujikwamua kimaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Walimu walioajiriwa mwaka jana wana malalamiko sana kuhusu malipo yao. Naomba kama itawezekana mngeweza kutupatia maelezo ya Walimu walioajiriwa na malipo yao kama wamelipwa au la.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iharakishe kutupatia hayo majina ili tufuatilie katika Halmashauri zetu. Kuna ubadhirifu sana katika

Halmashauri zetu hasa hizi pesa za elimu. Afisa elimu wa Wilaya yangu ya Kilosa kwa kweli amepitwa na wakati na umri pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba majukumu yote ya Walimu au uongozi wote wa elimu urudi Wizarani nina maana Maafisa Elimu wa Wilaya kazi zao ziwe kufuatilia tu Wizara ijihusishe moja kwa moja na malipo ya Walimu. Naamini kama Wizara itafanya hivyo, malalamiko angalau yanaweza kupungua.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *Loans Board* hasa urejeshaji wa fedha liangaliwe vema ili mfuko uwe *revolving fund* vizazi na vizazi waweze kupata *access*. Nashauri vyeti viwekwe alama mtu akipata kazi basi mwajiri wake aweze kupunguza mshahara kulipia mkopo ili uwe *revolving fund*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza *points* za Ualimu kuanzia *point* 27 mwakani 26, *very good!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo cha Ukaguzi wa Shule kipewe kipaumbele ili ukaguzi ufanyike na pia wapatiwe vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza Chuo cha *VETA* Ludewa kitakamilika lini? Vijana wengi wataweza kupata mafunzo ya ufundi kupitia chuo hiki na tangu mwaka 2005 nimeomba chuo hiki hapa Bungeni.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siungi mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina sababu za msingi za kutounga mkono hoja. Kwanza nikiwa Mbunge wa Jimbo ambalo kielimu liko nyuma tena bila sababu ya msingi. Lindi hata kwa idadi ya shule na vyuo vya ufundi iko nyuma. Mara nyingi Lindi hutoa wanafunzi wachache katika ufaulu jambo ambalo huwasababishia vijana wetu wengi kubaki mitaani na wengi wao kukimbilia Mikoa mingine yenye nguvu ya kiuchumi. Hali hiyo hupunguza nguvu kazi ya Lindi. Ni budi Wizara ikaongeza shule za Serikali na vyuo vya ufundi sanjari na Walimu wenye uwezo wa kufundisha. Mara nyingi vijana wanaohitimu mafunzo ya Ualimu hukwepa kufundisha Mikoa ya Kusini hasa Lindi kutokana na uchumi duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki za Walimu, siungi mkono hoja kutokana na Wizara na Serikali kwa ujumla kushindwa kutekeleza madai ya Walimu ya nyongeza ya mishahara. Hata kama Serikali haina uwezo wa kuwaongezea Walimu mishahara kwa asilimia 100 basi ilitosha kuwaeleza Walimu kuwa uwezo wa Serikali kwa sasa ni nyongeza ya asilimia ngapi? Kwani madai ya Walimu yanatekelezeka na siyo kutumia ubabe wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na madai ya Walimu kwa siku nyingi lakini Serikali hutoa hoja za kulishughulikia suala hilo kwa umakini. Ni umakini gani usiokwisha unaoendelea kuwatesa Walimu ambao ndiyo wakombozi wa watoto wa masikini wa nchi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuelimishwa wanafunzi, zimepatikana taarifa ambazo zimeelezea kufelishwa kwa makusudi kwa wanafunzi wa Kidato cha Sita kwa somo la *Islamic Knowledge*. Baada ya malalamiko na maandamano ya Waislamu ikaonesha kuwa wanafunzi wengi wamepasi, je, kwa masomo mengine hali ikoje? Waislamu wametaka Katibu wa Baraza ajiuzuru, Baraza livunjwe na iundwe Tume ya kuchunguza matokeo ya masomo yote kwa miaka 10 iliyopita ili kubaini ukweli. Je, Serikali hadi hii leo imechukua hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri na ushirikiano thabiti kutoka kwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na viongozi wote wa taasisi ndani ya Wizara hii. Pamoja na hayo, napenda kutoa ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhaifu wa usimamizi wa mfumo wa elimu ya watu wazima. Lengo la mfumo wa elimu ya watu wazima ni kuwezesha waliokosa elimu katika umri mdogo kupata elimu. Hata hivyo, mfumo wa utekelezaji wake kutoka ngazi ya Taifa (Wizara) hadi Halmashauri, kata na vijiji ni dhaifu na hivyo kushindwa kutekeleza malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watendaji wa usimamizi hawateuliwi kwa wakati na hawapewi vitendea kazi. Halmashauri zinashauriwa kusimamia uteuzi wa Maafisa

ngazi ya Wilaya, kata na vijiji lakini Halmashauri nyingi hazitekelezi na kuliona jambo hilo kama la hiari na siyo sera ya kitaifa. Halmashauri nyingi zinapishana uwezo wa mapato hivyo hata kama maafisa hao watateuliwa bado hawatapewa vitendea kazi wala kuwezeshwa kufanya kazi kwa ufasaha. Wizara inapaswa kusimamia mfumo huo na sera hiyo kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa utoaji fedha kwa ajili ya vifaa na ujenzi wa maabara sekondari. Mgawanyo wa fedha mpango wa MESS ni dhaifu. Bado shule nyingi za sekondari hazina maabara na shule tatu tu za sekondari Wilaya ya Muheza zimejenga maabara kati ya shule 25 tangu mwaka 2006/2008. Sio rahisi Serikali kusema itaboresha elimu ya sekondari bila kuwa na maabara na Walimu wa kutosha. Sio busara kuamini kwamba wananchi ambao uwezo wao vijijini ni mdogo wataweza kuendeleza ujenzi wa madarasa, nyumba za Walimu na maabara katika shule za kata wakati pia mchango wa Serikali ukiwa mdogo kama ulivyo sasa. Taarifa ya fedha zinazopelekwa kwa mpango wa *MESS* haziwekwi wazi, ni Waheshimiwa Wabunge na Madiwani wachache wanapata uwezo wa kujua kiasi cha fedha na matumizi halisi ya fedha hizo. Kikubwa kinachoendelea ni kugushi taarifa za utaratibu wa matumizi ya fedha hizo na kuzikuta shule nyingi bila vifaa vya kutosha kulingana na thamani ya fedha halisi zilizoingizwa kwenye akaunti za shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka uliopita hapa Bungeni kupitia ofisi ya Waziri Mkuu tuliletewa maonyesho ya vifaa vya maabara na gharama zake, tulipendekeza Serikali isimamie ununuzi wa vifaa hivyo

kwa fungu la *MESS* kwa vifaa vya maabara. Hili halikutekelezwa na hivyo kuachiwa mwanya wa ufujaji wa fedha za vifaa hivyo muhimu. Mabaraza ya Madiwani yanakutana mara tatu kwa mwaka na Kamati ya Elimu, Afya na Maji kila baada ya miezi miwili/ mitatu. Hali hii ya utendaji haitoi nafasi ya usimamizi bora wa fedha kama hizo za *MESS* na vifaa vya maabara. Matokeo yake Kamati ya Baraza kukuta taarifa tu za matumizi yaliyofanyika kabla Kamati kukutana. Udhaifu huu lazima ujadiliwe kwa uwazi kati ya Wizara ya Elimu na pia kutoa taarifa ya mgao wa fedha za *MESS* kwa Wabunge ili kusaidia usimamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya Walimu, kukua kwa madai na migogoro ya Walimu kunachangiwa na mambo makubwa matatu yafuatayo:-

(i) Kugushi kwa madai. Kumekuwepo kugushi kwa madai miongoni mwa Walimu wachache.

(ii) Kutowasilishwa kwa makusudi madai halali ya Walimu kupitia viongozi wa ngazi ya Wilaya. Hii inatokana na chuki binafsi kati ya baadhi ya Walimu dhidi ya baadhi ya viongozi wa Wilaya na hivyo kulipa visasi kwa kutowasilisha madai halali.

(iii) Kuzalishwa kwa madai hasa ya uhamisho kutokana na chuki binafsi. Viongozi kwa kutumia nafasi zao huamua kuwahamisha Walimu wapendavyo wakati mwingine uhamisho wa kila mwaka. Mfumo huo unaongeza gharama kubwa kwa Serikali na Taifa bila sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mambo hayo sio mageni na yanafahamika, je, ni vipi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inajipanga kuyakabili kwa dhati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo ya ufundi. Njia pekee itakayosaidia vijana kujenga mfumo wa ajira binafsi na mafunzo ya ufundi ni mpango wa ujenzi wa vyuo vya *VETA.* Hata hivyo ni mkakati unaokwenda "Taratibu Sana" na hivyo kutokukidhi haja kutokana na gharama kuwa kubwa na Wilaya kuwa nyingi na kuzidi kuongezeka kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi isaidie Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vilivyopo katika baadhi ya Wilaya vinavyosimamiwa na Wizara ya Wanawake, Jinsia na Watoto kuboresha vyuo hivyo kwa pamoja kabla ya ujenzi na chuo cha *VETA* katika Wilaya hizo. Moja ya Wilaya yenye chuo cha Maendeleo ni Wilaya ya Muheza, chuo cha Kiwanda. Tunaomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kusaidia Chuo cha Maendeleo - Kiwanda Muheza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, utaratibu unaotumika wa kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu bado haujakidhi

matarajio ya wanafunzi wa kipato cha chini kwani mikopo hiyo mara nyingi huwa wanapata wanafunzi ambao wazee wao wana kipato na sio waliokusudiwa kwani mikopo ni kwa ajili ya wanafunzi wenye kipato cha chini, walemavu na makundi mengine. Wizara ya Fedha (Hazina) itoe mikopo kulingana na vigezo vilivyokusudiwa au vilivyoelekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vyuo vya *VETA*, Serikali ione sasa kuna umuhimu mkubwa vyuo hivi kujengwa katika kila Mkoa ili kuleta ufanisi wa ajira kwa wanafunzi na kupunguza gharama kubwa za wanafunzi wa kipato cha chini kusafiri kufuata vyuo hivi jijini Dar es Salaam na hatari kwa watoto wetu kwani kwa mgomo huu baridi hatujui kama huko maskulini kutakuwa kuna masomo kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba madai yao ni makubwa lakini muangalie kwa jicho la huruma sana kwani Walimu wanakazi kubwa sana na wengine wana mazingira magumu sana na ukizingatia kuwa Mwalimu yeye ndiye alimtoa Rais, Mbunge, Waziri, Baharia, Mwanasayansi, Mwanadiplomasia, Mkemia na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio, ni rahisi sana kuandika mafanikio katika vitabu, lakini ukweli ukifuatilia hao wanafunzi walioandikishwa wanakaa katika madarasa ambayo mazingira yake ni magumu, wanafunzi wanakaa chini, madarasa mabovu, madawati hamna, shule zenyewe hazina vyoo. Suala la elimu ni kubwa na linahitaji kuangaliwa kwa mapana yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Mitihani Tanzania lina jukumu la kutekeleza Sera ya Mitihani kwa kuzingatia Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha, Baraza lina jukumu la kuendesha mitihani ya kuhitimu elimu ya msingi, Sekondari, Ualimu ngazi ya Cheti na Stashahada na kadhalika. Sasa inashangaza kwamba Baraza hilihili linapasisha wanafunzi wa elimu ya msingi ambao hawajui kusoma wala kuandika. Tumeona kupitia kipindi cha Haki Elimu cha televisheni. Je, kwa waliohusika na kitendo hiki cha aibu kwa Taifa letu wamechukuliwa hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu, sitaki kuongelea mgomo wa Walimu uliotokea, lakini kwa kweli Serikali iwaangalie Walimu kwa jicho la uangalifu mkubwa sana kwani kama walivyosema, wamerudi kazini kwa shingo upande basi hapa kuna neno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuandika hayo, naomba kuwasilisha, ahsante.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia kwa maandishi na pia nitashukuru sana kama pia nitapata nafasi ya kuongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nimshukuru Mungu kwa ulinzi na rehema zake za kutupa zawadi ya uhai hadi leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu hivi karibuni imekumbwa na changamoto nyingi, kubwa na

nzito sana hasa katika nyongeza za stahili za Walimu. Hili ni jambo ambalo linatakiwa kuchukuliwa kwa umakini mkubwa na wa kipekee na wenye uzito tofauti. Mimi nilitegemea kabisa mambo ya madai ya Walimu yangekwisha kwa mazungumzo na kuafikiana pande zote mbili kwa maana ya Walimu kwa upande mmoja na Serikali kwa upande mwingine. Ieleweke pia kilichotakiwa ni mjadala na kuona nini kifanyike ili jambo hili liishe kwa amani bila kinyongo na tusonge mbele kuelekea maendeleo endelevu. Kama tunadhani elimu ni ghali basi tujaribu ujinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hilo kwa kuwa tumeona elimu ni ghali na sasa tumechagua ujinga. Ni dhahiri kuwa madai ya Walimu ni makubwa na tukadhani hayalipiki, la hasha kama tutakuwa na nia thabiti ya kupunguza matumizi ya Serikali na kuzuia ubadhilifu Walimu yanaweza kulipika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikitika zaidi na kauli ya Waziri hasa katika fidia kwa waathirika wa elimu (wanafunzi) ambao wanatakiwa kulipwa. Athari za kuathirika kwa elimu zilizosababishwa na fedha zilizozidi kwenye Rada, nani atalipa fidia za athari za kielimu zilizojitokeza wakati huo? Kama kuna malipo ya athari basi zifanyike kwa pande zote za waliosababisha athari hizo au basi uamuzi huo wa Waziri na Wizara uangaliwe upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu, leo nchi yetu imetengwa katika viwango tofauti vya elimu kulinganishwa na fedha za mzazi ndani ya nchi ya kijamaa, mwenye fedha kidogo anapata elimu mbaya

na mwenye fedha nyingi atapata elimu nzuri sana. Hapa tumetengeneza tabaka kubwa na baya sana kwa mustakabali wa Taifa. Miaka ya zamani elimu itolewayo na Serikali ilikuwa bora sana kuliko watu binafsi na sasa imekuwa kinyume. Napenda kutoa rai yangu kwa Serikali, mbali na kutoa elimu bora pia elimu itolewayo iendane na hali halisi ya maisha ya kujitegemea na kutegemewa na siyo tu elimu ya kujibia mitihani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa elimu ya msingi inaishia darasa la saba na watoto humaliza shule wakiwa wadogo sana, napendekeza elimu ya msingi basi iwe hadi kidato cha nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuitaka Serikali iwe na wepesi wa kupeleka fedha hasa za maendeleo na hasa za kuendeshea shule na zile ambazo zimeidhinishwa zitoke na zifike kwa wakati ili wanafunzi waweze kusoma vizuri na kupunguza kadhia kwa Walimu na wazazi na walezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii pia kuwashukuru watumishi wote wa Wizara na wadau wote wa elimu na mwisho kabisa niwashukuru Waziri na Naibu wake kwa kuwa na Wizara nzito sana yenye changamoto ambayo wanaiongoza.

**MHE. KAPT. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natanguliza kusema naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Newala, tunacho Chuo cha Ualimu Kitangari, tunashukuru kwa hilo. Hata hivyo majengo na miundombinu ya chuo hayaridhishi kabisa, majengo haya yamejengwa miaka mingi na mengine yamejengwa kwa udongo wakati huo yakiwa ni majengo ya iliyokuwa "*Kitangari Middle School*" chini ya Kanisa Katoliki baada ya shule hizi kutaifishwa na Serikali ndipo ikageuzwa kuwa Chuo cha Ualimu. Maombi na ushauri wangu ni kuwa Wizara ya Elimu katika bajeti zake za kila mwaka itenge fedha za kutosha kujenga majengo ya kisasa na hasa madarasa, nyumba za Walimu, maktaba, jengo la utawala na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msaada wa Serikali ya Japan, tumejenga jengo la kisasa la maabara ya Fizikia, Kemia na Baiolojia katika shule ya sekondari Nambunga. Kiasi cha Tshs. 156 millioni kimetolewa na Serikali ya Japan na nguvu za wananchi karibu Tshs. 20 milioni. Wilaya imeomba Wizarani vifaa vya maabara ili maabara hiyo iweze kuanza kazi. Maabara hii itasaidia pia wanafunzi wa sekondari za kata za jirani za Mtangalanga na Chitekete. Tunaomba majibu ya Wizara kuhusu ombi hili na hatua za haraka ili maabara hii iweze kuanza kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Idara ya Ukaguzi wa Elimu ni pamoja na kutembelea shule na kufanya ukaguzi ili kukagua ubora wa elimu. Shughuli hii katika Jimbo la Newala haifanywi vizuri kwa sababu Idara ya Ukaguzi haina gari kwa hiyo shule hazikaguliwi ipasavyo. Naomba katika mipango ya Wizara, suala la kutupatia gari la ukaguzi lipewe kipaumbele,

kiwango cha ubora wa elimu kinashuka kwa kukosa kukaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uchakavu wa shule na vyuo, shule nyingi za msingi na sekondari pamoja na vyuo vyetu vimechakaa mno. Mazingira mabaya, vyoo navyo havifai, nashauri uwepo utaratibu wa kukarabati shule na vyuo vyetu lakini pia ukarabati uende sambamba na ujenzi wa *computer lab's*, maabara na vyoo vya kisasa na vifaa vyote viwekwe yakiwemo madawati na vitabu vya kufundishia na vya kujifunzia (kusoma) pamoja na kukidhi haja ya Walimu wa kufundisha. Ukarabati uende sambamba na kuweka umeme wa *solar* katika maeneo ambayo hayana umeme ili *computer* zifanye kazi na watoto wapate elimu kuliko sasa wanafundishwa *computer* kwa kuchorewa ubaoni na wengine hawajawahi kuiona kwani hata umeme hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chakula mashuleni, watoto hasa wa Shule za Msingi ni muhimu sana wapewe uji na *lunch* shuleni. Watoto wadogo hawawezi kuvumilia njaa ndio maana watoto wengi hawapendi shule na wanatoroka sana. Tujifunze mfano mzuri shule za *private,* watoto hawatoroki, wanapenda shule na wana afya nzuri tofauti na shule za Serikali. Majiji, Miji, Wilaya yashiriki ku-*provide* chakula kama enzi za baba wa Taifa hayati J.K. Nyerere lakini wazazi wanaweza kuchangia chakula cha watoto wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, futari shuleni, hili ni tatizo. Shule nyingi hawa-*provide* futari. Yapo malalamiko kwamba wanafunzi hawapewi futari, wanalazimika kuweka ugali maharage wa mchana ili iwe futari na ugali mahahare ya usiku saa 12 hadi saa moja usiku, wanaweka kwa ajili ya daku. Serikali iangalie matatizo ni mengi kwenye shule za sekondari za Serikali katika Mikoa yetu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushuka kwa elimu, elimu kwa ujumla inaendelea kushuka siku hadi siku lakini pia watoto wengi wanaacha shule. Hili linathibitishwa na tofauti kubwa iliyopo kati ya idadi ya waliopo kidato cha kwanza hadi cha nne na wale wa kidato cha tano hadi cha sita kwani *gap* ni kubwa ya walioandikishwa na wanaomaliza. Lakini pia tujiulize wale wanaoshindwa kufanya vizuri kidato cha nne wanaenda wapi, sio wote wanaojiunga na vyuo vya ufundi wala kurudia mitihani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za ufaulu nazo zaendelea kuonyesha kushuka kwa elimu hasa matokeo ya kidato cha nne, mfano mwaka 2010 ufaulu ulikuwa 50.2% wakati 2009 ufaulu ulikuwa 72.5%. Vilevile tofauti ipo kubwa ya ufaulu kati ya wanafunzi wa *government schools* na zile za *private schools*, *private* wanafanya vizuri zaidi na hii inasababishwa na kutokuwa na Walimu wa kutosha, maabara, vitabu, *computer lab's* lakini pia Walimu waliopo hawalipwi vizuri hivyo muda mwingi wanafanya juhudi zingine za kujiongezea kipato badala ya kufundisha. Vilevile madai ya Walimu bado ni mengi kwa Serikali hivyo hawana moyo wa kufundisha. Nyumba za kuishi

hawana, mazingira ya kazi kwa ujumla ni mabaya, yaboreshwe, elimu iboreke na ipande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya juu, upandishwaji wa hadhi ya vyuo kuongeza watoto wanaodahiliwa kwenye vyuo hivyo uende sambamba na kujenga miundombinu ya majengo ya madarasa na mabweni lakini vilevile mbinu ya ufundishaji iboreshwe ili tufikie *standard* inayotakiwa, tusifurahie ongezeko la vyuo ambalo halikidhi haja na viwango. Wanafunzi wengi wanakariri badala ya kuelewa, wanasomea mitihani tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhuru wa vyuo vikuu kujiendesha. Azimio la Kitaaluma la 1990 tulilosaini, halitekelezwi ipasavyo kwani vyuo vimekuwa vikiangaliwa na Serikali katika utendaji wa utawala wake. Nashauri Serikali itoe fursa kwa vyuo vikuu kujiendesha kiutawala, kitaaluma pia na uhuru wa kujichagulia uongozi wake wa juu wa chuo. Wizara ibaki na kazi ya kutunga Sera ya Elimu ya Juu na Mabaraza ya Vyuo yasimamie utekelezaji wa sera na sheria. Serikali iingilie iwapo sera na sheria hazikutekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya Walimu Kigoma. Wilaya ya Kigoma, Manispaa ya Kigoma Ujiji na Kigoma Vijijini na Uvinza, tunahitaji Walimu 2500 wapo 1981, tuna upungufu wa Walimu takribani 600 tunahitaji Walimu. Kiwango cha elimu kinaendelea kushuka mfano tathmini ya 2005 – 2010 inaonyesha kuwa ufaulu hasa darasa la saba unaendelea kuporomoka. Mwaka 2005 walifaulu 62%, 2006 walifaulu

65%, 2007 walifaulu 42%, 2008 walifaulu 34%, 2009 walifaulu 35%, 2010 walifaulu 34%, 2011 – 2012 hali ni hiyohiyo, mbaya. Pamoja na sababu zingine upungufu wa Walimu ni tatizo na ni sababu kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto na vijana wenye vipaji maalum vya ufundi, Sera ya Elimu ya Ufundi inasemaje juu ya wale watoto wenye *talents* na vipaji vya kubuni na kutengeneza vitu mbalimbali mfano silaha, umeme na vifaa vingine vingi? Wanasaidiwaje? Watoto na watu wengi wamegundua vitu mbalimbali tumewasoma kwenye magazeti lakini hatujui mwisho wao. Serikali inasemaje juu ya vipaji vya namna hiyo?

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Shukuru J. Kawambwa, Waziri na Mheshimiwa Philipo A. Mulugo, Naibu Waziri, Katibu Mkuu Mstaafu, Prof. Hamisi Dihenga, Naibu Katibu Mkuu, Bwana Selestine, Kamishna wa Walimu, Wakurugenzi wa Idara na wakuu wa vitengo; wakuu wa taasisi zote zilizo chini ya Wizara kwa mchango mkubwa wanaotoa katika usimamizi na utekelezaji wa sera na sheria za sekta ya elimu na mafunzo ya ufundi stadi. Napenda pia kuwapongeza wawekezaji binafsi waliojenga na kuendesha shule na vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuthibitisha kuwa naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo, elimu ya sekondari na msingi, jamii yetu imekwishatambua umuhimu wa elimu ya sayansi kwa

maendeleo ya teknolojia, ustawi na maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini mwetu. Hata hivyo utekelezaji wa nia njema ya Serikali yetu ya kuwezesha wanafunzi wengi kushiriki masomo ya Sayansi katika ngazi ya elimu ya juu haijawezekana kwa sababu ya shule nyingi za sekondari kutokuwa na maabara, Walimu na mafundi mchundo wanaohitajika kusaidia wanafunzi kujifunza kwa vitendo masomo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara iombe fedha za kutosha kujenga walau chumba kimoja cha maabara katika kila shule ya sekondari kwa mwaka. Hii iende sambamba na uwekezaji kwenye mafunzo ya Walimu na mafundi mchundo ili wapatikane wakutosha kwa shule zote. Ili kuwezesha shule za vijijini kupata Walimu, nashauri Wizara ishirikiane na TAMISEMI kujenga nyumba za Walimu kwenye shule zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mazingira ya Wilaya yangu, naomba Wizara inisaidie kuchangia ujenzi wa maabara na nyumba za Walimu. Aidha, Walimu walio tayari kuishi kwenye mazingira ya vijijini kwenye Wilaya mbalimbali wapangiwe huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za vipaji maalum, katika Wilaya yangu kuna shule ya sekondari Ilboru ambayo ni moja kati ya shule za vipaji maalum. Hivi karibuni nilifanya ukaguzi kwenye shule hiyo na kutambua jitihada zinazofanywa kuikarabati pamoja na kujenga miundombinu kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu. Napenda kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri inayoifanya kwenye shule hiyo. Kwa kuwa shule hiyo na nyingine zote za vipaji maalum zimekuwa zikifanya

vizuri kwa sehemu kubwa, nashauri kuwa ziwekwe chini ya usimamizi wa Wizara kama ilivyo shule ya msingi Arusha *(Arusha School).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya ufundi stadi, Serikali iliandaa mpango mkakati wa uendelezaji vyuo vya ufundi stadi nchini unaoonesha kuwa zitajengwa vyuo vya ufundi stadi kwenye Wilaya zote nchini kwa kuzingatia maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2010. Ni vizuri Serikali ikatoa kipaumbele kwa *VETA* kwa kuitengea fedha za kutosha kutekeleza mpango mkakati wa mafunzo ya ufundi stadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kuchangia hoja ya Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kuwapongeza Mawaziri, watendaji na Serikali kwa jitihada wanazofanya kupambana na changamoto mbalimbali zilizopo katika sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, naomba pia niseme kuwa mimi ni mdau wa sekta hii ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya elimu ina changamoto nyingi sana kwa Serikali kuweza kuzitatua changamoto hizo kwa wakati inakuwa vigumu haswa ukizingatia bajeti ndogo iliyopewa Wizara hii. Mimi ninaishauri sana Wizara na Serikali kuwapuuza

wanasiasa wanaowazuia kwenye majukwaa wananchi kuchangia michango ya maendeleo ya shule wanaposoma watoto wao. Imefika wakati hata Serikali iweze kukemea jambo hili kwa sababu jambo la maendeleo litafanywa kwa kushirikiana na wadau wote na isiwe Serikali pekee. Suala la kila jambo kufanywa na Serikali ni jema ila maendeleo yatachelewa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shule nyingi za vijijini haswa Shule za Msingi wanafunzi hushinda njaa kuanzia asubuhi hadi saa tisa mchana wanapotoka kwenda nyumbani. Lakini pia watoto hawa walio wengi wanatoka katika familia ambazo haziwezi kuwapatia watoto milo mitatu kwa siku. Kwa sababu hiyo, Serikali ingewapatia hata uji watoto hawa licha tu ya kupata chakula itawasaidia sana kujielekeza katika masomo yao na pia kuipenda shule. Naomba Mheshimiwa Waziri aje na tamko la kuonyesha ni jinsi gani Serikali imejipanga kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuitahadharisha Serikali kuhusu migomo ya Walimu. Walimu ni kada muhimu ambayo ikiamua kufanya ndivyo sivyo Taifa letu litakuwa na matatizo makubwa ambayo athari yake itaonekana baadaye kabisa. Naishauri Serikali kulichukulia jambo hili kwa umakini mkubwa. Pamoja na kuwa madai yao ni makubwa kuzidi uwezo wake ikae na Walimu na kubainisha ni jambo gani linawezekana na lipi haliwezekani ili kuweka umoja utakaoleta manufaa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na kuunga mkono hoja.

**MHE. DKT. TEREZYA L. HUVISA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri kwa kazi nzuri wanazofanya pamoja na watendaji wa Wizara. Elimu ni ufunguo wa maisha hasa kwa wananchi wasio na uwezo wa vijijini. Ninapongeza Wizara kwa kusimamia ujenzi wa Shule za Msingi na Sekondari nchi nzima. Vilevile ujenzi wa vyuo vikuu umetoa nafasi zaidi za kuwaendeleza wanafunzi wengi mpaka vyuo vikuu. Kama shule za kata za sekondari zisingejengwa pamoja na vyuo vikuu ina maana watoto wengi au vijana wengi wangezagaa mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Wizara isimamie kwa umakini upatikanaji wa zana za kufundishia hasa masomo ya sayansi. Wizara iwe makini kusambaza vitabu vya kufundishia pamoja na vitabu vya kiada ili wanafunzi waweze kujisomea. Shule nyingi za kata hazina maktaba sehemu ambayo mwanafunzi anaweza kujisomea hasa wakati wa mapumziko. Uwepo wa maktaba unasaidia wanafunzi kuwa na tabia ya kujisomea na kujenga udadisi na utafiti wa mambo anayofundishwa darasani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikisha wazazi ianze awamu ya pili ya ujenzi wa mabweni hasa kwa wasichana ili kupunguza ugumu wa maisha unaosababishwa na mazingira magumu

yanayowapata wanafunzi hasa watoto wa kike. Ninaomba Wizara iendelee kusimamia vizuri utoaji wa elimu nchini ili kuiboresha elimu na kuwawezesha wanafunzi kujiajiri wanapomaliza mafunzo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Wizara ya Elimu bado haikidhi kutatua kero na changamoto za Wizara hii. Yapo mambo ambayo Serikali ikubali kuyaangalia upya ili kupunguza manung'uniko ya Walimu na sekta ya elimu yenyewe kama vile kuwapatia Walimu posho ya kufundishia ili kuwapa motisha kutokana na Walimu kufanya kazi muda wote tofauti na kada zingine kama vile kilimo, afya na kadhalika ambao wanapata semina/mafunzo ambapo wanapata posho inayosaidiana na mshahara kukidhi au kupunguza makali ya maisha tofauti na Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha *OC* za Idara ya Elimu zielekeze wazi fedha za matibabu kwa Walimu ili watibiwapo waweze kurejeshewa ikiwa na pamoja na fedha za likizo, Walimu wapewe nauli na familia zao. Nashauri Idara za Elimu waandae utaratibu mzuri unaoonyesha kila mwaka Walimu watakaokwenda likizo na malipo yao ya nauli yawe yameandaliwa. Kwa kufanya hivyo, kutapunguza manung'uniko yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ucheleweshaji katika kuwapandisha madaraja Walimu na hata wale waliopandishwa hawalipwi stahili zao kuzingatia

kupandishwa kwao. Kwa mfano waliopandishwa mwaka 2011 Septemba hadi leo hawajalipwa. Nashauri Serikali ili kupunguza manung'uniko ni vema jambo hili likasimamiwa kikamilifu ili kila Mwalimu anapandishwa daraja iendane na stahili yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Ukaguzi, zipo kero katika Idara hii ya Ukaguzi ambazo hazitatuliwi kwa mfano fedha za kuendesha ofisi hizi ni ndogo sana, hazitoshi kwa mafuta, posho zao, kufanya *service* za magari na hata matairi ya magari hufikia kuwaomba au kusubiri matairi yanayotolewa kwenye magari ya Ma-*DC* ndipo wao wayaombe na kufunga kwenye magari yao. Hii ni hatari kwanza kwa usalama wao na vilevile ni kuidhalilisha Idara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya mitaala nako kunachangia, upungufu wa vitabu na mwisho kabisa elimu ya watu wazima imesahaulika. Nashauri kila shule ya msingi pamoja na kuwepo darasa la awali kuwepo na darasa la elimu ya watu wazima, hasa ikizingatiwa kwamba bado kuna idadi kubwa ya wananchi wasiojua kusoma na kuandika na Walimu watakaopewa kuwafundisha wapatiwe motisha kwa sababu watatumia muda wao ambao wangeweza kuutumia kujitafutia riziki kwa njia nyingine za kujipatia kipato.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ikubali kukaa na kujadili maslahi ya Walimu kwa njia ya

mazungumzo na maelewano. Pia kama Walimu wakiendelea kupandishwa madaraja na mishahara yao stahili kwa wakati basi malalamiko yatapungua. Kuna kila sababu ya kutoa motisha au posho za kufundisha ili Walimu wawe na moyo wa kufanya kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Walimu, Walimu walio wengi wanalalamikia kukatwa 2% bila ya kupewa kiasi chochote pindi wanapostaafu kwani CWT tayari ina vitega uchumi vingi kwa kutumia fedha za Walimu. Naishauri Serikali iangalie upya mazingira magumu ya Walimu wanapoishi na kufundishia, tukiwawekea Walimu mazingira mazuri hata matokeo ya wanafunzi ya kumaliza elimu ya msingi yatakuwa mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ilete haraka mabadiliko ya sheria ili elimu msingi iwe Kidato cha IV na mitaala pia iweze kurekebishwa kiasi kwamba mtoto amalizapo Kidato cha IV basi awe na elimu ya ujasiriamali ili aweze kujiajiri kama asipoajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Ukaguzi imedorora sana, hakuna ukaguzi unaofanyika hali inayopelekea elimu kushuka lakini pia wanafunzi wanamaliza darasa la saba wakiwa hawajui kusoma, kuandika na kuhesabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. SAID SULEIMAN SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Mloganzila - ujenzi wa hospitali

ya kiufundi ya kufundishia. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji, umeme na barabara ni kidogo sana, hazitoshi kwa kupeleka au kujenga miundombinu hiyo.  Naishauri Wizara iongeze fedha ili mradi huo uanze kama ulivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile hii itakuwa ni *teaching hospital*, hakuna fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa mabweni *(hostels)* kwa wanafunzi, naishauri Wizara ni vyema ujenzi wa mabweni uende sambamba na ujenzi wa hospitali ili itakapomalizika na mabweni yawe tayari kwa kupokea wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bodi ya mikopo, *means testing,* naishauri itumike kwa kuangalia vigezo hivi vitatu tu navyo ni hali ya Uyatima, Ulemavu na *Current Economical Status* ya Wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fani za kipaumbele, mfumo huu unaleta ubaguzi na sio halali kwa watoto wa kimaskini wanatoka katika shule ambazo hazina Walimu wa masomo ya sayansi, shule zenye ubaha wa maabara na vifaa vya kufundishia. Wale wanafunzi waliobahatika kujiunga na fani hiyo inakuwa sio chaguo lao stahili lakini wanafanya hivyo kwa sababu wanapata mkopo 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanisi wa utendaji kazi wa Bodi ya Mikopo, bado kuna tatizo la ucheleweshaji wa kupeleka fedha kutoka bodi ya mikopo kwenda kwenye vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, urejeshaji wa mikopo, Bodi ibuni mikakati imara na bora ya kuweza kukusanya mikopo ili iweze kupewa wanafunzi wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, school *wash - water, sanitation and hygien.* Shule nyingi hasa za awali na nyingi za sekondari hazina huduma ya kupatikana maji safi na salama, vyoo vya wanafunzi wa kike na kiume, Walimu, mpango wa *school health* haujafika shule nyingi hapa nchini. Shule zilizobahatika kuwa na huduma hizi zinakuwa hazitoshelezi, vyoo vinakuwa ni kidogo ukilinganisha na idadi ya wanafunzi, vyoo vingi ni vibovu, havina milango, havina maji wala sabuni na ni hatarishi kwa wanafunzi, hutumbukia ndani ya vyoo hivyo hali hii inawadhalilisha sana wanafunzi hasa wa kike wanapokuwa katika siku zao. Vilevile hali hii inapelekea wanafunzi wa kike kubakwa. Faida ya kuwepo huduma hizo ni kuongeza uelewa na hasara ya kutokuwepo huduma hizo ni utoro shuleni na kuwa na afya duni inayopelekea wanafunzi kutoelewa masomo yao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Mitihani la Taifa. Malalamiko mengi yametolewa juu ya muundo na utekelezaji wake wa kazi kama unawanyima haki jamii fulani katika Taifa letu, naishauri Wizara ilifanyie kazi tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi za elimu ya juu, miundo ya taasisi hizi za elimu ya juu, uwakilishi na utumishi haukuzingatia pande zote mbili za muungano.

Naishauri Wizara izingatie hali ya uwiano, uwakilishi na utumishi ulio sawa kwa pande zote mbili za muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na Wakurugenzi kwa kuwasilisha hotuba nzuri ya bajeti na yenye matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imekuwa inakumbwa na majanga mengi ikiwa ni pamoja na kuzama kwa meli, mara zote tunapopatwa na majanga haya tunakosa wataalam wazalendo na badala yake kuomba msaada wa wataalamu kutoka nchi kama Afrika ya Kusini na Israel. Misaada hii huchukua muda mrefu kutufikia wakati maisha ya waathirika yanazidi kuteketea. Nashauri Wizara ichukue hatua za makusudi za kusomesha wataalamu wa majanga mbalimbali ambayo hutukabili nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika siku za karibuni kumekuwapo na madai ya mishahara ya makundi mbalimbali wakiwemo Walimu, Madaktari na kadhalika, kwa kuwa kila kada ni muhimu, ni vema kukawekwa chombo cha kutazama mishahara ya makundi mbalimbali kama ilivyokuwa huko nyuma kwa kuwapo kwa *SCOPO.* Hatua hii itapunguza sana malalamiko kwani chambo hicho kitakuwa na vigezo maalumu vya mishahara na pia kuzingatia mfumuko wa bei.

**MHE. ASHA M. JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa sera nzuri ya elimu ya kuhakikisha kuwa kila mtoto aliyefikia umri wa kuanza shule, anaanzishwa shule. Je, kuna tathmini yoyote iliyofanywa kujuwa kwa kiasi gani sera hii ilivyotekelezwa kwani watoto wengi hasa katika familia za watu maskini wanakosa haki yao ya kupata elimu endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango mkakati gani kwa watoto wadogo chini ya miaka 12 ambao hawajaanza shule hadi sasa, watoto hao kuanzishwa shule?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya shule zimekuwa na utaratibu wa kutafuta fedha za mahafali kwa kuchapisha fomu na kuwapa wanafunzi kupita nazo wakiomba fedha. Kwa nini shule isiwe na utaratibu mwingine wa kutafuta fedha kwa ajili ya mahafali bila ya kuwatumia wanafunzi kuomba fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, migomo ya Walimu, tatizo hili sasa limeanza kuzoeleweka mbele ya jamii hali ambayo ni hatari kwa nchi yetu na inarejesha nyuma maendeleo na kudumaza elimu kwa ujumla. Je, Wizara imefanya tathmini kujua nini hasa chanzo cha migomo hii na ni utaratibu gani wa kinidhamu na kimaadili unatumika wakati wa kuwapata Walimu katika ajira zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa mitihani, Serikali inatumia fedha nyingi katika kudhibiti mitihani lakini bado tatizo la uvujaji wa mitihani linaendelea. Je, Wizara imeona suluhu la kuvuja mitihani ni kuwafutia mitihani wanafunzi tu? Aibu hii itaisha lini na Mwalimu yeye anapewa adhabu gani kwa kuwa ndiye chanzo cha uvujaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika eneo moja tu la Wizara hii ambalo ni mitaala ya elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali ilikiri kuwa matokeo ya mitihani yameshuka tangu mwaka 2008. Hii ni kwa sababu kumekuwa na udhibiti madhubuti wa uvujaji wa mitihani nchini. Je, Serikali haioni kuwa kuna haja sasa ya kutumia *"Oral Examination"* baada ya kubaini kuwa mitihani ya kuandika si kipimo halisi cha kuelewa kwa wanafunzi wetu? Kutokana na taarifa za Serikali zinazothibitisha kuwa ufaulu wa wanafunzi wa Kidato cha Nne haukutokana na uelewa wa wanafunzi bali ulitokana na wizi wa mitihani, mitihani kwa njia ya mahojiano itasaidia kupandisha kiwango na ubora wa elimu kama ilivyo nchini Ukraine, Russia na Kwingineko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni ulimwengu wa sayansi kwa hivyo masomo ya sayansi yana umuhimu wa pekee katika shule zetu.

Matokeo yake nchi yetu katika masomo ya sayansi vijana wetu hawapendelei kuyasoma kwa kisingizio kuwa masomo hayo ni magumu. Nchi haiwezekani kuendelea kuwa na vijana (wanafunzi) kupendelea sana kusoma masomo ya sanaa (*art*) basi Wizara itafute ufumbuzi wa changamoto hiyo ya masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya shule nyingi za msingi wameanzisha masomo ya ziada (*tuition*) ya lazima tena yenye malipo, mwanafunzi ambaye anashindwa kulipa ada huenda basi akarudishwa. Mtizamo wangu licha ya nia ya kuwaongezea elimu wanafunzi hao pia zoezi hilo Walimu wanalilazimisha kwa lengo la kujiongezea kipato, malipo ya kila wiki wazee wengine wanashindwa kuzipata hali hiyo inasababisha baadhi wanafunzi kushindwa kwa vipindi fulani kupata mafunzo ya ziada. Ipo haja Wizara suala hili waliangalie upya licha ya kuwa ninaamini siyo sera ya Wizara. Mfano hai wa hali hiyo uko shule ya msingi ya Msasani. Baya zaidi inaonekana hata wazazi hawakushirikishwa katika suala hilo. Naomba tena Wizara walifanyie kazi suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi yoyote inahitaji kufuatiliwa ili kuonekana utendaji wa kazi wenyewe. Hivyo basi kufanya ukaguzi wa shule zetu Kuna uzito wa pekee lakini hali halisi inavyoonekana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi suala la ukaguzi halionekani kuwa na kipaumbele kwao. Haiwezekani Wizara ipange kufanya ukaguzi katika asasi 20,045 na ukafanya ukaguzi wa asasi 6,228, ushahidi wa hilo unapatikana ukurasa 38, kifungu cha 55 cha hotuba ya

Waziri. Je, Wizara imejipanga vipi kuhakikisha kuwa ukaguzi unafanywa kwa mujibu ya wanavyojipangia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wako katika mazingira magumu ya kazi yao lakini pia walio katika mazingira magumu kwa wale Walimu ambao wako katika maeneo ya pembezoni. Ni lini Walimu hao watapatiwa motisha na nyumba za kuishi ili wawe na ari ya kufundisha ipasavyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumetokea nini kwenye shule zetu waliopasisha wanafunzi Kidato cha Kwanza, ili hali wanafunzi hao hawajui kusoma na kuandika. Ni vyema Serikali ikatoa ufafanuzi kuhusu kashfa hii.

**MHE. STEPHEN M. WASIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja hii muhimu kwa maendeleo ya elimu nchini. Katika kujadili hoja hii, ningependa kusisitiza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubora wa elimu, tumefanikiwa sana katika kupanua fursa ya elimu. Tumejenga shule nyingi za msingi na shule za sekondari, asilimia 95% ya watoto wote wanasoma shule za msingi, tumejenga shule za sekondari kila kata, vijana 15 milioni wanasoma sekondari, haya si mafanikio haba. Lakini ni kweli pia ziko changamoto nyingi ambazo zinahitaji kushughulikiwa ili kuimarisha ubora wa elimu. Katika elimu ya msingi, Walimu bado hawatoshi hususani kwa shule za vijijini. Hata katika Wilaya iliyo na Walimu wengi, bado wengi wao wanapenda kufanya kazi mijini na kuziacha shule za vijijini zikiwa na upungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya Walimu kazini iimarishe. Pawepo na *inservice training* ili kuongeza ubora wa elimu kwa Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi katika shule hizi za msingi uimarishwe ili kuimarisha ufundishaji katika shule zetu za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za sekondari ziimarishwe kwa kupatiwa Walimu wa kutosha. Ili kuimarisha elimu, vifaa vya maabara vipatikane. Wizara ya Elimu ishirikiane na Wizara ya Nishati na Madini kufikisha umeme katika shule zote za sekondari za kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya ufundi, ukosefu wa ajira kwa vijana wanaomaliza shule za sekondari na ongezeko la vijana hao kila mwaka, ni hatari sana kwa usalama wa nchi yetu. Ni vizuri suala la kuanzisha shule za ufundi ili kuwapa vijana wetu taaluma za kuwawezesha kujiajiri likaendelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhusiano wa Walimu na Serikali. Kumekuwepo hisia ya kuwepo kutoelewana baina ya Serikali na Walimu. Nashauri tuchukue hatua za makusudi ili kuboresha uhusiano baina ya Serikali na Walimu. Tusiruhusu wapinzani wa Serikali yetu wamiliki hisia za Walimu, kwa manufaa ya siku zijazo, tuangalie maslahi ya Walimu ili tupunguze migogoro. Posho za mazingira magumu zilipwe kwa Walimu hasa wa vijijini ili kuwapa motisha ya kufundisha vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya uraia, kwa muda sasa elimu yetu na mitaala yetu imepuuza kufundisha historia ya nchi yetu na misingi ya uraia wa nchi yetu. Nchi nyingine kama Marekani, hufundisha somo la historia ya nchi yao, sisi watoto wetu hawajui nchi yao ilikuwaje. Kutokana na ujinga wa kutojua historia ni rahisi kudanganywa. Ni vizuri tuanze kufundisha vijana wetu historia ya nchi yetu ili tuwe na vijana wenye kuthamini Utanzania wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na Naibu Waziri wake kwa hotuba nzuri waliyowasilisha. Nasisitiza utekelezaji mzuri wa mipango iliyoelezwa katika hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana mwanzoni niliuliza swali ndani ya Bunge kutaka kuelezwa zoezi la kutafsiri vitabu vya *New Oxford English Course for Schools* limefikia wapi. Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu kuwa ndio kwanza ameingia Wizarani, hivyo halifahamu na kwamba atalifuatilia ili baadaye aweze kunijibu. Nasikitika kusema kwamba hadi leo hii sijajibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitabu hivi ambavyo tayari vimetafsiriwa kwa lugha nzuri, vinavyovutia wanafunzi na hata Walimu, inaelekea kuna *reluctance* na kusitasita kwa Wizara juu ya matumizi ya vitabu hivi kulikoni? Nitashukuru kupata majibu ya Waziri kuwa lini vitabu hivi vitaanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Serikali iliahidi kuwa maabara zitajengwa katika sekondari mbalimbali ikiwa ni pamoja na sekondari za kata lakini hadi leo hii katika Jimbo langu ujenzi huo haujafanyika. Je, ni lini maktaba zitajengwa katika Jimbo langu hasa sekondari za Mtunduru, Sepuka, Puma na Ihanja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo shule za sekondari katika maeneo yenye umeme lakini shule hizo hazina umeme. Nashauri Serikali iweke mkakati wa kuweka umeme katika sekondari zilizopo kwenye maeneo yenye umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ukaguzi katika mashule ni muhimu, naomba ukaguzi uimarishwe na Idara hii ipewe vitendea kazi hasa magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua nini hatma ya Tume iliyoundwa na Rais kushughulikia tatizo la Bodi ya Mikopo inayopelekea kuwepo kwa migomo katika vyuo vikuu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatma ya wanafunzi zaidi ya 300 waliofukuzwa katika vyuo vikuu kikiwepo chuo kikuu cha Dodoma, vijana wanateseka mtaani, wengi ni watoto wa maskini, Serikali iingilie kati vijana hao warudi kumaliza masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana waliomaliza chuo kikuu hasa cha Dodoma wameshindwa kuajiriwa kutokana na vyuo husika kuwanyima kuchukua vyeti kwa kisingizio cha Bodi ya Mikopo kutopeleka ada kwenye vyuo husikia. Je, Serikali inatoa tamko gani kwa wanafunzi hawa kuzuiwa kuchukua vyeti wakati jukumu la kupeleka pesa ni Bodi ya Mikopo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna malalamiko ya kupandishiwa ada kuliko kiwango kilichowekwa na Serikali katika chuo kikuu cha *Saint Francies* cha Ifakara, hivyo vijana kushindwa kupata mikopo ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatma ya madai ya Walimu na kuboresha mazingira yao imefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshajenga *VETA* ngapi?

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kuendelea kuwatambua wanafunzi wa sekondari waliofanya vizuri kimasomo. Ni ushauri wangu kwa Wizara iwatambue hata wale wanaofanya vizuri katika vyuo vikuu ndani na nje ya nchi kwa kuweka vigezo maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yamezungumzwa na wachangiaji wengi pia mimi mwenyewe nimekuwa nikichangia kwa miaka iliyopita juu ya uboreshaji wa

mazingira ya kufundishia, nina imani Serikali itayazingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kuna matangazo yanayokuwa yakirushwa kwenye runinga kuonyesha kuwa wanafunzi takribani kumi wanakaa kwenye dawati moja na wengine kupindukia upande wa pili, je, ni kweli hali hii ipo? Kama si kweli, ni vyema Serikali ikawataka wale wanaorusha matangazo hayo waonyeshe hali halisi hata kama wanafunzi wanakaa chini kuliko kitu wanachokionyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali inafuatilia vipi fedha za elimu zinazopelekwa kwenye Halmashauri zetu? Je, kuna uhakika wowote kwamba fedha hizi zinatumika kama ilivyokusudiwa? Serikali ifuatilie suala hili kwani yapo malalamiko ya matumizi mabaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kuishauri Serikali ifuatilie suala la wahitimu wa Kidato cha Sita kufanya udahili wa vyuo vikuu kwa njia ya mtandao. Wengine wanaishi vijijini maeneo yasiyo na mtandao, kwao inakuwa vigumu sana kupata nafasi kwa wakati, pia mijini kuna wakati mtandao unakuwa si wa kuaminika na kusababisha watoto kuhangaika na kupoteza fedha nyingi bila mafanikio. Katika suala hili, Wizara ifanye utaratibu mzuri wa kuhakikisha kuwa hata wale watakaochaguliwa kujiunga na JKT wanawekewa mazingira mazuri ya kuwawezesha kujiunga na vyuo vikuu kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Elimu. Baada ya pongezi, naomba kuzungumza machache kuhusu Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa Walimu, zipo Wilaya ambazo maeneo ni magumu sana, Walimu wakipangiwa maeneo haya hawaendi kwa sababu ya mazingira magumu. Nashauri Wizara iruhusu Halmashauri kuingia mikataba na wanafunzi wenye sifa kwenda kusoma kozi ya Walimu na baada ya kuhitimu kozi hizo wafanye kazi katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masomo ya kufundishwa, watoto wetu wanasoma masomo mengi mno hasa wale wa madarasa ya chini ya hasa darasa la kwanza hadi la pili. Watoto hawa wasome Kusoma, Kuandika Kuhesabu, Hesabu, na Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitihani, utaratibu wa kusahihisha mitihani kwa kutumia komputa utaleta matatizo kwa sababu miundombinu haijawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kulipa mishahara, wataalamu wa elimu waangalie namna ya kupunguza usumbufu wa kufuata na kusafiri hadi mijini kunako benki na kuwaacha watoto bila elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vya Walimu, kwa kuwa vyuo vingi havina miundombinu ya kutosha na kwa hiyo haviwezi ku-*accommodate* Walimu wengi, nashauri Serikali iruhusu wanafunzi kusoma huku

wakijitegemea kwa malazi ili tuweze kudahili wanafunzi wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimba shuleni, ili kupunguza tatizo hili, Serikali ianzishe utaratibu wa kuongeza au kujenga shule na mabweni kwa ajili ya watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto kutumikishwa, watoto wasifanye kazi za vibarua na kuwatumikia watu binafsi iwe kwa malipo au bure.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kunipa fursa hii siku ya leo kuchangia Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kumpongeza Rais kumteua Waziri Mheshimiwa Shukuru Kawambwa na Naibu Waziri Mheshimiwa Philipo Mulugo kusimamia Wizara hii muhimu na nyeti. Pia nampongeza Naibu Katibu Mkuu na Mwanasheria wa Wizara kwa juhudi zao kusimamia Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ningeshauri pawe na mabadiliko makubwa katika uongozi na utumishi pale Wizarani, malalamiko ni mengi sana na wote wapate mafunzo ya *Customer Charter*. Ni vigumu Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu kufanya shughuli zote wao wenyewe, tunashauri *reform* kubwa katika utendaji wa kazi. Pia nashauri masuala yote ya elimu yaliyoko TAMISEMI yarudishwe Wizara ya Elimu panapoharibika

lawama yote hurudi Wizara ya Elimu, pia TAMISEMI ina kazi nyingine nyingi. Pia nashauri Wizara hii ipangiwe bajeti ya kutosha ili kuondoa upungufu mkubwa uliopo, bajeti iliyoko haikidhi mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara ya Elimu ingeangalia vyuo vikuu vyote kwa umuhimu wake na kutoa vipaumbele kutokana na elimu inayotolewa na pia ishirikishe Wizara zingine husika kuchangia na kutoa maoni ya kuboresha vyuo hivyo. Kwa mfano Chuo Kikuu cha Sokoine *(SUA)* ni chuo kikuu pekee nchini kinachotoa mafunzo ya kilimo, kina changamoto nyingi na Wizara ya Elimu pekee ndiyo yenye jukumu la kuhudumia chuo hicho lakini wenye kufaidika nacho ni Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Maji, Maliasili na Utalii. Wizara zote zingechangia kwa njia moja au nyingine na hata kwa mawazo chuo kingeboreka na upungufu huu usingekuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri Serikali iangalie namna bora ya kuchagua *(selection)* wanaoingia Vyuo vya Walimu. Leo hii wote wale walioshindwa kuingia Kidato cha Tano na kupata *Division IV* point 26, 27 na 28 ndiyo waliokuwa wanaingia Vyuo vya Ualimu, hawa ni wale ambao hawana pa kwenda, wengi hawakupenda Ualimu na hulazimika. Tungekuwa na mfumo wa kupata maoni ya wanafunzi kutoka Kidato cha Tatu na Nne wanaopenda Ualimu ili wawe na uzalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri mfumo wa kupata majina ya Bodi za Shule za Sekondari ungeangaliwa upya usiwe maoni ya Mwalimu Mkuu.

Bodi nyingi hazifanyi kazi inavyopaswa, pawe na uwazi zaidi na ushirikishwaji wa watu zaidi kupata bodi bora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba tuangalie namna ya kuboresha miundombinu na vifaa muhimu ya kufundishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Walimu ambao wanafanya makosa makubwa katika kazi wasihamishwe bali wafukuzwe. Wengi hufanya ubadhirifu wa mali ya shule, utovu wa nidhamu wa kuwa na lugha chafu, utoro, kutembea na watoto wetu wa kike na mara nyingi huhamishwa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wanaoishi katika mazingira magumu na wako maeneo ya vijijini wapewe motisha na kulipwa posho ya mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Walimu wangelipwa *basic salary* na kuongezewa kutokana na ufanisi wa kazi (*performance based increment*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Kitengo cha Ukaguzi kiondolewe Wizara ya Elimu na kupelekwa TAMISEMI kuleta ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pangekuwa na siku maalum ya mjadala na mahojiano juu ya kuboresha sekta hii ya elimu. Kama tutafanikiwa katika elimu basi tutafanikiwa katika sekta zote. Elimu ndiyo ufunguo wa maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia elimu zaidi ingetolewa kwa wanafunzi wanaochukua mafunzo mbalimbali na baada ya kufuzu wanakosa ajira kutokana na *course* waliochukua. Washauriwe kuchukua *course* watakayopata ajira baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri shule za awali ziboreshwe ili tuwe na msingi bora katika elimu. Pia tuanze kuwafundisha watoto wetu namna ya kujisomea na kujieleza. Leo wengi wanakariri na kutoa majibu yanayofanana hawawezi kujieleza, kutoa maelezo kwa lugha na maneno yao, wanaiga ileile iliyopo katika vitabu au aliyoandika Mwalimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba Serikali ikubali maombi ya Wilaya ya Babati kuanzisha Chuo cha Ualimu na Mafunzo ya Ufundi. Tumepata wafadhili na wako tayari kuanza kazi. Hadi leo hii bado makubaliano (MoU) hayajafikia muafaka, kitakuwa chuo cha mfano. Mkoa wa Manyara hauna chuo kingine cha aina hiyo na kinajengwa kijijini kabisa. Tunaomba Serikali itusaidie kufikia muafaka mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu watutembelee Mkoa wa Manyara, wajionee hali ya elimu na kujionea shule tatu za bweni za msingi zilizotumia fedha nyingi za Serikali na wananchi lakini bado hazifanyi kazi iliyokusudiwa na samani kuharibika.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza shukrani zangu za dhati kwa kupata nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu kupitia karatasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani hizo, naomba pia kutoa pongezi kwa Wizara, kuanzia Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu (Kaimu), Watendaji wa Wizara na wakuu wa taasisi zote zilizo chini ya Wizara hii na wakuu wa idara zote, kwa kazi ngumu lakini nzuri wanayoifanya ili kuhakikisha sera ya elimu Tanzania inatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kutoa maoni yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ugatuaji litazamwe upya kwani bado lina utata mkubwa kwani hata ninavyotaka kutoa maoni yangu, sina uhakika ni nani anayehusika kuyajibu labda Waziri anisaidie. Je, Waziri anapofika Wilayani au Mkoani ana nafasi gani kwa *REO's* au *DEO's*? Ana sauti? Je, Mwalimu wa sekondari na msingi yuko chini ya nani? Waziri wa TAMISEMI au Wizara ya Elimu? Yaani taabu tupu, mimi nawashauri kwa mtindo huu, tutachemsha tu ni bora Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ibaki kama ilivyokuwa zamani yaani ishughulike na elimu ya sekondari, shule ya msingi pia ufundi *(VETA),* halafu elimu ya juu irudi kama mwanzo yaani iwe kwenye Wizara ya Sayansi na Technolojia yaani iwe Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, kwa ushauri huo, naamini tutafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mihula ya shule ibadilike, irudishwe iwe kama zamani. Kutokana na matatizo ya uhaba wa Walimu hasa wa sayansi, ambao ndio wamekuwa wasimamizi wakubwa wa mitihani na kusahihisha na hivyo kusababisha upungufu mkubwa wa Walimu mashuleni hasa kwa kipindi wanachoenda kusimamia mitihani mfano muda wa kusimamia mitihani na kusahihisha unapofika Ma-*REO's* na Ma-*DEO's* huwa wanawateua Walimu wote wazuri na ambao ni waaminifu na wanaojituma kufanya kazi ili waende kusahihisha mitihani. Mitihani ya Kidato cha Sita hufanyika Februari kila mwaka na inasahihishwa mwezi Machi. Hivyo utaona ni namna gani miezi hiyo ya Februari na Machi watoto wanakosa taaluma toka kwa Walimu wao, kwani masomo huwa yanaendelea kwa kipindi hicho chote. Mwezi wa nne (Aprili) huwa ni *Midterm*) hivyo utaona ni jinsi gani mambo yalivyo mchanganyiko. Watoto wamewakosa Walimu wao kwa mwezi Februari na Machi, Aprili, wanaenda likizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wanapomaliza *midterm* tu May ikifika Walimu hao wanaondoka tena kwenda kusimamia na kusahihisha mitihani ya Ualimu – *Diploma, Certificate,* shughuli hiyo inafanyika hadi Juni, tayari muda wa likizo umefika. Loh! Jamani hii ni dhambi na dhuluma kubwa kwa watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya Oktoba, Novemba tayari ni kipindi cha mitihani ya Kidato cha Nne na Kidato cha Pili. Baada ya hapo Desemba ni kusahihisha. Kweli hapo naomba tumwogope Mungu, mimi nauliza hivi ni mtaalamu yupi aliyepanga haya? Alikuwa na nia thabiti kweli ya kusaidia elimu? Watoto

tunawalaumu eti ufaulu mdogo, atafauluje? Jamani, *please* naomba nishauri mitihani ya Kidato cha Sita (VI) pamoja na Ualimu iende pamoja kama zamani yaani mwezi Mei ili Juni itumike kusahihisha kwani watoto watakuwa likizo. Mitihani ya Kidato cha Nne (IV) na Kidato cha Pili (II) iwe kama zamani mwezi Novemba ili Desemba itumike kusahihisha wakati wa likizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Walimu walioadhibiwa kutokana na kuvujisha mitihani, imeonekana waliopata adhabu hiyo ni wanaotoka kwenye shule za Serikali tu. Sasa naomba kujua, je, waliotoka kwenye shule binafsi wanafanyiwa nini, yaani ni hatua zipi zimechukuliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu shule binafsi je, taratibu ambazo wanazipitisha kuzifuata, ni chombo gani kinahakiki taratibu hizo ili kuona kwamba hakuna udikteta wa kunyanyapaa na kuwatesa watoto wawapo katika shule hizo yaani haki kutendeka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Wizara itoe tamko au iweke sheria kwa shule zote za bweni iwe binafsi au Serikali kutowaajiri wasichana wadogo waliochini ya umri wa miakia 30 au zaidi kuwa waangalizi wa watoto wa kike mabwenini kwani kumekuwa na sintofahamu kwa mabinti hawa kuwanyanyapaa mabinti wenzao mabwenini. Naomba ma-*matron* hao wawe ni wamama na watu wazima angalau *40 years* na kuendelea. Nasema hivyo kwa sababu nina taarifa zisizo nzuri sana kwa baadhi ya Ma-*matron* mabinti katika baadhi ya shule

wanavyowafanyia watoto wetu mabwenini, ni kheri kuzuia kuliko kutibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi mpango wa *laptop* za kusambaza mashuleni uliishia wapi, ule wa kutoka *USA*? Mbona miaka inatembea bila jibu au hata kuzungumzia tu? Maana tangu Prof. Maghembe alipokuwa Waziri atueleze mpango huo naona kimya, naomba maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi suala la kusimamia fedha za rada liko kwa nani? TAMISEMI au Elimu? Tafadhali narudia, madawati yaliyopangwa kununuliwa kwa kutumia fedha hizo yapelekwe nchi nzima yaani kila Halmashauri ipate hata kama ni dawati moja *please*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze *TEA* kwa kampeni ya kukusanya fedha za kujenga hosteli za watoto wa kike. Hongera sana. Naiomba tu Serikali iendelee kuongeza bajeti kwa *TEA* ili waweze kukidhi haja yao ya kujenga hosteli za wasichana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho pia nawapongeza *TCU* kwa uzinduzi wa vitabu vya mwongozo. Naamini kupitia *TCU* mambo yataboreka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa CWT imeanzishwa kisheria na hivyo kuwalazimu Walimu wote kuwa wanachama bila hata ya kupatiwa elimu ya kwa nini wawe wanachama, matokeo yake hujikuta wakikatwa mshahara bila hata kupewa taarifa ya awali. Sasa swali langu la ushauri, je, kwa nini isiwe ni

suala la hiari kwa Walimu kujiunga na chama hiki (CWT)? Je, Serikali iko tayari kuleta marekebisho ya sheria ili kutengua sheria inayowalazimisha Walimu kujiunga (CWT)?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa CWT ina wanachama ambao ni Walimu nchi nzima na wamekuwa wakichangia fedha nyingi sana kwa taarifa nilizonazo ni 20% ya mshahara wa Mwalimu, hali hiyo inanipa picha ya kuona kwamba huenda CWT inapata, si chini ya bilioni 20 kwa mwezi. Kutokana na makato ya Walimu na ndio maana sasa wanajenga majengo ya uwekezaji kila Mkoa. Sasa nashangaa hivi uwekezaji huo kwa nini wasiwekeze kwa wateja wao ili waweze kufaidi matunda ya uanachama wao!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini CWT wasijenge nyumba za Walimu kwa kupitia mikopo au *Guarantee* ya *BOT* na malipo ya mapango ya nyumba hizo yakaelekezwa kwao kama ilivyo kwenye makato ya kuchangia CWT?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni nani anafanya ukaguzi wa mahesabau ya CWT? Je, Serikali kwa nini isiongee pia na Shirika la Nyumba, *NSSF, PPF* na kadhalika. Ili kupitia *guarantee* ya BOT waweze kusaidia kujenga nyumba bora za Walimu kote nchini na kwenye mazingira ya karibu na shule kwa shule za mijini na vijijini na tatizo hili kwisha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. FENELLA E. MUKANGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri katika Wizara hii muhimu yenye kuwezesha Wizara zingine kufanya kazi hatua kwa hatua kulingana na uwezo ulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri umuhimu wa kujipanga kwa makusudi kuhakikisha "*support forms*" za elimu yenye kujenga masuala ya kushirikiana, kujitolea na kujitegemea yanapewa kipaumbele tangu shule za msingi mpaka vyuo vikuu hata vyuo vya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi, misingi ya hivi vitu hauwezi kubebwa na kutolewa na Walimu tu katika vipindi vya dakika 45 darasani, mwanafunzi mwenyewe hata Mwalimu wa ngazi zote anatakiwa kuendeleza juu ya aliyofundishwa. Ili kufanikiwa kufanya hivyo, nashauri kuwe na msukumo wa makusudi wa kurudisha utamaduni wa kujisomea na kufanya kazi kwa matendo hasa muda wa ziada katika maabara kwa dhati. Isifanyike kiubabaishaji. Utamaduni wa kujisomea ni muhimu upewe msukumo wa makusudi na Wizara ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanafunzi, Walimu na Wakufunzi na hata wananchi wanapata nafasi ya kujisomea vitabu vyenye *"local content"* katika ngazi zote. Hii ina maana basi, maabara, maktaba na kadhalika ziwe kweli za hadhi hizo na ziwe za kutosheleza, wafanyakazi na vifaa, mpango wa uhakika unahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara iwe makini katika kurekebisha shule mbalimbali na umuhimu wa viwanja vya michezo, maktaba na maabara uwepo. Shule zisizo na viwanja, maktaba na maabara pale zinapotakiwa kuwa nazo zipewe muda maalum kuhakikisha wanavyo. Vipindi vya michezo mashuleni viwepo na wazazi pamoja na jamii inayoizunguka shule hizo wahusishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kuwe na mpango maalum wa kusomesha vijana wetu kuweza kufanya kazi katika fani mbalimbali za madini na gasi kama suala la dharura katika ngazi zote - "*artisaus*" na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muwashangae hao wenye kupotosha umma kuhusu suala la elimu nchini. Ni wapotoshaji. Ni hoja za kwenye majukwaa na muda huo waliopewa wakashindwa waambiwe tumetoka huko, tuko kazini tunatekeleza Ilani yetu na tutashinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asimilia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya miundombinu ya shule ya sekondari Same ni mbaya, Wizara itume mtu aitembelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shida kubwa ya Walimu kwenye shule za kata katika Jimbo la Same Magharibi, watoto wanafeli sana. Tunaomba Walimu

angalau saba (7) kwa shule moja. Kuna shule zina Walimu wawili hadi watatu tu, tunaomba msaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Dkt. Shukuru Kawambwa pamoja na Manaibu wake Mheshimiwa Mulugo na Mheshimiwa Majaliwa kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba juhudi kubwa imefanyika katika eneo la kuwezesha elimu kutolewa kwa wananchi wote, hasa waishio vijijini. Nazidi kushauri kuzidi kuboresha mazingira ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la migomo ya Walimu, napongeza sana Serikali kwa jitihada ilizochukua katika kuweka hali sawa juu ya mgomo wa Walimu. Binafsi naunga mkono suala la Serikali kuchukua hatua ya dharura ya kupeleka suala hilo Mahakamani, dola yetu ina mihimili mikuu mitatu Bunge, Serikali na Mahakama. Mahakama ndio mhimili pekee wa kutoa haki na katika kugoma, kuna wengi wanaonyimwa haki wasiostahili ambao ni watoto, ndio Taifa la kesho na (leo) na kwa kweli ndio *potential employers* wa Walimu. Hivyo sikubali kuwa njia ya kugoma ndio sahihi katika mazingira yetu badala yake ni vema kuendelea kukaa mezani ili kupata ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Walimu katika maeneo maalum ya vijiji vya pembezoni. Nashauri ili kupunguza tatizo la Walimu katika maeneo hayo ni

vema Walimu wanaotoka maeneo hayo wapewe kipaumbele ili waweze kupunguza tatizo la Walimu. Hivyo ni vema kuzingatia hilo badala ya watu ambao hawana nia ya kukaa maeneo hayo kupewa ajira na kisha kuripoti na kuondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wananchi kuchangia elimu ni muhimu sana kwani kwa sasa Serikali kutokana na kukabiliwa na majukumu mengi na idadi ya wanafunzi kuongezeka kwa kasi sana, tutajikuta tuna idadi kubwa ya wanafunzi ambao hawatapata nafasi ya elimu katika ngazi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ufaulu wa watoto, ikumbukwe kuwa upimaji wa wanafunzi waliofanya vizuri lazima pia upimwe katika makundi mawili: kundi la shule za vijijini ambazo hazina umeme wala mabweni na mazingira duni, shule ambazo zina mazingira mazuri. Ipo haja ya kutoa *support* kwa wanafunzi wanaotoka mazingira magumu, ama sivyo tutakuta tunawaendeleza watoto wa baadhi ya maeneo tu ambao wanasoma kwenye *facilities* nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, taarifa ya Kambi ya Upinzani inasema juu ya Waziri wa Elimu mtarajiwa lakini kwa tabia hizi za kuhamasisha watu kugoma na kufanya mambo kinyume na heshima na haki ya kuheshimu mihimili ya nchi, dharau na chuki hata kwa viongozi wengine basi itakuwa ni bahati mbaya kwetu Watanzania kupata uongozi wa aina hii. Ni vema kuzidi kuheshimiana na kuthaminiana.

**MHE. ABUU H. JUMAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Taifa limejikuta katika migogoro mingi na mgogoro wa mwisho kabisa ni wa Walimu pamoja na kwamba Mahakama ilitoa maamuzi na kubatilisha mgomo wa Walimu, Serikali isichukulie kama huu ni ushindi. Kuna ujumbe mfupi unaosambazwa katika simu za mkononi kuwa sasa Walimu watafundisha 1+3=13, 3x3= 333 yaani 333, 7x2=77 yaani 77 na kadhalika. Hatua hii ni ya hatari kuliko mgomo wenyewe. Naishauri Serikali iketi na Walimu meza moja ili kuona namna ya kutatua kero yao hiyo. Ni imani yangu kuwa endapo kutakuwepo na nia ya dhati, suala hili linazungumzika na linaweza kufikia tamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusisitiza kuwa mgomo wa kimyakimya (baridi) una athari kubwa sana kwa watoto wetu na Taifa zima. Nirudie kuisihi Serikali iliangalie jambo hili kwa uzito unaofaa ili kuliepusha Taifa na balaa la adui ujinga. Ikumbukwe kuwa toka Uhuru, maadui wakuu ni magonjwa, ujinga na umaskini tusipojihadhari hatutafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nzuri iliyofanyika katika shule za msingi na sekondari imepelekea changamoto kubwa katika elimu ya juu. Mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu imekuwa ni changamoto ya aina yake kwa Serikali. Ni vizuri Serikali iendelee kujipanga kuhudumia idadi kubwa ya wanafunzi hawa wa elimu ya juu la sivyo watoto wa maskini hawataweza kusoma au kwenda vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malimbikizo ya mishahara na stahili nyingine bado ni tatizo katika sekta ya elimu. Naipongeza Serikali kwa kulipa mishahara mipya kwa wakati mwezi huu wa saba. Kwa taarifa zilizopo, Serikali imelipa nyongeza ya mishahara ya asilimia 13 (13%) ambao unaanza mwezi huu wa saba. Hii itaondolea mzigo Serikali kwa siku za usoni kuhusu malimbikizo. Hata hivyo, Serikali ijizatiti kulipa malimbikizo sugu ya watumishi wote wakiwemo Walimu katika Jimbo langu ili wapate moyo wa kufundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata taarifa kuwa baadhi ya Wahadhiri wa *UDOM* ambao walipandishwa daraja toka Novemba, 2010 mpaka sasa hawajalipwa malimbikizo yao ya miezi takribani kumi na sita (16) sasa. Nyongeza ya mshahara walipata Desemba, 2011 baada ya kupandishwa daraja na hata hivyo hawajawekwa katika ngazi sahihi ya mshahara mpaka sasa. Watumishi wetu hawa watapoteza ari ya kulitumikia Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule zetu za kata zinapaswa kuangaliwa kwa jicho la pekee kwani zina changamoto lukiki mfano uhaba wa Walimu, nyumba za Walimu, madarasa, maabara na vifaa vingine muhimu. Shule hizi ndizo hasa zinazobeba 80% ya Watanzania waishio vijijini. Naiomba Serikali itupie jicho katika shule hizi pamoja na Jimbo langu ili tusiwe tunapeleka watoto kwenda kukua na si kusoma kwa sababu ya ukosefu wa vitu nilivyoviainisha.

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri na timu yake kwa hotuba nzuri, naunga mkono hoja kwa asilimia zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri anieleze, ni mwaka wa saba sasa tangu shule yangu ya Ushokola Sekondari waombe msaada wa kujengewa bweni la wasichana na kupatiwa vitabu na vifaa vya maabara. Maombi hayo niliyowasilisha mimi nikiambatanisha na barua yangu ya kuunga mkono maombi haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichoambulia kutoka "*TEA*" ni barua ya kuambiwa tumepokea maombi yenu na tunayafanyia kazi nadiriki kusema kuwa "*TEA*" inajali zaidi sekondari za mjini kuliko zile zetu za pembezoni maana haiwezekani miaka saba tumesubiri na hakuna chochote kinachoendelea, huu ni uonevu. Nafahamu kuna sekondari za mijini zilizowasilisha maombi ya nyuma yetu na zimesaidiwa, *honestly this is not fair*. Naomba maelezo.

**MHE. MAULIDAH A.V. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia leo niwe hapa na kuchangia Wizara hii ambayo ndio tegemeo la kila mja duniani hapa kwani bila ya elimu hakuna maisha wala kesho huko tunakoelekea utakuwa kiumbe mbumbumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ndio kila kitu, kinachoshangaza hapa kwetu viongozi tunaziba macho, masikio na kujifanya hatuelewi kinachoendelea ati kwa bababu maendeleo ya elimu

ni shule za sekondari za kata zilizojengwa kwa wingi nchini, hayo ndio maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri imeainisha changamoto nane ambazo zinawakabili lakini si hizo tu, naomba Wizara waone na hizo ambazo Kamati ya Huduma za Jamii wameorodhesha. Hizi zote ni changamoto zinazoikabili Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa sabini na saba (77) wa hotuba ya Waziri, imeorodhesha kazi ambazo ofisi ya Kamishna itatekeleza katika kipindi cha mwaka 2012/2013. Hizi kazi ikiwa Kamishna atakabidhiwa fedha yaani uwezo atazitekeleza kama ilivyoorodheshwa basi elimu itaboreka lakini haya ni maandishi ambayo tumezoea kuyasoma utekelezaji 'O'.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa themanini na tisa (89), Wizara kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania watatekeleza pia kwa mwaka huu 2012/2013 ni hayohayo, Wizara wana mipango mizuri lakini utekelezaji haupo, inasikitisha na kukatisha tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yangu Wizarani ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile fedha iliyokuwa ikiambiwa inalipwa kwa kila mwanafunzi (*capitation grand*) ambayo ni *dollar* za Marekani 10USD, zimeishia wapi kwani kinachozungumzwa ni maajabu. Naoimba Wizara leo iniambie kutoka Wizarani mpaka

Halmashauri, kufika shule inafika ngapi, wenyewe Wizara wanijulishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Kitabu cha Maendeleo, ukurasa wa thamanini na moja (81) *subvote 2001 Commissioner for Education* ni '*Nil*'. Hii ina maana gani, hii Kamisheni itafanyaje kazi bila ya fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, wazazi wanachangia sana elimu, je, ni lini Serikali itatoa kauli ya maandishi na kuwaambia wazazi wanatakiwa wachangie nini na kwa kipindi gani kuliko kuacha hivi - Walimu popote kutoa kauli au vikaratasi kuwapa watoto wapeleke kwa wazazi wao kuchangia kitu fulani hii hamuoni ni usumbufu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, kwa nini Wizara haijii na mahesabu ya kuonesha wazazi wamechangia shilingi ngapi kwa mwaka uliopita na hata kuwashukuru kwani sera ya nchi ni elimu bure au kuchangia kidogo lakini kinachotokea kuanzia dawati, *uniform*, vitabu vya kiada na ziada, malipo ya mitihani na hata *photocopy* za makabrasha, ni wazazi wanatakiwa kutoa fedha hii ni halali wazazi walipe karo na pia walipie elimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri, hebu tuache utani kwenye elimu, wahusika wakae chini, waangalie elimu ya nchi hii ilivyoshuka kwa watoto kufeli 88.6% na kupasi 11.4%, hii ni ajabu na wanaopasi ni shule za binafsi na *seminary* tu, hamuoni huku ni kujenga tabaka la walionacho na wasionacho? Kwani wanaosoma shule hizo zinazopasisha ni watoto ambao

wazazi wao wana uwezo wa kulipa mamilioni na fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgomo wa Walimu, kwa kweli kuna masikitiko makubwa hivi sasa kuhusu Serikali kutothamini kazi za Walimu na Madaktari na hii inasababisha kuwepo migomo na hata kwa wanafunzi kutokupatiwa mikopo kwa wakati haya yote yanasababisha elimu kuzorota, afya kukosa mwelekeo na wanafunzi kuendelea kuteseka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri, kwanza, Serikali itafute njia ya kupata fedha kwa vyovyote ili kuhakikisha shule zetu zina viwango vya kuwa na madawati, vitabu vya kiada na ziada, maabara na vifaa vyote vya maabara na Walimu wenye uwezo wa kufanya kazi na kuwapatia mshahara unaoeleweka na posho zote, bila hivyo tunajenga nchi ya wajinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mikopo ya wanafunzi iwekwe kwenye akaunti zao mapema, wanaporipoti shuleni wakute fedha ziko tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Serikali ikae upya na Walimu kutatua tatizo sugu linalowapata Walimu, usuluhisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, maagizo yaliyotolewa na Mahakama ya kuwataka Walimu walipe gharama/thamani ya fedha pamoja na au kufidia vipindi, hili lifikiriwe upya kwani Chama cha Walimu hawana uwezo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, Serikali izungumze na Walimu na kuwarudishia morali ya kufanya kazi, kwani inawezekana Walimu wameamua kurudi shingo upande na mgomo baridi unaweza kuwa na athari zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho narudia tena kuomba Serikali ikae, ifikirie tena kuhusu elimu ya nchi hii, Serikali ifanye kila njia kutafuta fedha kunusuru watoto wetu kuwa ni wajinga waliokosa elimu, miradi ambayo Serikali inajiingiza bila kuangalia elimu inavyoporomoka ni maajabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *VETA* ni elimu inayofaa sana kwani itasaidia vijana wetu kuendelea, lakini ufundi bila ya elimu ni kazi bure, wapate elimu ya msingi, ya sekondari, halafu ndio ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kuweka msisitizo elimu, elimu, elimu inamtoa mtu kwenye janga la umasikini na pia kupunguza gharama za matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami nichangie suala hili kama mchango wangu kwa kuwa elimu inashuka kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naishauri Serikali kutekeleza ahadi na kuboresha hali ya Mwalimu pia heshima ya Mwalimu irudi kama ilivyokuwa zamani

pawepo na Wakaguzi Elimu ngazi zote na kuwajengea uwezo Walimu wa kitaaluma zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wa Serikali na Walimu, ni sawa na kutengeneza Taifa ambalo kwa makusudi tena litakalokosa wasomi kwa elimu zote. Tukimjenga Mwalimu kwa kumpatia stahiki zake ataithamini kazi yake ya kufundisha na kufanya vizuri kwa heshima ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya Mwalimu ilivyo sasa kweli tutegemee elimu itakuwa bora elimu na si elimu. Tena Mwalimu anafanya kazi kwenye mazingira magumu, mwendo wa mbali bila vitendea kazi, nyumba hakuna, shule ina Walimu labda watatu au watano, mfano huko Kondoa maeneo ya Sambare na Changaa na karibu maeneo yote tu. Sasa Serikali iangalie pale palipo pagumu warekebishe ili wafundishaji wawe na moyo wa kufundisha na kuwaongezea posho zao na kuboresha mishahara yao, kuwajengea nyumba kama ilivyo maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitendea kazi katika sekta nzima ya elimu ni vichache sana tena baadhi ya shule hapa nchini mfano suala la sayansi, kweli nchi hii tutakuja kosa kabisa Madaktari kwani Daktari hupatikana kuanzia elimu ya msingi na kuendelea. Sasa unakuta shule nyingi hasa Wilaya ya Kondoa hakuna maabara, komputa, vifaa vya kufundishia kwa vitendo, nyumba za Walimu, maji na vitu vyote vya muhimu vinavyomgusa binadamu na hata shule nyingine zipo mbali na makazi ya eneo la shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la upatikanaji mimba wanafunzi shuleni hii inachangiwa na Walimu kutowafuatilia wanafunzi muda wa masomo na Walimu wengine hasa hii pia ilitokea shule moja ya Balangadido huko Kateshi. Mkuu wa shule huwa na mahusiano na wanafunzi nailisha sababisha mgogoro na wanafunzi walimvamia mkuu huyo na matokeo yake wanafunzi hao walichukuliwa hatua na kuwekwa ndani na hatimaye walifukuzwa 80 na kurudishwa kwa adhabu ya kulipa Sh.80,000/= kila mmoja na 17 waliwekwa ndani na kufukuzwa shule. Mheshimiwa Waziri haya mambo yapo maeneo mengi. Hii pia inachangiwa na elimu kusimamiwa na Halmashauri na kusahaulika Wizara muhimu kama hii, sasa Serikali itafute mbadala wa elimu, kujitegemea kuepuka lawama kwa Halmashauri kwani elimu ni mbovu mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali inajitahidi kujenga *VETA* ili vijana wetu wapate ufundi ili waweze kujiajiri lakini hiyo ni dhana tu, vyuo vingi havina vitendea kazi hasa huko Wilayani. Ni lini Serikali itaiwezesha na *VETA* ibadilishe mfumo hasa mitaala yetu hivi sasa inaendana na sayansi na teknolojia hasa ifikapo tarehe 3 Desemba, tunatoka kwenye digitali na kwenda kwenye analojia, sasa vijana wetu wanasomea miaka mitatu, wasiwasi wasijemaliza na wakashindwa kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwafundisha ufundi Mheshimiwa Waziri naomba kwenye mawasilisho yako tueleze tumewaandaa vipi kwa ujasiriamali? Vijana wote hawawezi kuajiriwa mfano

chuo kikuu *SUA* wanaandaa wahitimu wao kwa mikopo na mafunzo ya ujasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufikie dhana za ukweli kuhusu elimu na si kuridhishana kutoa ujinga tu. Mheshimiwa Rais Marehemu baba wa Taifa aliandaa mikakati ya falsafa mpya ya elimu ya kujitegemea kimasomo, elimu ya watu wazima, kisomo chenye manufaa hata hivyo hakubagua elimu, alitoa tamko la wote *(UPE)*, vyuo vya ufundi kwa wahitimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu dhidi ya ujinga, umaskini na maradhi kama adui wa Taifa. Sasa tuangalie mitaala na taasisi ya elimu ya watu wazima na hata sasa kwenye shule za msingi na sekondari, mitaala ina hamahama na hata Walimu kwa kufundisha mashuleni kwa kubadilisha kila mwaka inachangia watoto kutoelewa vizuri, elimu inazidi kushuka na hata Walimu kuandaa masomo ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narejea, shule za kata kujengwa mbali na wanakotoka wanafunzi kufika shule, je, Serikali itazivunja au kujenga bodi hasa katika Wilaya ya Kondoa?

**MHE. VITA R.M. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwapongeza Waziri wa Elimu na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara na Idara zake kwa kazi nzuri wanayoifanya kusimamia na kuiongoza sekta yetu hii ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imewasilisha bajeti yake lakini katika uchambuzi wangu wa haraka

nimeona kuwa katika fedha nyingi za matumizi ya kawaida ambazo ni za matumizi mengineyo, shilingi bilioni 329,962,472,935/= kiasi cha shilingi bilioni 306,000,000,000/= ni kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu. Hili ni jambo jema kwani fedha hizi ni 42% ya bajeti ya Wizara inaenda kuendeleza elimu ya vijana.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba hizi shilingi bilioni 306 zinafanya kazi ya *(human resource development)*, kuendeleza rasilimali watu, hivyo kwa nini tusiziweke katika kifungu cha bajeti ya maendeleo katika miaka inayokuja? Mimi naamini kuwa katika vifungu vya matumizi mengineyo kunakuza vifungu hivyo kuonekana vina fedha nyingi kumbe katika uhalisia wa kufanya kazi za kimsingi za Wizara kunakuwa na fedha kidogo sana ukiondoa mishahara ya watumishi wa Wizara, fedha zinazobaki za uendeshaji mambo ya msingi na ya kisheria zinakuwa finyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Awamu ya Nne, kwa ubunifu wa Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete na chini ya usimamizi wa wasaidizi wake na Makamu Wakuu wa chuo Prof. Kikula na Prof. Mlacha wamesimamia na kujenga chuo kikuu cha Dodoma maarufu *UDOM*. Ningependa tufahamu kwa kuwa mpango uliokuwepo ni wa kujenga vyuo sita na mpaka sasa kuna vyuo vinne vilivyojengwa na kuna vyuo viwili vimebakia chuo cha *Natural Sciences* na *Earth Sciences (Mining And Petroleum Development).* Vyuo hivi ni muhimu sana kujengwa hasa kwa wakati huu ambao nchi yetu inaendelea kuvumbua madini ya aina mbalimbali yakiwemo *gas* na urani. Hivyo

tunahitaji sana vyuo hivi tusomeshe vijana wetu hapa nchini kupata taaluma ya kuja kuendeleza miradi inayoendelea kugundulika nchini kwa kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa jinsi nilivyoona bajeti ya maendeleo ya chuo hiki *UDOM* imekuwa ikishuka mwaka hadi mwaka na mwaka huu wa bajeti 2012/2013 zimetengwa shilingi 3.3 bilioni ambazo niamini nazo ni za kuendeleza ujenzi wa chuo kwa kujenga vyuo hivi, haziwezi kutosha kumaliza ujenzi wake kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kufahamu mpango wa udhamini wa Serikali wa ujenzi wa chuo hichi (*UDOM*) upoje, bado unaendelea au umesitishwa? Sababu mpango ule ulisaidia kujenga vyuo hivyo vinne kwa muda mfupi sana lakini kwa mpango huu wa kutenga shilingi 3.3 bilioni kwa mwaka utachelewesha kufikia lengo la kupata vijana ma-*scientists* wa kuja kuendeleza na kusimamia kazi zitakazokuwa katika miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, tuendelee na mpango ule wa mwanzo kama haujasitishwa wa udhamini wa Serikali ili ku-*fast truck* ujenzi wa vyuo hivi vilivyobakia na kama mpango ule ulikuwa umesitishwa, naiomba Serikali kwa umuhimu nilioueleza na mambo mengine ya msingi ambayo chuo inayafahamu basi urejeshe ili tuweze kufikia azma tuliojiwekea.

Mshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja iliyoletwa mbele yetu. Aidha, baada ya kuunga mkono, naomba nichangie baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufaulu mdogo wa shule zetu za sekondari za kata. Napenda niipongeze kwa nia njema ya Serikali chini ya Chama cha Mapinduzi kwa kuwa na mpango kabambe wa kuhakikisha kwamba kila kata nchini inakuwa na sekondari ya kata. Nia hii njema imepokelewa kwa mwitikio chanya katika Wilaya mpya ya Kalambo na Jimbo la Kalambo na kujenga shule za kata karibu kata zote kumi na saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ambayo tunakabiliana nayo ni ufaulu usioridhisha na hivyo kuwakatisha tamaa wazazi na baadhi ya vijana kwa kuona jinsi waliotangulia walivyoishi vijijini baada ya kushindwa kufanya vizuri na hivyo kushindwa kuendelea na masomo au kujiunga na vyuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ni mbaya zaidi kwa wazazi wenye kipato cha chini pale wanapolazimika kuuza baadhi ya mifugo na wakati mwingine mashamba yao na hivyo kukatishwa tamaa ya kuendelea kuwapeleka watoto wao wengine pale ambapo hawaoni manufaa kwa watoto waliowapeleka shule kwani wamekuwa wakiishia vijiweni. Naishauri Wizara ifanye jitihada za kuhakikisha Walimu na hasa wa masomo ya sayansi wanapelekwa kwenye shule za sekondari za kata ili ufaulu uongezeke na kutowakatisha tamaa wazazi na vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitaala isiyoendana na uhalisia. Nimekuwa nikitatizwa sana na mitaala ya shule zetu za sekondari usiyotambua na kufundisha uhalisia kwa kutambua maeneo mbalimbali ya nchi na kutoa elimu ya kumwandaa kijana kwa ajili ya kwenda kutumia elimu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitaala ya zamani ilitambua uwepo wa michepuo mbalimbali na hivyo kuwa na shule za sekondari za kilimo, shule za sekondari wa ufundi na kadhalika, hali hii imebadilika na hivyo hushangai mwanafunzi anayesomea katika Mikoa inayoshiriki shughuli za kilimo kutoa wahitimu wasiofahamu wala kuenzi shughuli za kilimo. Naishauri Wizara itambue fursa zilizopo nchini na hivyo kwa shule za sekondari zilizopo Mkoa kama Rukwa, Njombe, Iringa, Ruvuma na mingine kama hiyo kuhakikisha masomo ya kilimo yanafundishwa na hivyo kuwa na ujuzi wa kushiriki kilimo. Hali hii inasikitisha, kuna vijana hawako tayari kushiriki shughuli za kilimo, hivi tunajenga Taifa la namna gani kwamba pindi watu wazima wakiondoka duniani basi tutakuwa hatuna kundi la wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa Walimu wa masomo ya sayansi, kama Taifa tuna upungufu mkubwa sana wa Walimu wa masomo ya sayansi. Hali hii hatuwezi tukakubaliana nayo kwani dunia ya leo karne ya sayansi na teknolojia haiwezi kwenda bila kuwa na Walimu wa kufundisha masomo ya sayansi. Naomba Wizara ifanye jitihada za kuhakikisha tunapata Walimu wa masomo ya sayansi hata kama ni kuwapata kutoka nje ya nchi ili tusiendelee kubaki

nyuma katika karne ya ishirini na moja. Ukosefu wa Walimu wa masomo ya sayansi unasababisha uhaba wa wataalam wengine kama Waganga na Wauguzi na Wahandisi kada ambazo ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maslahi ya Walimu bado hayajaboreshwa. Kiwango cha mshahara wa Tshs.277,000/ ni kidogo sana kwani ni wastani wa Tshs.9,000/= elfu tisa kwa siku ambacho kulingana na ukali wa maisha fedha hizi haziwezi kukidhi haja ya chakula cha familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, posho ya kufundishia imekuwa ni kiini macho na kitendawili. Ni mara kadhaa Serikali iliahidi hapa Bungeni kwamba Serikali iko tayari kuwapatia Walimu Posho ya Kufundishia *(Techining Allowance)* lakini hadi leo hakuna mkakati wowote wa kuwapatia fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, motisha kwa Walimu wanaosomesha katika mazingira magumu, mpaka sasa hazitolewi inavyotakikana. Ni jambo la kushangaza kwamba Wizara inampatia Tshs.500,000/= kwa mara moja tu na sio kila mwezi kama inavyotakikana na tarehe 5/10/2011 katika Siku ya Walimu Duniani, sherehe iliyofanyika Uwanja wa Majimaji Songea ambapo Mheshimiwa Rais aliahidi jambo hili la posho la mazingira magumu litapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za likizo kwa Walimu hazipatikani kwa wakati jambo ambalo linapunguza motisha ya kazi kwa Walimu. Ninaishauri Serikali kuwapatia fedha za likizo Walimu kwa wakati unaofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la kupandisha madaraja Walimu imekuwa kero kubwa sana. Mwalimu anapopandishwa daraja na mshahara wake anaandikiwa utabadilika toka kiwango A na kwenda B lakini cha kushangaza mshahara huo unachukuwa mwaka mmoja hadi miaka miwili ndio unabadilika na hata unaporekebishwa mshahara huo lakini malimbikizo ya mishahara hiyo *arreas* hazitolewi jambo ambalo ni kero kubwa, hivyo ni vyema Serikali ikitoa barua ya kupandishwa madaraja Walimu basi uandamane na kupatikana kwa marekebisho hayo ya mshahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kwa walemavu, bado ni tatizo kubwa kwa kundi hili ambapo linaendelea kunyanyasika hata hao wachache wanaokwenda shuleni kwani vitendea kazi au zana maalum za kujifunza kwa walemavu hakuna katika mashule na inapelekea kundi hili muhimu kuendelea kukosa elimu inayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko mengi sana kutoka kwa Walimu juu ya uwepo wa Waraka Na.C/AC.44/45/01/A/84 (awali) na Waraka

Na.CAC.44/45/01/A/121 unaosemekana umeufuta Waraka wa kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyaraka husika ziliandikwa na Katibu Mkuu, ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma zinabagua Walimu, zinakatisha tamaa Walimu kujiendeleza na masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapo juu, kufuatia malalamiko ya Walimu kwa Waraka wa kwanza, hatimaye, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejiment ya Utumishi wa Umma kwa kushirikiana na Chama cha Walimu Tanzania, waliuhariri kidogo Waraka huo katika kipengele cha nne, uhariri ambao kwa wenye macho wanauona kama hadaa kutokana na kasoro nyingi zilizomo kwenye Waraka huo ikiwa ni pamoja na kumbadilishia Mwalimu cheo cha jina tu, lakini unamzuia kupanda cheo cha mshahara kwa muda wa miaka mitatu zaidi bila kujali Mwalimu huyo amelitumikia daraja la mshahara alilonalo sasa kwa muda gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa kama Mbunge wa Jimbo la Kawe, nimezunguka Jimbo zima kutembelea shule 55 za Umma na kuzungumza na Walimu. Nyaraka hizi kandamizi ni kero kubwa sana kwa Walimu, ni rai yangu kwa Serikali kufanyia marekebisho Waraka huu wa mwisho uliorekebisha Waraka wa awali. Kero hizi ndogondogo ndizo zinazowakatisha tamaa Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa ajira za Walimu. Mfumo wa Walimu uliopo sasa una matatizo mengi sana. Mfumo uliopo sasa Mwalimu ameajiriwa na waajiri wafuatao:-

(i) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

(ii) Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

(iii) Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

(iv) Idara huru ya huduma kwa Walimu *TSD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huu ni mbovu na unawasababishia Walimu kero nyingi sana kwa kuwa Wizara hizi zinatupiana mpira wakati wa kutatua kero. Ni bora majukumu yote yanayofanywa na TAMISEMI na baadhi ya majukumu yanayofanywa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma yabakie Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili kuwaondolea Walimu kero zinazosababishwa na uwingi wa Wizara katika ajira ya Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Utumishi wa Walimu *TSD*. Idara hii hapo awali ilikuwa ni Idara ya Utetezi wa Walimu lakini sasa hivi ni Idara ya Utawala ambayo ndiyo inayoongoza kwa uzalishaji wa kero za Walimu nchini kwa kutowapandisha Walimu madaraja kwa wakati, kukalia taarifa mbalimbali za Walimu na hivyo kuwakosesha Walimu haki zao kama vile malimbikizo na mapunjo ya mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni ya Walimu na haja ya uhakiki wa madeni kufanyika upya. Zoezi zima la uhakiki wa madeni ya Walimu yaliyofikia Tshs.49.6 bilioni halikufanyika kwa uwazi jambo ambalo limesababisha Walimu wengi nchini kujikuta wanakosekana katika orodha ya malipo wakati madeni yao ni halali na viambatanisho vyote muhimu vilikuwepo. Licha ya kwamba Wakaguzi wa Ndani wa kila Halmashauri walihusika katika uhakiki wa kwanza uliofanywa na jopo la watu watano kwa kila Halmashauri, lakini cha ajabu Wakaguzi hao wamerudia tena kufanya uhakiki uleule wa kuwa peke yao na kuwaondoa baadhi ya Walimu kwenye orodha ya malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika fedha zilizopelekwa kwenye Halmashauri nyingi nchini kwa ajili ya kuwalipa Walimu hizikulipwa kwa Walimu kama ilivyotakiwa na Walimu wengi waliondolewa kwenye orodha ya malipo huku fedha zao zikiwa zimefika Halmashauri. Mfano Halmashauri ya Manispaa ya Arusha zilipelekwa shilingi 102,000,000/= lakini Mkurugenzi aliwalipa Walimu wachache kiasi cha Tshs.54,000,000/=. Walimu walipoamua kuandamana ndipo Mkurugenzi alipowalipa wote waliotokea kwenye orodha husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasemekana pia kuna Halmashauri moja, ambayo Mkurugenzi alikuwa akiondoa sifuri moja kwa kila Mwalimu anayedai mfano Mwalimu anadai Shs. 7,000,000/= inaondolewa sifuri moja na kulipwa Shs.700,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malamiko ya aina hii pia yapo katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, ambayo Walimu wanalalamika kupunjwa madai yao kwamba walicholipwa na walichohakikiwa ni vitu viwili tofauti. Mbaya zaidi licha ya Walimu kuwa na madai mbalimbali dhidi ya Serikali, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni iliwaelekeza Walimu wakafuate fedha zao benki lakini wanapofika benki wanakuta fedha kiduchu, pasipokuwa na maelekezo yoyote ya kiasi kilichoingizwa ni kwa dai lipi, kwa ufupi zoezi liliendeshwa kihuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai yangu kwa Wizara zote zinazohusiana na masuala ya Walimu kufanya uhakiki wa fedha zilizopelekwa Halmashauri. Kuna tatizo, Walimu wanalalamika wapeni nafasi msikie sauti yao! Hawahitaji fedha nyingi sana, kuna mambo madogo madogo wakitimiziwa tunaweza punguza *"tension"* kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwango vya kodi, kwa kuwa mishahara wanayolipwa Walimu ni midogo sana ukilinganisha na hali halisi ya ugumu wa maisha na kwa kuwa mikataba yao inawakataza kufanya shughuli nyingine za kiuchumi hali inayowasababishia Walimu wengi kufa wakiwa maskini. Ni jambo la busara sana kama Serikali itafikiria kwa kina viwango vya kodi ya mapato wanavyotozwa. Hii inaweza ikawa sehemu mojawapo ya kuwa-*motivate* Walimu wetu.

**MHE. ABAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuwapongeza Mawaziri katika Wizara hii ya Elimu na Ufundi Stadi kwa kazi nzuri wanazozifanya. Nawapongeza sana, Waziri Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa na Naibu Waziri Mheshimiwa Philipo Mulugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili naomba Serikali iangalie kwa makini changamoto zinazowagusa Walimu na kutumia busara sana katika kutatua changamoto zao.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau wengi wa elimu Tanzania ambao ni pamoja na Wabunge, Walimu, CWT, watafiti wa elimu, wamekuwa wakijadili changamoto ambazo zinaukabili mfumo, miundombinu na uendeshaji wa elimu hapa nchini. Baadhi ya changamoto ni hizi zifuatazo:-

(i) miundombinu pungufu (upungufu wa vyumba vya madarasa na nyumba za Walimu; kutokuwepo maabara na maktaba; upungufu wa madawati).

(ii) Zana pungufu (za kufundishia na kujifunzia) hizi ni pamoja na vitabu.

(iii) Mazingira mabovu yasiyompa hamasa Mwalimu kufundisha kwa ari. Hii inatokana na mafao (pamoja na mshahara) yasiyotosheleza; Walimu kucheleweshewa posho na stahili mbalimbali na kutotimiziwa maombi yao ya siku nyingi ya kuongezewa mshahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni baadhi tu ya changamoto, tukifanya uchambuzi wa kina zaidi na kuchunguza jinsi tendo la ufundishaji na ujifunzaji lilivyo katika hali halisi darasani na nje ya darasa, tunagundua upungufu mwingi uhusuo mbinu za ufundishaji zilizopitwa na wakati, vifaa visivyokidhi haja na viwango visivyofaa vya Walimu katika kudhibiti maarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya changamoto hizi ni yale ambayo yamekuwa yakijadiliwa Bungeni, katika semina na katika vyombo vya habari yaani:-

(i) Wanafunzi kuhitimu shule ya msingi bila kujua kusoma, kuandika na kuhesabu. La kushangaza ni kwamba wahitimu wengi wa darasa la saba walichaguliwa kuingia kidato cha kwanza katika mwaka uliopita (2011).

(ii) Ufaulu unashuka. Suala la kushuka "viwango" vya elimu linahusishwa na kushuka kwa ufaulu mwaka 2011, ufaulu katika mtihani wa kumaliza kidato cha nne ulishuka sana kiasi kwamba asilimia 50 ya wahitimu walishindwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni baadhi tu ya matokeo. Suala la msingi ni hili, je, changamoto hizi tuzikabilije? Tukitaka kutatua matatizo yote haya tuchukue hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kuwa hatua ambazo Serikali imekuwa ikichukua hazijasaidia vya kutosha. Nitatoa mfano wa uanzishaji wa shule za sekondari za kata. Shule hizi zimesaidia kuhakikisha kuwa wanafunzi wengi kutoka shule za msingi wanaenda sekondari, lakini changamoto zilizotajwa bado ziko palepale na matokeo yake hasi bado yako palepale, kwa nini? Kwa sababu Serikali haijawekeza vya kutosha. Bajeti ya elimu ni ndogo, ingawa malengo yaliyoelezwa katika Ilani ya CCM (2010-15) Ibara ya 85a-g yanafaa lakini utekelezaji wake utakuwa hafifu kutokana na ukweli kwamba bajeti inayotengwa ni ndogo sana. Tukichukua lalamiko la Wabunge kuhusu kutokuwepo ukaguzi wa shule wa mara kwa mara tunaweza kujiuliza kama ukaguzi haufanyiki, viwango vya elimu vitahakikishwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tutatue changamoto zinazoukabili mfumo wetu wa elimu hakuna njia ya mkato mbali na kuipa elimu na mafunzo ya ufundi kipaumbele namba moja. Ina maana kwamba hata Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 - 2015/2016) umekosewa katika mpangilio wa vipaumbele vyake. Bila elimu, hakuna maendeleo mengine yanayoweza kufanyika. Elimu ndiyo chimbuko la maendeleo yote, nchi ambazo zimeweka elimu kuwa kipaumbele namba moja, kisha zikaweka afya kuwa kipaumbele namba mbili na kadhalika, hazikukosea kwa kuwa zilipiga hatua za uhakika kwa haraka. Mifano ipo mingi, Cuba, China, Urusi na kadhalika. Mfano wa Cuba ni mwafaka kwa sababu ilipata Uhuru mwaka 1959 (sisi tulipata Uhuru 1961), haina rasilimali nyingi – zao lake kuu kwa muda mrefu

lilikuwa sukari lakini hivi sasa mifumo yake ya elimu na afya ni miongoni mwa mifumo bora duniani. Hii ni kwa sababu walitambua kuwa elimu na afya ndio ufunguo wa milango ya maendeleo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hayo niliyosema, napendekeza kuwa kama Taifa lazima tuangalie upya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Baada ya kipindi hiki cha miaka mitano (2010 – 2016) tubadili vipaumbele vyetu. Tukifanya hivyo hatutakuwa tunafanya jambo jipya kwani kwa muda mrefu katika Awamu ya Kwanza elimu ilitiliwa mkazo na ndiyo maana Tanzania ilipata mafanikio makubwa hadi ikawa imefuta ujinga kwa takribani asilimia 90.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongelea changamoto za kielimu, sasa nitajielekeza kwenye tuhuma za rushwa zinazowahusu Maafisa Wizara na kampuni ya Uchapishaji Vitabu vya *Oxford.* Wizarani kuna Kamati ya kupitia na kupitisha vitabu vinavyofaa kutumika kufundishia shule za msingi, shule za sekondari na vyuo vya Walimu. Kwa taarifa tulizonazo ni kwamba Shirika la Vitabu la *Oxford* la Tanzania na Afrika Mashriki limeshiriki katika kutoa rushwa kwa Maafisa Wizarani Tanzania na Kenya ili lipendelewe katika kupata tenda za kuchapisha vitabu vya kiada shule za msingi na shule za sekondari. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia na *SFO* ya Uingereza, Shirika la Uchapishaji la *Oxford* limekuwa likitoa rushwa kwa muda mrefu. Katika tukio la hivi karibuni lililohusisha fedha ya "chenji ya rada" , *Oxford* alipewa tenda ya vitabu *("titles")* 39 tenda ya takribani bilioni 40, wadau wa uchapishaji wa vitabu Tanzania wanadai kuwa

hakuna tenda iliyotangazwa na kwamba vitabu vya *Oxford* si bora kama ilivyokuwa zamani, siku hizi kuna ulipuaji mwingi na kwamba tusipoangalia vitabu hivi vitaua elimu hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maswali mawili ambayo ningependa Waziri ajibu:-

(a) Kwa kuwa *Oxford* imezuiwa na Benki ya Dunia kufanya biashara Tanzania na Afrika Mashariki kwa kushiriki ufisadi, kwa nini msiifukuze kampuni hiyo hapa nchini? Je, tenda iliyokuwa imepewa (vitabu 39) sasa nani atapewa tenda hiyo?

(b) Maafisa wa Wizarani waliopokea rushwa, watachukuliwa hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Oxford* si shirika pekee la kigeni la uchapishaji hapa nchini. Yapo mengi zaidi ya yale ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyataja Bungeni. Yeye alitaja *Oxford* na Macmillan tu, lakini kwa taarifa tulizo nazo yafuatayo yote ni makampuni ya kigeni:-

*(i)* *Oxford.*
*(ii)* *Macmillan.*
*(iii)* *Longman.*
*(iv)* *Longhorn.*
*(v)* *Ujuzi Publications.*
*(vi)* *Heinemann.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Oxford na Macmillan* zilifungiwa na Benki ya Dunia kutoshiriki kazi ya uuzaji vitabu Tanzania na Afrika Mashariki kwa jumla. Swali kwa Waziri, kwa nini *Machmillan* na *Oxford* zisifukuzwe hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tabia ya muda mrefu ya Wizara ya Elimu kukumbatia makampuni ya kigeni ya uchapishaji katika kuchapisha vitabu kwa ajili ya shule na vyuo vyetu. Serikali ya Tanzania ijifunze kutoka Kenya na Uganda ambapo Wizara ya Elimu hutoa tenda zaidi kwa mashirika ya uchapishaji vitabu ya wazalendo ili kuyawezesha yakue ili hatimaye yashindane katika tenda za Kimataifa. Tabia hii ya Wizara ikomeshwe. Watumishi Wizarani watangulize uzalendo, bila kufanya hivyo, tutaendelea kuwa tegemezi na mashirika hayo ya nje yataendelea kutuamlia mambo gani ya kujifunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nimalizie mchango wangu kwa mtazamo chanya kidogo. Wakati tukisubiri Mpango wa Maendeleo ubadilishwe ili elimu ipewe kipaumbele namba moja, yapo mengi ambayo Wizara inaweza kuyafanya ili kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji. Baadhi ya hayo ni:-

(a) Walimu walipwe stahili zao mbali na nyongeza ya mshahara wanayoidai.

(b) Vitabu vya kufundishia na kujifunzia vipatikane katika shule zote.

(c) Mkakati kabambe upangwe na Serikali kukamilisha ujenzi wa nyumba za Walimu, vyumba vya madarasa na utengenezaji wa madawati.

(d) Walimu wapewe mafunzo kuhusu mbinu za kisasa za ufundishaji. Mashirikia yasiyo ya Kiserikali kama mradi wa vitabu vya watoto na kadhalika yashirikishwe katika mafunzo hayo kwa sababu ya uzoevu wao katika nyanja hizo.

**MHE. MANSOOR S. HIRAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, mimi naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya madeni ya Walimu nchini. Naomba haya malipo yanayolipwa taarifa zipelekwe kwa Wabunge pia kwa vile sisi huwa tunapambana na maswali ya hao Walimu kwenye mikutano yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa vyuo vya VETA. Wilaya ya Kwimba imeahidiwa mara nyingi kujengewa chuo hiki, naomba kujua ni lini chuo hicho kitajengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya fedha za Rada. Fedha hizo zipangwe haraka na Mbunge wa Jimbo husika apewe taarifa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa utoaji wa elimu nchini. Mimi naishauri Serikali ifanye uchunguzi wa kina kujua kama Walimu wote wa *primary* na *secondary* na vyuo vya juu wanafundisha vizuri na *there is value for money* kwa sababu wana

mahudhurio mabaya shuleni. *Audit* ifanywe kwa undani ili tujue kama wanafundisha watoto wetu vizuri na wengine wafukuzwe ambao wanaleta mgomo bila sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho mimi naunga mkono hoja hii.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Rukwa unasikitisha sana, hakuna kitu chochote kinachowavutia watoto kwenda shule, hakuna bendi za shule, hakuna utamaduni, hakuna mipira ya michezo hata wazazi nao wanashawishika kuwaoza watoto wao mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Nkasi, kuna shule za msingi kumi na nne zinazofanya mitihani kwa njia ya kuhama shule zao kwenda shule nyingine kwa sababu inasemekana wasimamizi wa mitihani wanaogopa kufia majini. Je, ni kipi kibaya zaidi msimamizi kufia majini peke yake au watoto rundo kufia majini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka majibu ya hatma ya watoto wetu, kubaki kwenye shule zao na kufanyia mitihani kwenye maeneo yao bila bugudha, wasimamizi ambao wanaogopa kupanda maboti kwenda kwenye vituo walivyopangiwa wabaki majumbani kwao na wake zao kwani tunaona ni unyama tunaofanyiwa sisi na watoto wetu, litafutiwe ufumbuzi haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kujua kuna watoto wangapi wa darasa la nne walioshindwa kuingia darasa la tano na ambao wanaelekea kumaliza darasa la saba ambao hawajui kusoma na kuandika pamoja na kujua hatua mlizochukua kwa hao wasiojua kusoma na kuandika. Si vema wakaishia kwenye historia za Mkwawa na Ukoloni, halafu wakarudi majumbani, kwani katika umri wa kumaliza darasa la saba wanakuwa hawajui kitu chochote wala kufikiri kitu chochote juu ya maisha. Hivyo basi Serikali iweke utaratibu wa wanafunzi waliomaliza masomo bila kufaulu wajifunze kazi za mikono chini ya usimamizi wa kijeshi yaani JKT na hili zoezi liwe kwa wahitimu wa ngazi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maadili, wapewe Walimu mafunzo ya kutosha yanayohusiana na malezi ili watoto wetu wajifunze kutoka kwao. Waongezewe mishahara kwa kazi kubwa wanayoifanya. Fedha ipo Serikali ikusanye kodi tuache kukimbizana na ushuru wa wauza nyanya, mchicha na kadhalika. Si hivyo tu watoto wasinyimwe mapigo maana wanapowapiga hawatakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uwepo wa kuwahimiza wananchi wa Kasesya - Wilaya ya Kalambo kuhakikisha wanakuwa na shule yao karibu na maeneo yao kwani kupeleka watoto shule zaidi ya kilometa tano ni mzigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha *Last Events,* kinasema migomo na maandamano vitakuwa ndio chanzo cha taabu duniani. Pamoja na hayo

mafunzo yanayopangwa kwa ajili ya vijana wetu wasifundishwe kiundani wafundishwe juujuu kwani yawezekana wakawa kitanzi kwetu, wafundishwe hasa kazi za kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mawaziri, wakaze buti kwani Wizara hii ni ngumu hakuna kulala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. UMMY A. MWALIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Dkt. Shukuru Kawambwa na Mheshimiwa Philipo Mulugo, Naibu Waziri kwa kusimamia vyema utekelezaji wa sera, mipango na mikakati ya nchi katika sekta hii muhimu ya maendeleo ya watu binafsi, jamii na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujauzito mashuleni na haki ya elimu kwa wasichana. Changamoto ya ujauzito mashuleni imeendelea kuathiri masomo ya wanafunzi wa kike ambapo takwimu zinaonyesha kuwa kwa mwaka 2010 pekee, wanafunzi wa kike wapatao 48,000 waliacha masomo baada ya kupata ujauzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasichana wana haki ya kupata elimu, ni ukweli usiopingika kuwa elimu ndiyo silaha ya kweli itakayomkomboa mtoto wa kike, hivyo ningependa kutoa rai juu ya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuwekeza fedha za kutosha kwa ajili ya ujenzi wa mabweni na hosteli kwa ajili ya wasichana hasa wale waishio mbali na shule. Hapa napenda kutambua kazi nzuri inayofanywa na *TEA* ya kuanzisha kampeni ya kuchangia ujenzi wa mabweni ya wasichana, je, ni lini Wizara itakamilisha Sera Mpya ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi? Rasimu ya Sera hii inatoa nafasi kwa wasichana waliopata mimba kuendelea na masomo baada ya kujifungua. Hivyo nipatiwe maelezo ni lini sera hii itaanza kutumika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninaelewa kuwa tayari kuna hisia na maoni tofauti toka kwa wadau juu ya wasichana wajawazito kuendelea na masomo, rai yangu kwa Wizara ni kuhakikisha kuwa haki ya wasichana ya kupata elimu haiwekewi vipingamizi kwa kisingizio cha mila na desturi zetu. Hivyo Wizara ni lazima ihakikishe kuwa wasichana wanaopata mimba wakiwa shuleni wanapata fursa ya kuendelea na masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi zinazoendelea, nashauri mfumo wa kufundisha TEHAMA uanze sasa kuanzia shule za msingi, sekondari na kuendelea, ili vijana wetu waweze kwenda na kasi ya mabadiliko kwenye nyanja ya mawasiliano ya bahari duniani. Iwapo Serikali haina fedha ya kufanya hilo, basi ikaribishe hata ubia kwa mfumo *Public Private Partnership.*

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuja na mpango wa kuanzisha *VETA* katika kila Mkoa na kila Wilaya ili kukabili tatizo kubwa lililopo la upungufu wa ajira kwa vijana. Hata hivyo, mpango huo hauonekani kufanikiwa kwani Serikali haijatenga fedha zozote kwa ajili ya utekelezaji wake kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha iliyoombwa kwa ajili ya *VETA* ni fedha za kigeni 4,700,000/= fedha hizi sio za kutumainia kwani wafadhili kwa namna moja au nyingine wanaweza wakashindwa kutoa fedha hizo. Je, ni kwa nini Serikali isimaanishe katika kusaidia vijana hasa waliopo vijijini kwa kuhakikisha Serikali inatenga fedha za kutosha na kuanza na Wilaya chache kwa kuzitengea fedha *VETA* ili vijana wapate elimu ya ufundi na hatimaye waweze kujiajiri na kuondokana na umaskini ambao unawatesa kwa kiwango kikubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mpango wa Umoja wa Mataifa kwa nchi zilizoko chini ya umoja wa Mataifa kutekeleza Mpango wa Milenia wa Elimu kwa wote kwa shule za msingi. Serikali yetu haijaweka umuhimu wowote kwa *"Primary Education Development Programme"* kwa mwaka huu wa fedha 2012/2013 na kutenga fedha ili kuboresha elimu ya msingi. Pia hakuna fedha zozote zilizotengwa kwa mwaka huu wa fedha 2012/2013 kwa ajili ya mpango wa "*Improvement of Primary Education*". Ni muhimu

kuweka kipaumbele katika kuboresha elimu ya msingi kwani msingi wa elimu kwa mwanafunzi ukiharibika, matokeo yake ni wanafunzi wasiojua kusoma na kuandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya watu wazima hapa nchini haijapewa kipaumbele. Katika mipango ya Serikali ya kuhakikisha tunakuwa na Taifa lenye baadhi ya watu wazima wasiojua kusoma na kuandika, ni muhimu elimu ya watu wazima ikafufuliwa. Serikali ina mpango gani wa kufufua elimu ya watu wazima ili kuondoa na kupunguza idadi kubwa ya watu wazima wasiojua kusoma na kuandika ambao wameongezeka sana katika miaka ya hivi karibuni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache naomba kuwasilisha.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi uliyonipa ya kuchangia. Nimpongeze Waziri mwenye dhamana na timu yake kwa utekelezaji mzuri wa bajeti ya mwaka 2011/2012 na mpango wa 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai yangu kwa Serikali kupitia Wizara hii kuhakikisha kuwa lugha ya alama inaingizwa katika mafunzo katika vyuo mbalimbali vya sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na vyuo vyote vya kada zote za Afya, Elimu (*TTC*) Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii, Kilimo, Polisi, Sheria, Mahakama na kadhalika. Hii ni kuwawezesha wataalamu wote na walemavu wenye ulemavu wa viziwi na bubu waweze kuwa na mawasiliano chanya wakati wawili hawa

wakielimishana na kupeana ushauri au maelezo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingekuwa vizuri kabisa kama Bunge nalo lingekuwa na watumishi walio na elimu hiyo ya lugha ya alama ili *session* zote za vikao vya Bunge viweze kutafsiriwa na kuelezewa kwa walemavu wa aina ya bubu na viziwi ili wananchi Watanzania hawa waweze kuendena na wananchi wengine na kujua kinachoendelea nchini mwao kwa mazuri (maendeleo) na mabaya (changamoto) lakini pia waweze kusikia jinsi gani Wabunge wao na Serikali yao sikivu ya CCM inavyowajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wauguzi, Wakunga na muda wa mafunzo na hasa Wakunga (*Midwives),* miaka ya nyuma Wauguzi, Wakunga wamekuwa na miaka mitatu ya mafunzo ya Uuguzi na mwaka mmoja wa *Midwifery* (Ukunga) mwaka huo haukuwa na mchanganyiko wa masomo mengine, kwa hiyo angalau Mkunga huyo alikuwa na taaluma (*knowledge na skills* za kuridhisha). Mpango wa MMAM umekuja na program *(crash*) ambapo mwaka mmoja wa Ukunga pia una masomo ya *Mental Health, Communicable Diseases na Management and Leadership* haya yanasababisha Mkunga huyo asiwe na taaluma ya kutosha *(knowledge and skills*) za kutosha na hivyo kusababisha mhitimu asiweze kutoa huduma bora kwa wajawazito na hii hupelekea vifo vinavyotokana na uzazi. *Tanzania Midwives Association*, *Tanzania Nurses and Midwives Council* na *International Confederation for Midwives* mnamo June 2011 Africa Kusini wamezindua mpango unaoitwa *The*

*Competent Midwives* hii ina maana dunia nzima inaridhia mafunzo ya ukunga (*midwifery*) yatakuwa kwa miaka mitatu ili kuzalisha Wakunga *comptent* hii ikisaidiana na mipango mingine kupunguza vifo. Naomba Serikali kupitia MOE & MOHSW wawakubalie Wakunga hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SYLVESTER M. MABUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri na uzalendo wao katika utendaji wa utekelezaji wa majukumu waliyopewa na Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya elimu hapa nchini imekuwa na kupanuka kutokana na juhudi za makusudi za Serikali ya CCM na mwitikio wa wananchi. Hata hivyo, ukuaji wa sekta hii umejielekeza upande mmoja tu wa "*Quantitative*". Sekta ya elimu inakabiliwa na matatizo kadha wa kadha yakiwemo yafuatayo:-

(a) Ubora wa elimu umeshuka kwani shule nyingi hazina vifaa muhimu kama vitabu, madawati, vifaa vya maabara kwa shule za msingi na sekondari.

(b) Shule zina mazingira yasiyowapa moyo Walimu kufundisha (mazingira magumu) ambayo yameshusha morali (motisha) kwa Walimu kufundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza au kuondokana na mapungufu niliyoyataja hapo juu, naiomba Serikali yetu kuboresha mazingira ya kazi kwa Walimu, mishahara ya Walimu iangaliwe upya ili kuwapunguzia makali ya maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa elimu ya vyuo vikuu na elimu ya juu kwa ujumla, sekta hii katika siku za karibuni imekuwa ikikabiliwa na matatizo mbalimbali yakiwemo yafuatayo:-

(a) Serikali imepunguza *O.C.* katika vyuo vikuu vya Taifa (Serikali ) kutoka 1 billion kwa chuo kwa mwaka hadi Tshs 100 milioni kwa chuo kwa mwaka. Naiomba Serikali iliambie Bunge lako Tukufu sababu zilizotumika kufanya maamuzi makubwa kama haya ambayo yameathiri sana uendeshaji wa vyuo.

(b) Utaratibu unaotumiwa wa kuajiri watumishi wa kada zote katika vyuo vikuu vya umma haukidhi matakwa ya vyuo vikuu hivyo. Zamani ajira ilikuwa ikifanywa na Mabaraza ya Vyuo Vikuu hivi karibuni Serikali imeelekeza ajira katika vyuo vikuu ifanywe na Tume ya Ajira ya Taifa. Utaratibu huu umevikwaza vyuo vikuu. Mbaya zaidi vyuo vikuu vimekuwa vikidaiwa "*Bills*" za kuendeshea *"Interviews". Bills* hizi kwa taarifa tulizozipata kutoka vyuo vikuu zimekuwa mzigo mkubwa. Nashauri vyuo vikuu viachiwe jukumu la kuajiri vyenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata maelezo ya Serikali kuhusu deni la malimbikizo ya madai ya vyuo vikuu (*arreas)* ya Tshs.57 bilioni ambazo

zinadaiwa na vyuo vya umma. Serikali ina mpango upi wa kulipa deni hili ili kuwapatia moyo wa kufanya kazi Wahadhiri wa vyuo vyetu hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie mchango wangu kwa kuiomba Serikali ipeleke fedha za maendeleo kwa vyuo vikuu vya umma ili vyuo hivi viweze kutekeleza mipango na mikakati yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha pia naunga mkono hoja.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Tume ya Vyuo Vikuu. Tume ya vyuo imekuwa ikiwapangia wanafunzi vyuo vya kwenda wanapojiunga na elimu ya chuo kikuu, lakini gharama za masomo katika vyuo vyote zinatofautiana, vyuo vingine ada zao ziko juu sana. Hivyo wanafunzi wanashindwa kumudu gharama za masomo hasa watoto wa maskini. Aidha, muda wa kumaliza masomo unatofautiana kwenye kozi inayofanana kutoka chuo kimoja kwenda chuo kingine, mfano Shahada ya Sheria, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam masomo yake ni miaka minne wakati chuo cha Tumaini ni miaka mitatu, hivyo ipo haja ya kuangalia mitaala yao ili iweze kufanana na kuendana na changamoto za sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku hizi ukitaka kujiunga na chuo chochote au elimu ya sekondari unatakiwa kujaza fomu kupitia *Email* jambo ambalo kwenye shule

za sekondari hasa vijijini hawana huduma hiyo. Hivyo pamoja na kwamba ni jambo la kimaendeleo na inarahisisha mawasiliano lakini niiombe Wizara iruhusu kwenye shule ambazo bado huduma za umeme na *internet* hakuna wanafunzi wajaze fomu na kuzikabidhi kwa mkuu wa shule kisha kuziwasilisha Wilayani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Chama cha Mapinduzi inastahili sifa kwa kufanya kazi kubwa ya kuboresha elimu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ijitahidi kutekeleza yafuatayo:-

(i) Malalamiko ni mengi kwa wanafunzi wanaojiunga na vyuo vya Diploma na cheti. Tunaomba udahili wa wanafunzi hawa ufanywe na *NACTE* na sio *TCU*.

(ii) Maabara ziboreshwe kuongeza ujuzi wa kisayansi kwa wanafunzi wa sekondari.

(iii) Naomba ujenzi wa nyumba za Walimu upewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nitoe mchango wangu katika hoja iliyoko mbele yetu. Elimu ni muhimu sana kwa nchi yoyote duniani kwani baada ya afya ni elimu. Kuna umuhimu sasa tukaangalia upya masuala ya elimu yetu kwa sasa tena kwa ujumla, elimu ya awali, elimu ya msingi pia elimu ya sekondari. Elimu hizi ni bora zikaondoka TAMISEMI na zikarudi katika Wizara ya Elimu kwani TAMISEMI kwa sasa imekuwa ni kubwa sana na pale Halmashauri imekuwa ni hatari kwani imefikia Walimu wamekuwa wakishinda Halmashauri kwenye madai yao tu hivi ni saa ngapi Walimu hawa wanafundisha? Ni vema sasa tukaangalia suala hili kwa upana wake, kama hatukuwa makini lengo ambalo tulikuwa nalo hatutalitimiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Wizara ya Afrika Mashariki, Waziri alisema kuwa karibu tutaingia katika umoja wa elimu katika Jumuiya, hivi kweli tutamudu? Hapa kwetu migomo ya Walimu ndiyo hiyo, mishahara nayo tabu, nyumba za Walimu hakuna, hivi Waziri ana habari baadhi ya Walimu wanaishi kwenye godauni za kutunzia pamba na wengine kwenye baadhi ya ofisi za shule? Ndio nyumba za Walimu. Hivyo ni bora kuwajali Walimu, bila Mwalimu hakuna mwanafunzi, bila Mwalimu hakuna Mhasibu, bila Mwalimu hakuna Daktari, bila Mwalimu hakuna Fundi Mwashi. Elimu ni mwanga wa jamii, elimu kwa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Walimu, pia Wakaguzi wa Shule au Wakaguzi wa Elimu hakuna wa kutosha na waliopo hawana vitendea kazi kama

magari, pikipiki ili waweze fika huko kwenye ukaguzi kwa haraka na kufanya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tujiulize, elimu ya *VETA*, mitaala hivi sasa inaendana na zana nzima ya sayansi na teknolojia. Ifikapo Desemba tunatoka analojia na kwenda digitali ni vipi tumewaandaa vijana wetu kimasomo ili kufikia huko? Hivi sasa wanasomo miaka mitatu isijekuwa wakashindwa kuajirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwafundisha ufundi, tumewaandaa vipi kwa ujasiriamali, kwani vijana wote hawawezi kuajiriwa. Mfano, Chuo Kikuu SUA wanawaandaa wahitimu wao kwa mafunzo na mikopo ya ujasiriamali, huko *VETA* ni vipi? Haya yote ni ya kujiuliza kwani bila ajira na kujiajiri ni kazi bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za kata, bila vifuatavyo shule za kata ni bora kuzifunga, Walimu wa kutosha, madawati, nyumba za Walimu, mabweni kwa watoto wa kike na hata maabara. Bila mabweni kwa wasichana tutafuga mimba za utotoni na kuongezeka kwa UKIMWI, bila Walimu tukubali maziro kila baada ya miaka minne, bila maabara masomo ya sayansi ni ndoto, bila madawati uchafu kutokana na umaskini utatumaliza, bila nyumba za Walimu, Walimu hawatakaa katika shule na kulala pasipostahili, maisha shida, umeme tabu, maji kiama. Ni wajibu wetu kwa pamoja tukatambua hayo na kujua tuyatatue vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ni ufunguo wa maisha na pia ni mwanga wa jamii, ahsante.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Wizara kwa kazi nzuri na kubwa ya kuendeleza elimu kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiri kuwepo kwa mapungufu mengi lakini kazi ni kubwa, elimu imepanuka sana na kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuvuja kwa mitihani, naiomba Serikali ijitahidi sana kuhakikisha mitihani ya darasa la saba haivuji. Najua ni ngumu lakini wajibu ni kuhakikisha haivuji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. ESTHER L.M. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza Waziri Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa kwa hotuba yake nzuri aliyoisoma hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nianze kuchangia kuhusu kushuka kwa elimu Wilaya ya Bariadi. Sababu ya kwanza, shule za Bariadi zina mrundikano mkubwa wa Walimu mjini kuliko vijijini, mfano Sima “A” ina Walimu 60 wakati Guduwi “A” ambayo ni ya mwisho Wilaya ya Bariadi ina Walimu watatu. Sababu ya pili shule kukaa muda mrefu bila kukaguliwa na wakaguzi wa shule. Sababu ya ukaguzi kutofanyika, Wilaya toka ianze Idara ya Ukaguzi wa shule haijawahi kupata gari. Sababu ya tatu sasa Idara haijawahi kuletewa mafuta ili hayo mafuta iweze kuomba magari kwenye Idara nyingine ili ikafanye ikakague shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za msingi, Wilaya ya Bariadi tunazo 191 na sekondari 64 za Serikali. Kuna upungufu wa Walimu mjini na vijijini kwa shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu hawana molali ya kufundisha sababu ya kutokuwa na molali ya kufundisha ni mlundikano wa wanafunzi madarasani kwa sababu ya upungufu wa vyumba vya madarasa mfano mahitaji ya vyumba vya madarasa Bariadi ni 3,413 yaliyopo 1,589 upungufu 1,824, madawati mahitaji ni 42,104 yaliyopo 16,486 pungufu 25,608, Walimu kujikita kwenye biashara badala ya kufundisha, upungufu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia mfano vitabu, Walimu kutopata mafunzo mara kwa mara (kuwa-*brash*) pindi mtaala unapobadilika. Wanasiasa huchangia kushusha elimu kwa kushinikiza wananchi kugoma kuchangia maendeleo shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ili elimu iboreke shule za msingi na sekondari zikaguliwe mara kwa mara na wakaguzi wa shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia bajeti hii muhimu kabisa kwa maendeleo ya nchi yetu na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukishuhudia kushuka kwa elimu kila mwaka, ukweli ni kwamba elimu

bora itapatikana iwapo tu viwezeshi vitakuwepo kwa maana ya wanafunzi kuweza kuwa na elimu bora na hata wataalam bora ambao wataweza kulitumikia Taifa letu. Wanafunzi wawe na uelewa mzuri wa kuweza kuhamisha elimu waliyoipata kwa nadharia darasani kwenda kuutafsiri kwa vitendo. Viwezeshi hivi muhimu ni kama majengo, madawati, vitabu, maktaba, maabara, Walimu na mazingira imara na mazuri ya kujifunzia ambapo hamna kelele wala mwingiliano ambao hautasumbua uelewa baina ya mfundishaji na mfundishwaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajitahidi kuchambua changamoto kwenye hivi viwezeshi *(inputs)* mbavyo vikiwa imara tunapata *good product* (elimu bora) au wanafunzi bora waliohitimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya Walimu kwa wanafunzi ni changamoto kubwa sana. Mimi ni Mwalimu na ninajua/uzoefu ya kuwa idadi ya wanafunzi ikiwa kubwa kwa Mwalimu uelewa daima ni mdogo kwani uelewa kati ya mwanafunzi mmoja na mwanafunzi mwingine ni tofauti, wengine huelewa moja kwa moja, mwingine mpaka utoe mfano/mifano, mwingine lazima umshirikishe kwenye *discussion* na wenzake na kujisomea nyumbani. Kulingana na maelezo ya kitabu cha Waziri, uwiano wa Mwalimu na mwanafunzi ni 1:51 mwaka 2010 hadi 1:46 mwaka 2012, huu uwiano wa Mwalimu kwa mwanafunzi hata miujiza ishuke toka mbinguni hatuwezi kamwe kuwa na wataalam bora waliopata elimu bora. Hii ni *ration* ya shule za msingi kwa wastani wa nchi nzima lakini kiuhalisia shule za pembezoni na hasa zile za vijiji

unakuta uwiano ni 1:80 hadi 1:100, hii ni hatari sana kwa mustakabali wa elimu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni uhaba wa vitendea kazi kama vitabu kwa uwiano wa mwanafunzi. Hivi sasa vitabu ni changamoto kubwa sana. Mimi nakumbuka enzi zetu tulikuwa tunapata vitabu vya kuenda navyo nyumbani lakini kwa sasa ni ndoto, watoto hawana hata vitabu vya kujisomea nyumbani. Hii nayo inachangia sana kushuka elimu ya wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni kuhusu ukosefu wa madawati na kupelekea watoto kukaa chini tena kwenye vumbi, hata ufuatiliaji wa masomo unakuta haupo tena wengine wanafanyia mtihani na kusomea kwenye miti. Hili nalo ni janga, inabidi Serikali itoe suluhisho la haraka kwa haya kama kweli wana imani ya kuwapatia Watanzania elimu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umuhimu wa maktaba tena yenye vitabu vinavyoendana na karne ya sasa, kwani shule nyingi za msingi sekondari, hata *FDC* hazina maktaba na kama ipo ni jengo tu bila vitabu wala komputa. Tena cha kusikitisha kuna vyumba vya Walimu mfano kile cha Tarime havina maktaba inayokidhi hadhi ya maktaba bali ni ile maktaba iliyojengwa mwaka 1986, vitabu hamna, maabara hamna. Vilevile chuo cha *FDC* Tarime hakina maktaba kabisa wala vitabu. Ni kuhusu ukosefu wa maabara kwenye shule zetu, vyuo vyetu hasa vya Walimu na *FDC*, wakati huohuo tunasema tunatoa kipaumbele kwa masomo ya sayansi ambayo

yanaendana sambamba na uhitaji wa maabara, sasa bila maabara sayansi itafundishwaje, jamani tuwe wahalisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ambayo ni ya muhimu sana tena inayohitaji uharaka kushughulikiwa ni juu ya motisha kwa Walimu ili wawe na morali ya kufundisha watoto wetu, kuliko sasa Serikali inavyowabeza Walimu. Tuwape nyumba za kutosha kwa makazi yao, posho ya kufundishia, mshahara mzuri, hata usafiri kwa wale waishio mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwapongeza wote hasa Naibu Waziri kwa juhudi katika kuibua uozo ili kuboresha elimu ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia juu ya shule zilizoko pembezoni na hasa vijijjini ambapo Walimu wanafundisha kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa sita na dakika ishirini mchana. Baadaye wanakwenda kula na kurudi saa nane ambapo wanaendelea hadi saa kumi na moja. Hapa napenda kujua je walimu hawa wanalipwa posho ya ziada yaani (*overtime)* kwani wengine kwa maana shule zingine hazifundishi kwa ratiba hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kujua kama Serikali ilishafanya *analysis*, kujua ni jinsi gani hii ratiba ya kupumzika kwa ajili ya *lunch* inavyodhozotesha elimu ya vijana na watoto wetu. Kwani wengi wao huchelewa kurudi hadi saa 9 au 10 na hivyo kukosa masomo kwani wakifika nyumbani lazima wafanye kazi

na wengine hukaa mbali na shule wanazosoma. Hii ni hatari sana kwa mustakabali wa elimu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni kuhusiana na *drop out* ya wanafunzi na sababu walizotoa Wizara katika kitabu cha hali ya uchumi sura ya 19 ni kuwa kukatisha masomo shule za msingi ni takribani 3.4% na sababu kubwa ni utoro, mimba za utotoni na kushindwa kumudu mahitaji ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia hili la wanafunzi kuacha shule kwa sababu ya kushindwa kumudu gharama za msingi, hivi kweli Serikali imeshindwa kuwekeza kwa asilimia mia moja ili tuweze kupunguza utoro unaotokana na kundi hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kuiomba Wizara itupe takwimu za hao walio *drop out* ni asilimia ngapi ilitokana na sababu ya utoro wa kawaida na ni asilimia ngapi inatokana na mimba za utotoni? Pia asilimia ngapi ni ukosefu wa mahitaji ya msingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi sana nizungumzie kuhusu ujumla wa wanafunzi wetu hasa kwa shule za msingi na sekondari. Waziri kaeleza kuridhishwa na ongezeko la ufaulu. Lakini ukweli ni kuwa ufaulu kwa takwimu umeongezeka lakini kiuhalisia asilimia ya watoto waliofaulu na wenye uelewa ni ndogo sana labda asilimia 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe nina mfano, kuna mtoto wa kaka anaitwa Ghati Mwita, alimaliza shule ya msingi Nyabirongo eti kwenda shule

ya sekondari Mwema ambapo Mwalimu Mkuu wa shule ya Nyabirongo alileta *form* ya Ghati kujiunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri akanikuta nipo nyumbani kwa Mzee Matiko, kwa masikitiko ile *form* nilimpa Ghati aisome na alishindwa, hata jina lake kuandika hawezi. Cha ajabu Mwalimu Mkuu alisema kuna afadhali hivyo Ghati kwani kuna wengine hawajui kusoma wala nini na wamefaulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hasira nilimrudishia ile *form* Mwalimu Mkuu na kumwambia mwanangu haendi. Hii ni fedheha sana na Walimu katika shule hizi hadi leo hawajawajibishwa. Hili pia linachangiwa na kutokuwepo na ukaguzi ambao ungesaidia sana ku-*monitor* ufundishaji wa Walimu pia mrejesho wa kwamba wanafunzi wanaelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana kuwa ukaguzi ulifanyika kwa asilimia chini ya 50. Hii ni fedheha na ukiangalia ni majumuisho tu kwa shule za msingi na sekondari zilikaguliwa kwa asilimia chini ya 40. Daima kwa kasi hii hatutakuwa na elimu bora, bali bora elimu, yaani *quantity and not quality of education.* Hii ni changamoto kubwa ambayo sharti ifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya mkopo wa wanafunzi. Fedha iliyopangwa (Sh.306 bilioni) kwa ajili

ya mkopo wa wanafunzi ni ndogo sana. Serikali itumie *Treasury (Special) Bonds* kwa ajili ya "*Elimu Fund"* ambayo itawahusisha wawekezaji kama "*Micro Finance*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za maendeleo, hali kadhalika Sh.92.8 bilioni ni ndogo sana. Kutegemea bajeti ya Wizara Serikali haitaweza kutekeleza mategemeo ya kuleta maendeleo ya TEHAMA, vyanzo mbadala vitafutwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya msingi, ili kuhakikisha wanafunzi wote wanapata elimu kamili ya shule ya msingi hasa kujua Kusoma na Kuandika na Kuhesabu, mwanafunzi asivuke darasa bila kuridhisha kwamba amefahamu kwa kiwango husika. Mwalimu Mkuu wa shule ya msingi awe mkaguzi mkuu. Swali, nini kazi ya Waratibu wa Elimu wa Kata iwapo kama wanafunzi wanafika hadi darasa la saba bila ya kujua Kusoma na Kuandika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, migomo ya Walimu, ili kuzuia migomo kama ya hivi karibuni, Serikali iache kufanya kazi kwa mtindo wa zima moto (*fire fighting*). Serikali iwe *"Proactive*" na hatua stahili ichukuliwe bila kucheleweshwa *(action should be taken timely).*

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, viwango vya ukuaji katika utoaji wa huduma za elimu, ni ndogo sana na hii inasababishwa na mipango yetu ya elimu kutokaa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kwa nini tunaimba wimbo huu siku zote na Serikali haichukui hatua hata kama tafiti zimesema? Mfano utafiti uliofanyika 2010 chini ya *MOEVT PETS* ulionyesha yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, lazima kuwepo posho maalum ya Walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu. Pili, *Allowance* hizo ziangalie eneo na eneo kama shule zilizo milimani, sehemu za ndanindani kabisa ambapo hata miundombinu za jamii ni shida, shule za visiwani na kadhalika. Tatu, walishauri vivutio kama vile *Hardship Allowance, Promotion* za haraka, kupandishwa mishahara haraka, *Housing Allowance, Special Study Leave, Training Opportunities*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa hizi zikitolewa kulingana na mazingira ya sehemu mfanyakazi alipo, itaongeza mvuto kwa Walimu na watafika vituoni mwao watakapopangiwa kuliko hali ilivyo sasa. Nashauri Serikali iangalie yale iliyokuwa imeyakubali kama walivyo wenzetu Uganda, Malawi, Lethoto na Mozambique, tupunguze kero hii kwa kiasi kikubwa na Walimu wenyewe wataomba kwenda vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri Serikali iwe na mikataba na kila mwanafunzi anayejiunga na chuo kikuu na akapata mkopo akubali kuwa kwa kipindi cha miaka mitano ataitumikia Serikali popote itakapompeleka na baada ya hapo awe huru kwenda kokote anakotaka, ama sivyo kila siku tutafundisha Walimu na bado wataondoka, hawana kibano. Kwa

misingi hiyo, ni ngumu sana kufanikisha maendeleo ya elimu.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini vyuo vya Kislam au shule zinazotambulika kama Alharamain, wanapohitaji *equivalence* wananyanyaswa na kusumbuliwa sio kama vyuo vingine? Hii inaleta usumbufu na hata kuwadhalilisha.

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja asilimia mia kwa mia kutokana na kazi kubwa inayofanywa na Walimu wa shule ya msingi, sekondari na vyuo vya ualimu na vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ya Elimu iangalie *perfomance* ya wanafunzi wa Zanzibar na mtihani wa pamoja kati ya Zanzibar na Bara na jinsi wanafunzi wa Visiwani wanavyokuwa na nafasi ndogo ya ufaulu. Naomba Serikali iliangalie suala hilo kwa umuhimu wa kipekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Mitihani linawezaje kupitisha mwanafunzi asiyeweza kusoma wala kuandika wakati Walimu wanarekodi maendeleo ya mwanafunzi toka darasa la V-VII?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ijitahidi sana katika kuandaa miundombinu ya walemavu na kuwasaidia kupata vifaa, shule za walemavu na shule za wanafunzi wasio walemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu ni kubwa sana na inatakiwa ipewe fedha nyingi kuweza kusaidia kupambana na changamoto za elimu. Bajeti ni finyu, iongezwe kusaidia Walimu angalau wapewe posho ya mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza hotuba nzuri sana. Naamini tunajua kuwa Walimu ndio kiwanda mama cha kutoa wataalam wote duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, mishahara yao iangaliwe upya hasa ule wa kima cha chini, Wizara iwe karibu na Walimu ili iyajue matatizo na kuyapatia namna ya kuyatatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ijenge ukaribu na Chama cha Walimu ili kujadili hoja mbalimbali zinazowahusu Walimu ili kuondoa misigano na maandamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo itimize wajibu wake kwa umakini zaidi ili wale wote wanaostahili kupata mikopo basi wapewe bila ya matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Mitihani la Taifa liwe makini sana. Tatizo la kufutiwa matokeo mwaka uliopita limeleta hali tete sana katika Taifa.

**MHE. SALEH A. PAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Napenda kuwapongeza kwa hotuba nzuri yenye mwelekeo mzuri. Nawapongeza sana kwa uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la I-VII. Tunaamini kabisa kwamba tutaweza kufikisha na kufikia lengo la MDG ifikapo 2015. Kinachotakiwa ni kwenda na kasi hiyo kwa kuimarisha elimu, kwa kuongeza Walimu na vifaa elimu kama madawati na vitabu na vitabu vya kiada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya watu wazima. Wakati wa enzi za Mwalimu tulifikia *literacy level ya at least* 90% sijui hali ilivyo sasa, lakini naamini kwamba tumerudi nyuma, nadhani tuko chini ya asilimia 60. Hili ni eneo ambalo inabidi tulitilie mkazo iwapo tunataka maendeleo ya sayansi na teknolojia lazima tuwe na *literate society*. Enzi zile za elimu ya watu wazima ya Mzee Kibira, lazima zirudishwe kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishaji wa vyuo vikuu, napenda kuipongeza Serikali kwa upanuzi wa vyuo vikuu, *UDOM* itakapokuwa *"in full capacity"* kitakuwa na wanafunzi 40,000 kazi ya kuendeleza *faculties* ziendelee kwa kasi zaidi. Hongereni kwa kuongeza *College of Education intake by* 10,000 (2012/13), hongereni pia kwa kuendeleza *School of medicine intake* ya 3500 *this is a great achievement and must be fulfilled and achiewed by 2015 as per CCM election manifesto*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunapanua elimu ya chuo kikuu, ni vyema tukapanua elimu za ufundi. Wenzetu wa Uingereza wanakwenda sambamba na

ujenzi wa *polytechnic.* (*District Vocational Training Center Programmes*) ni *programme* ambayo inatakiwa iende kwa kasi kubwa. Napenda kujua *time frame* ya mradi huu, ni *programme* ya miaka mingapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha maabara kwa sekondari, Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya maabara kwa sekondari, kama kweli tunahitaji kwenda sambamba na sayansi na teknolojia hili lazima litiliwe mkazo. *SEDP II* itilie mkazo katika maeneo ya maabara na vifaa vya shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Secondary *Schools Rehabilitation Programme,* zamani DANIDA walifadhili mradi huu *in the 1990s*. Ni vyema mkabuni mradi wa ukarabati wa sekondari zetu. Hali ya miundombinu ya sekondari, majengo, mabweni, vyoo ni mbaya sana. Elimu lazima itolewe katika mazingira mazuri.

**MHE. MWIGULU L.N. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, niipongeze sana Serikali kwa jitihada zake za kuboresha elimu. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa jinsi wanavyomudu Wizara kwa nia njema ya kuboresha elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze kipekee kama nilivyotumwa na wazazi wa watoto walipata msaada wa Naibu Waziri kupata wa nafasi za vyuo kwa ushauri wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa jitihada zake za kuwa na sekondari kila kata. Hii itatusaidia sana kwa watoto wengi wa vijijini kupata elimu ya sekondari. Naiomba Serikali itoe kipaumbele ikianza na Walimu, vitabu, maabara na mabweni. Hii itasaidia sana kuwafanya wazazi walioshiriki katika kuboresha na kujenga shule hizi waweze kuona Serikali inajali na inaunga mkono nguvu ya wananchi, nguvu ilenge zaidi vijijini kwa upande wa Walimu kwani watoto hao hawana hata masomo ya ziada wala vitabu kwani hamna maktaba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naiomba Serikali itoe kauli sasa na kampeni kuwa tunachukua hatua gani kama Taifa, kwamba sasa tunaanza na mabweni kila kata, kama tulivyohamasisha wananchi wakati wa kujenga madarasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naiomba Serikali ianze utekelezaji wa mpango wa kila tarafa kuwa na sekondari yenye kidato cha tano na sita kwani shule nyingi sasa za kata wanaanza kutoa vijana waliomaliza kidato cha nne tokea shule za kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine niiombe Serikali ishughulikie matatizo ya mikopo ili kupunguza migomo katika vyuo vikuu kwani mingi inatokea kutokana na mapungufu kwenye Bodi ya Mikopo kwa ujumla wake. Pia Serikali inatambua uwepo wa Serikali za wanafunzi vyuoni, ikitokea migomo, Serikali huwatumia viongozi wa Serikali za wanafunzi kwa majadiliano na makubaliano, lakini punde mgomo unapoisha Serikali huwachukulia hatua wale

wawakilishi wa wanafunzi waliokuwa wakiongea kwa niaba ya wenzao. Hii ni kuwaonea sana viongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho niombe Serikali iangalie uwezekano wa kuwa na utaratibu wa kuwalipa posho Walimu katikati ya mwezi ili kupunguza makali ya maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Waziri wa Elimu, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na Watendaji wengine wa Wizara hii kwa utekelezaji wa masuala mbalimbali yanayohusu elimu hapa nchini ingawa kuna changamoto nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Elimu ya mwaka 2010 bado haijapatiwa ufumbuzi na sijui tatizo liko wapi kwani mabadiliko yanayoikumba jamii yetu ya mara kwa mara yanatulazimu kubadiilsha mitaala pamoja na sera ya elimu. Sera ya Elimu ya mwaka 1995 ina mapungufu makubwa ambayo yamepelekea sekta ya elimu kuwa shamba la bibi hapa nchini. Ili kuhakikisha kuwa sera hii inaanza mara moja kutumika Serikali haina budi kuiharakisha sera hii na kuipeleka kwa wadau ili kupata maoni na hatimaye ianze kazi mara moja. Vitu vya kuzingatia katika sera hi ni elimu ya uzalendo, utaifa, utamaduni wa asili, somo la maadili, sera ya lugha ya kufundishia, somo la ujasiriamali na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la matatizo ya Walimu nchini, kwa masikitiko makubwa, naomba kuishauri Serikali iangalie ni namna gani ya kuwakuhudumia Walimu hapa nchini. Mfumo wa sasa wa kuhusisha Wizara nyingi kuwahudumia Walimu hapa nchini ni tatizo kubwa sana. Mathalani Hazina, Wizara ya Fedha, Wizara ya Elimu na Wizara ya TAMISEMI zote huhusika kwa namna moja au nyingine kumhudumia Mwalimu. Je, Serikali haioni kuwa inaleta urasimu usio wa lazima katika kumhudumia Mwalimu? Kwa nini Wizara ya Elimu isihusike moja kwa moja na majukumu yote yanayomhusu Mwalimu? Naishauri Serikali kupitia Wizara hii iangalie ni namna gani ya kumhudumia Mwalimu ili aepuke usumbufu usio wa lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Elimu Tanzania (TET). Ifahamike wazi kuwa kuwepo kwa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) kulisaidia kwa kiasi kikubwa kuangalia, kuandaa na hata kuchapisha vitabu vilivyokidhi mahitaji ya Watanzania. Lakini kutokana na uchu na matumizi mabaya ya madaraka, Serikali iliamua kukwapua vitabu vya Taasisi ya Elimu na kuviuza bure kwa wachapishaji binafsi. Hali hii imepelekea tumekuwa na utitiri wa vitabu usio na tija katika nchi yetu. Naishauri Serikali iwezeshe Taasisi ya Elimu Tanzania iendelee na jukumu lake la kuandaa vitabu vya kiada katika shule za awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu. Vitabu vingine vya ziada ndivyo viandaliwe na wachapishaji binafsi. Hali hii itaepusha suala la rushwa katika sekta ya vitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Elimu ya Watu wazima (TEWW), ni ukweli ulio wazi na dhahiri kuwa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima imesaidia kwa kiasi kikubwa kuendeleza elimu kwa mfumo usio rasmi hapa nchini. Tatizo kubwa linaloikabili Taaisi hii ni upungufu wa fedha na kuwa chini ya Kamishna wa Elimu. Naishauri Serikali kupitia Wizara hii itenge fedha za kutosha za kuiendesha taasisi hii, pia iandae rasilimali watu wa kutosha na isiwe chini ya Kamishna wa Elimu, aajiriwe Katibu Mtendaji wa kuisimamia taasisi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la matabaka katika mfumo wa elimu nchini, elimu ni urithishaji wa maarifa, mila, desturi, mienendo na falsafa ya jamii toka kizazi kimoja hadi kizazi kingine. Lengo kuu la elimu ni kumtayarisha mwanajamii ili awe mtumishi mwema katika jamii yake. Katika daraja hizi mbili, jamii na msomi, jamii ni muhimu zaidi kuliko msomi, lakini msomi pia ana ngazi muhimu katika jamii yake. Mfumo wa utoaji wa elimu katika nchi yetu ambao umeruhusu matabaka katika shule zetu hadi sasa unalitesa sana Taifa letu. Mathalani kuwepo kwa Shule za Sekondari za Vipaji Maalumu (Serikalini) na kuwepo kwa Akademia za Kimataifa na *English Medium Schools*.

Mheshimiwa Spika, kwa hakika, tusipochukua tahadhari mapema, tutazalisha tabaka la juu la wasomi, tabaka la chini la wasomi ndilo litakalobeba mzigo mkubwa wa maumivu, litadharauliwa, litanyonywa, litaonewa, litadhalilishwa, litadhulumiwa, litatukanwa, litakashfiwa, litapuuzwa, litabaguliwa, litakandamizwa, litachukiwa, litateswa, litasulubishwa

na mbaya zaidi halitasikilizwa. Je, tunajenga jamii ya aina gani? Je, mustakabali wa nchi yetu uko wapi? Je, Taifa la walalamishi litakifikisha wapi kizazi kijacho? Tafakari!

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la rushwa katika vitabu. Napenda kuipongeza Serikali kwa dhati kwa kuyafungia makampuni mawili ya uchapishaji wa vitabu hapa nchini Oxford na Macmillan. Ni ukweli ulio wazi kuwa makampuni haya yamekiuka mfumo wa elimu hapa nchini hasa katika shule za msingi na sekondari. Kwa njia ya rushwa, makampuni haya yamefanikiwa kusambaza kwenye shule zetu vitabu visivyo na ubora, hali hii imepelekea hata watoto wetu wamalize darasa la saba bila kujua kusoma na kuandika. Ushauri kwa Serikali ni kwamba ondoa vibaraka vyote vya Oxford na Macmillan hapa nchini. Kampuni ya Aidan ni kibaraka cha Macmillan, isishirikishwe kwenye tenda yoyote ya vitabu hapa nchini. Maafisa Serikali waliohusika na sakata hili wafanyweje? Tutafakari kama kuongoza ni kuonesha njia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *EMAC* kuonesha upendeleo katika kupitisha vitabu vya kiada na ziada katika nchi yetu haliwezi kufumbiwa macho. Suala hili ndilo lililopelekea makampuni ya kigeni kama vile *Oxford University Press (OUP), Macmillan, Longman, Longhorn* na sasa tunatengeneza Taifa la wajinga wasiojua kusoma wala kuandika. Binafsi napendekeza *EMAC* ivunjwe ili kubuni chombo kingine mbadala ambacho hakitapokea rushwa ili kisimamie suala la vitabu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nataka nifahamishwe ni kwa nini wachapishaji wa Tanzania hasa weusi (wazawa) wakipeleka miswada yao *EMAC* inachukua zaidi ya miaka miwili kufanyiwa tathmini? Je, Mheshimiwa Waziri anaifahamu vizuri kashfa ya bosi wa *EMAC* aliyeko masomoni nchini Uingereza? Tafakari na chukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza shule za sekondari za kata, zisaidiwe kwa kupelekewa umeme, mabweni, maji, barabara, Walimu, vitabu na sanasana zipewe hatimiliki ya maeneo zilipojengwa ili kuepuka uhasama usio na maana yoyote ile. Serikali kupitia Wizara hii inaweza kufanikisha zoezi hili kwa kushirikisha Halmashauri zetu za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la siasa katika Taasisi za Umma za Elimu. Naomba kuulizia Serikali kupitia Wizara hii kuwa imechukua hatua gani hadi sasa kuhakikisha kuwa hakuna masuala ya siasa yanayoendeshwa katika Taasisi za kutolea elimu hapa nchini? Je, Waziri anafahamu wazi kuwa masuala ya siasa katika shule zetu za msingi na sekondari yanachangia sana ufaulu hafifu wa wanafunzi wetu? Naiomba Serikali itoe majibu sahihi kwenye maswali haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mabadiliko ya mitaala ya elimu kwa kiasi kikubwa huathiri sana wachapishaji na hata watumiaji wa vitabu vinavyohusika. Ni vigezo gani vinavyotumika kubadilisha mitaala ya elimu? Je, Sera ya Elimu

inahusikaje na mabadiliko ya mitaala ya elimu? Je, kuna semina yoyote inayotolewa kwa wadau wa elimu kama vile Walimu, wachapishaji na hata wanafunzi kuhusu mabadiliko ya mitaala yanayojitokeza hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la vifaa vya elimu maalum. Napenda kupitia Bunge lako Tukufu kuuambia umma wa Watanzania kuwa elimu maalum ya walemavu imesahauliwa kwa kiasi kikubwa sana hapa nchini. Je, kwa nini Serikali imesahau sekta hii ya elimu maalum? Je, katika mgao wa fedha za rada, sekta hii imetengewa shilingi ngapi? Serikali ina mkakati gani wa haraka, kati na ya muda mrefu wa kuiinua sekta hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgao wa fedha za rada, kwa kuwa Serikali haikuweza kusikiliza maoni ya Wabunge juu ya mgao wa fedha za rada kuwa zitumike kununulia madawati na kujenga nyumba za Walimu, je, ni makampuni gani yaliyopewa tenda ya kusambaza vitabu kutokana na fedha hizo za rada? Ni Halmashauri zipi zilizopewa fedha hizo kwa ajili ya ununuzi wa madawati? Ni asilimia ngapi ya fedha hizo zimepelekwa kuboresha elimu ya walemavu yaani elimu maalum? Ni asilimia ngapi ya fedha hizo zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Walimu, kama hakuna kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la bodi ya shule hasa shule za sekondari, ni muhimu sana ili kuboresha na kusimamia masuala yote yanayohusu shule husika. Je, shule zetu zote za sekondari zina bodi iliyo hai? Je,

wajumbe wa bodi hizo wanapatikanaje? Je, wananchi wa maeneo husika yaliyo na shule hizo wanashirikishwa vipi katika uundaji wa bodi hizo? Je, mfumo huo wa uendeshaji wa bodi hizo unakubalika? Kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Ukaguzi wa Shule hasa shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu, inakabiliwa na matatizo mengi sana. Ni kwa nini Idara hii inatengewa fedha kidogo? Serikali ina mkakati gani wa kuithamini Idara hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala mtambuka ambayo Serikali inabidi itafakari kwa makini. Je, Serikali ina mpango gani wa kurudisha mitihani katika ngazi ya Taifa ili kupima uelewa wa mwanafunzi; mtihani wa darasa la IV (nne), kidato cha pili na kidato cha tano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kuondoa tatizo la upungufu wa Walimu wa masomo ya sayansi katika shule zetu za sekondari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali inafahamu kuwa Chuo cha Ualimu Tarime kinakabiliwa na matatizo mengi sana hasa ya uchakavu wa majengo ambao unatishia maisha ya wanachuo na wafanyakazi wa chuo hicho? Serikali imechukua hatua gani hadi sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa Bodi ya Mikopo inachukua takribani asilimia 80 ya bajeti yote ya Wizara, je, Wizara inaridhika na hali hiyo? Kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya CCM ilielekeza kuwa kila Wilaya itakuwa na Chuo cha *VETA* kuanzia mwaka 2010-2015. Agizo hilo limetekelezwa kwa kiwango gani? Kwa nini hakuna Chuo cha VETA Wilayani Tarime?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali inakabiliana vipi na migomo ya wanafunzi na wahadhiri katika Vyuo vyetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali haitamki hadharani kuwa lugha ya Kiingereza imeshindwa kukidhi vigezo vya kufundishia na sasa Kiswahili ndiyo iwe lugha ya kufundishia na Kiingereza kuwa lugha ya mawasiliano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja asilimia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maabara mbili kila Wilaya. Katika Wilaya ya Uyui, mgao wote umekwenda Tabora Kaskazini badala ya mgao sawa Jimbo la Igalula moja na Tabora Kaskazini moja. Igalula inazo sekondari tano za kata zimetoa wanafunzi wa kidato cha nne, Goweko, Igalula, Tura, Lutende na Loya. Pamoja na upungufu uliojitokeza, Jimbo la Igalula linaomba pia lijengwe maabara mbili Goweko na Igalula kwani ni kongwe. Tabora Kaskazini maabara zimejengwa Ndono na Idete sekondari. Umuhimu wa maabara katika sayansi wote tunaujua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza idadi ya Wahandisi na *Scientist* wanawake Tanzania. Nilikuwa msemaji mkuu katika ziara ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu umeme vijijini Thailand na China Julai 2/11/2012. Katika uzalishaji umeme wa Tungataka *(Biomass)*, Gesi (Biogas), Taka (*Municipal solid wastes-power gen*) na umeme wa upepo, Wakuu wa Idara wote walikuwa Wahandisi wanawake. Napendekeza kwa kuwa umeme wa maji (*hydropower projects*), Mkuu wa Idara alikuwa Mhandisi mwanaume, Wizara ifanye ziara, Waziri au Naibu au Katibu Mkuu huko Thailand na kujifunza siri ni nini kwa kuwa na kiwango kikubwa cha Wahandisi wanawake huko ili nasi tujifunze na kuongeza idadi ya Wahandisi na Wanasayansi Watanzania wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina upungufu mkubwa wa vitabu, Walimu na vifaa vya kufundishia katika shule za msingi na sekondari Jimboni Igalula. Ukurasa wa 13 na 14, ugawaji vitabu 450 Wilaya (Halmshauri) ambazo ni Dodoma, Kinondoni, Ilala, Temeke, Mkuranga, Kisarawe na Bagamoyo. Wilaya maskini kuliko Wilaya zote Tanzania ni Uyui. Hii ni kutokana na utafiti wa mwaka jana wa Profesa Jeffrey Sykes (Mchumi wa Afya) hususan Jimbo la Igalula. Hivyo mgao mwingine wa vitabu tupatiwe Igalula Jimboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabweni shule za sekondari hasa kwa wasichana. Naendelea kuhamasisha wananchi Jimbo langu ili kupunguza mimba za utotoni kujenga mabweni kila sekondari

Jimboni. Ninaomba Wizara iniunge mkono kwenye hizi sekondari tano zilizopo na tano mpya zinajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vya ufundi stadi na *VETA* Wilayani, hatuna chuo, hivyo chuo chetu kijengwe Igalula, vijana wataondoka vijiweni na kuweza kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kumshukuru Mungu kwa kupata nafasi hii muhimu ya kuchangia Wizara hii muhimu sana kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukijua kulaumu lazima ujue na kusifu. Nichukue nafasi hii adhimu kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri sanasana wanayofanya japo bado kuna changamoto nyingi sana zinazotukabili na kuwafanya viongozi wa Wizara hii kufanya kazi katika wakati huu mgumu kwa kuwapa bajeti ndogo sana ambayo haikidhi mahitaji muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mtera lina Kata 19 katika kata zote hizo, kuna sekondari 12 ambazo hakuna hata moja yenye maabara, hivyo kuwafanya watoto wote kupata nusu elimu. Ombi kwa Serikali yetu kutujengea mabweni na maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Wilaya yetu ya Chamwino yenye Majimbo mawili hakuna Chuo cha ufundi stadi. Naomba Wizara itujengee *VETA* katika Kijiji cha *Mvumi Mission*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Rukwa kukosa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi-*VETA*. Wakati Sera ya Elimu inasisitiza kujenga Chuo cha Mafunzo ya Ufundi kila Wilaya, ni jambo la kushangaza Mkoa wote wa Rukwa hauna hata chuo kimoja. Naomba Mheshimiwa Waziri aeleze ni lini Chuo cha Ufundi kitajengwa Mkoa wa Rukwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupandishwa kwa shule za sekondari za Uchile na Vuma kuwa na kidato cha tano na cha sita. Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga Vijijini iliomba kupandisha shule hizo kuwa na kidato cha tano na cha sita toka mwaka 2010 lakini hadi sasa shule hizo Serikali haijazipandisha, naomba kupewa maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Ukaguzi iwezeshwe. Idara hii ni muhimu sana kusimamia suala la elimu. Hivyo ni vyema ikawezeshwa ili iweze kumudu shughuli za ukaguzi pia ijitenge kuliko ilivyo sasa, inakuwa ikitegemea fedha za ombaomba kutoka Ofisi za Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za rada kununua vitabu/madawati. Ni muda mrefu tangu fedha hizi ziletwe. Ni kitu gani kimechelewesha fedha hizi kuanza kufanya kazi? Mgao wa fedha hizi uwe na kipaumbele kwa Wilaya ambazo bado ziko nyuma sana kielimu ambazo hazina vitabu, hazina madawati pia zinakuwa za mwisho katika kufaulisha wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wa kike wanaopata mimba waruhusiwe kuendelea na masomo. Mtoto wa kike kupata mimba ni kitendo cha ajali. Watoto wa kike wanapambana na vikwazo vingi sana na wasababishaji wa vitendo hivyo ni sisi wenyewe wanaume. Walimu wa kiume wanawasumbua sana watoto wa kike hadi wanalazimika kushawishika hivyo waruhusiwe kurejea shuleni.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kulaani tabia iliyozuka ya Serikali kukimbizia masuala ya wafanyakazi Mahakamani, hasa pale wafanyakazi wanapoamua kufanya migomo kama njia ya kuwasilisha madai yao kwa Serikali kama ilivyotokea kwa Walimu hivi karibuni na zaidi inaonekana sasa Serikali imeamua kuja na mbinu mpya kwa kushirikiana na Wabunge wa CCM kwa kutoa kauli za kukidhalilisha na kukiondolea hadhi Chama cha Walimu (CWT). Hii haijengi bali inazidi kubomoa, haijengi kwa sababu inatengeneza mazingira ya mgomo baridi kitu ambacho ni hatari zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mikopo ya wanafunzi bado ni *disaster* na tutarajie migomo zaidi. Ni nini matokeo ya Tume ya Rais tuliyoambiwa mwaka jana kuwa iliundwa ili kutatua matatizo ya elimu ya juu ikiwamo suala la mikopo? Kwa nini tatizo la mikopo bado ni janga kwa wanafunzi wengi hasa watoto wa maskini waliopo kwenye vyuo vikuu mbalimbali nchini kikiwemo chuo cha TEKU-Mbeya ambako bado kuna kundi kubwa la wanachuo walio kwenye sintofahamu kuhusu mkopo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nashauri Wizara ya Elimu ipunguziwe majukumu ikiwemo *VETA* kuondolewa na kupelekwa Wizara ya Kazi na Ajira ambako kimantiki ndio *VETA* inatakiwa iwe. Pia nashauri majukumu ya kusimamia elimu yaondolewe kutoka Halmashauri/TAMISEMI na yote yawe chini ya Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna maendeleo bila elimu na hakuna elimu bila Walimu, Serikali haina namna zaidi ya kukaa na Walimu mezani na kujadiliana nao kuhusu hoja za matatizo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, viwango vya utoaji taaluma *(quality education).* Ni wito wangu kwa vyuo vikuu na Taasisi za elimu hapa nchini kuendeleza na kukuza ubora wa utoaji wa elimu. Aidha, vijana walioko vyuoni hivi sasa wanahitaji maarifa na ujuzi wa hali ya juu katika kukabiliana na maisha na kujenga Taifa letu changa na kwamba

wawe na uwezo wa kushindana Kitaifa na Kimataifa. Idadi ya wanafunzi wasiojua kusoma na kuandika kuongezeka. (TA-kutoa mihadhara na kushinda mitihani).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufanya utafiti juu ya soko la ajira *(Labour Analysis).* Vyuo vikuu vyetu vimefikia 45 hivi sasa kati ya hivyo 11 ni vya Serikali na 34 ni vya watu binafsi. Katika vyuo hivyo, fani mbalimbali zimekuwa zikitolewa na maombi bado yanaendelea kupokelewa na *TCU* juu ya uanzishaji wa vyuo vikuu mbalimbali hapa nchini. Kama Taifa ni vyema tufanye utafiti ili kujua mahitaji ya soko la ajira *(labour market)* yanayotegemea ukuaji wa uchumi nchini na katika Afrika Mashariki na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, hii itasaidia kujua kila programu inahitajika kwa kiasi gani katika soko la ajira mfano mainjinia, wahasibu, madaktari, maafisa kilimo, wachumi na kadhalika. Hii itasaidia pia kuvielekeza vyuo kuweka kipaumbele katika *programs* kulingana na mahitaji na hata kuwawezesha wanafunzi kujielekeza katika *program* zenye nafasi kubwa ya ajira. Hivi sasa hatuna taarifa sahihi na hata tunavyosema vipaumbele tunakisia tu na hatari yake ni kwamba tunaweza kuendelea kuzalisha wataalamu ambao hawahitajiki katika soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *data base* ya wahitimu wa vyuo vya elimu ya juu nchini. Idadi ya vijana wanaomaliza elimu ya juu imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka, lakini Serikali haina *data base* ya kujua kuwa nchi ina wataalamu wangapi na wa fani

zipi. Hii ingesaidia kujua mahitaji ya uchumi *(economic labour demand)* wa nchi yetu. Lakini pia je, Serikali inafahamu kwa sasa tunahitaji wataalamu wangapi na wa kada gani? Wakati huohuo inakadiriwa kuwa wanataaluma wenye ujuzi maalumu wapatao 300,000 huwa wanaondoka katika nchi za Afrika na kukimbilia nchi za nje, je, Serikali inafahamu ni wataalamu wangapi na wenye ujuzi gani wamekuwa wakiondoka nchini kila mwaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa gharama halisi ya kusomesha mwanafunzi wa chuo kikuu *(student unit cost).* Hivi sasa kumekuwepo na utozaji holela wa ada katika vyuo vikuu vyetu hapa nchini, program moja inatozwa ada tofauti tofauti katika vyuo vikuu vya Serikali. Mfano shahada ya sheria katika chuo kikuu cha Dar es salaam ni Tshs.1,500,000/= wakati katika Chuo Kikuu cha Dodoma ni Tshs. 950,000/=. Hata vyuo binafsi kila kimoja kinapanga ada kwa jinsi kiinavyojisikia na kufanya vingine kuwa na gharama kubwa sana na vingine kutoza gharama ndogo kuliko hata vile vya Serikali licha ya kuwa vyuo vya Serikali vinapata ruzuku Serikalini.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu unawaumiza sana Watanzania na Taifa hivyo ni wakati sasa tunapaswa tuwe na *SUC* itakayowezesha kudhibiti utozaji holela wa ada. Tangu mwaka jana Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi aliahidi Bunge kuwa ifikapo Desemba 2011 gharama halisi za kusomesha mwanafunzi wa chuo kikuu zitakuwa zimefahamika lakini hadi leo ahadi yake hiyo haijatekelezeka. Aidha, Waziri pindi atakapojumuisha bajeti ya Wizara yake

aliambie Bunge na Watanzania kwa ujumla gharama halisi ya kumsomesha mwanafunzi wa chuo kikuu ni shilingi ngapi ili kuondoa manung'uniko na utata uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya stahiki mbalimbali za wafanyakazi wa vyuo yakiwemo malimbikizo ya mishahara ambayo jumla yake hadi kufikia Mei, 2012 ni Tshs.37,534,356,650.81. Serikali ilipe mapema iwezekanavyo malimbikizo ya fedha za wanazuoni hawa ili kuwapa moyo wa kufanya kazi. Mchanganuo wa deni hilo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Dar es Salaam-Sh.13,825,367,770.00; *Nelson Mandela African Institute of Science and Technology* -Sh.631,733,028.00; Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili - Sh.2,889,585,335.00; Chuo Kikuu Huria cha Tanzania - Sh.1,977,341,298.00; Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Morogoro - Sh.4,339,483,002.54; Chuo Kikuu cha Dodoma - Sh.3,876,194,296.17; Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa - Sh.1,000,514,038.70; Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Biashara Moshi - Sh.1,930,127,929.00; Chuo Kikuu cha ARU - Sh.1,449,907,363.00; Chuo Kikuu cha Mzumbe - Sh.3,725,009,334.00 na Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Chang'ombe - Sh.1,889,193,255.44.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kutovihusisha vyuo vikuu vishiriki vya umma na masharti ya kutumia Sekretariati ya Ajira ya Umma, tungependa suala hili lifikie tamati mapema inavyowezekana ili kuyaachia majukumu hayo Mabaraza ya Vyuo kama Sheria ya Vyuo Vikuu Na.7 ya mwaka 2005 inavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umri wa kustaafu wanataaluma nchini (Madaktari wa Falsafa na Maprofesa). Serikali ilikwishaahidi juu ya kuongeza umri wa kustaafu kwa hiari wanataaluma kutoka miaka 60 hadi 65 na kustaafu kwa lazima katika umri wa miaka 70, lakini mpaka sasa wanataaluma wengi wenye umri wa kustaafu kwa hiari na wanataka kuendelea kulitumikia Taifa wanashindwa kwa sababu wanasuasua na mikataba ya miaka miwili miwili. Lakini haikubaliki kwa Profesa wa Tazania anabembeleza mkataba wakati katika nchi jirani za Afrika Mashariki Maprofesa na Madaktari wanastaafu wakiwa na umri zaidi ya miaka 65 na kwa lazima miaka 70 wanabembelezwa kwa kupewa fursa kuendeleza sekta ya elimu nchini mwao.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia lazima itambue kuwa kuwaandaa Madaktari wa Falsafa na Maprofesa ni zaidi ya miaka kumi, kwa nini haioni umuhimu wa kuendelea kuwatumia? Wakati Serikali ikiendelea kung'ang'ania kuongeza miaka ya kustaafu wataalamu hawa, wakati huohuo katika baadhi ya vyuo hapa nchini ma-*Tutorial Assistants (TA)* ndiyo wamekuwa wakifundisha, wakitunga na kusahihisha mitihani wakati ni kitu ambacho hakikubaliki huku vyuo binafsi vikiendelea kuwachukua wanataaluma hawa muhimu (mfano Chuo kikuu cha Dodoma, hii ni hatari sana kwa Taifa).

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo yanayozikabilia Ofisi za Ukaguzi wa Shule za Wilaya nchini. Ofisi za Ukaguzi katika Wilaya zimekuwa zikitengewa bajeti kidogo ukilinganisha na majukumu waliyoanyo. Mfano

mwaka 2011 walipewa kiasi kidogo cha fedha za kujikimu yaani Tshs.400,000/=, vifaa vya kufundishia vichache na duni, Wakaguzi kutokuthaminiwa na kutopandishwa madaraja, kutolipwa fedha za likizo, matibabu na hata uhamisho (MEATU).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitenga fedha ndogo katika Idara ya Ukaguzi wa Elimu nchini hiyvo kupelekea asasi 6,228 kati ya asasi 20,045 tu kufanyiwa ukaguzi katika mwaka wa fedha 2011/2012, hii ni asilimia ndogo sana ili kuweza kufikia lengo la kuendeleza elimu nchini. Uhaba wa vyombo vya usafiri kwa watumishi wa Idara ya Ukaguzi ili kuwawezesha kuvifikia vituo vya elimu na kuvikagua kwa muda muafaka mfano Wilaya ya Meatu. Hata baada ya kukagua, je, taarifa hizi hupelekwa wapi? Naishauri Serikali iipeleke Idara hii iwe chini ya TAMISEMI ili taarifa hizi ziwe zinawakilishwa katika Barala za Madiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hata kidogo suala la kuendelea na mchakato wa kuifanya Idara ya Ukaguzi wa Shule kuwa Wakala.

**MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kuhusu shule Kongwe za Bihawana na Msalato katika Jimbo la Dodoma Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bihawana Sekondari, shule hii ilijengwa mwaka 1961 na muasisi wa *Mission* ya Bihawana PadrI Giovanni Virdi (maarufu kwa jina la Padri Yohani) kama shule ya Kanisa Katoliki. Baada ya Azimio la Arusha (1967) shule hii ilitaifishwa na kuwa shule ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuitaifisha shule ilikuwa na idadi ndogo ya wanafunzi. Padri Yohani aliweza kuiendesha shule kwa mafanikio makubwa. Shule ilikuwa na chakula cha kutosha, maji ya kutosha na miundombinu ya kutosha. Baada ya shule kutaifishwa idadi ya wanafunzi iliongezeka lakini pasipo kuboresha miundombinu na mahitaji mengine ya shule. Shule ya Sekondari Bihawana sasa ina upungufu huu ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule ina maabara ndogo yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 20 tu kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo dispensary ndogo ya chumba kimoja tu na wala haina watumishi. Hali hii inafanya *dispensary* hiyo kuwa sawa na chumba cha *1st Aid* na wala siyo *dispensary* tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule haina kisima cha maji, wanafunzi wanakaa zaidi ya siku tatu bila kuoga. Hali hii inafanya mazingira ya shule kuwa magumu sana kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule iko umbali wa kilomita 24 nje ya Mji wa Dodoma, lakini haina gari. Lori walilokuwa nalo lilikwisha haribika miaka mingi na halitengenezeki! Je, mwanafunzi akiugua ghafla atasaidiwa vipi kukimbizwa hospitali wakati hakuna vyombo vya usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni maabara zipanuliwe, *dispensary* ipanuliwe na vifaa viongezwe. Kisima cha maji kichimbwe na gari la shule linunuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msalato Sekondari, shule hii ilijengwa na Kanisa la Anglikana mwaka 1961 ikiitwa wakati ule Mvumi *Girls Middle School*. Ilitaifishwa mwaka 1970, shule ina matatizo haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule haina wigo. Jambo hili linasababisha shule kuvamiwa ndani ya mabweni, wizi na utoro. Shule ina eneo kubwa la hekta 29.5, makisio ya kujenga wigo wa shule ni sh. 267,529,950 (makisio haya ni hadi Mei 2011), sasa gharama hii inaweza ikawa juu zaidi. Shule haina fedha, wazazi pia hawana uwezo wa kuchangia fedha nyingi kiasi hicho kwa ajili ya ujenzi wa wigo wa shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za *bill* ya maji kwa mwezi ni shilingi milioni 1.6, bajeti ya shule ni ndogo sana wala haiwezi kukidhi mahitaji ya maji katika shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule haina gari, gari lao limekufa na linahitaji shilingi milioni 10 ili lipate kufufuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule haina *title deed* tangu ijengwe mwaka 1961.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu ni kwamba, Wizara ijenge wigo kunusuru usalama wa mtoto wa kike katika shule hii. Kisima cha maji kichimbwe, gari linunuliwe na shule pia ikabidhiwe *Title Deed*, ili shule

iwe na uwezo wa kisheria wa kulinda mipaka yao ya shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yake ya wataalam ikiongozwa na Kaimu Katibu Mkuu Ndugu Gesimba kwa kujitahidi kufanya kazi nzuri katika mazingira magumu ya bajeti ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kurudia msimamo wangu kwamba tulifanya makosa kwa kuhamisha idara ya elimu ya msingi na elimu ya sekondari kuzipeleka TAMISEMI, mimi nilishiriki katika kuanzisha TAMISEMI na TAMISEMI ilipewa kazi mbili; kuwa kiungo kati ya Serikali za Mitaa na Serikali Kuu na kusimamia uendeshaji wa shule za msingi, *the day to day running of primary schools* na siyo *the management of education as a discipline*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya menejimenti ya elimu kama taaluma, *the Management of education as a discipline* ni kazi ya Wizara ya Elimu. Wizara ya Elimu ndiyo ina *instutional memory*. Huu ni msimamo wangu kama mwalimu wa siku nyingi, mtu ambaye anajua maana ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uganda walijaribu ku-*decentralise* Idara ya Elimu ya Msingi na ile ya Sekondari walipata matatizo ikabidi wazirudishe idara hizo kwenye Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inanikumbusha maneno ya busara ya Gavana wa mwisho Sir Richard Turnbull wakati akisindikizwa na Rais Nyerere Desemba 1962. alimwambia Rais Nyerere nanukuu: “*Mr President you can politicise everything but not education*”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Wizara ni ndogo sana ukizingatia umuhimu wa elimu kama kipaumbele cha kwanza katika kuelekea nchi ya ahadi, nchi yenye uchumi wa kati ifikapo 2025. Licha ya kwamba bajeti ni ndogo, lakini asilimia 85 ya bajeti hiyo inakwenda Bodi ya Mikopo na asilimia 15 inagawanywa kwenye idara za ndani za Wizara, Baraza la Mitihani Taasisi ya Kukuza Mitaala na Vyuo Vikuu vya Umma (Vyuo Vikuu saba na vyuo vingine vya Elimu ya Juu nane).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo la kulipia vijana wengi ada kwa ajili ya masomo ya elimu ya juu ni jambo zuri, lakini siyo *substainable*. Ni nchi chache zinaweza kulipia vijana wote wa vyuo vikuu. Ni vizuri kutafuta njia zingine za kusaidia kuwasomesha vijana hawa. Pia kuwepo na mkakati mzuri wa kurejesha mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuwekeza katika elimu *(investment in the human capital)* siyo tu kulipia karo za vijana wetu kwenye elimu ya juu kuna mambo mengi ya msingi yanayohitaji uwekezaji, kuna kuwekeza katika vitabu, vifaa vya maabara, mafunzo ya walimu, utafiti *accommodation* ya wanafunzi, ukarabati wa majengo, kuboresha maslahi ya walimu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vikuu vyetu vina hali mbaya sana. Vyuo hivi vinapewa fedha za mishahara lakini vinapewa fedha kidogo sana za matumizi ya kawaida *(other charges)* na za maendeleo *(capital development)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, , nimekuwa nikisema kwamba Idara ya Ukaguzi ni muhimu sana maana kazi yake ni kuhakiki ubora wa elimu inayotolewa katika shule zetu za msingi na sekondari. Katika Wilaya ya Ngara shule hazikaguliwi. Kama shule hazikaguliwi walimu hawatajali kutayarisha masomo *lesson notes* na hata kumaliza *syllabus*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kutaka kuanzisha Wakala *(Executive Agency)* wa Ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, tunaweza kuwa-*train* waratibu wa elimu kata kusaidia katika ukaguzi wa shule za msingi? Hili ni wazo langu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la *accountability*, kuna aina tatu ya accountability katika elimu; kwanza, *goal accountability*, hii ni kazi ya Serikali na Chama Tawala kuweka malengo ya Elimu jambo hili linafanyika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, *programme accountability,* hii ni kazi ya kutafsiri malengo kwenye *programmes,* utekelezaji eneo hili ni tatizo. Taasisi ya kukuza mitaala ina kazi ya kuandaa mitaala na *syllabus,* eneo hili liangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, *outcome accountability,* wanafunzi wanapofanya vibaya Walimu wanatakiwa kuwajibika pamoja na Serikali kwa ujumla kwa kutowekeza vizuri katika elimu, tatizo la vitabu na vitendea kazi ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aina ya walimu tunaowazalisha katika vyuo vyetu, nchi haiwezi kuendelea bila watu wenye elimu nzuri na tutashindwa kufikia ile nchi ya ahadi nchi yenye uchumi wa kati bila kuinua kiwango cha elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wanaokwenda kusomea ualimu ni wale waliopata *division IV point* 27, wakienda kwenye Vyuo vya Walimu wanawakuta wakufunzi ambao nao siyo mahiri sana. Matokeo, ni *Bare Foot Teachers,* hao ndio wanaokwenda kuwafundisha watoto wetu wa shule za msingi. Hawajawahi kusoma nadharia ya Profesa Benjamini *Bloom's Taxi Nomy*. Yaani hatua sita za kumfanya mwanafunzi aelewe anachofundiswa *six levels of learning that is knowledge, Comprehension, Application, Analysis, Synthesis* na *Evalution.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za binafsi ni biashara na mahali pengine ni biashara haramu. Kwa nini nasema hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya shule zinasajiliwa bila kuzingatia viwango. Karo ziko juu sana, sijui kwa nini Wizara isidhibiti karo hizi kwa kutumia *unit cost*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule hizi zinasajili watoto ambao hawakushinda vizuri ili mradi wajipatie *school fees*, shule hizi hazikaguliwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule hizi zimeanzishwa na wafanyabiashara ambao hawana ethics na siyo wataalam wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule hizi zimeajiri Waganda na Wakenya ambao siyo walimu *by profession*, hawana sifa ya ualimu. Sifa waliyonayo ni kujua kuzungumza Kiingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Ufundi, Ilani ya Uchaguzi inahimiza kuwa na Chuo cha Ufundi katika kila Wilaya. Hili ni lengo zuri, lakini basi, Serikali itenge bajeti ya kutekeleza lengo hili. Vyuo vya Ufundi vitasaidia kupunguza tatizo la ajira. Wakipata *skills* za ufundi wanaweza wakajiajiri.

**MHE. MARYAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuchangia hotuba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero za walimu kumekuwa na kero nyingi za walimu ambazo mpaka leo hazijatatuliwa. Walimu ambao wamepangiwa kwenda kusomesha shule za vijijini wamekuwa wakipata tabu sana. Wanasomesha watoto katika mazingira magumu, vile vile walimu hao wanaishi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali na Wizara itahakikisha inaboresha maisha ya walimu kwa kuwajengea nyumba bora na kuwalipa madai yao ya siku nyingi ambayo wamekuwa wakidai Serikalini siku zote bila mafanikio yoyote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana an kero hizi walimu wengi wamekata tamaa ya kuwasomesha watoto wetu walimu wengi ambao wanaishi pembezoni wamekuwa wakikopa pesa na kuingia gharama kufuata mishahara yao mjini. Vile vile, mishahara yenyewe wanayoifuata mjini ni midogo, haikidhi mahitaji wanaishia kulipa madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali kushirikiana na Wizara haioni sasa kuna umuhimu wa kuwasogezea walimu mishahara yao karibu na vituo vyao vya kazi ili kuepuka usumbufu wanaopata?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mabweni ya shule ya wanafunzi wa kike, hili nalo ni tatizo, watoto wanatembea umbali mrefu, hivyo kukutana na vishawishi kwenda au kurudi shule. Ikiwemo pamoja na ubakaji na mimba zisizotarajiwa. Je, Serikali ina mikakati gani kujenga mabweni ya wasichana katika shule zilizoko mbali na maeneo wanaoishi? Serikali ina mikakati gani kuhusu wanafunzi wa kike ambao wamepata mimba wakiwa shuleni. Kuhakikisha wanafunzi hawa wanarudishwa shuleni kuendelea na masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu ya sayansi kwa watoto wa kike, naipongeza Serikali kwa kutoa

kipaumbele kwa masomo ya sayansi kwa wasichana, lakini bado wanaoitikia wito huu ni kidogo sana na hiyo idadi ndogo sana Serikali bado haijaweza kuwadhamini wote Vyuo Vikuu. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhamasisha zaidi watoto wa kike katika masomo ya sayansi. Serikali ina utaratibu gani wa kuwadhamini wanafunzi wote wa kike ambao wamefaulu kujiunga na vyuo vikuu? Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha shule zote za sekondari na vyuo vikuu wanapatiwa vifaa vya maabara vya kutosha kufundishia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na usumbufu kwenye Bodi ya Mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya jamii. Wanafunzi hawa wamekuwa wakisumbuliwa na kupata usumbufu mkubwa kwenye Bodi ya Mikopo na hasa kwa wanafunzi ambao wazee wao ni maskini. Hii imekuwa ni kero, hawapatiwi mikopo kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile wengine wanakata tamaa ya kuendelea na masomo ya elimu ya juu kuna baadhi ya viongozi ambao wapo kwenye Bodi ya Mikopo wamekuwa si waadilifu wanajihusisha na vitendo vya ubadhirifu na kupelekea wanafunzi kukosa mikopo. Je, Serikali na Wizara imewachukulia hatua gani viongozi wa Bodi ya Mikopo ambao wamekuwa wakitajwa mara kwa mara kujihusisha na vitendo vya ubadhirifu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Vyuo vya *VETA*, vyuo vingi vya *VETA* vimekuwa vikiwasaidia vijana wengi na kupata elimu ya ufundi stadi ya kujiajiri

wenyewe. Lakini bado vyuo vingi vya *VETA* havina vitendea kazi, havina Walimu wa kutosha, vile vile bado ni vichache havikidhi haja ya vijana ambao ni wengi kwa sasa. Je, Serikali na Wizara ina mikakati gani kuhakikisha wanaboresha vyuo ambavyo vipo kwa sasa na Mikoa ambayo vyuo hivi havijafika wanajengewa kwa wakati muafaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu ya watu wazima, wananchi wengi ambao wapo pembezoni, hawajui kusoma na kuandika, lakini mpaka sasa hivi elimu ya watu wazima bado haijawafikia walengwa hasa waliopo pembezoni. Serikali na Wizara ina mikakati gani kuhakikisha hii elimu ya watu wazima inarudishwa mashuleni ili wananchi wasiojua kusoma na kuandika wapate fursa hii ya kujiunga na elimu ya watu wazima.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Mbozi Magharibi kwa miaka nenda rudi kumekuwa na uhaba wa walimu na kila mwaka tumekuwa tukiomba. Je, ni lini tutapatiwa walimu wenye kukidhi mahitaji na idadi ya wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mbozi Magharibi pamoja na nchi nzima hususani katika shule za msingi kumekuwa na ukosefu mkubwa wa madawati, hivyo kufanya wanafunzi wengi kukaa chini. Je, ni lini hili tatizo litapatiwa ufumbuzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti ya mishahara kati ya *Laboratory Engineer Scientists* na *Technician;* katika Vyuo Vikuu mfano, *UDSM* na *UDOM* wanalipwa

mishahara tofauti kwa maana ya midogo katika *scale* ya *PUSS* kuliko walimu wanaofundishwa *theoretical course* ambayo ipo katika scale ya *PUTS*. Tunaomba ufafanuzi juu ya hili. Vile vile *laboratory engineers scientists* na *technicians* wanaitwa *administrators* (watawala).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini tatizo la uhaba wa nyumba za walimu litapatiwa ufumbuzi? Je, nani wa kulaumiwa kwa ukosefu huu wa nyumba za walimu? Mbona ahadi zimekuwa nyingi na hazitekelezeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa elimu ni ufunguo wa maisha maendeleo ya nchi yoyote duniani yanategemea elimu, bila elimu ni vigumu binadamu kuweza kuendesha maisha yake. Tanzania tunakabiliwa na tatizo la kushuka kwa kiwango cha elimu kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu na hii inatokanana sababu mbalimbali ambazo zinaletea kiwango cha elimu kushuka. Sababu hizo ni:-

Katika elimu ya msingi:-

(i) Ukosefu wa vitabu mashuleni;

(ii) Upungufu wa walimu;

(iii) Mazingira magumu ya shule zetu kwa mfano, Walimu hawana usafiri, hawana nyumba bora,

uchakavu wa madarasa, ukosefu wa chaki na vitabu vya mwongozo wa Mwalimu; na

(iv) Mishahara midogo, hawana fedha ya kujikimu/*teaching allowance*, Walimu kutopandishwa madaraja kwa wakati, pia walimu waliojiendeleza elimu ya juu kusomea shahada ya kwanza akirudi kutoka masomoni hapandishwi daraja. Hii inakatisha tamaa ya kujiendeleza na kupunguza hamu ya kufundisha kwa bidii. Hawana fedha za motisha kwa kuishi katika mazingira magumu hasa wanaoishi vijijini.

Katika elimu ya Sekondari:-

(i) Ukosefu wa walimu hasa walimu wa sayansi;

(ii) Ukosefu wa maabara;

(iii) Upungufu wa vyumba na madarasa ya maabara; na

(iv) Mazingira magumu ya kufundishia hasa shule za Kata.

Katika Vyuo Vikuu:

(i) Migomo ya wanafunzi inasababisha kutomaliza *syllabus* kwa wakati;

(ii) Ukosefu wa mikopo kwa wanafunzi inasababisha wanafunzi kutohudhuria vipindi darasani kwa ajili ya kufuatilia mikopo yao;

(iii) Msongamano wa wanafunzi kwenye vyumba vya *lectures;* na

(iv) Wanafunzi kutokujituma katika kujisomea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, Serikali ichukue hatua za haraka kwa ununuzi wa vitabu kwa shule za misingi. Serikali iongeze kasi ya kusomesha walimu wa shule za msingi. Serikali iboreshe mazingira ya maisha kuwa na maisha bora hasa Walimu wajengewe nyumba za kuishi jirani na shule zao. Mishahara ya walimu iboreshwe. Madaraja ya mishahara yabadilike kwa kufuata muda muafaka. Walimu wa masomo ya Sayansi waongezwe kwa kusomeshwa wengi zaidi. Wanafunzi wa vyuo vikuu wapewe mikopo kwa asilimia mia moja hasa walimu wanafunzi wanao somea ualimu. Serikali ishughulikie matatizo ya walimu ili wafundishe vijana wetu, pia nchi iweze kupata wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Waziri, *Asalaam Alaykum*.

Nichukue fursa hii kukupongeza kwa hotuba nzuri iliyosheheni utekelezaji na mipango madhubuti, aidha kwa kazi nzuri unayofanya katika mazingira magumu, lakini ambayo ni uti wa mgongo katika maendeleo ya Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Naibu Waziri ambaye naye ni *asset* na mpambanaji makini

katika sekta hii, Rais hakukosea kuwachagua katika sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia pongezi ziende kwa Wakurugenzi wote chini ya Katibu Mkuu na Kaimu Kamishina viongozi wa wakala mashirika mabaraza taasisi tume na vyuo vikuu vilivyo chini ya Wizara na watumishi wote hasa Dorothy Mtendaji madhubuti.

Mheshimiwa Waziri nichukue fursa hii kwa niaba ya Watanzania watokao Kilindi kukushukuru sana kwa kusimamia ahadi yako ambayo imekuwa ni kilio cha muda mrefu kwetu sisi. Hakika Mungu hujibu maombi. Ahadi huko nyuma zilikuwa nyingi lakini kwa kuwafahamu wewe na Naibu Waziri hili sasa limekamilika. Wanakilindi tupo tayari na tunawaombea ninyi na wote watakaohusika afya njema na wepesi ili kukamilisha hilo. Ukurasa 98, Kilindi kupata *VETA* tunashukuru. Aidha, mmeonesha uaminifu kwani katika *Hansard* mkijibu swali huko nyuma niliahidi *VETA* –Kilindi. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo napata tabu niseme nini zaidi kwani huwezi kupata yote kwa wakati mmoja, lakini niombe tu: tukumbukeni kwenye mabweni mimba za utotoni zinasababishwa na watoto kupanga mitaani. Naomba fursa ikipatikana mtuangalie, aidha utoro shuleni utapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Wakaguzi wa Shule, naomba muwawezeshe gari moja mlilotupatia sasa limekuwa chakavu na kulingana na miundombinu ya Kilindi lina hali mbaya. Kazi nzuri iliyokusudiwa

inaelekea kuwa mbaya kwani kuzunguka na boda boda imekuwa ngumu. Naomba tuwapatie fedha na vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu ya watu wazima, kwa vile Kilindi wali-*base* kwenye elimu ya dini, elimu hii ya watu wazima ni muhimu sana kwa Wilaya hasa ukiona wakati wa uchaguzi kura zinavyoharibika, zaidi ya asilimia hamsini. Kupitia Mfuko wa Jimbo tulinunua pikipiki kwa ajili ya mratibu ili aweze kuwafikia walengwa. Cha kusikitisha hata hela ya mafuta hana. Naomba kama tuna nia thabiti, basi tuone jinsi ya kuimarisha kwetu Kilindi, elimu ndiyo mkombozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa Walimu; kwanza nishukuru kwa idadi ya Walimu mnaotupatia, hakika mbele za Mungu tunapangiwa. Tatizo kulingana na kwamba tupo pembezoni na miundombinu bado haikidhi, hawaji na wakija hukaa kidogo kisha kutafuta visingizio na kuondoka. Tumebuni motisha mbalimbali, lakini bado kikubwa pia ni nyumba, niombe tupewe *support* katika harakati ambazo tunafanya kujenga nyumba za Walimu, tunajenga lakini nguvu ya ziada inatakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeamua kuanzisha program kwa ajili ya kuwapatia *skills* wale wote waliokosa kuendelea na elimu ya sekondari na chuo au kidato cha tano na sita. Nimechukua wanafunzi wote kuanzia 2008-2011, nitakapokuwa tayari nitaomba mje mtuzindulie ili pia Wanakilindi nao wapate fursa adimu ya kukaa na Waziri au Naibu Waziri wa Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. FATUMA A MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shule za msingi ziwepo tena. Tunaiomba Serikali irejee katika miaka ya nyuma kuwa na shule za ufundi katika shule za msingi ili wakimaliza shule wawe wanajiajiri watoto wengi wanaomaliza shule za msingi wanaishia vijiweni. Au kuwa Wamachinga, lakini wangekuwa wanafundishwa ufundi fulani kama uashi, useremala, upishi, uhunzi, ufinyazi, kusuka kili na kadhalika wangekuwa wanajiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 45% ya Wamachinga wanatoka Mikoa ya Lindi na Mtwara. Kwa sababu hakuna viwanda, hakuna zile shule za ufundi za msingi. Tunaiomba Serikali irudishe shule za ufundi katika shule za msingi, Mkoa wa Lindi kulikuwa na:-

Wilaya ya Ruangwa, Shule ya msingi Mkowe na Mbekenyera; Wilaya ya Liwale kulikuwa na shule ya msingi Liwale Mjini, Mbarikiwa na Chimbuko; Wilaya ya Kilwa kulikuwa na shule ya msingi Singindo, Njinjo, Kipatimu na Kilwa masoko; Wilaya ya Nachingwea kulikuwa na shule ya msingi Kilimarondo, Mnerongongo, Marambo na Nachingwea mjini; Wilaya Lindi, kuna shule ya msingi Mtama na Lindi Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo shule 15, tunaomba shule hizo zifufuliwe, ziwe katika mfumo wa ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Idara ya Ukaguzi isaidiwe mafuta, huduma ya gari yaani *service* za magari. Vile vile *report* za ukaguzi zinapopelekwa kwa *DED* huwa hazifanyiwi kazi, hivyo, kuzorotesha elimu. Kwa hiyo, ripoti za ukaguzi zifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, shule za awali ziwepo kila penye shule za msingi. Ahsante.

**MHE. NEEMA M. HAMID**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuwapongeza Mawaziri katika Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, nikianza na Waziri, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa na Naibu Waziri kaka yangu Mheshimiwa Philipo Mulugo kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mengi ni mazuri, naomba nitoe changamoto chache tu ambazo zinahitaji kufanyiwa marekebisho. Naishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kuhakikisha kunakuwa na shule nyingi za msingi, sekondari za Kata na vyuo vikuu, lakini bado Serikali inahitaji kuboresha ubora wa elimu yenyewe inayopatikana na ubora wa wanaotoa elimu hiyo. Vinginevyo tutakuwa na Taifa lenye wasomi wengi waliohitimu vidato hadi vyuo vikuu wakiwa mbumbumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia ipitie upya mchakato wa kuchagua kozi za kusoma kwa wanafunzi wa vyuo ni tatizo. Mishahara ya walimu iboreshwe ikiwa ni pamoja na mazingira rafiki ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa elimu yetu ujikite katika changamoto tulizonazo, badala ya kujikita kuangalia *division one* na *GPA* bora. Pesa za mikopo vyuoni zitolewe *on time* wanafunzi wamekuwa wakilalamika sana.

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia. Elimu mahali popote ndio msingi wa maendeleo, hivyo basi, lazima kipaumbele cha kwanza kiwe ni elimu. Serikali haioneshi nia ya dhati kwa kuendeleza elimu kwa kuipa bajeti asilimia 4.3 ya bajeti nzima ya Serikali wakati wenzetu wa Rwanda ambao walikuwa kwenye vita wameweza kutenga 25% *(GDP)* ya bajeti kwa ajili ya elimu. Kwa mwendo huu tutafikia *vision* ya 20-25 kuwa *middle level country*? Wenzetu wa Rwanda siku siyo nyingi zijazo wataanza ku-*export* rasilimali watu. Tatizo letu ni kuwa na vipaumbele vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwa na nyumba imara, lazima msingi wake ujengwe imara. Hivyo hivyo, katika elimu ili mwanafunzi aweze kufanya vizuri lazima aandaliwe vizuri kuanzia elimu ya awali ili aweze kufanya vizuri ngazi za juu. Ni ukweli usiopingika matokeo ya mitihani kwa wanafunzi wanaomaliza darasa la saba hayapendezi, watoto wanamaliza elimu ya msingi hawajui kusoma wala kuandika hii inatokana na matatizo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi kuanzia darasa la kwanza mpaka la tatu wanasoma masomo mengi mno. Jumla ya masomo hayo ni kumi na moja, haya kwa mtoto hawezi kuyamudu. Ushauri kwa

wanafunzi hawa, Wizara irudishe ufundishaji wa kusoma na kuandika na kuhesabu. Baada ya hapo wakiingia darasa la nne ndio waendelee na masomo mengine yote na ule mtihani wa darasa la nne urudishwe kama kigezo cha kuwaangalia uwezo wao wa kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine ya wanafunzi kufeli ni kutokuwa na vitendea kazi na vile vile kutopewa chakula cha mchana mashuleni. Je, utaweza kusoma ukiwa na njaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, enzi za Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliweka msingi mzuri wa elimu na chakula kilitolewa mashuleni. Tulisoma kwa kutumia radio, kulikuwa na Walimu wa kutosha, vitabu vya kutosha, michezo mashuleni ilikuwepo hata kwa kiasi kikubwa, ujinga ulifutwa kwa elimu ya watu wazima hadi kufikia 2020. Je, elimu kwa watu wazima ikoje kwa sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine ya wanafunzi kufeli unakuta hakuna madawati, madarasa ya kutosha, wanafunzi wanasoma chini ya mti, wanakaa chini, baada ya miaka 50 ya Uhuru. Shule nyingi za msingi hazina matundu ya choo ya kutosha, inakuwa ni vigumu sana hasa watoto wa kike kuhudhuria shule siku zote hasa pakiwa hakuna maji wala vyoo. Kuna haja ya Serikali kuongeza *capitalist fees* ili watoto wote wapate chakula shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu kwa Walimu, imefikia wakati sasa Walimu nao wapewe heshima yao kama ilivyo kwa Madaktari, *Engineers,* Maprofesa na kadhalika. Utakuta hapa Bungeni wanapewa heshima kwa kuitwa Mheshimiwa Profesa, tukumbuke hawa wote wanatokana na kufundishwa na Walimu. Kwa nini Walimu nao wasipewe heshima yao kwa kuwa-*address*. Kama ilivyo kwa wenyewe Mheshimiwa Mwalimu kwa nini kuna ubaguzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wengi hawaendi kuripoti kwenye vituo vyao vya kazi, sababu unakuta hakuna nyumba za kulala na kuishi, mishahara yao ni midogo, halafu hailipwi kwa wakati na hata kile kipato kidogo cha posho ya kufundishia hakipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Mheshimiwa Makweta ilitumia fedha nyingi za walipa kodi na ikatoa maoni mazuri sana jinsi ya kuboresha maslahi ya walimu ikiwa ni pamoja na kuwalipa posho ya kufundishia. Je, Serikali ipo tayari kupitia upya ile Ripoti ya Tume ya Mheshimiwa Makweta?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupandisha vyeo Walimu, ni vyema akitakiwa kuongezwa mishahara, lakini abaki palepale kutokana na uhaba wa Walimu badala ya kuwapeleka Wilayani. Mfano, Walimu wengi ni Wakurugenzi wa Halmashauri, hii nachangia sana kwenye upungufu wa Walimu promotion isiwe ni kuwahamisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri Serikali itangaze nafasi za Walimu kwa waliostaafu hata waliorudi vijijini waajiriwe kule kwa kuwa watakuwa hawahitaji nyumba. Je, ni Walimu wangapi mpaka leo walio-*graduate* bado hawakuajiriwa ili waajiriwe? Shule ambazo hazitimizi vigezo muhimu kama vile vifaa vya kufundishia, vyoo, maabara, Walimu, maji na kadhalika zifungwe mara moja sababu zinachangia kutofanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitihani ya *multiple choice* isitungwe tena sababu inawafanya wanafunzi kutokufikia viwango, tunahitaji watoto waweze kuandika insha, kujenga hoja na wakifanya mahesabu wafikiri kwa kuonesha njia ya kupata majibu ndio maana madarasa ya awali wanashindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, elimu ya afya mashuleni, kuna mwongozo gani wa kutoa huduma kwa watoto wenye VVU mashuleni ili waweze kupimwa kama njia ya kuwazuia wasifikie hatua ya UKIMWI. Shule nyingi hazina *Title Deed* (hati miliki) na walaji wengi wa ardhi wanasogeza mipaka, Wizara ina mpango gani wa kuhakikisha kila shule ina hati miliki.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wawe na chombo kimoja cha kuwahudumia kuliko ilivyo sasa. Nashauri *TSD* ivunjwe na iondolewe huko iliko. Kiwe chombo kinachojitegemea na hata kiwezeshwe kulipa mishahara kwa kuwa ndicho chombo kinachosajili, kupandisha madaraja, kushughulikia nidhamu, tukiendelea na hali hii hii manung'uniko yataendelea kuhusu kucheleweshwa

haki zao. Aidha, chombo kimoja kitasaidia kufuatilia utumishi wao na utendaji wao kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mwalimu anayeweza kupanda daraja bila kukaguliwa angalau mara tatu ili wathibitishwe kazini. Hali kadhalika tunahitaji ukaguzi makini. Kutokana na wingi wa shule za Serikali na binafsi, hivyo, ukaguzi uwe taasisi inayojitegemea na kwa sasa iwe na *Accounting* yake na iwezeshwe kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Elimu ihusishe wadau wengi kadiri iwezekanavyo na ieleze jinsi ya kuwaendeleza watoto wa shule walioacha shule kufuatana na kuwa wajawazito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mihula ya kidato cha tano ibadilishwe irudi kwa utaratibu wa zamani ili walimu wapate nafasi ya kufundisha badala ya kuendelea kusahihisha mitihani mfululizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wenye ulemavu wawekewe miundombinu shuleni, pamoja na vyoo kwa ajili yao. Vifaa vyao ya kufundishia *Braille* vipatikane.

**MHE. OMARI A. BADWEL:** Mheshimiwa Waziri, kwanza nawapongeza sana wewe na Naibu Waziri wako kwa namna ambavyo mnafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha mchango wangu unahusu utaratibu mzuri ulioamuliwa na Serikali wa kurejesha usimamizi wa sekondari (shule) kuja katika

Halmashauri za Wilaya na ambao wanafanya kazi nzuri kusimamia shule hizo za sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu katika hilo ni kuongeza madaraka ya Halmashauri hizi katika kusimamia na kuziendesha shule hizo hasa katika suala la kuwateua na kuwawajibisha wakuu wa sekondari na kulihamisha jukumu hilo toka Mkoani kwani limepelekea kusababisha urasimu katika uchukuaji hatua za usimamizi wa shule hizo na kukwamisha mambo ya maendeleo ya shule hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Mkoa ukabaki kuwa msimamizi wa jumla wa shule hizi badala ya kushughulika moja kwa moja na baadhi ya vipengele vya uendeshaji shule hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nashauri pia lirejeshwe Halmashauri ni suala la uteuzi wa wajumbe wa Bodi za Sekondari kwani kwa uzoefu Mkoa hauwajui vema inaowateua, lakini pia uteuzi huchelewa sana kutokana na Mkoa kuwa na majukumu mengi.

Mheshimiwa Waziri, napendekeza kwako hebu angalieni kwa ujumla wake suala hili la ugatuzi wa madaraka ili kuona upungufu uliopo na yarekebishwe, lakini lengo kubwa iwe kuzifanya Halmashauri za Wilaya kuwa msimamizi na mwendeshaji Mkuu wa Shule za Sekondari.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pia niwapongeze kwa kuteuliwa kwao na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itafute ufumbuzi wa kuvuja kwa mitihani na walimu wanaotafuta umaarufu kwa kuwapa wanafunzi majibu ya mitihani ili shule zao ziongoze katika mitihani, wanafunzi kuonewa bure wanapoadhibiwa kwa kufutiwa matokeo na kuwaacha bila *formal education* nje ya mfumo wa elimu nchini. Nashauri Serikali itoe adhabu kali kwa walimu wahusika pale wanapobainika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekondari za Kata zinafanya vizuri, lakini zinaelemewa kwa kukosa nyenzo mbalimbali pamoja na vitabu, maabara na nishati (umeme). Naiomba Serikali ijikite kuimarisha shule hizi kwa kuzipatia vifaa vyote muhimu ikiwa ni pamoja na miundombinu, mfano, nyumba za walimu, usafiri na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. ANNA MARYSTELLA J. MALLACK:** Mheshimiwa Spika, elimu ni ufunguo wa maisha, tena ni taa inayomulika maisha yote. Lakini elimu ili iitwe elimu bora inatakiwa kuunganishwa na nguvu za Wizara nyingine kama Afya, Maji na Mazingira. haya mambo matatu yakiunganishwa hapo tutapata elimu iliyo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na elimu ya shule za msingi ambayo ndiyo elimu mama ambapo ukiboreshwa ukawa msingi bora ni mafanikio ya kupata wahitimu wazuri wa sekondari mpaka elimu ya juu yoyote ile sababu msingi umeandaliwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo sababu elimu ya msingi mazingira yake ni magumu hasa vijijini siyo ya kumjenga mwanafunzi katika ufaulu mzuri. Mfano, unakuta shule za msingi hazina vyoo vya kutumia wanafunzi, wanafunzi wanakwenda kuomba kujisaidia kwenye majumba ya walimu, shule haina kisima cha maji, watoto wanasoma bila kunywa maji wala hawanawi mikono wanapojisaidia kulinda afya zao. Je, mwanafunzi wa shule hiyo ana uwezekano wa ufaulu mzuri? Hivi ndivyo hali ilivyo katika shule nyingi za vijijini. Je, mwalimu aliyepata ajira mpya anakubaliana na mazingira hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara izingatie haya, iboreshe huduma nzuri katika shule za msingi ili watoto wasome bila matatizo ya kuathiri akili zao na waendelee kuipenda shule. Pia walimu wao wapate huduma nzuri za nyumba za kuishi, visima vya maji na vitendea kazi ili waipende kazi yao na kupunguza upungufu wa walimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo cha Elimu ya Sekondari kina jukumu la kusimamia utekelezaji wa sera ya elimu katika ngazi ya elimu ya sekondari ambayo kimsingi ni kiungo kati ya elimu ya msingi na elimu ya juu. Elimu ya sekondari pia hutolewa katika ngazi ya

kawaida *(O-level)* ambayo huchukua miaka minne na ngazi ya juu *(A-level)* ambayo ni ya miaka miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiomba Wizara iangalie sekondari ambazo zimekuwa za muda mrefu zipandishwe hadhi na kuwa *(A level)*, kwa mfano, Mwangaza Sekondari iliyopo Wilaya ya Mpanda, Mkoa wa Katavi, maana ipo moja tu katika Mkoa huo ambayo ni Mpanga *Girls* ambayo ni ya wasichana tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara hii ya Walimu inasimamia utoaji wa mafunzo ya ualimu wa ngazi ya cheti na stashada lakini kumekuwa na tatizo la upandishwaji vyeo kwa wale waliotoka masomoni. Hata wale waliopandishwa vyeo Serikali kupitia Wizara yake imekuwa haiwalipi mishahara mipya ya kupanda kwa madaraja yao. Sasa, je, Walimu hawa watakuwa na moyo wa kufundisha kwa bidii? Naiomba Serikali kupitia Wizara hii iangalie upungufu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo hiki cha Maafisa Elimu Wakaguzi kipewe kipaumbele kwa kutengewa fedha kwani Wakaguzi hawa wamekuwa wakishindwa kufanya kazi zao kwa usahihi. Kutokana na kukosa magari ya kufanyia kazi hasa kufikia vijijini kitu ambacho kinazorotesha sekta yote ya elimu. Serikali kupitia Wizara hii iangalie kitengo hiki cha ukaguzi ili warekebishe upungufu wote uliopo katika sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. NAMELOK E.M. SOKOINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wachumi wanasema baadhi ya mambo ambayo nchi ya Asia *Tigers* zilifanya ili kuweza kupiga hatua za haraka za maendeleo ni pamoja na kuwekeza katika sekta ya elimu. Tumeshuhudia jitihada mbalimbali za Serikali za kuendeleza sekta ya elimu nchini kuanzia elimu ya msingi hadi sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizo bado sekta ya elimu inakabiliwa na changamoto nyingi, tuna shule za msingi na sekondari nyingi zenye uhaba wa madawati, viti, vitabu, matundu ya vyoo, maabara, mazingira masafi, nyumba za walimu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri Serikali itazame upya tatizo la walimu na kulitafutia ufumbuzi hata tu kwa kukaa nao meza moja na kufanya mazungumzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za sekondari za Kata bado ni chache ukilinganisha na idadi ya watoto wanaomaliza shule za msingi. Pamoja na uchache wa shule za Kata, zilizopo pia ubora ni duni kwani kuna uhaba wa nyumba za walimu, ukosefu wa maabara na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali iwekeze kwenye elimu ya watu wazima. Miaka ya karibuni tuliona mpango kabambe wa kujenga shule za Kata mpango huu sina hakika bado upo ama umesitishwa, hatusikii tena ukihimizwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, mradi huu unafaa kuendelezwa kwa kasi ile ile kama siyo zaidi, leo tunaweza tusione faida yake, lakini ukitekelezwa kwa ufanisi miaka kumi ama ishirini ijayo Tanzania ya wakati huo haitakuwa kama hii ya leo, tutakuwa Taifa la waelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunganishe mchango wangu wa kuongea kwa mdomo kwa yale niliyobaki nayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iangalie Vituo vya Walimu, vituo hivi vinasaidia Walimu kujiendeleza na baada ya hapo kupanda daraja na kujiwezesha kuongeza elimu zao. Vituo hivi vimetelekezwa havina *fund* yoyote. Serikali ya Chama cha Mapinduzi, viangaliwe vyuo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule maalum Sinza, Mtoni, shule ya Uhuru walemavu, shule hizi zina matatizo makubwa ya majengo na vifaa vya kufundisha kwa Walimu. Miundombinu ya majengo ya walemavu si mizuri kwa afya zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wote wanastahili posho ya mazingira magumu kwa wale wa mijini na vijijini. Serikali iangalie bajeti ijayo kama imeshindwa kikubwa basi hata kidogo wapewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za awali zimepiga hatua, katika shule za msingi nyingi kuna shule za awali. Shule za awali haziwezi kuendelea bila kuwa na fungu angalau la kuwapa uji, watoto wale wanakuwa mali ya Mwalimu Mkuu tusiangalie shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya walimu ni mengi sana, hatuwezi kuyatatua yote, lakini niombe Serikali yangu sikivu iwasaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule ya msingi Bunge ambayo imebeba jina takatifu la Bunge, haina hadhi ya kuitwa Bunge kutokana na mazingira ya shule yalivyo. Niombe Serikali itafute wafadhili wakarabati shule hiyo yenye jina zito la Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Mheshimiwa Waziri na Naibu twende pamoja wakaone hali halisi ya shule zetu za Sinza, Mtoni, Uhuru na kukaa na Walimu wa shule za msingi na sekondari tujue matatizo yao badala ya kusikia tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam ni Jiji na ni Taifa, tukikaa na makundi ya Walimu Kimanispaa tutawasikia matatizo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ndiyo moyo wa maendeleo ya nchi. Katika maisha haya ya utandawazi tunahitaji kuwa na mfumo wetu wa elimu ambao utaweza kumjenga kijana wa Kitanzania kupambana na kijana wa Kenya, Marekani na India na kwingineko. Tujiulize kijana huyu amepatiwa ujuzi wa aina gani, anaweza kushindana na wenziwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mfumo wetu ni wa kuzalisha watoto wenye uwezo wa ku-*cram* badala ya kuzalisha vijana wenye uwezo wa kufikiri na kuchambua mambo. Ni dhahiri vijana wetu tunawaandaa ili wafanye mtihani na sio kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itabidi itazame kwa kina mfumo wa nadharia tunahitaji elimu itakayomwandaa kijana wa Kitanzania awe mshindani katika miongo hii ya utandawazi. Sasa hivi si muda wa kushindanisha shule gani zina *division one* nyingi, bali ni muda wa kushindanisha shule zenye kuzalisha wanafunzi wenye uwezo wa juu wa kufanya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhara haya ya mfumo huu yamejitokeza tulipoanza kuwakaribisha wawekezaji wa kuanza kuwachukuwa wafanyakazi wa nchi nyingine na kuwaacha vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wengi hufeli somo la hisabati na Kiingereza kwa sababu zifuatazo:-

Somo lina matatizo yake mbalimbali, hakuna vitabu vya kiada na ziada kwa walimu na wanafunzi, wanafuzi wengi darasani, hakuna vifaa vya kufundishia, mwalimu anayefundisha somo yeye mwenyewe hajalifaulu alipokuwa shule, leo unamwambia afundishe ataweza wapi kutoa matunda mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio kila Mwalimu anaweza kufundisha hisabati na Kiingereza kuna wengine wamefaulu, lakini *how to impart the knowledge it's a problem,* vizuri Wizara kuchagua Walimu watakaoweza kufundisha na atakayeweza kutengeneza vifaa vya kufundishia kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakaguzi waweze kuwapitia na kuwaangalia Walimu wa masomo haya hasa wale ambao ndio kwanza wanaajiriwa. Pia waweze kuwaangalia wale Walimu wanaofundisha katika Vyuo vya Ualimu pia pengine *methods* wanazofundisha ni matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara mnajitahidi kutoa mafunzo kwa walimu, lakini nina wasiwasi na mfumo na mpango wa utoaji. Inawezekana *desk* la mafunzo linatayarisha, lakini sio yanayohitajika kwa walimu. Hivyo, hata wakipewa huwa ni kazi bure *its waste of time, energy and money.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri apeleke *circular* shule zote na kuwataka Walimu waandike *needs* zao kwa kila shule, azipambue, afanye mafunzo kulingana na matakwa ya Walimu kulingana na Kanda na Mikoa. Hapa utaona kutakuwa na faida ya mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wa vyuo, nao sasa wanalia kama Walimu wa shule za msingi na sekondari, nao wana matatizo ya *arrears,* kuna waliochaguliwa na kupewa *post* toka mwaka 2010 mpaka hii leo hawakupata *arrears* kwa nini? Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atueleze kwa nini hawapewi, kuna tatizo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuona Katibu wa Baraza la Mitihani hataki kukubali kwamba mitihani inavuja. Mpaka aambiwe kwa hili hataambiwa kwa sababu kuna kula ndani yake, ni yeye mwenyewe afanye tafiti zake na ataliona hili. Haiwezekani mtu wa nje apate mtihani kama ulivyo bila kutoka huko unakotayarishwa. Kama mwalimu kaupata basi ni mtu wa mwisho anayepelekewa na wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa kwamba Mkurugenzi wa *IT* amesimamishwa kazi kwa sababu ya kuingiza matokeo ya *Islamic Knowledge* vibaya. Si somo hilo tu nina taarifa kwamba, hata wale waliochukuwa *Arts* hawakupata matokeo yao wanaambiwa wajiunge mwakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kosa sio lao kwa nini wawe *punished,* kuna haja ya kuwa na Tume Maalum kwa pande zote mbili za Muungano ili iweze kuleta jibu

la uhakika. Je, Wizara iko tayari kuunda Tume ili iweze kuangalia kwa undani ili Baraza liweze kujikosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo ni moja ya matatizo kwa wanafunzi kwa muda wa miaka minne sasa. Bado wanafunzi wanapata taabu na kuhangaishwa kwa pande zote mbili za shilingi, wao wapo kati na kubaniwa na chuo na Bodi ya Mikopo. Hata inawapelekea wanafunzi kutamka kwamba fedha hizi hawagawiwi wala si msaada bali wanakopeshwa na watahitajika kuzilipa. Wanafunzi wanaopokelea *Baclays bank* wao ndio wanaocheleweshwa mpaka mwisho wa muhula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri wakati wa majumuisho atueleze ni sababu gani za msingi ambazo zimepelekea ucheleweshaji mkubwa wa kutoa mikopo hii ya wanafunzi. Kuna wanafunzi ambao wapo nje ya nchi na hawa wa hapa hapa wakati wanapojaza fomu za *online* juu ya mikopo zinawapa shida hasa wanapomaliza na kutaka kuzi-*send* hukataa, haziendi kwa sababu kuna sehemu hukubali na nyingine hukataa hata kama *information* ni ya kweli. Hivyo, Mheshimiwa Waziri hili nalo alirekebishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi kwa vyuo vyote ambavyo vimewataka vijana wa kike kuvaa nguo za staha ili kutukuza mila na tamaduni za Kitanzania. Wakuu wa Vyuo endeleeni hivyo hivyo msilegeze kamba.

**MHE. RAMADHANI HAJI SALEH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukuwa nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kufika hapa tukiwa katika hali ya uzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ni muhimu kwa binadamu yeyote ukiacha kwa nchi yetu. Nchi yetu bado hatujajipanga vizuri katika eneo la elimu, kwani hadi leo baadhi ya vijiji vingi vimekosa shule na baadhi ya vijiji ambavyo wanazo shule wana ukosefu wa Walimu, miundombinu na vifaa vya kufundishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ijikite zaidi katika sekta ya elimu ili Taifa letu liweze kupiga hatua. Kama Walimu wetu hawataongezwa posho au kuongezewa mishahara yao basi tusitegemee Walimu hao kutoa elimu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tatizo la watoto wa kike ambao wanapata mimba wakiwa shule. Naiomba Serikali iweke mpango maalum wa kuweza kuendelea na masomo ili iwe fundisho la watoto hao kutokukosa elimu na kuweza kuacha kufanya vitendo vibaya ambavyo vinapelekea hata kupata maradhi ambukizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kazi kubwa inayofanya katika kusimamia sekta ya elimu hapa nchini. Naomba kutoa maoni yangu katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo ianze utaratibu wa kuwapa mikopo wanafunzi wa ngazi ya *Diploma* na Cheti ili tuweze kupata watendaji wa ngazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *NACTE* ishughulikie udahili wa wanafunzi wanaojiunga na vyuo kutokea katika mfumo wa Vyuo vya Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kutenga pesa za kutosha kwa *OC* ili kuziwezesha taasisi za elimu ya juu kujiendesha vyema. Hivi sasa hali si shwari kwa taasisi hizo kutokana na kiwango kidogo cha *OC* kinachopokelewa katika taasisi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la wafanyakazi wa vyuo vikuu na vyuo vikuu vishiriki ambao walikuwa wanafanya kazi ya kufundisha, lakini wasio Wahadhiri. Bahati mbaya kulikuwa na utaratibu wa ahadi ya malipo, lakini zoezi hilo halikwenda vyema. Naomba Serikali ilishughulikie tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu na wewe mwenyewe kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia hapa Bungeni kwenye Bunge lako Tukufu kwa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara ya Elimu na Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ninaloliona au linaloikabili Wizara hii ya Elimu ni; kwanza, Bodi ya Mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Ni kweli ni tatizo kubwa hapo mahali, wale wanafunzi ambao wameomba na kukubaliwa kupewa mkopo wanapokuwa hawapati mikopo kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia nyuma kwa kusema kuwa natoa hongera kwa Serikali yetu kwa kutoa mikopo kwa wanafunzi wengi kulingana na miaka yote ya nyuma. Lakini pale penye tatizo ni vizuri kuparekebisha. Wanafunzi wanapokosa kupata fedha za mikopo kwa wakati ni kweli wanahangaika mpaka wakati mwingine wanafikia kufanya fujo na maandamano mpaka kwenye Maofisi ya Viongozi Wakuu huko Wizarani, Mikoani na Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli inabidi uwatulize angalau waelewe hivyo hivyo na kutulia, nilikuwa namsihi Waziri pamoja na Bodi pale fedha za mikopo zinapopatikana kutoka Hazina watoe kwa wanafunzi wote wahusika wa mikopo. Mheshimiwa Waziri na Bodi ya Mikopo kuweni na ushirikiano pamoja na Waziri wa Fedha baada ya bajeti kutenga na kutoa feha za mikopo kwa wakati (mara zinapopatikana), kuwachelewesha wahusika ndio chanzo cha matatizo pamoja na migomo ya wanafunzi. Naamini Serikali

yangu ya Chama cha Mapinduzi ni sikivu na haishindwi inaweza kila jambo, muhimu ni kujipanga tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mambo mazuri sana yametendeka na Wizara ya Elimu na Ufundi, lakini tatizo lingine ni bajeti inayotolewa kwa Idara ya Ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi haufanyiki sawasawa inavyotakiwa. Nashauri idara hii iangaliwe vizuri, kuwepo pia na magari na usafiri ili ukaguzi ufanyike ipasavyo. Wizara naomba iangalie maabara, haiwezekani kuwa na Taifa ambalo hatuna wanasayansi. Tatizo hili mpaka sasa linakuwa kubwa kiasi kuna upungufu mkubwa wa walimu wa sayansi. Mpango maalum uwepo na utimizwe kusudi shule zetu za Kata (ingawaje wanajitahidi) kuwa na maabara na vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migomo sio suluhisho la matatizo, kwa hiyo yale mambo ambayo yanaweza kuzungumzwa (matatizo ya walimu) wasikilizwe, yawekewe mkakati wa kuyatatua. Yale ambayo hayawezekani Serikali haiwezi kujikwamua mahali ambapo haifikii wamekwishaelezwa na Mheshimiwa Rais na Viongozi wengine. Kwa hiyo haiwezekani *full stop*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa hayo maoni na ushauri, naunga mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ya madai ya Walimu. Walimu wa nchi hii wamekuwa wakilalamikia maslahi yao ya ualimu, mazingira magumu ya kufanyia kazi, kutokulipwa stahili zao kama vile malimbikizo ya mishahara, posho ya uhamisho, likizo, kutopandishwa madaraja na kadhalika. Mfano Wilaya ya Hanang baada ya uhakiki wa malimbikizo ya mishahara posho ya uhamisho na likizo, wanadai sh. 399,283,019/= malipo yaliyofanyika mwezi Aprili Mei ni sh. 79,613,031, madai yaliyobaki ni sh. 319,668,988/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri amesema hakuna madai ya Walimu. Je, madai haya ya Walimu yatalipwa lini? Uhakika naambatisha madai hayo. Hivyo, nipate jibu sahihi wakati Waziri unapotoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuwapeleka Walimu au CWT Mahakamani ni sahihi, wakati wana madai ya kweli? Wewe unadaiwa baada ya kukufanyia kazi, halafu nikitaka haki zangu unakimbilia Mahakamani, je hiyo ni busara? Waziri anataka walipe hasara iliyotokana na mgomo ikiwa na vipindi vilivyopotea. Je na wewe ukidaiwa riba ya madai mtaweza kulipa? Endapo Serikali haitalipa hayo madeni ya Walimu ni wazi Walimu hao wataendelea na migomo baridi ya kutofundisha wanafunzi, hivyo, athari itakayotokea ni watoto wetu kukosa elimu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifanye haraka kukamilisha malipo ya walimu na kuwapa motisha. Mwalimu wa Tanzania ni sawa na mtu aliyesukumwa juu ya mwembe akapanda juu ya mwembe, huko juu

akaanza kula embe tunda) akamsahau aliye msukuma na kuanza kumtukana na kumrushia kokwa aliye chini. Sisi sote tumetokana na elimu tuliyopata toka kwa Mwalimu wa awali mpaka kupata vyeo vya juu), tukawasahau waliotoa elimu. Tuwe na busara na upendo ndio dawa pekee ya kupunguza kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusahaulika kwa shule za ufundi; shule za ufundi hazina Walimu wa kutosha kwa baadhi ya idara na vifaa vya kufundishia. Mfano Bwiru *Technical*, Moshi Technical, Tanga *Technical*, Ifunda *Technical* na kadhalika. Serikali iongeze fedha ili shule hizo ziwe endelevu. Pia Chuo cha Ualimu wa Ufundi Kleruu kimesahaulika, hivyo kuna hatari baadaye kukosa Walimu wa ufundi kufundisha shule zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Hanang, Mkoa wa Manyara hakuna Chuo cha Ualimu. Je, haiwezekani kujenga chuo katika Mkoa huo hususan Wilaya ya Hanang? Napendekeza Hanang kwa kuwa kuna majengo na eneo katika mashamba ya *NAFCO BASOTU Plantation* ambapo Serikali inataka kubinafsisha shamba hilo, hivyo, ni vema Wizara ikaomba eneo hilo ili kuleta tija kwa wananchi, rasilimali watu.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana na watoto wengi hapa nchini, elimu ni tegemeo la kufanikisha ndoto zao na wanatumia msemo wa elimu ni ufunguo wa maisha. Bajeti ya elimu inashindwa kukidhi kwa kuwa shule nyingi sana zimejengwa kutokana na ongezeko la idadi ya watoto wanaojiunga na shule ili wakidhi mategemeo na

malengo yao ya maisha. Je, shule hizo ni shule kweli? Kwa maana inakidhi vigezo vya kuwa shule kwa mujibu wa mpango wa maendeleo ya elimu ya sekondari *(SEDP)?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwango kadhaa vilipaswa kufikiwa na kutekelezwa miongoni mwa vigezo hivyo ni uwiano kati ya wanafunzi na Walimu wa 30:1 uwiano wa vitabu vya kiada na wanafunzi wa 1:1 kwa kila somo, shule zote za kutwa zinatoa chakula cha mchana na kadhalika. Bado tuko mbali na malengo hayo ndiyo maana tunapaswa kuuliza wakati gani shule ni shule. Wizara ichukue changamoto hii, ishirikiane na wadau kuzifanya shule zetu ziwe shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ya shule zetu nchini, shule zetu nchini kwa upande wa sekondari na msingi zina upungufu mkubwa sana wa miundombinu ikiwa ni upungufu wa madarasa. Nyumba za waalimu maabara mabweni madawati na vinginevyo. Miundombinu ya shule inachangia kujengea au kubomoa ari ya wanafunzi kusoma. Nashauri Wizara kuwa na mkakati maalum wa kumaliza tatizo hili la miundombinu katika shule zetu ili kuongeza ari ya wanafunzi kusoma na kufaulu, hivyo kufanya kiwango cha elimu kupanuka na kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeaminiwa kwa muda mrefu kwamba kwenda shule ni jambo zuri na mtu yeyote anayepinga shule au asiyepeleka mtoto shule haelewi thamani ya shule, lakini hatujaangalia athari ya sasa kwa watoto hao. Watoto hao wanalazimika kukaa kwenye madarasa yasiyo na zana, bila vitabu

au kitu chochote cha kusisimua akili yao, bila Mwalimu kwa sehemu kubwa ya siku na bila kumwelewa Mwalimu hata anapoingia darasani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukilinganisha na sekta binafsi zinazoendesha shule na shule za umma kuna utofauti mkubwa sana wa miundombinu ya shule. Ufaulu wa wanafunzi na kadhalika. Kwa pamoja tunapaswa kuangalia shule na utoaji wa elimu kwa namna ile ile ambayo sekta binafsi inaangalia bidhaa zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Elimu kwa sasa inalenga shabaha ya upatikanaji na si kuboresha elimu, hivyo, msisitizo mkubwa unatakiwa uwe katika ujuzi atakaopata mwanafunzi na sio miaka aliyokuwa shuleni na kuongeza walimu wengi wenye ujuzi ili kupunguza idadi ya wanafunzi kwa kila darasa na kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapata kiwango bora cha elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta binafsi zinazoendesha shule za msingi, shule nyingi za binafsi zimekuwa na mitaala au ufundishaji wa masomo tofauti, mfano Kifaransa na kadhalika. Watoto wetu wengi hata Kiswahili chenyewe kumudu ni tatizo, leo wanafundishwa lugha nyingine za kigeni ikiwemo Kiingereza na Kifaransa. Huku ni kuwachanganya watoto hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara isimamie shule hizo na kutoa mwongozo ambao utafuatwa na shule zote binafsi na ningeshauri msisitizo utolewe kwa lugha ya Kiingereza tu kwa kuwa lugha hiyo ni ya Kimataifa.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maslahi ya Walimu, naishauri Serikali kufanya haraka mchakato wa kuwapatia maslahi stahiki Walimu hao kwani kazi ya Mwalimu sote tunaijua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naishauri Wizara pale Mwalimu anapopandishwa cheo, basi Serikali imlipe mafao yake sambamba na uteuzi bila ya kumchelewesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi kirefu Serikali imepuuza makaazi ya Walimu katika sehemu zetu mbalimbali za Kata, Wilaya na Majimboni na kusababisha Walimu kukataa kwenda kufanya kazi huko. Hivyo, naiomba Serikali kuweka mpango mkakati na wa makusudi wa kuondosha tatizo hilo angalau kwa kiwango cha kati na naiomba Serikali kupitia Wizara hii ikija tena mwakani watueleze utekelezaji wake kwa takwimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgomo wa Walimu kwanza napinga vikali na kulaani mgomo uliofanywa na walimu wa hapa nchini mwetu. Tena naunga

mkono hatua zote zilizochukuliwa na Wizara hiyo ya kuwachukulia hatua za kinidhamu kwa waliohusika na kadhalika. Hivyo, nashauri kuwasimamia Walimu wetu kuachana na tabia hiyo chafu ambayo wamekuwa wanaifanya kwa kufuata mkumbo wa siasa na utashi wa watu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Wizara iweke utaratibu maalum wa kuwajazisha mikataba Walimu wote nchini kuwa atakayejiingiza katika migomo atakuwa amejifukuzisha kazi mwenyewe au adhabu kali nyinginezo ikiwemo kukatwa mshahara au hata kifungo.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu bora ni Walimu bora, kauli ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuhusu mgogoro uliowasilishwa na Chama cha Walimu Tanzania (CWT) iliyotolewa Bungeni tarehe 10 Agosti, 2012 haiwezi kuleta matumaini kwa pande zote mbili wala kuleta ufumbuzi wa mgogoro huo wenye athari kwa sekta nzima ya elimu nchini na maisha ya wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari ilishawasilisha taarifa tarehe 20 Julai, 2012 kuwa imeongeza mishahara kwa wastani wa asilimia 14 tu kwa Walimu. Aidha Serikali imerudia ahadi ile ile ya kutumia Bodi ya Mishahara na Maslahi, ahadi ambayo ilianza kutolewa Bungeni kutoka mwaka 2010 bila utekelezaji kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi wa Mahakama wa tarehe 2 Agosti, 2012 haukutoa ufumbuzi kuhusu madai ya Walimu bali ulibatilisha tu mgomo na kurejesha pande mbili kwenye majadiliano. Hata hivyo, ikumbukwe kuwa tayari walimu na Serikali walishashindwa kukubaliana mbele ya msuluhishi na kutakiwa kuchukua cheti cha kushindwa kusuluhisha mgogoro tarehe 25 Julai, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo majadiliano ambayo yameagizwa na Mahakama kwa kushirikisha wataalam wa Sheria za Kazi yanapaswa kuwekewa utaratibu na chombo cha tatu *(third party)* kwa mujibu wa Katiba, ibara ya 63 Bunge na Wabunge ndio wenye wajibu wa kuishauri na kusimamia Serikali. Hivyo, katika majumuisho, Wizara ikubali kwamba majadiliano yanayoendelea yashirikishe wataalam watakaoteuliwa na Bunge kupitia ama Azimio la Bunge au Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na madai ya nyongeza ya mishahara na posho bado kuna malimbikizo ya madeni ya walimu wa zamani na walimu wapya. Kauli ya Serikali kuwa malipo ya bilioni 52 yameweza kulipa madeni ya walimu wote nchini mpaka tarehe 30 Juni, 2012 haina usahihi. Hivyo, Serikali ieleze ni kwa nini bado kuna orodha ndefu za Walimu wenye maelezo na vielelezo vya madai mbalimbali katika maeneo mengi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, pamoja na hatua kwa CWT kuhusu fidia Serikali itoe onyo kwa viongozi wake wa Serikali waliokiuka ibara ya nne (4) na 107A za

Katiba. Katika kipindi cha mgomo katika mwaka wa fedha 2011/2012, kupitia michango yangu Bungeni nilishauri hatua za Serikali katika masuala mbalimbali ya elimu ya msingi na sekondari katika Jimbo la Ubungo ambayo mpaka sasa sijapata majibu. Narejea tena mwaka wa fedha 2012/2013, kupewa majibu kwa yafuatayo:-

Mosi, kuhusu mgogoro wa shule ya sekondari Mburahati ambayo kwa sasa iko katika majengo ya shule ya msingi. Uamuzi unapaswa kufanywa kwa kushirikiana na Manispaa ya Kinondoni ama kutafuta eneo mbadala la kuhamishwa shule hiyo au kuigeuza shule ya msingi kuwa ya sekondari.

Pili, kukamilisha kuanzisha shulez a kidato cha tano na sita ambapo shule za sekondari Kibamba na shule ya Makuburi (Yusuph Makamba) zilipendekezwa tangu mwaka 2011.

Tatu kuboresha mfumo wa mabasi yaliyotolewa na *CRDB* kwa ajili ya wanafunzi kwenye barabara ya Morogoro kuweza kufika pia katika maeneo ya pembezoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika aya ya 88, Wizara imeeleza majukumu ambayo imetekeleza kwenye mwaka wa fedha 2011/2012, kupitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ikiwemo kuchangisha bilioni 1.07 kwa ajili ya kituo cha wanafunzi. Hata hivyo, katika aya ya 136 hakuna malengo yaliyowekwa kwenye mwaka wa fedha 2012/2013, kuhusu maendeleo ya ujenzi wa kituo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo Wizara irejee kauli ya Rais Kikwete wakati wa harambee ya ujenzi wa kituo husika na kutenga fedha katika bajeti ya mwaka 2012/2013, kwa ajili ya kuharakisha ujenzi. Aidha Wizara izingatie kuwa kwa mujibu wa mpango wa Taifa wa miaka mitano kipengele cha A.1.5, kiasi cha shilingi bilioni nane kilipaswa kutengwa kwenye mwaka wa fedha 2012/2013, kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa Chuo kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam warejee michango yangu niliyotoa kupitia Wizara ya Nishati na Madini kuhusu Chuo hicho kishiriki katika masuala ya sekta ndogo za mafuta na gesi asili. Hata hivyo, iambatane pia na kuhakikisha ujenzi wa bomba la gesi unaoendelea Dar es Salaam kwa ajili ya majumbani uhusishe pia mtandao kufikishwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kushirikiana na *TPDC* ili kupunguza gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu aya ya 102, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shiriki Muhimbili mwaka wa fedha 2011/2012, nishauri Wizara kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kutatua mgogoro wa ardhi katika Kata ya Kwembe eneo la Mloganzila kuhusu fidia ya ardhi. Katika kipindi husika Serikali kupitia kampuni ya udalali imekwenda kuvunja nyumba za wananchi katika eneo husika kwa notisi ya muda mfupi huku kukiwa na kesi mbili Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake ni kuwa kuna kaya zimekosa makazi na kuwa wakimbizi wa ndani *(internally displaced persons IDP)*. Kwa kuwa watu hawa ni wahanga wa ahadi za Mawaziri wa Serikali wa nyakati mbalimbali kwa wananchi hao kuhusu fidia ya ardhi. Naomba Serikali iende kukutana na wahanga husika na kutoa misaada ya kibinadamu kufuatia maafa yaliyowakuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika aya ya 143, Serikali imeeleza kuwa itaanza ujenzi wa miundombimu ya barabara, maji na umeme katika eneo la Mloganzila hatua ambayo naiunga mkono. Hata hivyo, kiasi cha bilioni mbili kilichotengwa kupitia *addendum* kwenye mradi 4391 bado ni kidogo kwa kuzingatia Mpango wa Taifa wa miaka mitano kipengele A.1.5 ulihitaji kutengewa jumla ya bilioni 13 kwa mwaka 2011/2012. Aidha Wizara ya Afya ifanye mkutano maalum na *TANROADS, DAWASA* na *DAWASCO* na *TANESCO* ili kuunganisha nguvu za kuharakisha utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika aya ya 79, Tume ya Vyuo Vikuu imeeleza kuwa imefanya tathmini ya kitaalam katika vyuo 16 kikiwemo cha Saint Joseph *University in* Tanzania kilichopo katika Jimbo la Ubungo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wabunge tupewe ripoti ya tathmini hiyo kwa ajili ya kutimiza vizuri wajibu wa Kikatiba wa kuishauri na kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya Taifa kiutaalam na stadi ni duni sana kwa kuzingatia kuwa ni asilimia tatu tu ya nguvu kazi Tanzania ndio yenye utaalam wa

juu wakati asilimia 84 ikiwa haina utaalam au ina stadi za chini kabisa. Ili kufikia malengo yaliyowekwa na Mpango wa Taifa wa miaka mitano ni lazima kwa wastani kila mwaka kuanzia mwaka 2011 ilipaswa kuwe na wahitimu angalau 80,000 kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya 2011/2012 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2012/2013 hayaoneshi lengo hilo kufikiwa. Chanzo kikuu cha hali hiyo ni mfumo mzima wa uwekezaji katika elimu ya juu ikiwemo sera ya ugharamiaji wa elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012, niliomba kupatiwa nakala ya ripoti ya Kamati iliyoundwa na Rais kuhusu ugharamiaji wa elimu ya juu, lakini mpaka sasa Wabunge hatujapewa nakala kumeza kutimiza vizuri zaidi wajibu wa kuishauri na kuisimamia Serikali kuhusu suala husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya ombi hilo ni Kamati ya Huduma ya Jamii kueleza katika taarifa yake ya tarehe 13 Agosti, 2012, kuwa itafuatilia na hivyo kimsingi kurudia kazi ambayo ilikwishafanywa na Kamati na Tume nyingine kwa fedha za walipa kodi. Matokeo ya hali hiyo na migogoro pia kuendelea katika elimu ya juu na Serikali kushughulikia chanzo badala ya matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika muktadha huo na kwa kuzingatia upungufu wa wataalam ambao unaikumba nchi yetu, Wizara ya Elimu na Mafunzo itoe kauli ya kuwezesha kurudishwa masomoni kwa

wanachuo waliofukuzwa au kusimamishwa katika vyuo mbalimbali vya umma ikiwemo *UDOM, MUHAS* na *UDSM*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wanafunzi 150 walisimamishwa masomo mnamo tarehe 14 Desemba, 2011 na tarehe 10 Januari, 2012 kwa kile kilichoelezwa kuwa ni chanzo cha migomo ya tarehe 11 Novemba, 2011 na tarehe 9 Janunari, 2012 huku chanzo halisi kikiwa ni madai ya mikopo ya elimu ya juu. Toka wakati huo wanafunzi husika wamekuwa wakirudishwa kwa awamu huku kukiwa na tuhuma za ubaguzi na upendeleo katika taratibu za kurudisha wanachuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira hayo hata idadi ya wanafunzi waliorudishwa na waliobaki haiko bayana, suala ambalo Serikali inapaswa pia kulitolea ufafanuzi kwa mujibu wa Taarifa nilizonazo takribani wanafunzi 30 bado hawajarudishwa ambao wako kwenye makundi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwao wako viongozi 11 wa *DARUSO* ambao wamehukumiwa kwa madai ya kujadili maamuzi ya Baraza la Chuo,makosa ambayo ilipaswa ihukumiwe *DARUSO* kama chombo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kundi wanachuo wanne lenye kujumuisha wajumbe wa *DARUSO* Bodi pamoja na baadhi ya Wabunge ambao wanapaswa kupewa msamaha kwa kuwa wanahukumiwa kwa kile kinachoelezwa kuwa walikuwa vinara wa kushawishi maamuzi kwenye vyombo vya Kikatiba vya *DARUSO*.

Kuna kundi la wanafunzi nane baada ya mapitio ya maamuzi ya Baraza la Chuo bado wameachwa na kundi lingine walifukuzwa mmoja wengine bila hata ya kuitwa.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kusema naunga mkono hoja hii. Aidha, nampongeza sana Waziri Kawambwa na Naibu wake Mulugo kwa kufanya kazi kwa bidii na kuleta utulivu kwenye elimu hasa elimu ya juu. Pamoja na pongezi hizo, naomba Serikali izingatie na itekeleze haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukamilishaji wa maboma ya madarasa na nyumba za Walimu Jimbo la Msalala, kumekuwepo tatizo la upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini za kukamilisha miradi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na hata nyumba za walimu kupitia mradi wa kuboresha elimu uliokoma awamu ya tatu wa MMEM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa mradi huu wananchi walihamasishwa na kuchangishwa fedha na vifaa kwa ajili ya kujenga maboma ya madarasa na nyumba za walimu na Serikali ilikuwa inatoa fedha za ukamilishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo ulitekelezwa kwa mafanikio makubwa kwenye Mikoa mingine, lakini kwa Mkoa wa Shinyanga hususani Wilaya ya Kahama mradi haukuanza mapema kutokana na ukosefu wa elimu na uhamasishaji mdogo, hivyo wananchi

walianza kuuelewa mradi na kuanza kuchangia miaka ya mwisho ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya hali hii hadi mwaka 2005 Jimbo la Msalala liliachwa na maboma ya nyumba za Walimu 58 na vyumba vya madarasa 97 huku nguvu za wananchi zinazofikia shilingi 510 milioni zikiwa zimetumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokamilishwa kwa maboma hayo hadi sasa ambayo kwa makisio ya sasa zinahitajika shilingi 1.3 bilioni kukamilika, kumewavunja moyo sana wananchi kuchangia miradi mingine hasa kwa kuwa baadhi ya majengo hayo yameanza kubomoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hiyo ya nguvu za wananchi kuwa hatarini kupotea bure, ukiongeza na hali ngumu ya uchumi inayoukumba Mkoa wa Shinyanga kutokana na ukame wa mfululizo na kukosekana kwa bei ya mazao ya kilimo(hasa pamba) na mifugo kunafanya uchangiaji wa wananchi kwenye miradi hii na miradi mingine usiwezekane kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, wingi wa miradi inayohitaji uchangiaji wa nguvu za wananchi katika sekta za afya, elimu na maji nako kunafanya wananchi kukata tamaa na wengine kuichukia Serikali na Chama kwani mara nyingi uchangishaji umekuwa ukiambatana na mabavu toka kwa Watendaji wa Vijiji na Kata wenye dhamana ya kukusanya michango hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali katika hali ya dharura na kwa dhana ya kuboresha elimu na uchumi wa Mkoa wa Shinyanga itenge fedha na kukamilisha maboma hayo. Kwa kutambua uhaba wa fedha Serikalini, nashauri angalau ifanyike kwa awamu mbili mwaka huu 2012/2013, (shilingi 650 milioni) na mwaka 2013/2014, (shilingi 650 milioni).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Chuo cha Ufundi Kahama, Wilaya ya Kahama ina migodi miwili ambayo inazalisha ajira ndogo ndogo za moja kwa moja na za kujiajiri nyingi, lakini vijana wa Kahama hawazipati kwa kukosa ujuzi stahili. Kwenye ilani tuliahidi kujenga *VETA* kila Wilaya na kipekee wakati wa kampeni, Mheshimiwa Rais aliahidi kujenga chuo Jimboni kwangu eneo la Bugarama ambalo tayari limeshatengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa elimu ubadilishwe ili kuwajengea wanafunzi uwezo wa kujiajiri baada ya masomo, mara kadhaa nimeshauri kuhusu mfumo wetu wa elimu kuwa umepitwa na wakati, unazalisha vijana wasioweza kujitegemea. Naungana na Mheshimiwa Abiya Nyabakari kuhusu vijana kufanya kazi kupitia mafunzo au malezi wanayoyapata shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda sasa umefikia wa kuimarisha elimu ya kujitegemea. Tunasema Kilimo Kwanza, lakini hakiko mashuleni. Lazima vijana wajifunze kutumia mbolea kwa vitendo, kutumia *powertillers* kwa vitendo, kulima kisasa na hata kufuga kisasa. Watoto wajue kufuga nyuki, samaki na

kadhalika kwa vitendo, tuachane na mitaala ya Kiingereza tufuate mfumo wa elimu wa China, India na hata Mauritius.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mgogoro wa Walimu, nimetoka Jimboni wiki iliyopita, nimeongea na baadhi ya Walimu kimsingi hawana motisha ya kazi. Pamoja na madai yao ya nyongeza ya mishahara ya 185% kuwa ni makubwa na hayahimiliki kwa sasa, naishauri Serikali ione uwezekano wa kukubaliana na walimu na kuwaboreshea mishahara na marupurupu mengine angalau kwa awamu kati ya sasa na 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ilivyo hivi sasa Walimu wanaendesha mgomo baridi na bila kificho. Wengine wamesikika wakionesha nia ya kukikomoa chama cha CCM 2015, hasa kwa kuwa wengi wao ndio wamekuwa wakitumika kama wasimamizi wa uchaguzi. Hili ni bomu kwa CCM 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na malalamiko yao ya nyongeza ya mishahara lakini kuna tatizo la madai yao mbalimbali, wapo ambao wamepanda vyeo lakini hawajarekebishiwa mishahara. Wako ambao wana matatizo ya kinidhamu wanalipwa nusu mishahara, lakini *TSD* hawapewi fedha za kuendesha vikao na kushughulikia matatizo haya ya nidhamu kwa wakati. Ni vema sasa *TSD* ijengewe uwezo ili ishughulikie matatizo ya nidhamu ya walimu kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja hii.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri na timu yake yote kwa kuandaa hotuba ya bajeti yenye maelezo ya ufafanuzi wa kina. Vile vile nampongeza Waziri na timu yake yote kwa kazi nzuri ya kuhakikisha Taifa limepata watu walioelimika kwa manufaa ya Taifa. Pamoja na pongezi naomba kushauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naishauri Serikali itazame upya rasilimali za majengo na vifaa vya kufundishia zilizokuwa za kidato cha kwanza hadi cha sita ambazo kwa sasa zinapokea watoto wa kidato cha tano na sita tu. Rasilimali hizo kwa sasa hazitumiki mfano, vyumba vya madarasa havitumiki. Pia vifaa vya kufundisha kidato cha I hadi cha IV havitumiki. Naishauri Serikali au irudishe madarasa ya kidato cha kwanza na cha nne au iongeze watoto kidato cha tano hadi cha sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke mikakati thabiti ya kujenga mabweni ya watoto hasa wa kike na nyumba za walimu. Naishauri Serikali ikope fedha kupitia Mifuko ya Jamii, *NSSF, PPF, PSPF* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika baadhi ya shule hapa nchini hasa sekondari, baadhi ya walimu hawaingii madarasani badala yake wakati wa masomo wanafanya kazi zao binafsi. Nashauri ufanyike ukaguzi wa mara kwa mara tena wakushutukiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kitengo cha ukaguzi kiboreshwe kwa kukiongezea fedha na vitendea kazi hasa magari, pikipiki na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri lugha ya kufundisha katika shule za awali mpaka Chuo Kikuu iwe ni Kiingereza. Pia somo la Kiswahili lipewe kipaumbele katika mpangilio wa masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, bwana wa viumbe vyote na pia napenda nimpongeze Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kazi yao nzuri ya kuiendeleza sekta hii ya elimu. Pia napenda nimpongeze Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa ufuatiliaji wake mzuri katika sekta hii kwa kiasi kikubwa sekta hii imeongeza ufanisi mzuri na inaridhisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ni muhimu sana katika Taifa lolote lile kwani ndio silaha madhubuti ya kukabiliana na changamoto mbalimbali za maisha. Taifa lolote lililokuwa na watu wengi wenye kuelimika basi ni rahisi kuweza kuvumbua mambo mengi na vipaji ambavyo vitawasaidia katika kumudu maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo katika sekta ya elimu katika nchi yetu yameendelea kwa kiasi kikubwa sana, kuna shule nyingi sana katika kila Kata zimejengwa pamoja na Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo ambacho ni miongoni mwa vyuo vikubwa Kusini mwa Jangwa la Sahara. Hii ni dhahiri kuwa sekta hii ya elimu yafaa kupongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya kuwa Serikali imejitahidi kuweka mazingira mazuri ya elimu, lakini bado kuna wanafunzi wanaomaliza shule huku hawajui kusoma na kuandika. Hali hii inasikitisha sana na inaonekana dhahiri kuwa inasababishwa na ukosefu wa walimu pamoja na vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali matatizo haya ndio yanayosababisha kuporomoka kwa elimu nchini. Hivyo basi, Serikali iandae mpango wa kudhibiti uvujaji wa mitihani, hili ndilo ambalo linaatthiri elimu kwa kiasi kikubwa nchini na wale wote watakaobainika kuhusika na uvujaji huu wa mitihani basi wachukuliwe hatua kali za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wamekuwa wakilalamika sana juu ya maslahi yao kuwa ni duni, mazingira magumu wanayofanyia kazi na kutolipwa stahili zao kama vile malimbikizo ya mishahara, posho ya uhamisho, likizo na kutokupandishwa madaraja. Naishauri Serikali ishughulikie madai haya ya walimu ili walimu wafanye kazi zao kwa uadilifu na wanafunzi wetu waweze kufaulu kwa kiasi kikubwa.

**MHE. LOLESIA J.M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri na Ushirikiano mkubwa sana hasa ninapofuatilia masuala mbalimbali ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu ni Wizara muhimu sana katika maendeleo ya nchi. Mwananchi akiwa na elimu anakuwa na uwezo wa kutatua changamoto alizonazo. Hivyo, naiomba Serikali iweke kipaumbele katika elimu hasa ya msingi na sekondari, shule nyingi hazina walimu wa kutosha. Baadhi yao wanapopangiwa shule zenye mazingira magumu wengi hawaendi. Naomba ule mpango wa kuwapatia posho maalum walimu walio katika mazingira magumu uanze mara moja. Hii itatoa motisha kwa walimu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili linalokera sana kwa Walimu wetu ni madeni ya Walimu. Walimu wengi bado wanadai madeni kulingana na kila mmoja jinsi ambavyo hajalipwa. Baada ya uhakiki Walimu wengine walipewa taarifa kuwa madai yao si ya kweli. Niiombe Serikali ifanye uhakiki mwingine maana Walimu wengi bado wanayo malalamiko makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu linahusu Chuo cha *VETA.* Kwa kuwa ni sera ya Taifa kwamba kila Wilaya ijengwe Chuo cha *VETA* katika Wilaya ya Geita na Mkoa mpya wa Geita hatuna Chuo kabisa. Kulingana na hali halisi iliyopo Wilaya ya Geita ina shule za sekondari zaidi ya 40. Hivyo, watoto wanaomaliza sekondari ni wengi sana. Hata hivyo, shule za msingi ni zaidi ya 200, wahitimu kutoka shule hizo ambao hawapati nafasi za kuendelea na masomo ya juu ni wengi sana. Hivyo, hitaji la Chuo cha Ufundi ni la msingi sana na ni la muhimu sana. Nichukue fursa hii kuiomba Serikali iweke kipaumbele cha kujenga Chuo

cha *VETA,* Geita ili kunusuru vijana wetu wengi katika Wilaya ya Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naunga mkono hoja.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri sana ambayo amejielekeza kujibu maagizo ya Ilani ya CCM. Ningeshauri kila Wizara iwe inatekeleza na kuwe malengo ya Wizara kutokana na maagizo ya Ilani na wabainishe kama Waziri wa Elimu alivyoweza kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu, naomba Wizara ihakikishe kuwa wanafunzi wa darasa la saba wa Wilaya ya Nkasi, Jimbo la Nkasi Kusini katika shule 14 wanafanya mitihani katika shule zao. Shule hizi ni shule za msingi zilizoko mwambao mwa Ziwa Tanganyika, sababu kubwa ni hatari kwa wanafunzi, kuwasafirisha mara kwa mara kwenda kufanya mitihani, usafiri wa maji siyo mzuri. Pili, ni haki ya vijana kufanyia mitihani katika shule zao, watoto wanakosa kufanya vizuri katika mazingira mageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukaguzi wa shule za sekondari na msingi, Kitengo hiki kiimarishwe ili kuongeza ubora wa elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mikopo ya elimu ya juu; kwa mtindo huu mikopo haiwezi kuwa endelevu kwani haiwezekani kila mwaka watoto wanaongezeka na kwamba Serikali iwe inagharamia fedha itatoka wapi? Ni vizuri utafutwe utaratibu wa kupata njia

itakayomudu mzigo unaongezeka mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wilaya ya Nkasi hasa Jimbo la Nkasi Kusini kupata Chuo cha *VETA*. Vile vile Mkoa wa Rukwa hauna *VETA,* baada ya Katavi kuwa Mkoa. Naomba Chuo hicho kijengwe mara moja Mkoani Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Chala, Wilayani Nkasi, naiomba Wizara kuanzisha *VETA* katika Chuo hiki ambacho kinayo majengo mengi yanayokaa bila kazi. Wizara inaweza kuanzisha Chuo kwani gharama za majengo inaweza kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo Vikuu, vingi vinakusanya fedha, lakini hazionekani kwenye taarifa ya fedha mfano, *UDOM* inakusanya fedha kidogo kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu mstaafu, Kaimu Katibu Mkuu, Kaimu Kamishna wa Elimu, Wakurugenzi na Viongozi wote kwa kutayarisha bajeti nzuri na ya kisayansi. Ni matumaini yetu kuwa, utekelezaji wake utakwenda sambamba na utayarishaji wa bajeti ili maendeleo yapatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na wananchi wa Jimbo la Kondoa Kaskazini kuchangia kwa kiwango kikubwa katika ujenzi wa shule za sekondari kutoka shule za sekondari saba mwaka 2005 mpaka shule za sekondari 32 mwaka 2007. Kuna tatizo kubwa la upungufu wa walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano:-

- Shule ya sekondari Sakami, mahitaji ni Walimu tisa, waliopo ni Walimu watano, kuna upungufu wa Walimu wanne;

- Shule ya sekondari Kinyasi, mahitaji ni Walimu tisa, waliopo ni Walimu wanne, kuna upungufu wa Walimu watano;

- Shule ya sekondari Kikilo, mahitaji ni Walimu tisa, waliopo ni Walimu watano, kuna upungufu wa Walimu wanne; na

- Shule ya sekondari Changaa, mahitaji ni Walimu tisa, waliopo ni Walimu watano, kuna upungufu wa Walimu wanne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa Walimu kimasomo hasa masomo ya sayansi ni kama ifuatavyo:-

- Shule ya sekondari Busi, somo la hisabati, mahitaji ni Walimu wawili, hakuna hata mmoja, kuna upungufu wa Walimu wawili;

- Shule ya sekondari Kinyasi, somo la hisabati, mahitaji ni Mwalimu mmoja, hawajapatiwa huyo mwalimu, kuna upungufu wa Mwalimu mmoja;

- Shule ya sekondari Kiteo, somo la hisabati, mahitaji ni Mwalimu mmoja, hakuna hata mmoja, kuna upungufu wa Mwalimu mmoja;

- Shule ya sekondari Loo, somo la hisabati, mahitaji ni Mwalimu mmoja, hakuna hata mmoja, kuna upungufu wa Mwalimu mmoja;

- Shule ya sekondari Mtobubu, somo la hisabati, mahitaji ni Walimu wawili, hakuna hata mmoja, kuna upungufu wa Walimu wawili;

- Shule ya sekondari Sakami, somo la hisabati, mahitaji ni Mwalimu mmoja, hakuna hata mmoja, kuna upungufu wa Mwalimu mmoja;

- Shule ya sekondari Kikilo, somo la *biology*, mahitaji ni Mwalimu mmoja, hakuna hata mmoja, kuna upungufu wa Mwalimu mmoja;

- Shule ya sekondari Changaa, somo la *biology*, mahitaji ni Mwalimu mmoja, hakuna hata mmoja, kuna upungufu wa Mwalimu mmoja;

- Shule ya sekondari Diki, somo la *biology*, mahitaji ni Mwalimu mmoja, hakuna hata mmoja, kuna upungufu wa Mwalimu mmoja;

- Shule ya sekondari Kalamba, somo la *biology*, mahitaji ni Mwalimu mmoja, hakuna hata mmoja, kuna upungufu wa Mwalimu mmoja;

- Shule ya sekondari Busi, somo la *chemistry*, mahitaji ni Mwalimu mmoja, hakuna hata mmoja, kuna upungufu wa Mwalimu mmoja;

- Shule ya sekondari Changaa, somo la *chemistry*, mahitaji ni Mwalimu mmoja, hakuna hata mmoja, kuna upungufu wa Mwalimu mmoja;

- Shule ya sekondari Kalamba, somo la *chemistry*, mahitaji ni Mwalimu mmoja, hakuna hata mmoja, kuna upungufu wa Mwalimu mmoja;

- Shule ya sekondari Kikore, somo la *chemistry*, mahitaji ni Mwalimu mmoja, hakuna hata mmoja, kuna upungufu wa Mwalimu mmoja;

- Shule ya sekondari Kinyasi, somo la *chemistry*, mahitaji ni Mwalimu mmoja, hakuna hata mmoja, kuna upungufu wa Mwalimu mmoja;

- Shule ya sekondari Kisese, somo la *chemistry*, mahitaji ni Mwalimu mmoja, hakuna hata mmoja, kuna upungufu wa Mwalimu mmoja; na

- Shule ya sekondari Masawi, somo la *chemistry*, mahitaji ni Mwalimu mmoja, hakuna hata mmoja, kuna upungufu wa Mwalimu mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na upungufu huu mkubwa wa walimu na hasa tukizingatia shule nilizozitaja hakuna kabisa walimu wa masomo hayo na huu ni mfano tu. Je, Wizara ina mpango gani wa dharura wa kuwezesha upatikanaji wa walimu kwa masomo niliyoyataja ili wanafunzi wanufaike na elimu wanayoipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha kuna upungufu mkubwa sana wa vitabu vya kiada, mfano uwiano wa mwanafunzi kwa kitabu,

- *Geography* 1:6;
- *English* 1:4;
- *History* 1:8;
- *Civics* 1:8; na
- Kiswahili 1:4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ichukue hatua ya dharura na ya makusudi kabisa ili vitabu vipatikane ili wanafunzi waweze kunufaika na elimu inayotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti ya elimu wahusika wangeangalia sana shule za Korogwe Vijijini ambapo Mheshimiwa Naibu Waziri ameshazunguka na kuona matatizo yake Jimboni kwangu. Naomba walimu wa shule wa kutosha kwenye Wilaya ambazo hazina walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ina changamoto nyingi, ila tunaomba kuna shule ambazo hata uwezo wa kununua vitabu ni shida, tunaomba msaada wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MATHIAS M. CHIKAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote nitamke kuwa naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika nyanja ya ubora wa elimu hapa nchini kwetu. Kwa sasa Serikali yetu imeweza kujenga shule nyingi za Kata nchi nzima. Tatizo lililopo sasa ni kuwa shule hizi zinatoa elimu kwa vijana hawa, elimu ambayo haina ubora mzuri. Ili kuongeza ubora wa elimu katika shule zetu ni vizuri tukaanzia kwa Walimu. Tuwape Walimu wanaofaulisha motisha ya fedha ili waendelee kuongeza juhudi za kufundisha Kimataifa mpango huu unaitwa *CODE - cash on delivery*. Kwa kila wanafunzi

wanaofanya vizuri Walimu husika walipwe kiasi cha fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, naomba kuunga mkono hoja na kusisitiza tu umuhimu wa kuwamotisha Walimu ili waweze kuzingatia utoaji wa elimu bora kwa kuwalipa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Mzumbe kuna watumishi walitumwa Dar es Salaam kununua mabasi mawili kwa ajili ya usafiri wa wanachuo na watumishi. Walitumwa wakanunue magari mapya. Magari mawili hayo yalipoletwa chuoni yakagundulika kuwa ni machakavu yaani yametumika. Kwa hiyo, fedha za kununua magari mapya imenunua yaliyotumika! Magari hayo yapo tu hayafanyi kazi ni mwezi wa nne sasa. Namwomba Mheshimiwa Waziri aeleze hawa watumishi wamefanywa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Walimu kinakusanya fedha nyingi sana kupitia makato kwa mishahara ya Walimu mpaka chama hicho kinawekeza fedha hizo kwenye miradi kama jengo la Mwalimu Nyerere. Lakini fedha inayokwenda Mikoani na Wilayani kwa kazi za Vyama vya Walimu huko ni kidogo sana. Nadhani ingekuwa vizuri kama fedha hizi zingetumika kuanzisha *SACCOS* Wilayani ili kuwapunguzia makali ya maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Chunya ni pana sana kieneo na Walimu hupatia mishahara yao kupitia benki ambazo zipo mjini Chunya. Sasa Mwalimu anatoka Namkumwe au Udinda au Kambikatoto au Lualaje kwenda Chunya ambapo ni kilomita zaidi ya mia moja. Fedha nyingi anapoteza kwa nauli au malazi pale Chunya. Serikali ina mpango gani kuwasaidia watumishi hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wenzake hapo ofisini kwa kazi nzuri wanayoionesha kwa Watanzania ili kuendelea kujali na kutambua uwezo wa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia suala dogo tu nalo, Zanzibar na Tanzania Bara tumeungana elimu ya juu tu lakini hilo naona kikwazo kwa Wazanzibar kufaulu vizuri kwa kuingia sekondari. Kwa nini Serikali hizi mbili zisiungane kuanzia shule za msingi ili kuwa na silabasi moja kuanzia mwanzo hadi kufikia vyuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kila nchi ina msingi wake wa elimu wa kuanzia ndio unapoanza mvutano wa upande mmoja kuwa chini na upande wa pili kuwa bora. Najua kwamba, hilo ni suala la kikataiba na hivyo ilivyokuwa mchakato umeanza, ni bora mchakato wa elimu kuungana kuanzia elimu ya msingi hadi vyuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAHRA ALI HAMAD:** Mheshimiwa Waziri nakutakieni kila la kheri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. MUHAMED SEIF KHATIB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri kwa hotuba ya ufasaha na usahihi. Nampongeza pia kwa kazi nzuri sana anayoifanya pamoja na wasaidizi wake. Naomba kuchangia jambo moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kuwa hivi sasa kuna upungufu mkubwa wa Walimu wa shule ya msingi na sekondari huko Tanzania bara kwa nini Wizara ya Elimu ya SMT na ile ya SMZ wasikubaliane kuwaajiri Walimu wengi kutoka Zanzibar ambao wengi hawana ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kuwa mitaala ya elimu ya sekondari na ualimu ya bara na ya Zanzibar inafanana. Kwa hivyo, hakuna tatizo lolote la kielimu. Hata hivyo SMT na SMZ wanaweza wakawa na semina, kongamano au kozi maalum kutoka Zanzibar kwa mitaala ya SMT na hivyo kurahisisha ufundishaji, kwa nini tulalamike kwa ukosefu wa Walimu wakati wapo wengi kutoka Zanzibar!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukaguzi hafifu wa shule, Wizara ijipange vizuri kusimamia na ufuatiliaji mashuleni ili kuimarisha ufanisi wa utekelezaji na utendaji mashuleni. Bajeti itolewayo ni ndogo mno na hii imesababisha ukaguzi na usimamizi shuleni kuwa mdogo. Je, Walimu wanaotakiwa kukaguliwa na kupandishwa vyeo angalau mara tatu imekuwa vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile kuna mamlaka na Wizara zaidi ya mbili zinaohudumia Walimu na hivyo kusababisha migongano, kuingiliana na kuzorotesha huduma kwa Walimu, Serikali ina mpango gani wa kuondoa kero hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *VETA* kujengwa Wilaya ya Serengeti kwa vile idadi ya watu na hususani vijana wanaohitimu kidato cha nne hadi kuhitimu vyuo hawapati ajira hilo linaongezasana kiwango cha ujangili katika mbuga ya hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Ni vyema kujenga Chuo cha *VETA* ili kupanua ajira na kupunguza ujangili kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzisha mafunzo ya maadili *(medical ethics)* katika Vyuo vya Udaktari na afya kwa ujumla somo hili liwe mojawapo ya masomo yanayofanyiwa utahini *(examinable subject)*. Hii itasaidia sana kuimarisha taaluma ya afya na kuimarisha maadili.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kazi nzuri na muhimu ya kuelimisha jamii na vijana wetu kwa jumla. Pamoja na pongezi, naomba nichangie machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kuendana na mahitaji ya nchi, hapana shaka mahitaji ya elimu yanaendana na wakati. Kwa wakati wa sasa mahitaji ni elimu itakayomfanya mwanafunzi kujitegemea atakapomaliza masomo yake. Hii ni tofauti na elimu wakati wa ukoloni ambapo wahitimu wote waliajiriwa ofisini. Kwa hivyo, lazima mitaala sasa ibadilishwe kulingana na mahitaji ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya ufundi, Taifa letu lazima lianze kuwaandaa vijana kupitia VETA na vyuo vingine ili tuwe na Taifa la wataalam wengi wa ufundi ambao utasaidia sana maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali kwa kujenga shule nyingi za Kata. Hata hivyo, ni muhimu shule hizo ziwe na vifaa vya kufundishia na vya maabara. Ili watoto na wanafunzi waelewe wanachokisoma darasani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi za Serikali, suala la mikopo bado ni kitendawili. Mara nyingine mikopo inakwenda kwa wale wenye uwezo na wasio na uwezo wanakwama. Utaratibu mzuri ni ule utakaowafanya vijana wenye sifa wapewe mikopo na wale wasio na sifa wasipewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migomo ya Walimu na wanafunzi, migomo ni matokeo ya kutoridhika, Serikali lazima ikiri na baadaye ijisahihishe kuwa inadaiwa na Walimu haki zao. Kwa nini Serikali inadaiwa na Walimu wanyonge. Aidha, kwa nini haifuatili matatizo ya wanafunzi mpaka wanafika mahali wanagoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasemekana ubora wa elimu yetu uko chini. Ubora wa elimu unatokana na mambo mengi yakiwemo walimu bora, vifaa vya kufundishia, vitabu na majengo. Serikali isiangalie wingi wa majengo tu au wingi wa wanafunzi lakini ubora wa elimu ni muhimu sana kwa sababu tutatoa wahitimu watakaoweza kufanya kazi popote duniani na hii itakuwa ni sifa kwa nchi yetu.

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu *(Subhanah Wataala)* kwa ukarimu, neema na rehema zake nyingi anazonineemesha. *Alhamdulillah*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ni kitu muhimu sana kwa mwanadamu, vitabu vya dini vikimnukuu Mtume Muhammad *(Swalallah Alayhi Wasalaam)* vinaeleza kuwa elimu ni neema kubwa inayoshika nambari ya pili baada ya afya kwa mwanadamu. Kauli hii inapata nguvu kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Aya mwanzo ya *Qur-an* kushushwa inahimiza elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo Serikali inawajibika kuongeza nguvu katika elimu. Bajeti ya elimu iongozwe ili kukidhi haja ya sasa ya elimu.

Napongeza juhudi za Serikali kujenga shule za sekondari za Kata kwani majengo ya madarasa ndio mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi hizi ni lazima ziende sambamba na kupelekwa vifaa vya elimu katika shule hizi ikiwemo madawati vitabu na vifaa vya maabara. Pia walimu wenye weledi, utu na uzalendo wapelekwe kwenye shule hizi. Pamoja na hayo Serikali itilie maanani sana mafao ya walimu katika nyanja zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Mitihani *(NECTA)*, kwa vile elimu ni kitu bora, ni wajibu itolewe kwa ubora. Baraza la mitihani ni *challenge* au changamoto kubwa kwa ubora wa elimu nchini. Kuna wasiwasi, hofu na mashaka makubwa juu ya uaminifu wa Baraza la Mitihani. Inakuwaje mwanafunzi anafaulu darasa la saba na asijue kusoma na kuandika!

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuwaje mwanafunzi anafaulu kwa daraja la kwanza kidato cha sita na asiweze kumsaidia hata *homeworks* nduguye wa kidato cha pili au cha tatu *(form II* na *form III)* kwa masomo yale yale ambayo yeye amefaulu kwa *division one*? Hapa inaonekana wazi kuwa Baraza la Mitihani kuna biashara binafsi ya watendaji wake kuiba mitihani na kuiuza! Serikali iwe macho na hili ili kuepuka Taifa kuwa na wasomi vihiyo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani kubwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Kikwete na Mheshimiwa Waziri wa Elimu Shukuru Kawambwa na Naibu Waziri

wake Philip Mulugo kwa uwezo na uzalendo wao. Nawashauri sana sana walipangue na kulisuka upya Baraza la Mitihani kabla hali haijakuwa mbaya zaidi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Ukaguzi wa shule ili ufanisi upatikane, ni lazima kila jambo likaguliwe. Idara hii imekufa! Haionekani kabisa ni vipi inawajibika. Shule nyingi nchini za msingi na sekondari za Serikali na za binafsi hazikaguliwi! Walimu wanafika shule na kuwaambia wanafunzi watoe vitabu vya kusomea *(text books)* na kuwaacha wajisomee na kuandika kazi zao peke yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu anaondoka kwenda kufanya shughuli zake nyingine. Kwa kuwa anaporudi anamletea Mwalimu Mkuu chai, basi naye Mwalimu Mkuu anashindwa kufanya wajibu wake na hapo ndio uozo unaendelea!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ada za shule *(school fees)*, hili ni tatizo sugu hasa kwa shule za binafsi, shule hizi pamoja na kujitahidi kuziba pengo la upungufu wa shule ada zao ni kubwa sana. Baadhi ya shule za kutwa zinatoza mpaka 2,000,000/= kwa mwaka kwa *O level* na 3,500,000/= kwa *A. level*! Hii ni hatari. Je, shule hizi ni kwa ajili ya kuwasomesha watoto wa nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilitoa hoja hii na Serikali ilisema itaunda tume kuangalia jambo hili na tathimini ingeletwa Bungeni katika mkutano wa saba. Jambo la kusikitisha hata katika hata katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya mwaka huu hakuligusia!

Nahitaji Mheshimiwa Waziri anipe majibu juu ya kadhia hii. Ni lini ada zitakuwa na *regulatory board*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naomba kuwasilisha.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupongeza Wizara hii inajitahidi pamoja na mapungufu yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri Serikali iweke hamasa kwa sekta binafsi, wajenge nyumba za kukodisha kwa Walimu, maeneo mengi nchini yana udongo wa kufaa kutengeneza matofali ya kuchoma. Inawezekana kabisa Halmashauri za Wilaya na Vijiji zikagawa maeneo yao kwa watu *private* ili wajenge nyumba za kukodisha kwa Walimu *around the Ward schools*. Hii ni dhana ya *diversification* ya biashara kwa mkulima, mfugaji na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mjenzi ata-*charge* kodi ya pango ya bei nafuu, mfano, akijenga vyumba sita vya *unit* ya *room* mbili kila moja anaweza ku-*charge* 15,000 kwa mwezi kwa kila *unit*. Mwisho wa mwezi anapata 90,000, akijenga *more units* anapata pato zaidi *its a matter of advocacy,* hawajui kama wanaweza kufanya *business* ya *real estate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natilia mkazo Idara ya Ukaguzi, Walimu wengi wanakwepa vipindi kwa sababu nyingi za kweli, nyingine uzembe na *non-commitement*, nashauri Serikali ifuatilie *intensively*

ukaguzi. Serikali iwezeshe idara hata kama kwa pikipiki, idara hii ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimba za watoto wa shule za msingi na sekondari zinatokea mara nyingi ni wazazi kutokufanya kazi yao ya malezi, lazima yaanzie nyumbani. Serikali iwape maelekezo Walimu Wakuu wayaseme haya katika mikutano ya wazazi shuleni, watoto hawa wasirudi watafutiwe MEMKWA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wanaosomeshwa na Serikali wasaini *Bond* kuwa hawataondoka katika shule aliyekuwepo kuingia kazi nyingine au *private school.* Bila kufundisha kwa miaka mitatu baada ya kuhitimu kutoka Chuo.

Mheshimiwa Spika, mitihani ya *multiple choice* sio mizuri kabisa. Tunahitaji kuwapa *chance* wanafunzi kutumia akili zao kwa kufikiria mfano, hesabu, mwanafunzi wa sekondari pengine atajaribu ku-*compute* kupata jibu. Mwanafunzi wa shule ya msingi atacheza bahati nasibu atabuni, nashauri Serikali ibadili mtindo huu, inawezekana sehemu ndogo tu ikawa *multiple choice.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe maelekezo kuwa sekondari wanafunzi wafanye *quiz* ngapi na *test* ngapi kwa mwaka. Taarifa kutoka kwa wazazi wa watoto wa sekondari ya Iringa wanasema kwa mwaka mmoja shule hii wanafunzi hawapewi *test* hata moja. Nashauri wanafunzi wafanyishwe *test* nyingi mara moja kwa kila wiki mbili au wiki nne. Hii itawafanya wanafunzi wawe *more prepared*. Hata hivyo,

wanahitaji *course work, so its important* wafanyishwe *tests.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule nyingi za Kata hazina Bodi za Shule, inawezekana masharti ni magumu, lakini nashauri Serikali pengine iweke *category* ya *Board Members* vizuri zaidi. Mfano, Wachungaji wa maeneo, wafanyakazi wa kampuni za uwekezaji, Imam wa maeneo au Shehe, yeyote ambaye ana uelewa katika eneo ili asaidie kufanya maamuzi katika shule hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya China inasema Serikali ya Tanzania ikifadhili wanafunzi 100 kusoma China katika kila sekta na wao watafadhili wanafunzi wengine 100. Nashauri *Higher Education Board* walione hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Mitihani linafanya vizuri. Nashauri waendelee kuwa *strict* kwa wafanyakazi wenzao watakokuwa wanashawishika kuuza mitihani, udhibiti *so far* ni mzuri, *please keep it up*!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kidato cha pili kurudishwa kufanya mitihani, ni njia mojawapo ya kumpima mwanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali itoe maelekezo kwa wakuu wa shule na idara za elimu zielekeze shule za sekondari na za msingi kutafuta *partnerships* na shule za nje ya nchi. Hii itasaidia ku-*exchange knowledge* na *skills*. Ziko shule za msingi na sekondari Ulaya wanafunzi wanaweza kujenga,

kupaka rangi nyumba na madarasa, zahanati na kadhalika. *Exchange* ya lugha pia ni wazo zuri, tuwape *chance* wanafunzi ku-*explore* mambo yaliyopo duniani, sio *facebook* na *blogs* tu lakini kuwa na *pen pals* kunasaidia huyu mtoto wa Kitanzania kujua *how to draft a letter to a friend learning how to reply in English et cetera*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Serikali kurudisha michezo mashuleni, kuna haja Walimu *qualified* wa michezo *example, basket ball, football, netball, cricket* kutupa *dise, javeline et cetera* wapelekwe mashuleni. *Talents* kama za Thabit anayecheza *basketball* zinaweza kupatikana pia kwa vijana wengine warefu. *Olyimpic games* zilizomalizika jana, vijana wa kuleta ushindi wanaweza toka maeneo kama Manyara, Arusha (Masaini) na kadhalika. Serikali isiendelee kushabikia kina Simba na Yanga, ziko *talents* huko vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuendelea kupandisha *points* za wanafunzi wa kusomea ualimu (kutoka *points* 32- 27) na baadaye 26 mpaka 24. Ni hatua nzuri kuhakikisha huyu anayetarajiwa kuwa Mwalimu na yeye ana kiwango kizuri cha ufaulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ipitie upya malalamiko ya walimu kama ni staili zao walipwe, kuendelea kulalamika kutaliweka Taifa hili mahali pagumu na hususan Chama Tawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Waziri na Naibu Waziri wa Elimu kwa jinsi ambavyo wanajituma katika kuiongoza Wizara. Naomba kwa dhati kabisa tatizo la migomo ya Walimu ya mara kwa mara litafutiwe majibu kwa sababu lina athari kubwa kwa ustawi wa elimu hapa nchini. Tujaribu kuangalia motisha iliyokuwa inatolewa hapo siku za nyuma irudishwe hasa maeneo ya mazingira magumu na hasa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa elimu unatakiwa kuangaliwa upya. Mfumo tulio nao hauruhusu muhitimu kujiajiri anapohitimu masomo yake. Nashauri kuanzia shule za msingi yafundishwe masomo ya ziada kwa ajili ya kuwawezesha kujiajiri mfano wa masomo hayo ni uhasibu, ufundi uashi, useremala, kilimo na kadhalika. Masomo haya yakifundishwa kwa vitendo vijana wetu watakuwa na uwezo wa kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ina tatizo kubwa sana la ajira njia mojawapo ambayo ingesaidia kupunguza tatizo hilo ni kufundisha masono ya ufundi kuanzia shule za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Wizara ya Elimu kwa kuona umuhimu wa kuimarisha elimu ya sekondari hasa kwa kidato cha tano na sita, Wilaya ya Mbarali ina *high school* moja tu ambayo ipo Kata ya Madibira. Tunatarajia kuanzisha shule ya sekondari *high school* ya Rujewa, shule ambayo ni ya muda mrefu sana, ni shule ya kwanza ya sekondari Wilayani Mbarali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shule hii ya Rujewa sekondari ambayo tunataka ifunguliwe mwaka huu. Madarasa yapo, hosteli kwa ajili ya wasichana ipo. tumwekwama mahitaji madogo madogo kama madawati, umeme, vifaa na Walimu. Naomba sana ushirikiano wa Wizara ili shule hii iweze kufunguliwa. Jitihada bado zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za Kata zina tatizo kubwa sana la upungufu wa Walimu na hasa Wilaya ya Mbarali. Tatizo lingine ni shule za Kata kukosa umeme, tatizo hili ni kubwa. Nashauri shule zote zipewe umeme wa *solar*. Umeme wa *solar* utawezesha shule hizi kujifunza masomo ya sayansi.

**MHE. DKT. ABDULLA JUMA ABDULLA SAADALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Wizara kwa ujumla kwa kazi nzuri wanayofanya, kwa kweli ni wapiganaji *front liners* hongereni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Chuo Huria kuna haja ya Serikali kuwapangia kozi za kutoa kulingana na vipaumbele vya nchi, kilimo na uvuvi, miundombinu, afya mawasiliano, *emergency* na elimu. Nasema hivi kwa sababu ukiangalia kozi wanazosomesha na wahitimu wake wanaishia ofisini tu *non goes to the field,* kwa hivyo wanachezesha kalamu tu. Ombi, wafungue kozi zenye kipaumbele cha nchi sio *public relation, business administration* na kadhalika yaani wote ni ma-*clerk*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili wale vijana wanaomaliza kama mafundi mchundo na fundi stadi kutoka *VETA* na wa ngazi za daraja la chini nashauri hawa wafanyiwe *satellite course* ambazo zitawezesha hawa kupanda daraja na pengine mpaka kufikia *diploma* na *degree*. Wasibaki tu kama mafundi wasio na mbele wala nyuma tena hawa wengi wao huwa wabunifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *branding* na kuendeleza vipaji na ugunduzi, nashukuru jitihada za Wizara na msisitizo uelekezwe kwenye kuendeleza vipaji. Ili tupate ujuzi na *brand* ya teknolojia hizo. Tunaziona kwenye maonyesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja hii kwa masikitiko makubwa sana kwa Serikali kushindwa kumaliza mgogoro wake na Walimu na kusababisha migomo. Nashauri Serikali yangu ichukue tahadhari kubwa na madhara yatakayowakumba wanafunzi wetu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuulizia ni kwa nini wanafunzi wengi toka Jimbo la Nyanghwale wametuma maombi ya kujiunga na vyuo mbalimbali nchini kutochaguliwa pamoja na *point* nzuri ya 27-28?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mimi Mbunge wao kuleta maombi Wizarani? Naomba ufafanuzi ili wananchi wa Jimboni kwangu wajue ya kuwa Mbunge

wao nimeyafikisha maombi yao Wizarani. Pia naishauri Serikali ijenge Chuo cha *VETA,* Mkoa mpya wa Geita ili vijana wetu tuwasaidie mafunzo mbalimbali ili waweze kujiajiri na kuajiriwa ili kupunguza wimbi kubwa la vijana kuwa wazururaji na wavuta bangi na madawa ya kulevya mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba Wizara hii kuichunguza vizuri Baraza la Mitihani kuna dhuluma kubwa inafanywa kuwadhulumu wanafunzi wa Kiislam kuwafelisha kwa makusudi na kuwadhoofisha kiakili na kimaendeleo yao ya kimaisha. Ushahidi mwingi upo toka baadhi ya *Islamic secondary* kwa hujuma zilizofanyiwa huko nyuma na hivi karibuni kwa matokeo ya mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naiomba Serikali iangalie upungufu mwingi ulioko mashuleni Jimboni kwangu kama madawati, vitabu, hostelui, nyumba za Walimu, madarasa, ukweli upungufu ni mkubwa sana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutamka kuwa, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Manispaa yangu kuna Chuo cha Elimu kwa ajili ya kozi za ualimu lakini hali ya majengo kwa kweli hairidhishi. Naomba Wizara ikumbuke chuo hiki cha Walimu kilichopo Tabora Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tabora ina Kata 24, kati ya hizo Kata 14 inazo vijijini ambavyo vina upungufu mkubwa wa Walimu hasa katika shule za msingi ambazo zipo vijijini. Naomba kutoa ushauri, nilipotembelea Kata hizi waliniomba hawa vijana waliohitimu vizuri darasa la 12 na 14 ambao wako tayari kwenda kwenye kozi za ualimu ili waweze kurudi katika vijiji vyao. Je, kama inawezekana naomba utaratibu katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tuna matatizo ya Walimu wa sayansi na hesabu, tunaomba mtufikirie. Hata hivyo, sina budi kushukuru kwa Walimu ambao tumewapata kwa ajili ya sekondari, lakini kulikuwa na tatizo la mishahara yao kwani mnapowatuma hakikisheni mnatayarisha fedha zao za mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Kitengo cha Ukaguzi na mtaala mpya wa elimu, bajeti inayotengwa kwenye kitengo hiki mwaka hadi mwaka hairidhirishi na ni ndogo sana isiyotosha kufikia hata moja y a kumi ya ukaguzi katika shule zote za Serikali nchini (kuanzia *primary schools*). Pamoja na kutambua kwamba Wizara imeachana na mtaala wa zamani wa kufundishia wa *content based* uliokuwa unaangalia *theory* zaidi na kuanza kufundisha kwa mtaala mpya

wa *competent based,* je, ni kwa kiasi gani Wizara imejiandaa hasa katika kuwandaa Walimu kufundisha kwa mtaala huu mpya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu fika kwamba, mtaala wa zamani umetumiwa na Walimu kwa zaidi ya miaka 30 na hali iliyopo kwa sasa ni Walimu kukosa mafunzo thabiti ya kukabiliana na huu mtaala mpya na wengi wameendelea kufundisha kwa mtaala wa zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ya Kitengo cha Ukaguzi kuendelea kutengewa bajeti ndogo, maana yake ni kwamba, shule nyingi zitaachwa bila kukaguliwa na hapa tutegemee nini katika ufundishaji hasa wa Walimu wengi ambao hawaujui ipasavyo mtaala mpya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali inavyoendelea sasa huko mashuleni ni dhahiri kabisa Walimu wamegoma kimya kimya baada ya madai yao kutupwa. Je, bila ukaguzi tutegemee elimu bora au bora elimu? Hii si sababu ya wanafunzi kumaliza elimu ya msingi bila kujua kusoma na kuandika? Nani anawajibika katika hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, wanafunzi wanaokamatwa kwa udanganyifu wa mitihani na kufutiwa matokeo yao. Kwa miaka kadhaa tumeshuhudia wanafunzi wanaokamatwa kwa udanganyifu wa mitihani wakifutiwa matokeo yao na kupewa adhabu mbalimbali ikiwemo ya kurudia

mitihani yote baada ya muda fulani (mwaka mmoja au miwili).

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo linalojitokeza hapa ni kwamba, ni wanafunzi pekee ndio wanaopewa adhabu kubwa *on the spot* lakini wengine waliosababisha udanganyifu kama Walimu, Wasimamizi na baadhi ya watumishi wa *NECTA* wasio waaminifu huachwa mpaka uchunguzi ufanyike na wakati mwingine hakuna hatua za kisheria zinazochukuliwa na hivyo udanganyifu katika mitihani huendelea mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini uchunguzi huu wa kina haufanyiki kwa wanafunzi na badala yake tumekuwa tukipewa sababu zile zile kila mara kwamba wanafunzi hao mara waliandika majibu yaliyokosewa wote au miandiko ilifanana au majibu yamefanana na kadhalika. Swali hapa ni nani anayeruhusu uzembe huu kufanyika kama si wasimamizi wa mitihani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini hata mara moja wanafunzi hawaitwi na kuhojiwa ili kueleza ukweli wote ambao ungesaidia kuwabaini hata wale wanaochangia udanganyifu huu? Kama sheria ni msumeno ni lazima ikate kote kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwa wale wanwaofutiwa mitihani kwa masomo waliyofanya udanganyifu, mfano, kwa masomo matatu, lakini wanafutiwa masomo waliyodanganya tu? Hata huo msamaha ambao *NECTA* inatoa kwamba wanafunzi warudie, ni kwa nini wanatakiwa

kurudia masomo yote kama *private candidates* ilhali hawakuwahi kupewa matokeo yao yote ya awali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni kwa nini basi wasirudie kwa masomo yale tu waliyofutiwa mtihani? Kwa nini wafanyishwe mitihani kama *private candidate* wakati wanatumia namba zao zile zile za mitihani? Ningeshauri Wizara iliangalie jambo hili ili kulinusuru Taifa kuwa Taifa la wajinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, vyuo vikuu na usajili; pamoja na nia njema ya Serikali ya kuanzisha vyuo vikuu vingi vya Serikali na vya binafsi, lakini tatizo kubwa linalojitokeza ni upungufu mkubwa wa wahadhiri na hata watumishi wengine katika vyuo hivi. Imegundulika kwamba katika vyuo vingi vya binafsi wahadhiri ambao sio *qualified* wamekuwa wakifundisha katika ngazi ya shahada. Mfano, *tutorial assistance (TA)* ambao wamemaliza shahada moja wanapewa vipindi vya kufundisha wenzao hao hao wanaofanya shahada ya kwanza!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa vipi mtu mwenye kiwango kile kile cha elimu akamfundisha mwenzake wanaosomea *level* ile ile aliyonayo yeye? Ni kwanini hawa *TAs* wasipewe kazi ya kusimamia semina kama ambavyo linafanyika katika vyuo vikuu vya Serikali? Wizara inajua kwamba Chuo Kikuu cha *Saint* John hakina Wahadhiri wa kutosha na kinatumia *TAs* kufundisha masomo au kozi mbalimbali? Naomba Wizara ifanye uchunguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, elimu na Soko la Ajira la Pamoja la Afrika Mashariki; kama nchi ni lazima ijipange vizuri kutengeneza ajira kwa watu wake. Ajira inatengenezwa kuanzia kwenye utoaji wa elimu bora kuanzia shule za awali mpaka vyuo vikuu. Je, ni kweli elimu yetu ya Tanzania ya sasa inatosheleza? Ni kwa namna gani wanafunzi wanaomaliza shule bila kujua kusoma kuhesabu na kuandika? Wanaweza kushindana kwenye soko la pamoja la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewaandaa vipi vijana wetu kushindana na wenzao wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ni kwa vipi wanafunzi wanaomba mikopo elimu ya juu kupewa kwa makundi na kwa kufuata vigezo vya kusomea ualimu na ualimu wa masomo ya sayansi pamoja na kozi zinazohusiana na masomo ya sayansi pekee wanaweza kushindana kwenye soko la ajira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni kweli kwamba Tanzania hii tumekuwa na Wahasibu, Wanasheria, Wanauchumi Watawala na hata wasanii wenye utaalam na watu wa lugha wa kutosha? Fani hizo kama si kipaumbele cha nchi hii nani atachukua nafasi hizi katika soko la ajira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nchi tunatakiwa tusomeshe wanafunzi wote bila kubagua fani wanazotaka bila ubaguzi na wote wenye sifa wapewe mkopo au *scholarships* ili wapate kusoma na kuziba nafasi mbalimbali wanaposhindana na wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MUSSA Z. AZZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na matatizo mengi ya mikopo ya elimu ya juu, Serikali inalemewa sana. Serikali ya China imetoa ofa ya nusu kwa nusu, mfano, Serikali ikiwalipia wanafunzi mia moja Serikali ya China itatoa *scholarship* ya wanafunzi mia moja, je, mtapokea ushauri huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote kwa hotuba nzuri vile vile niwapongeze kwa kazi nzuri mnayoifanya katika kuendeleza, kusimamia na kuboresha elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko naleta kilio cha Walimu nchini. Walimu ni kada ya watumishi wa nchi hii ambao wanachezewa. Inakuwaje Serikali imewafanya Walimu wawe watu wa kulalamika? Siku hizi ofisi zote zina *computer,* sasa inakuwaje:-

(i) Mwalimu anaajiriwa anamaliza miezi hata miaka kadhaa bila kulipwa stahili yake (mshahara) huyu anaishije?

(ii) Walimu wapandishwe madaraja lakini wasilipwe mshahara unaoendana na madaraja hayo.

(iii) Inakuwaje Walimu hawalipwi stahili zao za likizo uhamisho matibabu na kadhalika hadi wagome? Je, hii haina maana kuwa Serikali ndio wanasababisha migomo ya Walimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wote wanafanya kazi katika mazingira magumu kwani wanatakiwa kufundisha mchana na usiku wanatakiwa kufanya maandalizi na kusahihisha kazi za wanafunzi. Mwalimu mzuri hufanya kazi zaidi ya saa kumi na mbili kwa siku. Hivyo, wote wanastahili kufikiriwa kulipwa posho ya mazingira magumu. Napendekeza kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mishahara ya Walimu iangaliwe upya kwani hali ya maisha imepanda sana, hivyo iboreshwe. Serikali itenge fedha za kutosha kulipia madai yote ya walimu na kuweka utaratibu thabiti wa kuhakikisha malimbikizio haya hayatokei tena. Hii itaepusha migomo isiyo ya lazima. Walimu walipwe posho ya mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Idara ya Ukaguzi wa shule ambayo kazi yake mojawapo ni kusimamia na kuhakikisha kuwa kanuni na viwango vya elimu vilivyowekwa vinatekelezwa, inakuwaje tunawapata wanafunzi wanaomaliza darasa la saba, lakini hawajui kusoma na kuandika? Serikali ina mpango gani wa kuondoa aibu hizi? Pili, ni lini idara itawezeshwa ikapewa fedha na magari ili waweze kutimiza majukumu yao ya ukaguzi itakiwavyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri

wanayoifanya. Pamoja na pongezi hizo ninayo machache ya kuishauri Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera unahitaji Chuo cha *VETA* kwa ajili ya vijana wa Mkoa huo. Ni muda mrefu sasa tumeomba Chuo hiki, lakini Serikali imeendelea kutoa maelezo yale yale kuwa wameanza na baadhi ya Mikoa. Sina tatizo na hilo, lakini Mkoa wetu wa Kagera uliopo pembezoni unastahili kuangaliwa kwa jicho la huruma kutokana na jiografia yake na matatizo ya wakimbizi na vita vya Kagera iliyoudumaza Mkoa wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali isikie kilio chetu katika mwaka wa bajeti wa fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu katika shule za sekondari na misingi ni tatizo kubwa sana. Naipongeza Serikali kwa juhudi waliyoonesha mwaka jana kwa kuajiri Walimu wa sekondari na msingi. Hata hivyo, bado walimu hawatoshi hata kidogo hasa katika sekondari za Kata. Ni vema Serikali ikaongeza idadi ya Walimu na ijitahidi kugawa Walimu wa sayansi angalau kwa kila sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maabara ni muhimu sana kwa masomo ya sayansi hasa maabara ya fizikia, kemia na baolojia, majengo ni muhimu, walimu na vifaa vya maabara. Pia vitabu vya sayansi ni muhimu katika suala zima la ufundishaji wa sayansi, hivyo ni muhimu vitabu vipatikane. Shule za sekondari za kidato cha tano na sita *(form five na form six)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wetu wanaomaliza kidato cha nne hasa shule za Kata wanashindwa kuendelea kutokana na uhaba wa shule za kidato cha tano na sita. Naishauri Serikali ije na mkakati mzuri wa kujenga angalau kwa kuanzia shule moja ya kidato cha tano na sita kwa kila Kata mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la nyumba za walimu bado linasumbua nchi yetu. Ni mkakati gani Serikali imeuandaa kumaliza tatizo hili katika mwaka huu wa fedha 2012/2013?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabweni kwa ajili ya wanafunzi wetu hasa wa shule za Kata ni muhimu. Sababu ziko wazi kwa nini mabweni yanahitajika, mojawapo ni sababu za kuzuia ongezeko la mimba kwa watoto wetu wa kike, lakini pia kuwapunguzia watoto wetu wote adha ya kutembea umbali mrefu na hivyo kuwakosesha muda wa kutosha kujisomea watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sasa tatizo la malimbikizo ya madeni ya Walimu yamekuwa yakisumbua Taifa letu. Naishauri Serikali ijitahidi sana kumaliza tatizo hili na kujitahidi kutozalisha madeni mapya. Pia lipo tatizo la kuchelewesha mishahara ya Walimu wapya hadi miezi sita bila ya baadhi ya Walimu wapya kulipwa. Hili ni tatizo na kero kubwa sana kwa Walimu wetu wapya na inawakatisha tamaa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa hongera Mheshimiwa Waziri, hotuba imeandaliwa na kuwasilishwa kwa ustadi na kitaalam. Hotuba kwa mfano, imerejea Ilani ya Uchaguzi kupima mafaniko ya utekelezaji na kuibua changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano *(The FYDPI* 2011/2012 – 2015/2016, ni vema siku zijazo taarifa ikaainisha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya sekta nchini iliyoelezwa katika ukurasa wa 15 wa hotuba ya bajeti, mafanikio hayataji mafunzo ya ufundi sanifu *(NACTE)* kwamba tumefanikiwa kiasi gani? Ufundi stadi *(VETA)* umeainishwa vizuri. Changamoto nazo hazizungumzii ukosefu wa fedha katika ngazi ya kati ya mafunzo ya ufundi, badala yake elimu ya juu imetajwa kuhitaji vyanzo mbadala wa fedha, ikumbukwe kuwa vyuo vikuu walipewa 4% ya *SDL* katika bajeti ya mwaka uliopita (*page* 18 (d)).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu majukumu ya *NACTE,* kama yalivyoainishwa katika ukurasa 96 na majukumu ya Chuo cha Ufundi, Arusha, yaliyoainishwa katika ukurasa 109, hawawezi kutekeleza hayo kwa ubora bila fedha na taasisi ni ukombozi kwa Taifa (Kada ya kati ufundi sanifu).

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa kuboresha *skills* katika Taifa kwa ujumla, ukurasa 33 *quote partly*): *"….. the estimated gap in highly-skilled workers required for Tanzania to realize the MIC status is enormous*." Tunahitaji bidii zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa kuboresha *skills* katika kada ya ufundi ngazi ya kati, ukurasa 34 wa Mpango wa Maendeleo, inakadiriwa kuwa ili kutimiza lengo la idadi ya wahitimu wa *VETA* kufikia 2015 kuwa 635,000, Tanzania *MIC*, Taifa linahitaji kwa uwiano wa *ILO* wa 1:5:25 (ngazi ya juu (*TCU),* kati *(NACTE)* na chini (VETA)). *By* 2015 utahitaji angalau mafundi sanifu 127,000 wafanyao kazi hawawezi kupatikana bila fedha, *we need to invest*. Hivyo kama *budget speech* ilivyosema kuhusu vyuo vikuu, iwekwe pia kwa vyuo vya ufundi vya kati, kupata vyanzo mbadala vya kugharamia elimu ya juu na ufundi kati.

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza juhudi kubwa na nzuri zinazofanywa na Wizara katika kuendesha na kuboresha sekta ya Elimu na Ufundi nchini. Hongera Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Makamishina, Wakurugenzi na Watumishi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Magu ikijumuisha Wilaya mpya ya Busega ilianzishwa mwaka 1972, miaka 40 iliyopita haina Chuo cha Ualimu, *High School* na Chuo cha *VETA*. Je, Wizara itatusaidiaje wana Magu na sasa Busega pia kupata Chuo cha

Ualimu na *High schools* tutumie utaratibu upi ili ombi hili liweze kufanikiwa haraka inavyowezekana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Magu lina sekondari takribani 20 ambazo zote (isipokuwa mbili au tatu) hazina maabara. Wizara ina mkakati gani wa kushirikiana na wanachi ili kuondoa kero hii inayosababisha wanafunzi wengi kutofanya vizuri katika mitihani hasa ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majengo mengi sana ya shule za msingi katika Jimbo la Magu yana hali mbaya sana ya kukosa sakafu. Ukizingatia kuwa shule nyingi sana pia hazina madawati. Je, Wizara ina mpango mkakati gani wa kuondoa kero hii kubwa kwa kuweka sakafu, kupata madawati ya kutosha ili kuwezesha watoto wetu kusoma vizuri na kuondoa kero ya kukaa chini kwenye vumbi? Jimbo la Magu lina mgao gani kwenye chenji ya rada?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Wizara isianzishwe utaratibu wa kuwapeleka vyuo vya *VETA* nchini kwa *crash programme (say* ya mwezi mmoja au miwili) Watanzania wenye ujuzi wa stadi moja au nyingine ambao wameupata kwa utendaji kazi wao wa miaka mingi) ili ujuzi wao ufanyiwe tathmini *(evaluation)* ili ukikidhi wapewe vyeti vinavyoendana na ujuzi wao? Hili nilijifunza, linafanyika katika nchi ya Trinidad and Tobago niliko kwenda mapema mwaka huu kwenye ziara ya mafunzo. Naomba Wizara ilione hili na ilifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Watanzania wengi wanaoaminika kugushi ama kudai kupata vyeti hasa za digrii za juu *masters* na *Phd*. Baadhi yao walishatajwa kwa maandiko na ushahidi ulidaiwa kuwepo. Je, Wizara (Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania) imefikia wapi katika kulifuatilia suala hili, ni lini itatoa tamko rasmi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ikaze buti, isonge mbele bila woga. Iangalie pia njia bora ya kumaliza mgogoro na Walimu *once and for all* ikiwezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. GREGORY G. TEU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya mpaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kwa haya yafuatayo:-

Kwanza, je ukarabati wa nyumba za walimu na baadhi ya majengo ya Chuo cha Ualimu, Mpwapwa pamoja na shule ya sekondari Mpwapwa utaanza lini kwa kuzingatia uchakavu wa nyumba na majengo haya tangu ukoloni, tusipoziba ufa tutajenga ukuta. Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii ibaini uchakavu wa nyumba na majengo ya maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sura ya nyumba na majengo haya ni nzuri sana, kinachokosekana hapa ni ukarabati ambao haujafanyika kwa muda mrefu, hivyo kuonekana yamechakaa sana. Iwapo ukarabati huu utafanyika sura ya nyumba na majengo haya itarudi na kuleta sura na mandhali ya kuvutia kuliko ilivyo sasa. Makisio ya ukarabati wa nyumba za Walimu wa Chuo cha Ualimu Mpwapwa yalishaletwwa Wizarani na Mkuu wa Chuo.

Pili, Serikali iangalie uwezekano wa idara na kitengo cha elimu kilichoko chini ya TAMISEMI kurejeshwa Wizarani ili kuepusha mwingiliano uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Waziri na Naibu Wazirri pamoja na maofisa wote wanaowasaidia. Naomba kutamka kuwa naunga mkono bajeti hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango cha elimu kinachotolewa na vyuo vikuu vilivyoanzishwa hivi karibuni, ni cha chini sana kutokana na sababu zifuatazo:-

(1) Wanafunzi wanaomaliza shahada ya kwanza katika vyuo hivyo ndio wanaotumiwa kusomesha Walimu hawa, hawana ujuzi na uzoefu wa kutosha wa kusomesha. Matokeo yake ni kuwa wanafunzi wanapewa maswali, mapenzi baina ya Walimu hao na

wanafunzi. Mitaala haitekelezwi inavyotakiwa na mengine mengi;

(2) Vyuo hivi havina miundo mbinu ya kutosha kama madarasa ya kufundishia, vyoo na mazingira mengine ya kufundishia.

(3) Hakuna *external examiners*. Hii inasababisha mitihani kutungwa chini ya kiwango. Vile vile kwa sababu *syllabus* haifundishwi yote, basi mtihani hutolewa kwa ile sehemu tu iliyofundishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni baadhi tu ya hali halisi ilivyo katika vyuo hivi. Je, Serikali haiyajui haya? Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania inakagua vyuo hivi hawajapata malalamiko haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu hutoa mikopo kwa kujuana. Wengi wa wanafunzi wanaocheleweshewa mikopo ni wale waliokuwa hawana wakubwa wa kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake ni kuwa wanafunzi hawa hucheleweshewa kupata mikopo. Wanapopeleka malalamiko Bodi hii haichukui hatua yoyote. Naiomba Bodi hii itoe mikopo kwa uadilifu ili kupunguza malalamiko ya wanafunzi na migomo.

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa hotuba nzuri ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba utaratibu uliopo hivi sasa wa kuhudumia masuala yote ya Walimu

uangaliwe tena kwa kina kwa sababu huu ndio wenye urasimu mkubwa na pia kusababisha malalamiko mengi ya Walimu na kucheleweshwa kwa haki zao na kupelekea Walimu kutoa maamuzi magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Idara ya Ukaguzi iboreshwe na kupewa uwezo zaidi kifedha na nyenzo ili ifanye kazi zake kikamilifu bila kusuasua hasa ukizingatia shule zimeongezeka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango gani mahsusi wa kuwasaidia watoto wa kike waliopata ujauzito wakiwa shuleni kuendelea na masomo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa sera ya elimu mpya ishirikishe wadau wengi ili iungwe mkono na wengi. Pia tatizo la wanafunzi wasiojua kusoma na kuandika kujiunga na elimu ya sekondari litafutiwe ufumbuzi wa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nachukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa utendaji wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili la Wizara ni mhimili mkubwa sana kwa mustakabali wa Taifa letu. Tunatakiwa kuliangalia eneo hili hasa macho mawili. Naomba Mheshimiwa Waziri anijibu maswali yangu yafuatayo:-

Naomba Serikali itueleze imejipanga vipi kulipa malimbikizo ya madai mbalimbali ya Walimu na ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua Serikali imejipanga vipi kuboresha maslahi ya Walimu katika maeneo ya mishahara, usafiri, posho ya mazingira magumu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua lini Serikali itahakikisha zinapatikana nyumba za kutosha kwa ajili ya makazi ya Walimu na hasa vijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua Serikali imejipanga vipi katika kuhakikisha Walimu wanapata nafasi ya kujiendeleza pindi inapohitajika kufanya hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua lini Serikali itapunguza *(gap)* upungufu wa Walimu, imejipanga vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua lini Serikali itatujengea Vyuo vya Ufundi vya *VETA* katika kila Wilaya na hasa Wilaya yetu ya Mufindi na Jimbo la Mufindi Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lini Serikali itaboresha vitendea kazi ili kazi ya kufundisha kwa Walimu iwe nyepesi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Serikali ikaangalia upya bajeti ya Wizara hii ya Elimu kwa kuiongeza fedha, bila elimu nchi haiwezi kwenda na iwe Wizara ya kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukaguzi wa shule ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni, usemi huu umebeba hekima na busara katika kulinda na kuzingatia haki ya mwajibikaji pale ambapo inadharauliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waswahili wanasema usimdharau Mkunga wakati uzazi ungalipo, hivyo basi, tusiwadharau Walimu wakati bado Taifa hili lina mahitaji makubwa ya Walimu ili waweze kuwasomesha vijana na watoto wetu ambao ndio tegemeo la baadaye katika kuja kuliendeleza na kulinusuru Taifa hili na vijana wasio na elimu na ambao Taifa hili litakuwa linawategemea.

Mheshimiwa Spika, katika nchi yoyote duniani watu huwekeza katika elimu. Hapa kila mmoja wetu humu ndani anajisifia elimu aliyonayo na kwamba bila Mwalimu tusingeweza kujisifu na kujigamba na kutangaza viwango tulivyonavyo vya kielimu. Lakini Mwalimu ambaye ndiye aliyefanya kazi ngumu, ambayo leo sisi tunajisifia, kwa kweli ndiye ambaye anadharauliwa, lakini pia maslahi yao hayaangaliwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumdharau Mwalimu ni kuidharau elimu na kuidharau elimu ni kulidharau Taifa lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za wenye mahitaji maalum, watoto wenye mahitaji maalum nao sina budi tuwaangalie kwani nao ni viumbe wa Mungu na wala hawakufanya kosa wao wala wazazi wao kuzaliwa wakiwa katika hali hiyo ya ulemavu na ni vyema tukafahamu kwamba kila mmoja wetu hapa ni mlemavu mtarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pana shule moja pale Dar es Salaam inasomesha watoto wenye mahitaji maalum kama vile viziwi, mabubu, *albino* na walemavu wa viungo (mazezeta), shule hii ina eneo kubwa lakini majengo pamoja na vifaa vya kufundishia ni duni na vimechakaa sana, lakini pia ni vichache na havitoshi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa shule hizo ni ile shule ya wenye mahitaji maalum iliyopo Yombo. Shule hii inafundisha watoto elimu ya kujitegemea, mfano, kuchonga, kuchomea, *computer* katika darasa la wanafunzi 12 wanaojifunza kutumia *computer,* wana mashine moja ya ku-*print (printing machine)* na wana *computer* moja ya kizamani sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha na inahuzunisha sana kwa wale vijana na namna wanavyoonesha jitihada ya kutaka baadaye waweze kujitegemea kwa kadiri ya hali zao walizojaaliwa nazo,

lakini wamesahaulika katika suala la vifaa hivyo vya kufundishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba shule hii tuiangalie ili tuweze kuwasaidia watoto wetu hawa kwani huu ndio muda wao kujijengea msingi wa baadaye na hasa ukizingatia kwamba hawana uwezo wa kufanya kazi kama wengine wenye viungo vilivyo sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naomba kuwasilisha.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujenga sekondari katika kila Kata na Kata zingine zaidi ya sekondari mbili, tatizo ni upungufu wa Walimu pia shule za msingi nyingi hazina madawati kabisa, pia upungufu wa nyumba za Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni kuhusu walimu wanaoishi mbali na *bank* inawachukua muda wa siku nne kwenda na kurudi na pia inawagharimu pesa. Wanatumia kiasi cha sh. 50,000 mpaka 60,000 kwa safari ya kufuata mshahara. Walimu wote wanaoishi hasa mwambao mwa Ziwa Tanganyika wanafanya kazi katika mazingira magumu sana tena sana, wanastahili kuongezwa pesa kwa ajili ya nauli katika kufuata mshahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu shule binafsi, hakuna mpangilio maalum wa ada, kila shule inajipangia ada yake. Naomba Serikali isimamie kuhusu ada maana hii imekuwa biashara ya ajabu kuliko ada ya chuo kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuangalia mikopo, mikopo ya vyuo vikuu itolewe kwa watoto ambao wazazi wao kweli hawana uwezo kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wote wanaosoma katika shule binafsi haina haja kuwapatia mikopo maana wazazi wao waliweza kulipa ada kubwa tu kuliko hata hivyo ya Chuo Kikuu, sasa vipi wapewe mikopo wakati walikuwa wanalipiwa shilingi 2,000,000 hadi 3,000,000 bado nauli na kadha wa kadha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia vipi leo Tanzania kila mtu kuitwa *Doctor* wakati hana hata Diploma au *Degree* ya kwanza, wote hawa wanaitwa Madaktari feki, wachukuliwe hatua mara moja. Ni kudhalilisha waliosoma, ni aibu sana, nchi yetu haina tofauti na watoto walioingia sekondari wasiojua kusoma wala kuandika, ni mkumbo sawa na hawa vihiyo wa kujiita Madaktari feki na Maprofesa feki.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hoja hii na nampongeza sana Waziri, Naibu Waziri na Uongozi wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri na kwa uongozi mzuri wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu bora inaweza kutolewa iwe ni pamoja ya kukarabati majengo na miundombinu ya shule. Shule nyingi za Jimbo langu ni chakavu sana na zilijengwa miaka ya 1950's hadi leo hakuna ukarabati wa maana uliofanyika. Naomba Wizara isaidie kukarabati shule hizi na pia kuwapatia madawati hasa shule za Dulamu, Matowe, Usuka, Ilawega, Igodiraha, Igelehedza, Mambegu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwapatia vijana ufundi wa fani mbalimbali ili waweze kujiajiri, naiomba sana Wizara ijenge Chuo cha Ufundi *VETA* katika Wilaya mpya ya Wanging'ombe na Chuo hicho kijengwe Igwachenya ambapo ndio Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kusimamia elimu bora, naishauri Wizara iimarishe Kitengo cha Ukaguzi, uzoefu unaonesha Walimu wetu kwa kutafuta visingizio mbalimbali hawafanyi kazi yao ipasavyo. Hivyo, tukiimarisha ukaguzi tatizo hili tutalidhibiti kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za watu binafsi ni muhimu, lakini naiomba Serikali iweke usimamizi wa ku-*regulate* uendeshaji wake ikiwa ni pamoja na ada za shule hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kutunga mitihani kwa mtindo wa *multiple choice* kwa masomo yote uangaliwe upya na hasa masomo kama hisabati isewe kwa *multiple choice*. Utaratibu huo ndio umezaa

kupata wafaulu kwenda kidato cha kwanza wakati hawajui kusoma wala kuhesabu.

**MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kuchangia bajeti ya elimu kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuelezea suala la kushuka au elimu duni inayotolewa nchini. Mchango wangu hapa ni jinsi ya kupata suluhu au jinsi ya kuboresha elimu yetu. Ushauri wangu ni kuwa, tuna upungufu katika mfumo wa kiutawala (*administration structure)*. Upungufu katika eneo hili kwa kiasi kikubwa unachangia uduni wa elimu, lakini pia huduma mbovu zinazotolewa kwa wadau wa sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo kubwa katika kudhibiti na kutawala sekta ya elimu. Sekta imeshindwa kutumia fursa ilizonazo na kuleta na kutumia zile zinazojitokeza. Sekta ya elimu inayumba na ina hali mbaya lakini nieleze lililo wazi kuwa elimu ni kitovu, hivyo kuyumba kwa elimu sekta nyingine zinayumba pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano mdogo wa matokeo ya michezo ya *Olympic* ya London 2012. Tumefanya vibaya katika ushiriki, acha hiyo aibu ya kukosa medali. Tukirejea historia, sekta ya elimu ndilo lilikuwa jiko la kuandaa na kupika wanamichezo. Mifano ni mingi, sekta ya elimu ni kitovu, ina fursa bali hazijatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tena kupendekeza sehemu kubwa ya suluhisho la tatizo hili. Dawa muhimu ya tatizo hili ni sekta ya elimu kuwa chini ya Wizara moja, pendekezo ni kuwa Walimu wote wa shule zote kuanzia awali, msingi, sekondari, vyuo vya elimu, idara za ukaguzi na vyuo vikuu vyote viwe chini ya Wizara moja. Tumekosea na tumejipiga risasi miguuni kwa baadhi ya majukumu ya sekta ya elimu kuyawekea chini ya TAMISEMI, Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mahitaji ya wafanyakazi ni kuwasikiliza na kuwathamini. Kwa Walimu kuwajibika kwa mamlaka nyingi, ni dhahiri kuwa tunapunguza ufanisi unaokusudiwa. Halmashauri za Wilaya zimekuwa na upungufu katika utawala kwa kuipeleka elimu TAMISEMI, tumekopa matatizo ambayo tungeweza kuyaepuka, lakini pia mlipa mpiga zumari ndiye mchagua wimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utendaji wa ufanisi wa Walimu ikiwemo kuwapa motisha ni vigumu kutekelezwa pale ambapo Waziri mwenye dhamana ana mipaka katika kutunza au kuadhibu watendaji wa sekta. Tukirejea utaratibu wa miaka ya 1970, moja ya ufanisi ni timu za ukaguzi ambazo zilikuwa na mtiririko wa uwajibikaji toka Makao Makuu. Watendaji hawa walikuwa na mamlaka na walifanya kazi nzuri kuwa chini ya Wizara moja kulisaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo dhana ya gharama katika kuweka sekta hii peke yake, niweke wazi kuwa wale wanaofikiria suala la gharama hawatafakari madhara ya elimu duni tunayoendelea kutoa *(semi*

*cooked manpower)*. Mbali ya tofauti hiyo ya gharama ambayo kimsingi ni ndogo, napendekeza Serikali sasa ijiandae kuongeza bajeti ya elimu mara mbili katika mwaka wa 2013/2014, haina jinsi, lazima tuwekeze katika elimu kwa nguvu na kasi kubwa sana. Kipaumbele iwe elimu, elimu na elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze mpango wa kuwa na chuo cha ufundi *VETA* kwa kila Wilaya. Kwa masikitiko makubwa narejea ombi langu la kila mara. Mkoa wa Kagera hatuna Chuo cha Ufundi kwa kiwango cha Vyuo tunavyoviona katika Mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu ni kuwa, basi tujengewe chuo angalau kwa Mkoa mzima kuliko ahadi. Tupate chuo kama kile cha Chang'ombe Mikumi au kile cha Mwanza. Uwepo wa chuo kama hiki ni muhimu kutokana na hali ya kijiografia inayofanya Mkoa kuwa kando na mbali na vituo vya *VETA* vya Mwanza na kwingineko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuamua na kuongeza nguvu katika kuhamasisha masomo ya sayansi na hesabu. Vijana wetu kutokuwa na uelewa au hali ya kumudu hesabu kunaathiri maendeleo yao. Kama Taifa na hasa Taifa changa tunahitaji vijana walio wengi wenye fani za sayansi na hesabu ili kujenga kada ya watendaji adimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kuhusu elimu ya kimkakati. Nchi za Mashariki ya Mbali ambazo mara nyingi tunazitolea mifano wamekuwa na utoaji wa elimu kimalengo na kimkakati. Vijana wao

walipelekwa na wanapelekwa kwenye nchi zenye teknolojia na ujuzi wanaoutaka ili kuchuma na kuhemea kirahisi. Naishauri Serikali yangu kwa kasi kubwa kama ilivyokuwa zamani ianze kupeleka vijana wetu ughaibuni kwa udhamini wa Serikali kwa gharama nafuu, tuanze na Mataifa rafiki kama China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nisisitize haja ya Serikali kutambua na kutumia michango ya wadau mbalimbali. Maendeleo ya sekta hii yanahitaji mchango wa Watanzania wote. Muhimu hapa ni Serikali kutambua na kuthamini mchango wa kila mdau. Pia Serikali ijipange kutafuta na kutumia michango ya wananchi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze hotuba yangu kwa kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawamba; Naibu Waziri, Mheshimiwa Mulugo; Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Elimu kwa kuwasilisha bajeti yao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inazo changamoto nyingi sana ambazo zinahitaji sana busara na hekima ili kusaidia kutoshuka kwa elimu yetu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili elimu yetu iweze kuboreka, ni vyema Serikali ingeweka mkakati madhubuti wa kuboresha maslahi ya Walimu wetu kwa sababu Walimu wetu pote nchini wanafanya kazi zao

katika mazingira magumu sana, mishahara yao bado ni midogo ukilinganisha na kazi kubwa wanayoifanya, wanadai malimbikizo ya muda mrefu, hawalipwi posho, hawafanyi kazi za ziada ukilinganisha na kada nyingine kama Madaktari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule nyingi hazina nyumba za kuishi Walimu na hata zenye nyumba, majengo yao sio mazuri, hayafanyiwi ukarabati ,kwa mfano, shule ya Kalenga ina nyumba za Walimu, lakini hazikaliwi kutokana na kutokarabatiwa tu. Ni sababu gani inafanya nyumba zile zisikarabatiwe, Walimu hawana nyenzo za kufundishwa na vitabu vya kufundishia, mitaala mipya ikitolewa hakuna hata semina elekezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wengine wanacheleweshwa kupandishwa madaraja. Wengine wanapandishwa madaraja bila kupandishwa mishahara yao. Si vibaya kama Mheshimiwa Waziri wakati wa kujibu hoja angetueleza tatizo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo cha Ukaguzi wanafanya kazi zao katika wakati mgumu sana, hakuna vyombo vya usafiri, hawana vifaa vya kazi. Ningeiomba Serikali iweke mkakati madhubuti wa kuboresha kitengo hiki kwa sababu elimu inashuka kutokana na kutokuwa na ukaguzi madhubuti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali imeamua kufuta udahili wa wanafunzi wa elimu ya juu kupitia utaratibu wa *mature age entry* kwa ajili ya mwaka ujao wa masomo? Hatua hii imepunguza kwa kiasi kikubwa

udahili wa wanafunzi wa elimu ya juu na ukiangalia wanafunzi wanaochangia kwa utaratibu huu kwa asilimia kubwa hawategemei mikopo ya Serikali wanajilipia wenyewe. Wengi wa wanafunzi hawakuwa na sifa toshelezi kwenda moja kwa moja vyuoni. Hivyo, huamua kufanya kazi kwanza kusoma stashada ama shahada baadaye kufanya kazi za ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali isiwakatae watu hawa kwani uzoefu unaonesha kwamba watakaoathirika zaidi ni Walimu wa shule za msingi na sekondari wanaotaka kujiendeleza. Inaleta ugumu sana kumlazimisha mtu aliyemaliza shule miaka mitano ama kumi iliyopita kurudia kufanya mitihani ili apate sifa za moja kwa moja kuingia Chuo Kikuu. Ni vyema Mheshimiwa Waziri atueleze ni kwanini udahili huu umefutwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitaala kubadilika badilika, kwa kuwa sasa hivi kumekuwepo na tatizo kubwa la kubadilika badilika mara kwa mara kwa mitaala kiasi kwamba inawachanganya Walimu na wanafunzi na mitaala ikibadilishwa Walimu hawapewi semina elekeze ili waielewe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viboko mashuleni, nilipofanya ziara ya kutembelea baadhi ya watoto wa shule wanalalamikia hii adhabu bado haiawa wazi sana. Serikali itoe tamko kuhusiana na mwongozo huo kama adhabu hiyo ipo na ni viboko vingapi vinaruhusiwa kwa kosa gani viainishwe ili kuondoa utata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Wizara iongeze Walimu katika shule za sekondari zote Meatu, maana karibu zote zina wanafunzi kati ya watano mpaka kumi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Februari, 2011 Wizara ilikubali kutoa gari kwa ajili ya Idara ya Ukaguzi Meatu, naiomba sasa Wizara itimize ahadi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. RASHID ALI OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nachukua fursa hii ya mchango wa maandishi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwepo wangu hapa Bungeni nikiwa mzima wa afya pamoja na Wabunge wenzangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyokuwa katika mchango wangu wa kuzungumza kwa mazungumzo, nitaanza kuchangia kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya madeni ya Walimu hadi kufikia Novemba, 2011 yalikuwa yameshakusanywa yakiwa na thamani ya jumla ya sh. 7,177,043,245.16 kazi hii ilifanywa na Kamati Maalum iliyoundwa kwa kushughulikia madai ya Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai haya yaliwasilishwa Hazina, madai haya yaligawika sehemu mbili, malimbikizo ya mishahara ambayo ni kiasi cha sh. 3,723,931,264.28, yasiyo malimbikizo ya mishahara kiasi

cha sh. 3,453,111,980.88. Figa mbili hizi ndio zilifanya jawabu ya figa ya jumla ya deni 7,177,043,245.16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba, lawama zote ni lazima zielekezwe upande wa Serikali. Ni ukweli usiofichika, watu kama Walimu hali zao duni za maisha, umaskini uliokithiri, unyonge, mishahara midogo kulingana na upandaji wa gharama za maisha na Serikali haina habari nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda mrefu wa madeni bila kushughulikiwa, ni lazima uamuzi wa walimu kugoma, kuandamana au kutogoma na kuhudhuria kazini haitoshi, lazima kiwango cha elimu kishuke siku hadi siku pamoja na migogoro, itawale hadi ndani kwa kulaumiwa Walimu kumbe adui mkubwa ni Serikali kwa kutowashughulikia Walimu hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa njia ya maandishi niishauri Serikali kupitia Bunge lako Tukufu, taarifa ya Wizara imeahidi kukamilisha malipo ya madai hayo yalipwe kwa wakati. Serikali ifanye kadiri inavyowezekana japokuwa Walimu wameacha mgomo. Serikali ikae chini izungumze na Walimu juu ya kuboresha maslahi yao kwa sababu Walimu wako katika hali mbaya kimaisha. Serikali iboreshe kitengo cha ukaguzi, wapatiwe magari na mafuta ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa heshima ya Bunge lako Tukufu nitoe angalizo kwa Serikali isicheze na wataalam katika nchi yetu. Wataalam wa elimu ni afya, nchi yetu inaweza ikafikia mahali pabaya. Hili ni suala la maisha ya watu na kuelimika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa; Naibu Waziri, Mheshimiwa Philipo Mulugo; Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii. Pamoja na pongezi hizo napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejenga shule nyingi za *O level* (kidato cha I na IV). Je, Serikali imewaandaa vipi vijana wanaomaliza kidato cha nne wanaokosa nafasi ya kuendelea kidato cha tano kuweza kujitegemea? Je, wanawezeshwa kujitegemea kwa kuwa wajasiriamali, wakulima wazuri baada ya kumaliza elimu hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo ulazima wa mafunzo ya ufundi stadi na kadhalika katika shule za sekondari ili kuwawezesha vijana kujitegemea baada ya kumaliza masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mgomo wa Walimu lisipuuzwe kwani kwa sasa Walimu wana mgomo baridi ambao ni mbaya zaidi. Kazi ya kuhakiki madeni sio kazi kubwa kiasi cha kuishinda Serikali na kama tatizo ni mishahara na posho kama Walimu walivyodai ni vizuri Serikali ikakaa na viongozi wa walimu kutafuta suluhu. Watoto wetu hwafundishwi kikamilifu na kama Taifa tunazidi kuathirika kielimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo cha Ukaguzi wa Elimu kimesahaulika kabisa, Wakaguzi wa elimu hawana vitendea kazi kabisa, waliopandishwa ngazi hawajalipwa mishahara stahiki, wanaishi kama watoto yatima. Kama Serikali haitaki Kitengo cha Ukaguzi, basi kifutwe kuliko kuwatesa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo inalalamikiwa kuwa inachelewesha mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, lakini tulipokagua hesabu za baadhi ya vyuo vikuu tulikuta wahasibu wa vyuo hivyo kukaa na fedha za wanafunzi kwa muda mrefu bila sababu za msingi. Bodi ya Mikopo hulaumiwa bila kujua kuwa Bodi hutegemea fedha toka Hazina. Nawashauri uongozi wa Bodi wawe wazi kwa wananchi pindi fedha zinapochelewa kutoka Hazina na pia fedha zinapocheleweshwa na wahasibu wa vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo iwawajibishe watendaji wake wasio waaminifu wanaoliibia Serikali kwa kuingiza majina bandia kwa nia ya kuliibia Taifa, wizi huo ulionekana Chuo Kikuu cha Mkwawa baada ya ukaguzi wa *CAG*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za binafsi hutoza ada kubwa kwa kisingizio cha kutoa elimu bora kuliko shule za Serikali. Kila mmiliki wa shule akitoza ada kwa jinsi atakavyojisikia. Hii siyo haki hata kidogo. Naiomba Serikali kuunda chombo cha kusimamia uendeshaji wa shule za binafsi (*Regulator)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mtendaji Mkuu wa Baraza la Mitihani la Tanzania kwa kudhibiti wizi wa mitihani. Mtendaji Mkuu, Joyce Ndalichako nakushauri kusimamia Baraza hili ili uwadhibiti wanaotaka kuchafua sifa nzuri ya baraza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ni jambo muhimu sana katika maisha ya binadamu. Ni vyema Serikali iweke mfumo wa watoto kujifunza kwa mitaala ya Kiingereza ili watoto wote wa maskini na wenye uwezo waweze kufaidi lugha hii ya Kiingereza pamoja na ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mikopo ni vyema Serikali ijitahidi kutoa mikopo kwa wanafunzi wote wanaofaulu bila kuangalia vigezo vya ajabu ajabu ambapo wakati mwingine vinapelekea ubaguzi. Kwa kufanya watoto wa maskini kuweza kupata elimu bora na si bora elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maktaba ya Mkoa wa Kigoma, maktaba ni sehemu muhimu sana katika maisha ya elimu. Je, Serikali ina mpango gani kuhusu ujenzi wa maktaba ya Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu operesheni iliyofanywa na Naibu Waziri na kugundua watoto takribani 1,000 wameachishwa kuendelea na masomo kwa sababu waliingia kwa mgongo wa rushwa na kinyume na sheria. Je, Serikali haioni huu ni uzembe katika sekta ya elimu na kuadhibu watoto wadogo, ni

laana, ni vyema wangeadhibu wazazi na Walimu kuliko watoto ambao ndio Taifa la leo na kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri wanayofanya. Maoni yangu ni katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo, hii ni taasisi inayotoa huduma ya mikopo kwa wanafunzi na fedha hizo zinatoka Hazina. Sioni mantiki ya Bodi hii kuwa chini ya Wizara ya Elimu inaongeza tu urasimu. Napendekeza Bodi hii iwe chini ya Wizara ya Fedha ili ifanye kazi yake kwa ufanisi wa bila kuathiri *ceiling* ya Wizara ya Elimu. Hivi sasa sehemu kubwa ya bajeti ya Wizara ni mikopo ya wanafunzi, hii haileti picha sahihi ya fedha halisi inayopata Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za kulipia mitihani, miaka miwili mpaka mitatu hapo nyuma ada ya mitihani ilifutwa. Hii ilisababisha wanafunzi wote kuendelea na masomo kidato cha nne. Kwa sasa Wizara imerudisha tena utaratibu wa kulipa ada. Kwa watoto ambao wazazi wana uwezo mdogo hii itawafanya wasiendelee na masomo. Naomba Serikali ikatafakari tena ili kuona utaratibu wa kuondoa kabisa ada ya mitihani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa mabweni na maabara katika shule za sekondari. Wananchi wa Jimbo la Mbinga Mashariki wamefanya kazi kwa bidii na wamejenga madarasa. Naomba Wizara ifikirie sana juu ya ujenzi wa mabweni katika sekondari za Ruanda, Hagati, Matiri na pia kujenga maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za Wizara hii ni kidogo sana, nashauri kutokana na umuhimu wa sekta ya elimu katika Taifa kwa kuwa ndiyo sekta mama katika uzalishaji na maendeleo endelevu bajeti yake iwe ni 25% ya bajeti yote ya Taifa. Hasa wakati huu wa ushindani na kasi ya ukuaji wa sayansi na teknolojia duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kuwa viwango vya udahili vya vyuo vikuu vya umma uheshimiwe na ikiwezekana hata vyuo vikuu binafsi viwe na viwango vinavyoshabihiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa msingi wa utoaji wa mikopo unaokubalika duniani ni uwezo kifedha, basi wanafunzi maskini wanastahili zaidi kupewa mikopo kuliko wanafunzi wanaotoka kwenye familia zenye uwezo kiuchumi, kigezo cha kufaulu kwa kiwango cha daraja la kwanza na la pili si kigezo pekee kwani wengi wanaofaulu katika viwango hivyo hutokea kwenye familia zenye uwezo wa

kuwasomesha watoto wao kwenye shule bora za binafsi na chache za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vigezo vya kudahili wanafunzi vyuo vikuu vizingatie mazingira yasiyoridhisha ya kutoa elimu hasa matatizo ya upungufu wa Walimu katika shule za sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe ruzuku (ufadhili) kwa wanafunzi wanaotoka kwenye familia maskini badala ya kutoa mikopo tu. Naamini uwezo huo tunao suala ni maamuzi ya vipaumbele vya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na udhaifu katika sekta ya elimu kumesababisha janga kubwa la ukosefu wa ajira kwa vijana wetu wanaomaliza elimu ya msingi, elimu ya sekondari na hata wa elimu ya juu (vyuo vikuu au vyuo vya ufundi). Wahitimu wetu hawaajiriki kwa sababu hawakuandaliwa inavyopaswa kitaaluma kuweza kukidhi mahitaji ya soko la ushindani lililopo ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika soko la Afrika Mashariki, wahitimu wetu wanakosa kujiamini na hivyo kushindwa kushindania nafasi wanaposhindanishwa na wahitimu wengine wanaotoka katika nchi nyingine kama Kenya. Ni wazi kwamba, udhaifu wa wahitimu wetu unatokana na mfumo hasi wa elimu yetu katika mfumo rasmi.

**MHE. WARID BAKARI JABU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Waziri kwa uwasilishaji wa bajeti yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Wizara ya Elimu kupitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kuendelea ujenzi wa Chuo cha Sayansi Baharini Buyu (*Marine Science Institute*) Tawi la Zanzibar na naiomba Serikali kumaliza ujenzi huo, lakini ni lini nyumba za wafanyakazi zilizopo eneo la Mazizini zitafanyiwa ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vikuu vinaajiri wafanyakazi kupitia Sekretarieti ya Ajira nayo inaangalia *GPA* ya mtahiniwa. Ushauri, *indicator* hii sio nzuri kwani inawapendelea wanaotoka vyuo binafsi kuliko vyuo vya Serikali kama *Universty of* Dar es Salaam ambao wanatoa wanafunzi wanaofaulu bila ya rushwa au kupewa mtihani. Hivyo bora udahili ufanywe na chuo husika kwani ndio wanaojua mwalimu wa aina gani wanamhitaji baada ya kumhoji na kumuona alivyo sio kuletewa na Sekretarieti ya Ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wa shahada ya kwanza kwenye taasisi ambazo ziko chini ya *NACTE,* udahili wa wanafunzi hutokea kwenye mfumo wa *NT1-NT8,* wanafunzi hudahiliwa kutokea kwenye mfumo ya *TCU,* sasa hata Bodi ya Mikopo hawakubaliki kwenye mfumo huo. Mfumo huo husababisha vyuo kukosa wanafunzi wengi. Je, Serikali haioni kuwa utaratibu huu haufai kwa sasa kwani unafanya vyuo vingi kujiendesha kwa hasara na ukizingatia wanafunzi vyuo hivyo hawapati mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji kwa bajeti nzuri. Nawapongeza kwa ushirikiano mzuri na Kamati na kupokea ushauri kwa lengo la kuboresha utendaji wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wa wiki moja kujadili bajeti ya elimu ni mdogo. Kwa hiyo, naomba muda wa Kamati kuchambua bajeti iongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya elimu ni ndogo sana na ni vigumu kuibaini fedha halisi inayotolewa kwa Serikali kwa sababu fedha nyingine ya elimu ipo chini ya Halmashauri. Hali kadhalika Walimu wenyewe wapo chini ya Halmashauri na pia chini ya Wizara na hivyo masuala yao inabidi yaletwe Wizarani na kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Walimu na shule zirudishwe na kushughulikiwa mahali pamoja Wizarani. Bajeti ya Wizara, sehemu karibu asilimia 50 ni kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi, elimu ya juu. Hii ni hatari kwa sababu ina maana bajeti ya elimu ya msingi, elimu ya sekondari na elimu ya ufundi zinazidi kupata fedha finyu na kwa sababu hiyo huduma hiyo itazorota na kushusha mafanikio tuliyopata hapo nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie upya jinsi ya kutoa mikopo kwa elimu ya juu itafika mahali bajeti nzima wala haitatosha kwa mikopo. Ni kwa nini kusiwe na chombo nje ya Wizara ya Elimu kitakachoshughulikia masuala ya mikopo na Wizara ya Elimu ibaki kutoa elimu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mishahara ya Walimu ni midogo sana, naomba Serikali iangalie mishahara ya wafanyakazi wote kulingana na upeo wa elimu, miaka ya mafunzo na unyeti na ugumu wa kazi. Hali ilivyo sasa haina uwiano na wafanyakazi wanaona ni kelele na migomo ndiyo inayoweza kuwasaidia kupata maslahi zaidi. Hili Serikali ni lazima waliangalie, la sivyo leo Madaktari kesho Walimu, kesho kutwa Wanasheria, italeta mtafaruku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri CWT ambayo inasemekana inawakilisha Walimu wote imekuwa ikilazimisha Walimu kujiunga nayo, ni kwa nini sasa wasiachwe Walimu wasiotaka chama hicho na wanaotaka chama kingine kama vile Walimu Wenye Taaluma walivyoonesha nia ya kuwa na chama chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini Wizara isiwezeshe shule za sekondari na hata *primary* kuwa na vifaa vinavyoweza kutoa mafunzo ya ufundi na kuliongeza somo hilo kwenye mitaala ili watoto wanaohitimu kwenye ngazi mbalimbali wanatoka na ujuzi na hivyo kuweza kujiajiri wanapomaliza masomo katika ngazi yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ilikuwepo zamani ambayo shule zilitoa mafunzo ya uashi, ushonaji, upishi na kadhalika. Lakini pamoja na hili pia somo la biashara katika ngazi zote lingefundishwa ili kuwapa uelewa wa biashara na kuwawezesha kuendesha biashara zao kitaalam na siyo kama hali ilivyo sasa.

Mheshmiwa Spika, mimi ni mjumbe wa Kamati ya huduma za jamii nawapongeza Wizara kwa kuchukua ushauri wa Kamati na naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. MAUA A. DAFTARI:** Hongera Mheshimiwa Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri unazofanya. Pongezi za pekee kwa Walimu wote nchini wa ngazi zote kwa kazi nzuri wanazofanya wasichoke waendelee kufundisha ili Taifa lifaidike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ubora wa elimu yetu; kidogo kuna kushuka ubora wa elimu yetu inawezekana, Walimu wanaofundisha hawana ubora wa taaluma, wanafunzi kuendelea kuuza vyakula vya Walimu mashuleni, wanafunzi kwenda kutafuta maji wakati wa muda wa kusoma, wazazi kutokuwa na muda wa kukaa na watoto kupitia masomo waliyosoma, wanafunzi kuwa watoro na wasiojituma katika masomo, malumbano ya Walimu na vyama vyao na Serikali yanashusha morali ya Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri tuendelee kuelimisha jamii umuhimu wa kukaa na wanafunzi wetu wakiwepo majumbani, Serikali ikae na Walimu kutafuta ufumbuzi wa matatizo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Walimu kusimamiwa na vyombo vingi kunaleta urasimu mkubwa usio wa lazima, turudi kama zamani, Walimu kushughulikiwa na chombo kimoja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, *training and retraining* ya Walimu; uwepo mfumo mzuri wa kundeleza Walimu. Hii itasaidia sana kutokana na kukua kwa teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, Wizara iitake Bodi ya Mikopo ya wanafunzi iboreshe utaratibu, uwepo na uwazi na ukidhi matakwa na malengo yaliyowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, elimu kwa umma; kila mara tunaelezwa na kuelimishwa kuhusu madhara ya kutoa rushwa na ufaulu wa wanafunzi, lakini njia inayotumika kila leo ni *negative,* sasa tuelimishe mema yaliyofanywa na Wizara na Serikali yake badala ya kuwatafakari na kuchukua hatua, basi iwe tumeweza, tumefanya na iwe endelevu.

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikae chini ijadiliane na Walimu, itatue mgogoro kati yake na Walimu. Pamoja na falsafa kwamba ualimu ni wito bado Walimu ni wafanyakazi na wana mahitaji yao binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu itolewe kwa wanafunzi wote wenye ufaulu tofauti na ilivyo sasa ambapo kuna ukiritimba mkubwa bila kuwa na refarii huwezi kupewa mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa vya kufundishia hasa katika masomo ya sayansi katika shule zetu za kata utakuta Wilaya moja inakuwa na shule zaidi ya 15 lakini hazina maabara hata moja. Wizara iangalie upya wahitimu wa Vyuo vya Ualimu wapewe ajira mapema kuliko ilivyo sasa ambapo wahitimu wanasota uraiani kwa muda mrefu bila ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kwa wenye mahitaji maalum, kundi hili ni kubwa sana hasa vijijini, lakini kundi hili limesahaulika, tuiombe sasa Wizara husika kuelekeza Walimu wa kutosha katika shule za vijijini na sekondari zetu za Kata ili kuwapa uwezo wanafunzi wenye mahitaji maalum.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kusimamia elimu hapa nchini. Maoni yangu ni kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuleta haraka Bungeni Muswada wa Sheria ya Bodi ya Mikopo. Kuboresha masomo ya sayansi kwa ujenzi wa maabara na maktaba. Wanafunzi wanaotokea katika vyuo vya Diploma na Cheti wapewe mikopo. vyuo vya Diploma na vyeti wadahili wenyewe katika bodi zao za vyuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Waziri Mkuu, Waziri wa Elimu, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, kwa namna walivyotatua matatizo katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka ya 2010/2011, Walimu wa Halmashauri ya Moshi walikuwa na kero nyingi. Kero hizo zilikuwa; wananyanyaswa, wanatukanwa, hawasikilizwi, mishahara yao ilikuwa inapatikana tarehe 5 hadi 10 ya mwezi unaofuata,

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliokuwa wanawanyanyasa ni ofisi ya elimu, ofisi ya fedhana ofisi ya utawala. Walimu wakapeleka malalamiko yao kwa Wabunge wa Halmashauri ya Moshi, kwa *RC* na kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *RC* Mkoa wa Kilimanjaro akaita makundi yote ya Walimu, akaita Walimu wa kawaida wa *primary* na sekondari, akaita Walimu Wakuu wa *Primary School* na *Secondary Schools,* Waratibu wa Elimu wa Kata, wawakilishi wa Walimu na watumishi wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla ya mazungumzo na makundi haya akaunda timu ya watafiti kutafiti matatizo ya Walimu. Ripoti ya timu hiyo ikathibitisha kwamba, Walimu wanaonewa, wananyanyaswa. Mkutano wa *RC* na makundi haya ukathibitisha kwamba Walimu wananyanyaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yafuatayo yalitolewa na yatekelezwe:-

Hatua za kinidhamu zichukuliwe, kuonya, kuwashusha madaraka, kuhamisha watumishi 32 kwa Idara zilizohusika, Idara ya Fedha, Idara ya Utawala na Idara ya Utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu akahamisha Wakuu wa Idara saba kutoka Halmashauri ya Moshi kwenda Halmashauri nyingine. Baada ya hatua hizo amani kwa Walimu wetu ikarudi katika Halmashauri ya Moshi. Nashauri matatizo ya Walimu yanapojitokeza yashughulikiwe mara moja.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kwa niaba ya wananchi wa Ludewa, nataka niwapongeze Mawaziri wote wawili wa Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa na Naibu wake Mheshimiwa Philip Mulugo kwa utendaji wao mzuri na uliotukuka. Mimi binafsi nina imani kubwa na uongozi wenu, msiniangushe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imani yangu kwa Mawaziri hawa wawili ni kubwa kwani nina imani watasimamia na kutekeleza vema makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara yao kama ilivyoainishwa kwenye ukurassa wa 89 wa kitabu cha bajeti ya Wizara kwamba, mwaka huu watajenga Chuo kimoja cha Serikali cha *VETA* Ludewa katika mpango wa Wizara wa kuimarisha utekelezaji wa

awamu ya kwanza ya ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi katika Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwe muwazi, wananchi wa Ludewa tumeipokea habari hii ya ujenzi wa *VETA* kwa furaha kubwa sana, ikizingatiwa kuwa ujenzi wa Chuo hiki umepigwa danadana kila mwaka toka mwaka 2008/2009, nina imani kuwa Mheshimiwa Kawambwa Waziri na Naibu wake Mheshimiwa Mulugo *this time* mtahakikisha chuo hiki kinajengwa Ludewa.

Mheeshimiwa Spika, wananchi wa Ludewa tumechoka kupigwa danadana kila mwaka. (Rejea kumbukumbu za *Hansard* za Bunge) Chuo cha *VETA* Ludewa ni ukombozi mkubwa kwa vijana wetu ukizingatia kuwa miradi ya Liganga na Mchuchuma itaanza kuendelezwa hivi punde. Ili vijana wetu waweze kunufaika na miradi hii, ni lazima wawe na mafunzo ya elimu ya ufundi.

Mheshimiwa Waziri, naamini nyie hamtanipiga danadana kwa sababu wewe Mheshimiwa Kawambwa na Mheshimiwa Mulugo ni waungwana. Naamini mtaitekeleza kwa vitendo hii kauli yenu ya ukurasa wa 98 kwenye kitabu cha bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mwisho kwa niaba ya Wanaludewa nawatakia wote afya njema na Mwenyezi Mungu awape baraka tele na kila neema mnazohitaji katika utendaji wenu ili mhakikishe kwamba kweli *VETA* inajengwwa Ludewa. *Thanks in advance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa mara ya kwanza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Elimu inahitaji kuangaliwa kwa makini sana. Kwani kuna maeneo mengi sana yanayohitaji kufanyiwa marekebisho makubwa na mengi sana. Eneo la kwanza, ni ufinyu wa bajeti tukihitaji kutekeleza majukumu ya Wizara hii, lazima bajeti ya Wizara hii iwe na bajeti ya kutosha kwani tunahitaji kuimarisha mifumo ya elimu kwa ujumla jambo ambalo linahitaji fedha nyingi sana ambazo zinahitaji mafungu makubwa ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchakavu wa majengo ya shule na nyumba za walimu; watoto wanaosoma katika shule hasa za vijijini zina hali mbaya sana. Ni vyema Serikali kupitia Wizara ikaandaa mchakato wa kufanya maboresho na kukarabati majengo hayo ili kiwe kivutio kwa wanafunzi na Walimu wajitume katika kufanya kazi wakiwa wanaishi katika nyumba nzuri na bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Mpanda Vijijini kuna upungufu mkubwa sana wa Walimu hasa katika shule za sekondari ambazo zina upungufu mkubwa sana. Hatuwezi kuboresha elimu kama hakuna Walimu, kazi ya Walimu ni kubwa sana na mafanikio ya elimu mpaka kuwe na idadi ya kutosha ya Walimu ili iende sambamba na uwiano wa wanafunzi madarasani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Mpanda Vijijini nina shule za sekondari tisa ambazo zina upungufu mkubwa wa Walimu. Niiombe Wizara iweke kipaumbele cha kuleta Walimu wa kutosha ili kuweza kutoa elimu nzuri katika shule za Ikola, Kabungu, Mpanda Ndogo, Katuma, Mwese na Mishamo ambako kuna upungufu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Walimu wafanyea kazi nzuri kwa kujituma, lazima tufanye maboresho ya mishahara ya Walimu ili iweze kukidhi mahitaji yao. Ni vigumu Mwalimu kufanya kazi ya kujituma kama hapati malipo mazuri ya kuvutia. Naishauri Wizara iandae mpango maalum wa kuboresha elimu kwa kuwaongezea mishahara Walimu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iangalie mpango mahsusi wa maboresho wa kuangalia vyuo vikuu vitoe huduma iliyo nzuri ambayo itawaandaa vijana walio wengi katika stadi mbalimbali. Lakini kumekuwepo suala la malalamiko mengi ya mikopo. Ni vizuri Bodi ya Mikopo ikaangalia upya na kutazama upya kwa wanafunzi hasa wa watoto yatima na wenye hali mbaya za kimaisha (maskini) wapewe nafasi za upendeleo. Ni vizuri Serikali kupitia Wizara ya Elimu ikafanya upembuzi wa kuangalia wale wanaostahili kupewa mikopo hiyo kuliko ilivyo sasa. Kwa kuwaangalia watoto ambao hawana sifa za kutosha ndio walio wengi waliopata mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaunga mkono hoja hii endapo nitapata majibu ya kutosha katika maeneo niliyoyachangia.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Waziri wa Elimu pamoja na timu yake kwa jitihada kubwa wanazochukua kupambana na changamoto zilizopo katika sekta ya elimu nchini. Ieleweke kuwa ni kutokana na mahitaji makubwa ya elimu kwa Watanzania ndiyo maana Serikali inaonekana kuelemewa na mahitaji ya huduma lakini kuna kazi kubwa na nzuri Wizara inafanya, naipongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kufahamu ni lini mpango wa ujenzi wa sekondari mbili kwa kila Halmashauri utaanza maana tangu bajeti iliyopita mpango huo ulisemwa, lakini hadi leo haujatekelezwa. Katika Jimbo langu ambalo sasa limekuwa Wilaya ya Busega, Mkula Sekondari ilipendekezwa, kwa kuwa Wilaya hii mpya haina *High School* hata moja, tulitegemea uboreshaji wa shule hiyo ungetusaidia ili kuomba ifanywe *High school*. Pia naomba kufikiriwa shule ya sekondari ya Nassa ifuatie katika utaratibu kwani Wilaya yetu itakuwa na shule moja tu chini ya mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kurejesha heshima ya taaluma ya ualimu, naomba Serikali kupitia Halmashauri za Wilaya na kwa kuhamasisha wananchi, nguvu ya makusudi ielekezwe kujenga nyumba za Walimu. Serikali iangalie mfumo wa ujuzi wa nyumba za gharama nafuu kupitia Shirika la Utafiti wa Ujenzi ili kupunguza gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sasa hivi kuna *solar system* zinazofaa kwa vijijini zinazosambazwa na Kampuni ya *Artienergy* ambapo nyumba moja inagharimu shilingi 190,000/= tu. Hizi zingefaa sana kuboresha mazingira ya ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa elimu nchini sasa unawafanya wahitimu wawe tegemezi na wasio na ubunifu hasa baada ya kuandaa JKT na elimu ya kujitegemea, nashauri kwa namna fulani hata bila ya kuanzisha masomo pekee, elimu ya ujasiriamali ianze kufundishwa mashuleni kuanzia chini hadi chuo kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi kila taaluma ni kiwanda cha ajira, lakini inasikitisha kuwa Afisa Kilimo, Afisa Uvuvi na Mwalimu anamaliza *degree,* lakini bado analia hana ajira. Hii ni tofauti sana na wenzetu wa nchi jirani. Kujiamini na ubunifu lazima ujengwe kwa Walimu wetu ili nao wawajengee wanachuo/wanafunzi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi kwa kuweka masuala ya elimu chini ya Wizara mbili, Wizara ya Elimu na TAMISEMI una changamoto zake. Inasikitisha unapokuta shule ya msingi au sekondari inafungwa na Wakaguzi kwa sababu ya kukosa vyoo. Hivi Maafisa wanaohusika na ufuatiliaji walikuwa wapi hadi inafikia hatua ya kufunga shule?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni nani awajibike? Wanafunzi ndio wanaoathirika! Nadhani ipo haja ya kuchukua msimamo mkali kuhusu hili, iwapo *DED*, Afisa

Elimu, *MEK, WEO* na *VEO* wapo inakuwaje shule inafungwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Busega, mathalan shule sita zilifungwa mwaka jana kwa kukosa vyoo na sasa kuna shule imefungwa kwa zaidi ya miezi minne kwa sababu madarasa yalianguka, shule ya msingi Nyamajeshi katika Kata ya Lamadi, hatma ya watoto hao itakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kuwalaumu wananchi kwa sababu wao wanahitaji kuhamasishwa na kuongozwa na viongozi na watendaji wao wa Serikali. Naomba msimamo wa Serikali na hatua za madhubuti za namna ya kuwakomboa wanafunzi wa shule ya msingi Nyamajoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ilianzisha shule za Kata kwa lengo na madhumuni ya kuepusha msongamano wa watoto lakini pia ilizingatia umbali uliokuwepo kwa vijana kwenda na ama kufika salama, lakini hasiwahi masomo au kutofika salama kwa kushambuliwa na wanyama wakali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo tukubali kwamba shule za Kata zilikuwa ni njia moja ya kuwakomboa watoto wa Kitanzania kielimu, lakini malengo hasa hayakufikiwa kutokana na kasoro zifuatazo:-

Ukosefu wa Walimu, kutowapatia uwezo Walimu katika kuishi maeneo husika, vitendea kazi katika sekta ya elimu, kutowapatia mishahara walimu kwa wakati. Hizi ni miongoni mwa changamoto zinazoikabili sekta ya elimu siku hadi siku na zinahitaji kupatiwa ufumbuzi unaofaa ili kutoa elimu bora kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna chombo ambacho kinaonesha unyanyasaji juu ya vijana wetu ambao wanaomba kujiendeleza masomo ya elimu ya juu na chombo ambacho kinashusha hadhi ya Mheshimiwa Waziri kwa kuonekana kwamba yeye ndiye mhusika Mkuu wa suala zima la mikopo, hakuna kama Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ni matumaini yangu kwamba, kuanzia sasa Bodi hii haitatoa mikopo kwa kuzingatia wapi unatoka katika Jamhuri ya Muungano, haitoangalia unatokana na familia gani na kwamba kutakuwa na uvumilivu mkubwa wa kuwavumilia vijana ambao uwezo wao na uwezo wa familia zao ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza za Mitihani Tanzania limekuwa likilalamikiwa hasa katika usahihishaji wa mitihani na kuonekana kwamba kuna upendeleo wa ama kiimani, jambo ambalo linatoa taswira ya kuwagawa Watanzania katika misingi ya imani. Hivyo basi, kwa kuwa Tanzania hatutawali kwa misingi ya dini, ni vyema masuala ya usahihishaji wa mitihani yaangaliwe katika misingi ya haki na sio imani ya dini fulani.

**MHE.LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote kwa kazi nzuri na hotuba nzuri ya bajeti 2012/2013. Nawatakia utekelezaji wenye mafanikio makubwa. Baada ya pongezi napenda kutoa ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa elimu unahitaji kufanyiwa mabadiliko ili wahitimu waweze kutumia elimu yao kujiendeleza kiuchumi (wajiajiri wenyewe). Kwa mfano, elimu ya ufundi pamoja na kilimo kwa vitendo irudishwe mashuleni kama ilivyokuwa miaka ya sabini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masomo ya Sayansi yasifundishwe kinadharia tu, shule zihamasishwe kuchangia maabara kwani Serikali haina rasilimali fedha za kujenga maabara na kununua *equipment* kwa shule zote za sekondari hapa nchini. Aidha, zipo hata *mobile laboratory* za *science* ambazo ni rahisi kutumia kwa shule zaidi ya moja, maabara hizi zinapatikana Afrika ya Kusini na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi kubwa ya vijana wanaomaliza shule za msingi na sekondari wanashindwa kujiajiri kwani hawana *skills*. Nashauri Serikali ijenge angalau chuo kimoja cha ufundi kila Wilaya, Vyuo hivi viwe *integrated* na kilimo kwa sababu kilimo ndicho kilicho na ajira ya uhakika. Ardhi ipo, hivyo elimu itumike kuwatayarisha vijana wachangie juhudi za Serikali za kilimo kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maadili mashuleni hususan wale wa sekondari. Vijana wanaotumia madawa ya kulevya na *other substances* wanaongezeka kila kukicha. Napendekeza au kushauri Serikali iongeze Walimu wanaolea vijana (yaani *counseling* na *guidance*). Aidha, Serikali ishirikiane na *NGOs* ambazo zinashughulika na kuboresha maadili ya vijana pamoja na kutetea haki zao. Pia napenda kuikumbusha Wizara kwamba ni wajibu wao kuwakumbusha viongozi wa dini wajibu wao wa kutoa elimu ya dini mashuleni kama Serikali ilivyotoa siku maalum ya kutoa elimu ya dini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri Wizara kuhamasisha ushirikiano kati ya Wazazi na Walimu katika malezi ya watoto kimasomo na kimaadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuiomba Wizara iwatumie walimu vizuri, inakuwaje Mwalimu mwenye *degree* anapelekwa kufundisha shule ya msingi wakati huo huo shule za sekondari hazina Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siridhiki kabisa kwani hawa Walimu wenye shahada wengi wao wanalundikana katika shule za msingi mijini. Naomba Walimu wenye *degree* walio Morogoro Mjini wahamishiwe vijijini kwenye shule zetu za sekondari. Wizara inashindwa nini kuhakikisha kwamba kunakuwepo na uwiano mzuri wa idadi ya walimu wa ngazi zote mjini na vijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi Waratibu Elimu wa Kata wanatakiwa kufanya kazi gani? Ni nini wajibu wao hasa? Inakuwaje Mratibu Elimu anashindwa hata kusaidia kufundisha pale ambapo kuna Mwalimu mmoja tu katika shule za msingi? Wengi wao wanakaimu Afisa Mtendaji Kata pale ambapo Mtendaji anakuwa hayupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara itoe mwongozi wa namna ya kuwatumia Waratibu Elimu pamoja na Walimu Wakuu wa shule za msingi, wasipewe kazi za Serikali za Mitaa kama Watendaji wa Vijiji au Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iangalie upya suala la michango mashuleni kwa mfano, suala la michango ya madawati, hivi kweli madawati yatachangiwa zaidi ya miaka kumi? Mbona wahitimu hawaondoki na madawati na majembe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika shule za sekondari kuna michango ya mitihani, mchango ya walinzi, vyoo na kadhalika. Naomba Serikali itoe tamko kuhusu michango na hatimaye ikubali kwamba Serikali kupitia TAMISEMI inawajibika kulinda mali kwa kulipia walinzi wa shule. Napenda kuiambia Serikali kwamba wazazi wamechoka kuchangishwa bila ukomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri Serikali iangalie uwezekano wa kuwapatia watoto chakula mashuleni, kama haiwezekani kwa watoto wote naomba watoto wenye VVU wapate chakula cha mchana ili waweze kutumia dawa kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vituo vya MEMKWA, nashauri Serikali itoe ruzuku kwa *NGOs* au Mashirika ya Dini ambayo yameendelea kutoa elimu ya MEMKWA. Naomba *specifically* Walimu wanaofundisha vituo hivi walipwe na Serikali kama Wizara ya Afya inavyotoa ruzuku ya mishahara na dawa kwa hospitali teule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri atoe tamko kuhusu suala la Walimu wenye shahada kufundiha katika shule za msingi mijini pamoja na hili la kutoa ruzuku kwa mashirika au *NGOs* zinazotoa elimu ya MEMKWA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi akiwasilisha bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Naipongeza Serikali kwa namna inavyojitahidi kutoa fedha kwa ajili ya Wizara hii, natambua kuwa ili Taifa lolote ulimwenguni liweze kuendelea linahitaji kuwa na msingi bora wa elimu katika ngazi zote kuanzia elimu ya awali, elimu ya msingi, elimu ya sekondari, elimu ya ualimu na elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri hakika kuwa sekta ya elimu nchini inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo upungufu wa walimu katika maeneo yote muhimu. Aidha, uhaba wa vitendea kazi vya kufundishia pamoja na uhaba wa madarasa, nyumba za walimu, zipo pia changamoto za usimamizi wa mitihani ambapo kumekuwepo na utovu wa

maadili katika kusimamia mitihani ya Kitaifa, matokeo yake yanaonekana katika kuzorota na ubora wa elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye mahitaji ya Jimbo langu la Mbogwe ninaloliwakilisha, Jimbo langu ambalo limepewa heshima ya kuwa Wilaya katika Mkoa mpya wa Geita. Jimbo letu linakabiliwa na upungufu mkubwa wa Walimu kwa shule za msingi na sekondari. Naomba liongezewe Walimu ili kuongeza viwango vya ufaulu kwa wanafunzi ambao ndio Taifa la kesho. Tunahitaji kubwa la kujengwa Chuo cha Elimu na *VETA* ili kutoa fursa kwa wananchi wa Wilaya yetu ya Mbogwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Wizara ifikirie kuweka kipaumbele cha kujenga Chuo cha *VETA* kwa Wilaya yetu ili kuwawezesha wananchi hasa vijana wanaohitimu masomo yao ili hatimaye waweze kujiajiri wenyewe baada ya kupata stadi zao katika masomo ya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri madai ya walimu yashughulikiwe kwa wakati ili kunasua uwezekano wa kuzuka kwa migogoro kama migomo ambayo hasa inachukua sura mpya kwa kuwafundisha watoto wa shule yaani wanafunzi kuanza kujifunza tabia ya kutotii sheria kwa kushiriki maandamano

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuwapongeza Mawaziri na watendaji wa Wizara hii kwa juhudi zao. Naomba mwaka huu wa fedha Wizara iangalie suala la Walimu hasa wa Sayansi kwenye Wilaya ya Misungwi maana ni wachache sana. Vile vile tuangalie namna ya kutoa motisha kwa wanafunzi wa shule za Kata badala ya hizi za vipaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Elimu na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hoja, naomba nitoe ushauri kuwa Wizara iangalie kwa makini suala la kushuka kwa kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi, Idara ya Ukaguzi ni muhimu sana kwa elimu iliyo bora, tunapowaacha Walimu wanajiendesha wenyewe bila kukaguliwa hatuwatendei haki watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa muda mrefu sasa Wizara inasema Idara ya Ukaguzi wanataka kuifanya kuwa Wakala, kauli hii imewachosha Wakaguzi kwani toka wameanza kusikia bado michakato inaendelea. Nashauri Wizara ione umuhimu wa kuwajali Wakaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti ya mwaka 2011/2012, Halmashauri zilipata sh. 400,000/= tu, hivi kweli kwa fedha hii wanaifanyia kazi gani? Haitoshi

hata zile huduma za kijamii hawapati, mfano, mtumishi wa Idara ya Ukaguzi anafiwa au anafariki, anayepaswa kumhudumia ni Katibu Mkuu Wizara ya Elimu. Hajapata mshahara mpaka awasiliane na Katibu Mkuu, ana madai yoyote anadai mpaka Katibu Mkuu, kweli Wizara inawatendea haki Wakaguzi hawa? Kama imeshindwa kuhudumia Idara hii basi ni bora Wakaguzi hawa warudishwe darasani wafundishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena na tena Idara ya Ukaguzi iangaliwe kwa macho mawili kwani Idara hii naamini ndiyo jicho la Wizara ya Elimu na ilianzishwa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MHE. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali pamoja na Watanzania wote kuitikia wito wa kujenga sekondari kila Kata na hata kila kijiji kwa mfano katika Jimbo langu la Karatu. Changamoto kubwa kwa Serikali ni suala la Walimu na maabara kwa shule zetu. Napenda kuishauri Serikali kuunga mkono juhudi za wadau wa elimu, Mashirika yasiyo ya Kiserikali katika kuboresha elimu yetu na kuzalisha Walimu bora na wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa *PPP* uimarishwe, Serikali itoe msisitizo mkubwa kwa shule zetu kuwa na maabara ili wanafunzi wetu wafanye mazoezi ya vitendo *(practical)* kuliko kufanya mazoezi ya vitendo nadharia *(alternative practicals)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kumaliza uhaba wa Walimu, pale inapoonekana nia ya Halmashauri kuanzisha vyuo vya ualimu, Serikali isaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Karatu iko kwenye matayarisho ya mwisho ya kukamilisha ujenzi wa chuo cha ualimu Ayalabe. Majengo yote muhimu ni tayari, tunaomba Serikali itoe kibali chuo hicho kianze na kipate kukiwezesha wakufunzi na vifaa. Mheshimiwa Waziri naomba kauli yako kwa hitaji hilo la msingi kwa mustakabali wa elimu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, posho na stahiki za Walimu, hili limekuwa tatizo sugu kwa walimu kote nchini. Nashauri Serikali iwe makini sana katika kulipa posho na stahiki za Walimu kwa muda muafaka. Athari za kutotekelezwa kwa madai haya ni kubwa sana. Moja ni matokeo ya kazi zao. Kufeli kwa wanafunzi darasa la saba, kidato cha nne ni athari ya Walimu kutoridhika na utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kupata maziwa mengi na matamu ni lazima kumtunza vizuri yule ng'ombe unayemkamua, usipomtunza na hata kumbembeleza, ng'ombe ana tabia ya kurudisha maziwa yake mwilini pamoja na kwamba wewe utafanya kila hali ili kumkamua. Serikali inatumia nguvu kubwa na kila hali kuhakikisha Walimu wanarudi kazini bila kuweka mazingira sawasawa, bado tatizo ni kubwa maana ufanisi wa kazi yao bado ni *zero*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwafukuza kazi watumishi kwa kudai haki zao si suluhu ya matatizo ya elimu nchini. Mpaka sasa pamoja na Serikali kulipa madeni ya Walimu hali bado ni mbaya kwa Walimu kudai malipo yao katika Halmashauri zetu, nashauri Serikali iongeze kasi kumaliza madeni ya Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ukaguzi wa shule, kitengo hiki hakifanyi kazi yake sawa sawa, naishauri Serikali kupitia Wizara ya Elimu kuimarisha kitengo/Idara ya Ukaguzi wa shule, kuhakikisha Walimu wanajiandaa vizuri, kwa mfano, Walimu wawe na sehemu *of work, Lesson plan, Lesson notes, evaluation and remarks*. Hivyo suala la wanafunzi kufaulu mitihani bila kujua kusoma na kuandika halitakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Baraza la mitihani, napenda kuishauri Serikali juu ya uvujaji wa mitihani kuwa makini sana, kutenda si kosa bali kurudia kosa ndiko kosa. Uvujaji wa mitihani limekuwa tatizo sugu kwa nchi yetu, naomba hilo lifike mwisho sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imesikia kilio cha Wazazi, wanafunzi na Watanzania wote kuhusu kufutwa kwa matokeo ya mitihani kwa baadhi ya wanafunzi na kwamba Serikali imekubali wanafunzi hao kufanya mitihani mwakani, naomba Serikali/Baraza la Mitihani kuwaruhusu wanafunzi hao kufanya mitihani kama *school candidates* na isiwe *private candidates*, kwa kufanya hivyo tutakuwa tumewatendea haki wanafunzi hao? Naomba kauli ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kwa wenye mahitaji maalum, pamoja na bidii kubwa inayofanywa na Serikali kuhusu miundombinu katika shule zetu kuhusu wanafunzi wenye mahitaji maalum bado hitaji la kuwaandaa Walimu kwa elimu ya wenye mahitaji inahitajika sana. Pia kuna hitaji kubwa la vitendea kazi na vitabu/vifaa kwa wenye ulemavu.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wa shule ya Sekondari Tabora *boys,* Mkoani Tabora wanalalamikia madai yao kwa muda mrefu sasa bila mafanikio. Kila wakifuatilia Manispaa wanaambiwa *documents* zao zimepotea/hazionekani. Wapo waliohamia pale kutoka maeneo mengine, alipofuatilia malipo na kusafirisha mizigo na familia yake anaambiwa hawezi kulipwa kwa sababu aliajiriwa akiwa Wizara ya Elimu na sasa yuko TAMISEMI, hivyo apeleke madai yake Wizaraya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu walipohamishiwa TAMISEMI mafaili yao yote pia yalihamishiwa kuwafuata na *document* zao zote, zilishafungwa, wanapoelezwa waende Wizara ya Elimu siyo kuwapa usumbufu usio wa lazima, Serikali itoe maelekezo kuhusiana na madai haya ili Walimu hawa wapate haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe miongozo kwa Halmashauri za Wizara na Manispaa kuwa, Maafisa Elimu baadhi wanajiona kama Miungu watu, Walimu wanaofuatilia madai yao wanawapa lugha chafu sana na kuona kama hawa Walimu hawastahili

kwenda Ofisini kwao, lugha hii inakatisha tamaa sana. Afisa Elimu Taaluma wa Manispaa ya Tabora Mr. Makali analalamikiwa sana kuwa na kauli chafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji elimu iliyo bora na siyo bora elimu, tunahitaji elimu inayotolewa imjenge mwanafunzi kufikia na kuweza kukabiliana na changamoto za duni ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha Serikali kuleta mfumo wa mitihani wa kuchagua (*multiple choice)* ni kuendelea kukandamiza elimu hapa nchini. Serikali ieleze kwa nini ilibadili mfuo wa zamani nak uja na mfumo usiojenga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaishangaa Wizara ya Elimu kwa jinsi wanavyopelea elimu hapa nchini, mwaka huu watoto wamepewa likizo mwezi wa sita kama kawaida, tena wanapewa likizo tangu tarehe 03/8/2012 mpaka tarehe 10/9/2012 kwa ajili ya sensa kufika kila shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini shule zimefungwa mapema? Vipindi hivyo vitafidiwa vipi na lini? Kama shule ina Walimu 7-10 wakachukuliwa watatu hao saba waliobaki wasingeweza kuendelea kufundisha watoto wetu. Serikali itoe majibu ya msingi kuhusiana na hali hii tunayoiona kwani ni kuendelea kudhoofisha elimu kwa kisingizio cha sensa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo cha Ukaguzi kwenye Halmashauri hawafanyi kazi kwa ufanisi, hakuna vitendea kazi, usafiri, mafuta, mafungu ya

kwenda vijijini. Wakaguzi wanakaa ofisini, Serikali imejipanga vipi kujenga uwezo kwa Kitengo hiki muhimu sana kwa ubora wa elimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri kwa Serikali, TAMISEMI imezidiwa na mambo mengi, hivyo mengine kukosa ufanisi, Sekta ya Elimu iondolewe TAMISEMI na kurudi Wizarani au iundiwe mfumo wake yenyewe ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi na kuinua elimu ya watoto wetu.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja. Nianze kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tatizo la Walimu vijijini; katika maeneo ambayo hayana Walimu wa kutosha yapelekewe Walimu, mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Songea Vijijini tunalo tatizo kubwa la upungufu wa Walimu. Mkutano uliopita niliiuliza Serikali kwa nini haioni umuhimu wa kuongeza Walimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea, uchaguzi uliopita Kata mbili za Halmashauri ya Wilaya ya Songea zilihamia Manispaa ya Mji wa Songea, uhamisho huo ulihusisha shule na idadi ya Walimu wa shule hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhamisho huo umeleta punguzo kubwa la Walimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea kwani mpaka sasa idadi hiyo bado inahesabika ni ya Walimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea wakati tayari wako Manispaa. Naomba hao ambao sasa ni pengo kubwa kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni inayoongoza mgao wa Walimu katika shule zetu inazifanya shule za vijijini kukosa Walimu. Uwiano wa 1:45 ni uwiano usiotekelezeka, yako maeneo ya vijijini ambayo shule moja ina jumla ya wanafunzi labda tuseme 150 toka darasa la kwanza mpaka la saba. Kwa kigezo cha uwiano shule hiyo itatakiwa kuwa na Walimu watatu tu. Walimu watatu watafundishaje darasa la kwanza mpaka la saba? Kwa nini kigezo hiki hakiletwi na kubadilishwa ili kuwapa haki ya elimu watoto wa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mafao ya Walimu; ni kweli hawana posho za mazingira magumu. Wanaofundisha vijijini wapewe posho ya mazingira magumu. Serikali isaidie kujenga nyumba za Walimu wapate makazi mema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati maalum wa kujenga maabara bado kuna tatizo kubwa sana la kuwafundisha sayansi watoto wetu. Naomba mkakati wetu wa kuhakikisha kuwa maabara zote zinajengwa, ukamilike.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na uzima kuniwezesha kushiriki katika Bunge hili katika shughuli za kila siku. Nakupongeza wewe Waziri pamoja na Naibu Waziri, Katibu wako Mkuu kwa mchango mzuri mnaoutoa kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza mchango kwa kusemea maslahi ya Walimu. Kabla ya yote, Serikali inapaswa kufahamu ukweli kwamba Walimu ni kiungo

muhimu sana kwa nyanja zote za maendeleo ya nchi yoyote duniani. Kama hakuna Walimu hakuna elimu na hakuna maendeleo yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana halisi ya maneno yangu tukikosa elimu tutakosa Madaktari, Mainjinia, Marubani, Wahandisi, Wavuvi bora, Wakulima bora, wafugaji bora, Wabunge, Mawaziri mpaka Rais. Ni kusema kuwepo kwa elimu ndio kuwepo Taifa na kukosekana kwa elimu ni kukosekana kwa Taifa lenye umakini. Serikali iangalie kwa umakini maslahi ya Walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu. Walimu wapatiwe mafao yao katika muda muafaka, Walimu wapatiwe motisha hasa wale wanaofundisha vijijini katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wizi wa mitihani ni kitendo kibaya ambacho kinatia aibu Taifa na kwa kiasi kikubwa kimezoeleka sana na kutaka kufikia hatua mbaya kwa Taifa. Athari kubwa inayopatikana kwa wizi ama kuvuja kwa mitihani ni kuanguka kwa kiwango cha elimu, kuwa na wasomi wengi wasio na kiwango. Taifa letu linakosa wataalam wenye sifa, kwa hiyo tunakosa watu wabunifu na Taifa letu linakuwa tegemezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la wizi wa mitihani si la wanafunzi tu bali Baraza la Mitihani la Taifa linahusika moja kwa moja ndio mhusika mkubwa wa dudu hili. Serikali inapaswa kutofumbua macho tatizo hili, wahusika wachunguzwe na wakibainika wachukuliwe hatua muafaka.

Wizara ya Elimu fuataeni nyayo za Waziri wa Maliasili na Utalii (Kagasheki) kwa maslahi ya Taifa na watu wake, kwa kuwa waathirika wakubwa ni watoto wa wanyonge, naomba tuwasaidie kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mkanganyiko wa matokeo ya mtihani wa Dini ya Kiislamu, kumekuwa na malalamiko kwa wahusika wa mtihani wa dini ya Kiislamu kwamba wamechukuliwa kwa sababu mtihani huo huo mmoja umetolewa matokeo mara mbili na kuonekana kwamba kuna lengo la makusudi la upendeleo wa upande fulani. Hili ni jambo zito, hivyo busariainahitajika. Naomba Mheshimiwa Waziri atakaposimama anipe maelezo ya kutosha kutokana na tatizo hili ili kuondoa mkanganyiko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Sasa tunaanza na majumuisho na tunaanza na Mheshimiwa Majaliwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAMISEMI (ELIMU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi ambaye anafanya kazi sambamba na ofisi ya Waziri Mkuu kushughulikia elimu, naomba kuchangia hoja nikiwa najibu hoja mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakizitoa kama mchango juu ya mwenendo wa elimu na mafanikio ya kielimu ambayo Watanzania wanayasubiri kwa hamu na sisi tumejipanga vizuri katika kuhakikisha kuwa utoaji elimu pia unapata mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge walizungumzia pia suala la upungufu wa Walimu nchini. Ni kweli tunao upungufu wa Walimu kwa maeneo yote ya shule za msingi na sekondari lakini maelekezo kwa Wakurugenzi na Maafisa Elimu pindi tunapowatuma Walimu ambao tumewaajiri wahakikishe wanakwenda kuripoti maeneo ambayo yana upungufu mkubwa wa Walimu. Kufuatia ajira ambazo tumezifanya na kama ambavyo nimeendelea kujibu katika maswali mbalimbali ambayo Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiyauliza, tatizo hili litaendelea kupungua kadri tunavyowaajiri Walimu wetu na tunao uhakika kabisa kuwa ifikapo mwaka 2014 tutakuwa tumepunguza kwa kiwango kikubwa upungufu wa Walimu nchini.

Mheshimiwa Spika, tuna uhakika pia kuwa idadi ya Walimu kwenye shule zetu za msingi na sekondari zitakuwa zimekaribia takwimu ambazo tunazitahitaji ambazo ni Mwalimu mmoja kuwa na wanafunzi 40 kwa shule za sekondari na Mwalimu mmoja kuwa na wanafunzi 45 kwa shule za msingi lakini lengo la Serikali siyo kufikia lengo hilo, mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kuwa tunakuwa na Walimu wengi wa kutosha ili waweze kupunguza mzigo mkubwa ambao wanao wa kufundisha na kusahihisha madaftari, lakini pia kufanya tathmini ya vijana wetu ambayo ni sehemu ya mitihani. Lengo kubwa hasa ni kumwezesha Mwalimu kufanya kazi yake vizuri aweze kufanya kazi ile kwa urahisi lakini pia kwa viwango vizuri vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge nao walichangia eneo la uchakavu wa miundombinu mbalimbali kwenye shule zetu za msingi na sekondari ambapo jambo hili tunaendelea kuliandaa vizuri na uchakavu huu ni kweli tunazo shule 3425 za Serikali nchini kati ya hizo tuna shule zetu mpya 3337 zilijulikanazo kama shule za sekondari za kata. Kati ya shule 3425 tunazo shule kongwe ambazo miundombinu yake sasa imechoka, majengo hali siyo nzuri, mifumo ya maji taka na maji safi imeharibika sana, vyoo na hata majengo yake yamechakaa.

Mheshimiwa Spika, mkakati ambao tumeuweka Ofisi ya Waziri Mkuu tukishirikiana na Wizara ya Elimu ni kuendelea kuzitengea fedha kwa ajili ya ukarabati wa shule hizo na tumeendelea kufanya hivyo kuanzia mwaka wa fedha 2009/2010, mpaka sasa na tumeshatuma zaidi ya shilingi bilioni 7.8 katika kipindi hiki cha miaka mitatu ili kuhakikisha kuwa miundombinu ya shule hizi inarekebishwa na kuweza kuzirejesha katika sura yake ya kawaida na mwaka huu wa fedha 2012 kufikia mwezi Juni, tumeshatuma shilingi bilioni 3.2 kwa shule 63 zile kongwe ili kuanza kuzirejesha katika uhai wake ziweze kuvutia mazingira mazuri ya kufundishia na kusomea kwa Walimu na wanafunzi pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mkakati endelevu ambao tunaendelea nao na tuna uhakika kuwa hali hii ya miundombinu itarejea katika hali yake ya kawaida. Bado tunaendelea kwa kuwa mwaka huu tumetenga shilingi bilioni 56.2 ambazo tunazipeleka katika Halmashauri zetu na tumetaka tukamilishe angalau shule mbili na kila shule tuweze kujenga nyumba mbili

za Walimu, vyumba vinne vya madarasa, tuwe na maabara moja, tuwe na maktaba lakini pia tuweze kuweka umeme ambazo ziko kwenye mtandao wa umeme kama hakuna tutaweka *solar* na kuweka matanki ya maji kwenye shule ambazo haziko kwenye *line* ya mabomba, tutajenga vyoo nane (8) vya wanafunzi kwa shule hizo mbili. Kwa hiyo, kila shule itakuwa na miundombinu hiyo na tumeshazitaja tayari na Waheshimiwa Wabunge wanazo orodha ya shule hizo. Kwa hiyo, tunaamini baada ya kukamilisha kupitisha bajeti ya Wizara ya Elimu lakini tukikamilisha kikao hiki cha Bunge na kuridhia matumizi ya fedha, tutaanza kupeleka katika kila Halmashauri ili shule ziweze kuimarishwa miundombinu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama vile haitoshi bado tumeendelea kuhakikisha kuwa shule hizi zinasimamiwa vizuri na Walimu na Bodi zao na Kamati zao kwa shule za msingi na fedha hizi tunapozituma tunazipeleka moja kwa moja kwenye Halmashauri za Wilaya na zikifika, Mkurugenzi anazipeleka kwenye shule ya sekondari husika ili Bodi ifanye kazi ya usimamizi ili waweze kushiriki kikamilifu katika kuhakikisha kuwa fedha hizi zinatumika kama ambavyo zimekusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili, Mbunge wa Dodoma Mjini, Mheshimiwa Malolle aliweza kutoa takwimu kuwa ziko shule mbili za Mkoa wa Dodoma za Msalato na Bihawana, shule kongwe, ni kweli na hizi ni miongoni mwa shule 64 kongwe ambazo tumeziandalia fedha kwa ajili ya kuzikarabati. Kwa hiyo, tuna uhakika baada ya muda mfupi kadri tunavyokwenda shule hizi zitakuwa na mabadiliko

makubwa na zitakuwa na mazingira mazuri ya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado kwenye eneo la madarasa tunao upungufu mkubwa wa madarasa lakini pia tunao upungufu mkubwa wa nyumba za Walimu, tunao upungufu mkubwa wa maabara na maktaba. Tumeziagiza Halmashauri nchini kutenga bajeti zao ili tuweze kuboresha. Katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha wa 2012/2013, Halmashauri zetu nchini zimetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, kwa sekondari zimetengwa shilingi bilioni 27, kwa shule za msingi wametenga shilingi bilioni 14, kwa upande wa nyumba za Walimu wa sekondari nchini kwenye Halmashauri zetu wametenga shilingi bilioni 17 na shule za msingi shilingi bilioni 13. Kwa hiyo, hii ni njia ambayo tunaitumia kuagiza Halmashauri zetu kutenga kwenye bajeti na sisi Waheshimiwa Wabunge ni miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Madiwani katika Halmashauri zetu kwa hiyo, ni nafasi nzuri kwetu kusisitiza kuwa bajeti tuliyoipanga na fedha zinapopatikana ziende zikafanye kazi hii ili tuweze kupunguza tatizo la miundombinu ambalo tunalo kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wamekuwa wakizungumzia tatizo la madeni ya Walimu. Ni kweli kuwa madeni bado tunayo, madeni haya ya Walimu tunayo maeneo makuu mawili. Eneo la kwanza ni lile la malimbikizo ya mishahara ambalo Mwalimu hupanda daraja na kuwa na mabadiliko ya mshahara wake. Eneo hili utaratibu wake wa malipo unaratibiwa kwa ushirikiano na Wizara ya TAMISEMI,

Hazina na Utumishi. Tunaendelea kulipa kwa utaratibu ambao Hazina wanapeleka fedha zile katika mishahara ya Walimu moja kwa moja. Eneo la pili ni lile ambalo linajumuisha uhamisho, matibabu, masomo na likizo ambalo Mkurugenzi wa Halmashauri anawajibika kuhakikisha eneo hili linalipwa malipo yake kama ambavyo imewekwa. Lakini pia tunalo tatizo la Walimu kadhaa ambalo nimepata meseji kutoka kwa Walimu kwamba wanakosa mishahara yao wengine hawana mshahara wa mwezi mmoja mpaka miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili tumefanya ufuatiliaji wa kina kwa kufuatilia katika Halmashauri husika kitu tulichogundua ni kuwa Walimu wengi ambao kwa sasa wamerukwa na kompyuta ni wale Walimu ambao hawakuingia kwenye zoezi la uhakiki wa utumishi wao lakini kuna Walimu ambao wamerukwa kutokana na matumizi ya mfumo mpya wa *Lawson* ambao tunautumia kama mtandao wa kuratibu shughuli zote za malipo kutoka TAMISEMI kwenda Hazina ili kuweza kuhakikisha kwamba watumishi hawa wanapata mishahara yao.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo tumeagiza waimarishe malipo ya mishahara ya Walimu ambao wamerukwa ili kila Mwalimu apate stahili yake ya mshahara kamili badala ya kumkopesha kila mwaka. Kwa hiyo, tunaamini kuwa eneo hili baada ya kuimarisha utaratibu wetu wa mtandao huu wa *Lawson,* tutakuwa tumekamilisha ulipaji wa madeni ya eneo hili la mishahara ambayo imerukwa na eneo la madeni hayo mengine ambayo tulikuwa tumehakiki na

kulipa kwenye zile shilingi bilioni 52, yale tunaendelea kuyalipa na sasa hatua tuliyofikia ni nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la TAMISEMI ambako tulipewa shilingi bilioni 44, shilingi bilioni 25 zilizolipwa na Hazina taarifa tulizonazo, asubuhi nilikuwa ninazungumza na Naibu Waziri wa Wizara ya Fedha kuwa tayari walishaanza kuzituma katika Halmashauri kuwaingizia mishahara yao. Lakini kwenye eneo hili tulikuwa na shilingi bilioni 19 ambazo tulikuwa tunalipa kupitia kwenye maeneo haya ya uhamisho, matibabu, masomo na likizo.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili tumelipa zaidi 90% kwa sababu tulikuwa na Halmashauri tano (5) ambazo hatukumudu, walipelekewa fedha kidogo na kwa kupelekewa fedha kidogo hawakuweza kufanya zoezi la ulipaji. Kwa hiyo, tunaamini kwamba Hazina tumeshawaandikia barua na tumewataka wapeleke kwenye Halmasahuri zetu ili Walimu waweze kulipwa na tunaamini watalipwa. Ninataka niwasihi Walimu kuwa eneo hili tumesikia malalamiko makubwa lakini pia Waheshimiwa Wabunge leo wamelieleza vizuri, tutajitahidi kuhakikisha tunasimamia eneo hili ili kuondoa madeni ambayo yanajitokeza mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati ambao tumeuweka kwa sasa tumeagiza Halmashauri zote kuweka rejista ambayo itakuwa inarejista kadri madeni yalivyoingia kwenye Idara ya Elimu na watumishi wengine kwenye Halmashauri zetu. Lakini kwenye sekta ya elimu tumeshaagiza kuwa na mtumishi mmoja

ambaye atakuwa anashughulikia kuratibu madeni ya Walimu badala ya kuwa madeni yanaingia na Afisa Elimu anarundika.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru Mheshimiwa Majaliwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAMISEMI (ELIMU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninawashukuru sana, hakikisheni pesa hizi zinawafikia Walimu, hatuoni sababu watendaji wa Halmashauri wanalipwa na Walimu hawalipwi. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye hoja hii ambayo ni muhimu sana kwa mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla sijaanza kufanya hivyo, nitangulize kwa kusema kuwa ninaunga mkono hoja na ninawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri kwa kazi nzuri ambayo wanafanya na hasa kwa ushirikiano wao na ofisi yangu ya Mwanasheri Mkuu wa Serikali. Ninawapongeza sana Walimu na ninawaomba wajongee kwenye Kauli ya Ualimu Ustahimilivu Pamoja na Uvumilivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge ambao wamejitambulisha kama ni Walimu na wamezungumza kwa uchungu kuhusu haki za Walimu. Nina hakika kuwa michango ya Waheshimiwa Wabunge itatusaidia Serikalini kuboresha elimu ya kawaida ya watoto wetu pamoja na ile ya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Waheshimiwa Wabunge waliosema kwamba Serikali pamoja na Chama cha Walimu (CWT) warudi kwenye meza ya mazungumzo. Nimesimama kwa sababu moja, kwenye hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani ambaye amezungumza mara mbili, jana na leo, katika ukurasa wa 13 wa kitabu chake anasema kuwa kile kitendo cha Serikali kukimbilia Mahakamani ili kuepusha masuala yenye mvutano kama madai ya Madaktari na madai ya Walimu yasijadiliwe Bungeni, kunazidi kuzorotesha utoaji wa huduma katika sekta husika. Anaendelea kusema kusema, nanukuu:-

*"Aidha, ni kulihujumu Bunge haki yake kwa mujibu wa Ibara ya 63 (2) na (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayolipa Bunge haki na nguvu ya kusimamia na kuishauri Serikali. Huku ni kudumaza demokrasia na kwa maana hiyo ni kudumaza maendeleo,* kwa kuwa demokrasia huchochea maendeleo*".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwangwi wa maneno haya umesikika pia kutoka kwa baadhi ya Wabunge kutoka sehemu zote za Bunge hili, maneno haya yanahitaji kujibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaridhika kwa muda niliokaa Bungeni kwamba elimu ya uelewa wa mambo ya Katiba inahitajika kutolewa Bungeni pamoja na nje ya Bunge. Ninafahamu kuwa Waheshimiwa Wabunge wanauelewa mzuri wa dhana ya mgawanyo wa madaraka, dhana ya utawala wa sheria na dhana ile ya *checks and balances* ya mihimili ya dola. Bahati nzuri, watu wanaohusika, tunaowazungumzia na ambao nimetangulia kuwaomba kuwa na uvumilivu na ustahimilivu, ni wanataaluma na ni watu ambao wanategemewa na jamii na ambao mimi ninawaheshimu sana kwa sababu na mimi nimewahi kufundishwa na nimewahi kufundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ni mwajiri Mkuu na kama waajiri wengine, Serikali inapaswa kuzingatia sheria. Kwa kifupi migomo siyo haramu, migomo ni haki ya wafanyakazi kwa mujibu wa Sheria. Ni njia pekee ya kupitia vyama vyao kumshurutusha mwajiri kuboresha maslahi yao lakini mgomo wa maslahi, mgomo ambao tunazungumzia hapa, ni mgomo wa maslahi siyo mgomo wa mapunjo na huo mgomo unaruhusiwa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sheria zinazohusika ziko sheria tatu ambazo Waheshimiwa mimi ninaamini mnazifahamu. Sheria ya Mahusiano Kazini, Sheria ya Mamlaka ya Ajira na ile Sheria ya *Public Service Negoting Machinery Act* pamoja na Kanuni ambazo zimetungwa kwa mamlaka ambayo mlimpa Waziri. Katika utekelezaji wa sheria hiyo, kupitia kifungu cha 66 cha Sheria ya Mahusiano Kazini, Waziri ametunga

Kanuni ambazo mwajiri yeyote pamoja na Serikali anatakiwa kuzifuata, hizi hapa, ambazo ni *Employment and Labour Relations Code of Good Practice.* Ukitaka kuendesha mgomo, ufuate utaratibu fulani na pia Sheria hii ya *Labour Court Rules* ukiwa kwenye Mahakama ile unafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea hapo na kwa vile nimesema kuwa ule ulikuwa ni mgogoro wa maslahi na kisheria unaruhusiwa, ni kwamba imefika mahali hamkuelewana, hamkufikia muafaka, katika hatua hiyo hampigani ngumi. Hizi Kanuni zinasema mfanye nini na sisi Serikali tulichofanya, hatusemi na ninaomba nirudie, sisemi kuwa hao Walimu walikosea, sisemi hivyo kwa sababu tuko Mahakamani, ninachosema ni kwamba sisi tuliona mgomo ule utaleta athari kwa sababu utaratibu ni kwamba lazima ufanye mambo kwa nia njema, uzuie athari za mgomo na sisi tuliona kuwa kuna athari zitatupata kama Serikali, tukaenda kuomba Mahakama ikatukubalia. Kwa hiyo, hatukukimbilia Mahakamani kama mbumbumbu kwa Madaktari na kwa Walimu pia, lakini hii haimaanishi kwamba ule mlango wa mazungumzo umefungwa. Hapana! Mlango wa mazungumzo upo na tutaendelea kuzungumza na tunafahamu kuwa Walimu ni watu waelewa, tutakubaliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tena haki ya kugoma inaambatana na wajibu wa kugoma. Huwezi kuwa na haki peke yake na hii ni kwa pande zote, Serikali pamoja na huyu anayegoma. Kwa hiyo, ninafikiri kuwa ni vizuri mazungumzo haya yaendelee kama tulivyoshauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia, Bunge halina nafasi, narudia tena, Bunge halina nafasi, Bunge halina mamlaka ya kushiriki katika mchakato huu wa wafanyakazi kugoma. Ndiyo maana ya mgawanyo wa mamlaka, haya siyo mamlaka ya kwetu. Wabunge wengine ninazo habari kwamba wanashiriki kwenye vikao vya wafanyakazi, msiwapotoshe wafanyakazi. Kama utataka kuzungumza nao basi nakuomba usome sheria vizuri, uende pale umejiandaa, uwaeleze vizuri, lakini kusema tu na watu wengine wanakusikiliza, kuna watu ambao wanaelewa sana utaratibu huko nje kuliko sisi na akikusikia unavyozungumza anasema huyu Mbunge gani. Kwa hiyo, nawaomba Wabunge wenzangu tujue kwamba kama Bunge hatuna mamlaka hayo. Kuna Mbunge mmoja alifukuzwa kwenye usuluhishi, wenzake waliuliza, huyu nani, wakasema ni Mbunge, wakasema atoke, kama hatoki hatuendelei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mheshimiwa Mnyika, nafikiri amesema kwamba Serikali itoe tamko kwa wale watu ambao wamevunja Katiba, Ibara ya 4 na Ibara ya 107. *Rulling* ya Jaji imeandikwa kwa Kiingereza na nafahamu kama Mheshimiwa Mnyika anajua Kiingereza, hakutaja kama kuna watu wamefanya hivyo. Alichosema Jaji ni kwamba suala la kuamua nani mkosefu siyo la Serikali wala siyo la Chama cha Walimu. Kwa hiyo, alipoishia hapo maana yake ni kwamba mwende mkazungumze. Lakini tutazungumza kwa msingi mmoja kwamba tunazungumza, Wanachama wa Chama cha Walimu mnisikilize vizuri, kwamba tutazungumza *in good faith*, narudia, kwamba tutazungumza kwa nia njema na

nina hakika kwamba wenzetu pia watakuja kuzungumza kwa nia njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kupitia kwako narudia kuwaomba Wabunge, msijiingize kwenye mambo haya ya migogoro ya wafanyakazi. Wengine wanasema kwamba tuungane tuwe kitu kimoja, tuwatetee. Sasa Bunge hili ni Bunge la vyama vingi, haiwezekani, *otherwise* ingekuwa Upinzani wote wameunda Serikali ya Umoja, lakini Upinzani ni upande mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga tena mkono hoja, nakushukuru sana kwa kuniruhusu kuzungumza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana *Attorney General,* sasa namwita Naibu Waziri wa Elimu, una dakika zako 20 tu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu hii leo ili niweze kujibu hoja za Wabunge waliochangia katika hotuba za bajeti Kuu ya Serikali, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Hotuba ya Waziri Kivuli na Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iliyotolewa jana na Waziri wa Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii pia kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuniteua tena kwa mara ya pili kuendelea kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Hii ilionyesha imani kubwa ya Rais aliyonayo kwangu na ninaahidi kufanya kazi kwa umakini, uadilifu mkubwa na uchapakazi uliotukuka na wenye tija kwa Watanzania wote kwa kadri ya Mwenyezi Mungu atakavyoniongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa umahiri wake, kwa kuiongoza nchi yetu kwa amani na utulivu. Aidha, nampongeza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mohammed Gharib Bilal, kwa kumsaidia Rais kwa hekima na busara katika kutekeleza majukumu waliyonayo. Vilevile napenda kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kayanza Peter Pinda, kwa ufanisi wa kazi nyingi za kiserikali na majukumu makubwa aliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Spika, Naibu Spika, na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuliongoza Bunge lako Tukufu kwa busara na hekima kubwa kwa muda wote wa majadiliano ya hotuba za bajeti kwa mwaka huu wa fedha 2012/2013. Aidha, napenda kuwashukuru sana Wenyeviti wa Kamati za Bunge kwa ushirikiano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, napenda niwashukuru sana wapigakura wangu wa Jimbo la Songwe huko Chunya kwa ushirikiano wao mkubwa wakiongozwa na Katibu wangu Mkuu, Ndugu Agapto Kilongozi, Elias Ntemvi na Ndugu Mwashilindi kwa ushirikiano mkubwa sana wanaonipa. Hivyo, naahidi kuwatumikia ili kuleta maendeleo katika Jimbo letu na wao wanayaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, namshukuru mke wangu mpenzi Elizabeth Kirigha Mulugo na familia yangu kwa uvumilivu wao mkubwa katika kipindi chote wanachonikosa nyumbani kwa kazi na wanakosa mapenzi ya Baba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo, Waziri wangu mpendwa, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, nakiri kabisa nachota busara zake, upole wake na uvumilivu anaonipa na ushirikiano mkubwa anaonipa kwa kunituma kufanya kazi ya kuleta mafanikio ndani ya Wizara ya Elimu. Ananipa ushirikiano mkubwa sana wakati wote ninaofanyakazi naye. Ninajifunza mambo mengi sana kutoka kwake.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwashukuru Katibu Mkuu Mstaafu, Kaimu Katibu Mkuu, Kaimu Kamishana mpya wa Elimu, Wakurugenzi wote na Wakuu wa Taasisi za Elimu na watendaji wote wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa ushirikiano wao katika kuandaa bajeti hii. Pia namshukuru sana Dereva wangu, Ndugu Msafiri Mkuyawa kwa

kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa usalama mkubwa katika safari mbalimbali za kikazi hata kule Jimboni Chunya mbali sana. Nampongeza sana Dereva huyu kwa sababu anaendesha gari kwa umakini mkubwa, ni lazima tuwajali madereva wetu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie fursa hii kukushukuru tena na kumshukuru Spika, kwa kunipa nafasi ya kujibu hoja za Wabunge. Aidha, napenda niwapongeze Wabunge wote kwa kuchangia bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, mmekuwa mkitupongeza kwa kazi tunayoifanya, changamoto hazikosi, tunawaahidi kuendelea kuzifanyia kazi na kuwatumikia kwa moyo mnyoofu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hoja ninazotakiwa kutoa ufafanuzi hapa ni nyingi sana, nitatoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja na zingine tutazijibu kwa maandishi na kuwapatia Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nianze kujibu hoja moja baada ya nyingine. Mambo mengi ya kisera atayazungumza Waziri wangu, lakini mimi nijikite kuzungumzia mambo ya elimu ya msingi, sekondari, vyuo vya ualimu na *VETA* na baadhi ya taasisi kama Baraza la Mitihani, *NACTE* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Kassim Majaliwa ametoka kuelezea upungufu wa Walimu nchini, ndivyo hivyo lakini *source* kubwa inatoka kwenye vyuo vyetu vikuu

vyenye *program* za elimu na vyuo vya ualimu kwa *program* za Stashahada na Cheti. Tumejipanga kweli, kama ambavyo kila siku nimekuwa nikijibu maswali hapa kwamba vyuo vingi Tanzania, asilimia 90 ya vyuo vyote vina program ya elimu na vyuo vya Diploma na vyenyewe vinatoa kozi ya ualimu ambavyo mpaka sasa viko 103, vyuo 34 vikiwa ni vya Serikali. Kwa hiyo, tunahakikisha kabisa kwamba ndani ya miaka mitatu, tatizo la upungufu wa Walimu litakuwa limepungua kama si kuisha, tuna uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa Walimu wakishatoka Wizara ya Elimu tunawapanga kwenye Halmashauri, kwa hiyo, ni jukumu la Halmashauri ambapo Mheshimiwa Majaliwa yupo kule kuanza kuwapanga Walimu kwenye shule za sekondari na shule za msingi. Tumewaomba sana Ma-*DEO, REO* pamoja na Wakurugenzi watusaidie sana, wawapange Walimu sehemu zile ambazo hazina Walimu, kuliko Walimu kuendelea kurundikana sehemu za mijini na sisi tutapita huko kuhakikisha hiyo kazi inafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jenista Mhagama wakati akichangia siku moja na hata leo nimeona karatasi yake hapa anajaribu kuelezea uwiano wa *ratio* za Walimu na sisi Wizarani kwenye kikao cha menejimenti, tumeona ni kweli kabisa alichokuwa anakisema kwamba baadhi ya shule, yeye alisema Peramiho na hata sisi Wabunge tuna Majimbo yetu huko, baadhi ya shule zina wanafunzi pungufu sana unakuta shule nzima ya msingi ina wanafunzi labda 120 lakini ukienda katika *ratio* ya kiutalaam pale Wizarani tunapiga 120 gawa kwa *ratio* ya wanafunzi

Mwalimu mmoja awe na wanafunzi 40, kwa hiyom unakuta hiyo shule itakuwa na Walimu wanne (4).

Mheshimiwa Spika, sasa Walimu wanne hawawezi kufundisha darasa la kwanza mpaka la darasa la saba. Kwa hiyo, hilo tumeliona, tutaanza kugawa Walimu sasa kulingana na madarasa yaliyopo kwamba darasa la kwanza mpaka darasa la saba kuna masomo hayo, ni lazima tuwape Walimu bila kufuata ile *ratio* ambayo ilikuwa inatuchanganya kidogo. Tutafuata *ratio* kiutalaam lakini vilevile tutajenga hii hoja kwamba hii ni shule, ina darasa la kwanza mpaka darasa la saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite kuzungumzia Idara ya Ukaguzi ambayo Wabunge wengi mmechangia hapa namna ya kuimarisha Idara hii. Kwanza niahidi Bunge lako Tukufu kwamba tayari Serikali kupitia Wizara ya Elimu imeliona suala hilo na tayari kuna mchakato wa kuunda Idara ya Ukaguzi iwe kama Wakala ambao sisi binafsi tumeona kwamba itakuwa ni kitu kizuri sana ikijitegemea ili iwe na nguvu ya kisheria ya kwenda kuzikagua shule, kushauri na hata ikibainika hata kufunga, kuliko Waziri wa Elimu akipitia shule zipo nyingi sana. Sasa hivi shule za msingi zipo takribani 16,300, ambapo shule za sekondari zipo kama zaidi ya 4367.

Mheshimiwa Spika, hizi shule ukizijumlisha zinakuwa kama vile shule 18,000, peke yake Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa hawezi kuzikagua, peke yake Mheshimiwa Mulugo hawezi kuzitembelea kwa wakati. Kwa hiyo, hiki chombo tunapokiunda kitakuwa na mamlaka moja kwa moja ya kuzikagua na kutoa ripoti

ili ziweze kuwa na mafanikio. Kuliko labda hii ya sasa hivi kwamba shule zote unakuta ni shule za Serikali na ni shule za Katibu Mkuu, shule za msingi za mazoezi, Katibu Mkuu huyohuyo ndiye mwenye Wakaguzi anawatuma kukagua, kwa hiyo hata kama ripoti ikija mbaya mimi kama mwenye shule najitetea tu na siwezi labda hata kuzifunga. Lakini tukipata chombo ambacho ni mahsusi, kimekaa kisheria, kitaweza kufanyakazi kama inavyofanya kazi *EWURA* au kama inavyofanya kazi *NACTE, NECTA,* wanakuwa na chombo ambacho kina mamlaka ya kuweza kuwawajibisha moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Idara ya Ukaguzi mwaka huu kabla hatujafikia kuunda kiwe chombo, tumesikiliza michango ya Wabunge toka Bunge la mwaka jana na Bunge la mwaka huu tumeongeza bajeti kutoka shilingi bilioni tatu na nusu, tumefikia shilingi bilioni nne na nusu ili angalau Idara ya Ukaguzi iweze kupata hela za kuweza kutembelea hizi shule na kuzikagua. Kwa hiyo, tutakwenda kwa mfumo huo. Tuna hakika kabisa kwamba Idara ya Ukaguzi itakapofanya kazi kabla haijawa wakala itatusaidia kuweza kukagua nyaraka za elimu mbalimbali na kuona uendeshaji wa shule za binafsi na shule za Serikali na hata kuangalia ufundishaji wa Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mbunge mmoja alipokuwa anachangia hapa leo amesema kuna meseji za Walimu zinatumwa kwamba Mwalimu ameahidi kwamba yeye atakapofungua shule ataanza kufundisha 3x3 anaweka jibu ni 333, 1+3 anaweka jibu ni 13. Ni kazi ya Idara ya Ukaguzi kwenda

kuhakiki hayo kama kweli yapo ili tuweze kuchukua hatua. Nami niwahakikishie Wabunge kwamba mimi bado ni kijana, ni mwepesi, natembea, siyo mtu wa kukaa ofisini mara kwa mara, nitahakikisha natembea kuangalia Walimu wenye moyo wa namna hiyo. Kama kuna Mwalimu amesema kwamba atakwenda kufanya kazi hivyo, nikimkuta nitachukua hatua pale pale. Nikimkuta Mwalimu atakayekuwa anawafundisha watoto 7x7 anaweka jibu 7777 badala ya 49, naahidi kumchukulia hatua kwa sababu atakuwa amekiuka sheria ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuwa na Walimu wa mfumo huo, hata kama kuna mgogoro. *AG* ametoka kueleza namna ambavyo Serikali imeshughulikia mgogoro mpaka tumefika hapa na Waziri ameendelea kueleza hata juzi alieza namna ambavyo tutaendelea kukamilisha kulipa madeni ya Walimu. Sisi tutawajibika kuwalipa na tutawajibika kukaa nao na kuweza kuangalia migogoro inakwendaje, lakini siyo sasa iwe ndiyo kisa cha kutuharibia watoto wetu wa kitanzania ambao wanahitaji elimu madhubiti. Kwa hiyo, naomba Walimu watakapofungua shule, wafanye kazi hizi kwa uaminifu. Kazi ya Ualimu, *off course,* ni wito na mambo mengine yanaendelea kushughulikiwa na tutaendelea kuzungumza na CWT kama ambavyo Waziri ameahidi kuyafanyia kazi masuala hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala lingine la udahili holela wa wanafunzi wa kidato cha kwanza. Hili mimi nilishaliita nikasema ni janga la kitaifa. Nimefika Kigoma, Mbeya-Mbozi, tumewachukulia hata

hatua Walimu, Kigoma tumewaweka ndani Walimu 11 na Mbeya nilipofika nikamkuta Mwalimu mmoja naye nikamweka ndani na kesi iko Mahakamani na sehemu zingine katika nchi hii kuna wanafunzi wameingia sekondari ambao siyo haki yao. Wanafunzi wanakutwa mitaani pale basi baadhi ya Wakuu wa Shule wamefanya hivyo, wamewachukua wanafunzi, wanashirikiana na wazazi, wanaingiza wanafunzi kiholela, lakini Maafisa Elimu wapo kule, Ma-*DEO* wapo kule na Waratibu Kata wapo kule wanatakiwa kuangalia mifumo yote hii ya elimu inavyoendeshwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge na ninyi mkienda kule kwenye Majimbo mtusaidie kukemea haya. Mimi ninaahidi hapa kwenye Bunge lako Tukufu kama nilivyosema nitatembea nitafika huko na niliahidi kwamba nitakwenda Mwanza kwa sababu na kwenyewe kumetokea matatizo hayo, wanafunzi takribani 865 wamedahiliwa kuingia sekondari udahili holela na nina taarifa kwamba hata viongozi wa Elimu Mkoa na Wilaya wamehusika na ninajua hapa wananisikia. Nikimkuta *REO* amehusika namsimamisha kazi siku hiyohiyo, *DEO* kama amehusika namfukuza kazi siku hiyohiyo, nikimkuta Mratibu Kata amehusika namsimamisha hapohapo au awe Mwalimu Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hili kosa siyo kosa la kupeleka *TSD* wala siyo kosa la kinidhamu, kosa hili ni kosa la jinai kwa mujibu wa sheria ya Wizara ya Elimu ya mwaka 1978, Na.25. Huwezi kumdahili mwanafunzi kuingia sekondari ambaye hajateuliwa na Kamati ya Mkoa kuingia sekondari. Tunaposema hapa kwamba

tunataka ubora wa elimu *(Quality Education)* inatoka wapi kama tunaingiza watu holela sekondari? Wazazi, Walimu, Waratibu Kata, Ma-*DEO*, Maafisa Elimu wa Mikoa, Waheshimiwa Wabunge, mtusaidie kupiga vita suala hili, ni suala ambalo sasa limekuwa ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigoma kulikuwa na wanafunzi 493, leo Kanda ya Ziwa Mkoa wa Mwanza, Mara, Kagera, Geita kuna wanafunzi 865. Suala hili ni kubwa na tukiliachia hivi bila kuchukua hatua mwaka kesho litakuwa kubwa zaidi. Kwa hiyo, mimi ninawaahidi watu wa Mwanza kwamba baada ya kumaliza Bunge nitakwenda Jimboni kidogo nikatembelee Jimbo langu lakini mwezi wa Tisa mwanzoni nakwenda Mwanza, Kagera, Magu, Geita, Shinyanga nitafika Tabora mpaka Singida kuhakikisha hili suala ninalimaliza na wale wote ambao wamefanya hili wakae mkao wa kula ninakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika zinayoyoma lakini nizungumze tu kwa kifupi kuhusu suala la udanganyifu wa mitihani. Hili nalo ni kero kubwa sana katika Taifa letu. Wote tunatembea hapa tunaenda nchi za Afrika tunaona, suala hili wenzetu wanalikomalia kweli, lakini sisi Tanzania hapa hata wanafunzi wakifanya udanganyifu wa mitihani basi tunaona kwamba ni kitu cha kawaida, hiki siyo kitu cha kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge mlipokuwa mnasoma shule za msingi miaka ya themanini na miaka ya sabini, hebu angalieni tulivyokuwa tunaheshimu na kuliamini Baraza la Mitihani, angalieni

tulivyokuwa tunaheshimu ile mitihani, hata ikifika kule Kijijini usiku inalindwa na Polisi. Wale Walimu Wakuu walikuwa wanaaminika kweli, lakini leo hii suala la udanganyifu baadhi wamekuwa siyo waaminifu na udanganyifu huu labda niseme hapa kwamba hautokei kwenye Baraza la Mitihani kwa sababu kule ndiyo kunaitwa kuvuja kwa mitihani, *NECTA* tumeshadhibiti. Nampongeza sana Mama Ndalichako amedhibiti kweli udanganyifu pale Baraza la Mitihani. Kumbe wanawake wanaweza! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yule Mama amedhibiti mitihani, toka amewekwa pale sijasikia uvujaji wa mitihani ndani ya Baraza la Mitihani, lakini wizi wa Mitihani unatokea mashuleni, unatokea madarasani, Walimu wanashindwa kusimamia vizuri. Walimu wanawapa majibu wanafunzi. Nimemwomba Mama Ndalichako afanye namna yoyote mwezi wa kumi na moja kwenye Mkutano wa Bunge lijalo, nimemwagiza aje hapa atoe semina kwa Wabunge wote muone namna Baraza la Mitihani linavyoendeshwa na jinsi mitihani inavyovuja, labda hata Wabunge mpate hiyo elimu itatusaidia sana mkienda kwenye Majimbo mkaelimishe wapigakura wetu na wananchi kwa ujumla. Lakini vinginevyo suala la udanganyifu wa mitihani si suala la kuliangalia kama tunavyoliangalia kiurahisi. Mwaka kesho sijui kama litatokea lakini tuombe Mungu lisitokee ni suala ambalo kwa kweli halipendezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto 9600 kufutiwa matokeo na sheria inatutaka tufute matokeo, sasa Wabunge tukifuta wanasema ooh, tusifute. Wabunge

mnapendekeza hivi lakini sheria zinatutaka tufanye hivi na sisi ndiyo tunaotunga sheria hapa. Lakini mimi niseme kwamba suala hili likitokea tena tutaendelea kuwawajibisha wale wote wanaohusika. Nashukuru Waziri kesho atatoa kauli ya Serikali hapa, tuliahidi kwamba tutatoa kauli muone namna tulivyolishughulikia suala hili, namna tulivyounda Tume, tukapata majibu na tukawachukulia hatua wale Walimu Wakuu na wasimamizi waliovujisha hii mitahani kwenye ngazi ya shule. Kitu ambacho kilikuwa kimebakia ni zile shule za *private*. Sisi kwenye Serikali tumeshawawajibisha, nimemuagiza Kamishna wa pale Wizarani kwangu awaandikie barua Mameneja wa shule za binafsi na wamiliki na wao wawawajibishe Wakuu wao wa shule na Walimu Wakuu. Kwa sababu kama sisi kwenye Serikali tumeshawawajibisha Walimu wetu ngazi ya shule, halafu kule nako kuna Mwalimu Mkuu wa shule ya *private* naye watoto waliibia mitihani na yeye alichangia na yeye awajibishwe.

Mheshimiwa Spika, nitakapoona hakuna Mkuu wa Shule ambaye amewajibishwa kwenye shule za *private,* tutawanyang'anya udahili, hatukufungii shule, lakini tunakuandikia barua usidahili wanafunzi wa *form one* mwaka 2013. Kwa hiyo, Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti wa *TAMOSCO* yupo hapa, Bwana Mboka Mwambusi, unaniangalia hapa na wewe ukaongee na wamiliki wa shule zote Tanzania Bara, wawachukulie hatua Walimu waliovujisha mitihani ngazi ya shule zenu za *private*. Hii mimi itanifariji na tunaona kwamba tunaisaidia Serikali katika kudhibiti udanganyifu wa mitihani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mihula ya shule, Mheshimiwa Mama Margaret Sitta amechangia hili, Mheshimiwa Hokororo, Mheshimiwa Martha Mlata na wengine wengi tu wamechangia suala hili. Suala hili kweli Serikali imeliangalia na imeona ni hoja ya msingi kabisa na tumemwagiza Kamishna tukimaliza Bunge tu hapa apelike Waraka kwa Ma- *REO* na Ma- *DEO*, mwaka 2013 turudi kama ilivyokuwa mihula ya zamani, tumeona *effect* yake ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu hawa wa sayansi ambao ndiyo wanakuwa wachache muda mwingi unakuta wanasimamia mitihani na kusahisha mitihani. Tumesema turudishe mihula iwe miwili, mwezi wa sita watoto wanapokwenda likizo ndipo Walimu wakasahihishe mitihani ya Taifa, mwezi wa kumi na mbili kukiwa na likizo ndipo watu wakasahihishe mitihani ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuanzia mwaka 2013, mihula ya sekondari itabadilika, mtihani wa kidato cha nne utafanyika Novemba kama ilivyokuwa zamani badala ya Oktoba, mtihani wa kidato cha sita utafanyika mwezi Mei pamoja na Diploma kama ilivyokuwa zamani. Tumeshafanya mawasiliano na watu wa *NACTE* na watu wa *TCU* namna yaku-*select* wanafunzi kwenda vyuo vikuu wamesema haina athari, ili Walimu hawa wabaki waendelee kufundisha mashuleni, tunakosa Walimu kwa sababu wengi wanazunguka kwenye kusahihisha na kusimamia mitihani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo tumeliona, ni kitu ambacho kitafanikisha Walimu waweze kubaki kwenye shule wafundishe. Kwa sababu mitihani ya *form six* inafanyika mwezi pili, sasa mwezi wa pili watu wako madarasani, wanasimamia wiki tatu, mwezi wa tatu wanaenda kusahihisha wanakaa kule, wakirudi mwezi wa nne wanakwenda *midterm,* mwezi wa tano wanaenda kusimamia mitihani ya *Diploma* ya ualimu, mwezi wa sita wanaenda kusahihisha. Kwa hiyo, unakuta Walimu walikuwa wanazunguka hivi. Tukiweka mihula miwili itasaidia sana na ili mambo yaweze kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa vyuo vya *VETA*, tumeshaongea kwamba mwaka huu tayari Wizara imepanga tunazo shilingi bilioni nne (4) za kuanza angalau kila Wilaya ambapo tumechagua Wilaya nne (4) tuanze kuweka shilingi bilioni moja moja, tuanze angalau ili na mwaka kesho tumalizie. Lakini nilikuwa naomba nitoe wito kwa wananchi wote kwenye hizo Wilaya ambapo vyuo hivyo vitaanza kujengwa kwa mwaka huu wa fedha, Wilaya ya Namtumbo, Wilaya ya Kilindi, tumeenda Kikanda, Wilaya ya Chunya na Wilaya ya Ukerewe, fedha hizi zitaenda huko, lakini tumesema wananchi watusaidie kama ambavyo tulijenga shule za Kata, mawe, tofali, mchanga kama wapo karibu wananchi wa maeneo yale watusaidie, kwa sababu kujenga chuo kimoja cha *VETA* pamoja na karakana zote ni shilingi bilioni sita (6), Serikali pekee yake tutakuja kufika hapa mpaka Bunge la mwaka 2015 hatujamaliza baadhi ya Wilaya ambazo tumezi-*target*. Kwa hiyo, naona wakitusaidia gharama itapungua kidogo. Tukiweka angalau shilingi bilioni mbili

kila chuo tutaweza, Serikali sasa hivi itoe shilingi bilioni moja na Halamshauri kule wanakowachangia kwenye Wilaya husika ili na mwaka kesho twende kwenye hatua zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala lingine watu wamechangia hapa juu ya *TSD* kwamba Mwalimu anahangaika kwamba aende wapi, mara sijui TAMISEMI mara Wizara ya Elimu, mara Utumishi, Mwalimu sasa anahudumiwa na nani? Mheshimiwa Waziri atakuja kulifafanua vizuri lakini kwa haraka haraka tu ni kwamba kipo chombo ambacho Serikali imesharidhia kiundwe, *Teacher's Professional Registration Board* ambayo itamhudumia Mwalimu na kitakuwa Wizara ya Elimu pale. Kwa hiyo, baadhi ya *functions* za *TSD* zitakuwa huko ili Mwalimu aweze kuhudumiwa vizuri. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kengele ya mwisho?

**MWENYEKITI:** Ndiyo, ya mwisho.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo baadhi ya maeneo angalau nimechangia lakini Mheshimiwa Waziri atakuja kufafanua zaidi. Nawashukuru sana, naungana mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa mwenye dhamana, Waziri Kawambwa, Waziri wa Elimu, una dakika arobaini.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuweza kufanya majumuisho ya hoja yangu baada ya michango ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitangulize kuanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye ameniwezesha mimi kuweza kusimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu kujadili kwa kina hoja hii ya Wizara ya Elimu. Michango ilikuwa mingi sana, wengine wamepata nafasi ya kuzungumza lakini wengi wamechangia kwa maandishi na niseme kwamba katika michango hii muhimu tumeisikiliza kwa makini na tutahakikisha kwamba tunaifanyia kazi hivyohivyo kwa umakini na kwa uadilifu kwa sababu hayakuzungumzwa tu kwa maneno lakini yamezungumzwa pia kwa hisia kubwa. Kwa hivyo, ukichanganya zile hisia ambazo zilikuwa zinazungumza na umuhimu wa michango hii, sisi tunaliahidi Bunge lako Tukufu kwamba tutayafanyia kazi kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo ada lakini kabla sijataja majina ya wale ambao wamechangia, nitaomba kwanza kwa sababu ni jana tu tumemaliza zoezi hili la kumchagua Mbunge wetu katika Bunge la Afrika, nimpe hongera nyingi sana Mheshimiwa Saidi Mtanda kwa kushinda katika uchaguzi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona nimpongeze rasmi kwa sababu alikuwa ndiye Meneja wa Kampeni ya Mbunge wa Bagamoyo mwaka 2005. Ndiye aliyeniwezesha kufika hapa Bungeni kwa ushirikiano wa wananchi wa Bagamoyo kwa hivyo, nampa sifa sana kwa kufanikisha hili leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa kama ilivyo ada nitaje majina ya wale ambao wamechangia kwa kuongea na wale ambao wamechangia kwa maandishi. Naanza kwa kuwatambua Mheshimiwa Martha Mlata ambaye amemwakilisha Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Huduma ya Jamii, Mheshimiwa Susan Lyimo, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Josephine Chagula, Mheshimiwa Agness Elias Hokororo, Mheshimiwa Maulidah Anna Komu, Mheshimiwa Thuwayba Muhammed, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mheshimiwa Rashid Ali Omar, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Sylvester Mabumba, Mheshimiwa Dkt. Anthony Mbassa, Mheshimiwa Mary Chatanda, Mheshimiwa Abia Nyabakari, Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina, Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mheshimiwa Ezekia Wenje, Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mheshimiwa Rachel Mashishanga Robert na Mheshimiwa Mch. Luckson Mwanjale. *(Makofi)*

Wengine Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mheshimiwa Maryam Msabaha, Mheshimiwa Betty Machangu, Mheshimiwa

Prof. David Mwakyusa, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Zabein Muhita, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Azza Hilal Hamad, Mheshimiwa Saidi Mtanda, hawa wawili watakuwa wameandikwa bila ya kuchangia, naomba nifute majina hayo mawili yaliyotajwa, Mheshimiwa Azza Hilal Hamad hakuchangia kwa kuzungumza wala Mheshimiwa Saidi Mtanda. Mheshimiwa Dkt. David Malolle na Mheshimiwa John Mnyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niwatambue wale waliochangia kwa maandishi nao ni Mheshimiwa Abdulsalaam Amer, Mheshimiwa Aden Rage, Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina, Mheshimiwa Desderius Mipata, Mheshimiwa Moza Saidy, Mheshimiwa Stephen Wasira, Mheshimia Amina Andrew Clement, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Agnes Hokororo, Mheshimiwa Albert James Mtangi, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mheshimiwa Anna MaryStella Mallack, Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mheshimiwa Augustino Masele, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Charles John Mwijage, Mheshimiwa Christina Mughwai na Mheshimiwa Christowaja Gerson Mtinda. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Clara Mwatuka, Mheshimiwa David Silinde, Mheshimiwa Desderius Mipata, Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya, Mheshimiwa Dkt. Anthony Mbassa, Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu, Mheshimiwa Dkt. Haji Mponda, Mheshimiwa Dkt.

Terezya Huvisa, Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, Mheshimiwa Dkt. David Malolle, Mheshimiwa Eng. Athumani Mfutakamba, Mheshimiwa Eng. Gerson Lwenge, Mheshimiwa Eng. Ramo Makani, Mheshimiwa Ester Matiko, Mheshimiwa Ezekia Wenje, Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Gregory Teu, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Hamoud Jumaa, Mheshimiwa Hussein Mzee, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Mheshimiwa Josephine Chagulla, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa Livingstone Lusinde na Mheshimiwa Lolesia Bukwimba. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mheshimiwa Mansoor Shanif, Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi, Mheshimiwa Maryam Msabaha, Mheshimiwa Mary Chatanda, Mheshimiwa Maulidah Komu, Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Meshack Opolukwa, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mheshimiwa Munde Tambwe, Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan, Mheshimia Mustapha Akunaay, Mheshimiwa Mwanamrisho Abama, Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mheshimiwa Namelock Sokoine, Mheshimiwa Nassib Suleiman Omar, Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid,

Mheshimiwa Ester Matiko, Mheshimiwa Omary Badwel na Mheshimiwa Pindi Hazara Chana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Rashid Ali Omar, Mheshimiwa Rebecca Mngodo, Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Mheshimiwa Said Suleiman Said, Mheshimiwa Saleh Pamba, Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mheshimiwa Susan Anselem Jerome Lyimo, Mheshimiwa Ummy Ali Mwalimu, Mheshimiwa Yussuph Haji Khamis na huyo ndiyo wa mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uwezekano wa Wabunge kadhaa wamekosekana katika orodha hii ya wachangiaji hasa katika wachangiaji wa maandishi. Naomba nikiri makosa hayo na kwa vile bahati mbaya sana wataalamu wangu hawakuweza kuikamilisha orodha hii kwa wakati kwa hivyo imenisababishia kwamba nimekosa kuwataja baadhi ya Waheshimiwa. Wale ambao wataweza kuniwasilishia harakaharaka basi baada ya majumuisho haya nitajitahidi niweze kuwatambua ama pengine kwa bahati nzuri ofisi itaniwasilishia hapahapa haraka kabla sijamaliza majumuisho ili niweze kukamilisha majina kuwatambua wale wote ambao wamechangia kwa kusema na wale ambao wamechangia kwa kuandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba michango ni mingi, kwa hivyo bila shaka hatutaweza kuijibu au kuitolea ufafanuzi michango yote, lakini nilihakikishie tu Bunge lako Tukufu kwamba michango yote hii ile ambayo tutaitolea ufafanuzi hapa na ile ambayo tutashindwa kuitolea ufafanuzi

hapa, yote tutayatolea ufafanuzi ama majibu kwa maandishi na kitabu kile cha majibu tutakigawa kwa kila Mheshimiwa Mbunge, tutajitahidi sana ikiwezekana kabla ya kuondoka lakini wasiwasi kwa sababu muda mchache pengine tutawasilisha katika Bunge lijalo ama kabla ya Bunge lijalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kufafanua baadhi ya hoja hizi na nitaanza na hoja zile ambazo zimewasilishwa na Kamati yangu ya Huduma za Jamii, nitatoa ufafanuzi wa hoja ambazo zimewasilishwa na Kambi ya Upinzani na muda ukiruhusu basi nitaenda katika hoja moja moja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hoja ambazo zimewasilishwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, kuna suala la mfumo wa kuhudumia Walimu nchini kwamba wana vyombo vingi zaidi ya kimoja hivyo kusababisha adha nyingi. Suala hili linashughulikiwa kupitia Ofisi ya Rais, Menejimeti ya Utumishi wa Umma na tayari Rasimu ya Waraka wa Sheria ya kuanzisha Chombo cha Maadili ya Walimu umeshawasilishwa kwa Mwanasheria ili irekebishe Sheria Na. 25 ya mwaka 1978 na Sheria Na. 8 ya Utumishi wa Umma ambazo zina vifungu ambavyo vinakinzana na uanzishwaji wa chombo hiki. Tutasimamia suala hili kikamilifu ili kuhakikisha kwamba tunaunda chombo ambacho kitasimamia maslahi ya Walimu na taratibu zao pamoja na zile za kitaaluma ili madhila ambayo Walimu wameyalalamikia mengi yaweze kupata ufumbuzi katika utaratibu huu mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni malipo ya madeni ya Walimu nchini na Kamati ilihoji vifuatavyo, kwamba taratibu za malipo ziwekwe wazi, taratibu za madai zilivyofanyika ziwafikie wahusika na fedha za utekelezaji wa malipo ya madeni ambazo hazijatumika ziwekwe wazi. Napenda kulitolea ufafanuzi jambo hili ifuatavyo na kwa bahati tumetanguliza taarifa kamili kwenye vijitabu hivi ambavyo vimesambazwa leo asubuhi katika kila meza ya Mbunge. Kijitabu hiki kinasema kwamba, ni tamko la Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuhusu hali ya ulipaji madeni ya Walimu.

Mheshimiwa Spika, kijitabu hiki kinatoa kwa ukamilifu kabisa taratibu nzima ambayo imefanywa kwa ajili ya kulipa madeni ya Walimu kama vile ambavyo yamewasilishwa Serikalini na katika kijitabu hiki kimetangulia kusema kwamba hoja hii ya madeni ya Walimu iliwasilishwa rasmi mwezi Juni mwaka 2011 mwaka jana na kupitia vyombo vya habari na Chama cha Walimu kilisema kwamba kinakidai Serikali ama wanachama wake wanaidai Serikali jumla ya shilingi 29,237,007,865 haya ndiyo madeni ya Walimu yote. Sasa sisi upande wa Serikali tukasema kwamba Chama cha Walimu badala ya kuyaeleza haya katika vyombo vya habari, ni bora Chama cha Walimu kikae na Serikali kikamilifu ili tuweze kuainisha madeni haya ili kuwa na uhakika kama hiyo shilingi bilioni 29 ni chini ya hapo au ni juu ya hapo kwa sababu haya ni maisha ya watu ambao ni watu muhimu sana katika maisha yetu. Hatuwezi tukayaweka haya yakawa ni hoja ya siasa katika majukwa na vyombo vya habari, haiwezekani.

Wala hii sio namna ambavyo tunaweza tuka-*deal* na matatizo ya Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, Serikali, kwa nia thabiti kabisa ikaita Chama cha Walimu, tukae kitako kuhusu madeni ya Walimu na Serikali ikaunda Kamati ya Makatibu Wakuu na Kamati hii ya Makatibu Wakuu ilihusisha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Umma, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Chama cha Walimu Tanzania na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Kwa hivyo, ni jopo kubwa zaidi, lakini cha umuhimu zaidi ni kwamba, Chama cha Walimu wenyewe wakawemo, kwamba hizi shilingi bilioni 29, lazima tuzihakiki ili kama ni deni ambalo linahitajika kulipwa, basi lilipwe kwa ukamilifu wake, ili Walimu tuwaondoshee madhila haya ya kuidai Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawashukuru sana Chama cha Walimu walikubali kukaa chini na jopo kubwa hili na tukahakiki madeni yale ama tukayapitia. Vithibitisho vilivyoletwa vikaonekana kwamba, havitoshi. Chama chenyewe, kilikubali kwamba, havitoshi, havikidhi haja na havileti uhakika kwamba hayo ndio madeni ya Walimu. Kwa pamoja Chama cha Walimu Tanzania, pamoja na Serikali, tukaingia katika mlolongo sasa wa kuyatafuta madeni halisi ya Walimu na mchakato huo sasa, kwa kujibu suala hili la Kamati yangu, mchakato huo ukazaa madeni ya Walimu kwamba sio ile shilingi bilioni 29 lakini ni shilingi bilioni 52,053,314,237/= karibu mara mbili ya fedha

ambazo Chama cha Walimu kilisema kwamba Walimu wanaidai Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali kama ingekwenda tu papara kwenye gazeti ikasema sisi tunalipa hizo shilingi bilioni 29, tatizo la Walimu lingekuwa halijaondoka kwa sababu deni lile halikuwa shilingi hizo, lilikuwa zaidi ya pesa hizo karibu mara dufu ya pesa hizo. Kushughulikia matatizo ya Walimu, inabidi tushughulikie kwa ukamilifu, kwa unadhifu na kwa nia safi. Sio kwa hoja ya kutaka kujuliakana kwamba tunaongea zaidi au tunaweza kuongea kwa sauti kubwa. Wengine kama Shukuru Kawambwa, ameumbwa hivyo hawezi kuongea kwa sauti kubwa na kusimama kwenye majukwa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha muhimu ni utendaji kwamba kinachotakiwa ni kutenda; kama kuna deni lilipwe, lakini usiende ukasema tu, ukaliweka kule mbiombio kabisa, Serikali, ilipe shilingi bilioni 29, kumbe sio deni la Walimu. Nawashukuru kwamba Chama kimefanya kazi thabiti ya kukaa na jopo moja kwa moja, tukasema sasa shilingi bilioni hizi ni 52 na kati ya hizi shilingi bilioni 52 ambazo kazi yenyewe ni kubwa iliyoihusisha Kamati hii iliyoihusisha TAMISEMI, iliyohusisha Wizara ya Elimu na uhakiki kuweza kufanywa ndani ya Halmashauri zile, kwa kuwashirikisha Maafisa Elimu Mkoa, Afisa Elimu Wilaya na Wakaguzi Kanda, Wakaguzi Wilaya, wote hawa wameshiriki katika kuyafafanua madeni haya; ni jambo ambalo limefanywa kwa kina mpaka Chama cha Walimu Tanzania, kikaridhika kwamba sasa hapa tumefika mahali pazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalisema hili makusudi baada ya kusema shilingi bilioni 52 ili kuondosha hoja ambayo inasemwa kwamba, madeni ni mengi, sio haya. Hii kazi imefanywa kwa ukamilifu na kwa kuhusisha *parties* zote na katika shilingi bilioni hizi 52, shilingi bilioni 29,367,525,809/= haya ni malimbikizo ya mishahara na shilingi bilioni 22,685,788,427/= haya ni malimbikizo yasiyokuwa ya mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ambayo tumeitoa inasema kwamba, pesa hizi za malimbikizo yasiyokuwa ya mishahara, Hazina imetoa pesa ile yote ili iweze kulipwa na Wizara lakini pia iweze kulipwa na TAMISEMI. Pesa yote hiyo imetolewa na Hazina ili iweze kulipwa kwa Walimu hawa wote. Kwa hivyo, tangu mwezi Januari 2012, wakati Wizara ya Fedha ilipotoa fedha hizi, mchakato wa malipo sasa ukaanza. Wizara ya Elimu, ikaendelea kulipa na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI ikaanza kulipa katika kila Halmashauri na kijitabu hiki ambacho kila Mbunge anacho pamoja na Mheshimiwa Sukum ambaye alihoji kuhusu Hanang, kinaonesha madai na malipo ambayo yamefanywa katika Wilaya yake na katika kila Wilaya ya mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikumbushe Bunge lako Tukufu kwamba hii ni kazi ya Chama cha Walimu Tanzania pamoja na Serikali kwa ujumla wake kila ngazi. Isije orodha hapa ambayo hata Chama cha Walimu wenyewe Tanzania haiwezi ikaikubali kwa sababu haikuingia kwenye orodha hii; tuliwaambia hatukubali shilingi 29, tunataka kujua madai ya kweli, tufanye kazi pamoja. Hawa watu ni watu muhimu, ni watu makini, lazima tuwafanyie kazi inayoendana na

hadhi yao katika nchi yetu. Hatuwezi kufanya kazi za magazetini, tufanye kazi ambayo inajibu masuala yao. Kwa hivyo, fedha hizi zimelipwa kama zilivyooneshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya hii shilingi bilioni 22 ambayo ni malimbikizo yasiyokuwa ya mishara, shilingi bilioni zile 29 ambazo ni za mishahara, zinalipwa na Hazina moja kwa moja kwa utaratibu wa *Pay Roll* kwa sababu ya mishahara ile ina makato yake, lazima Hazina ifanye makato yale yanayohusika pamoja na michango katika Mifuko ya Hifadhi ambayo inafanywa moja kwa moja, kwa hivyo, pesa hizi zimelipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba katika kulipa madeni haya kupitia Wizara ya Elimu na TAMISEMI, uhakiki ambao ulipita ulisababishia baadhi ya Walimu wakalipwa zaidi ya kile walichokidai na kuna baadhi ya Walimu ambao walilipwa pungufu ya kile walichokidai na kuna Walimu ambao walilipwa sawasawa na kile walichokidai. Hili la kulipwa zaidi ya walichokidai, mimi nilihoji kwa sababu kazi hii niliifanya mpaka kuhakiki na yale mafaili, wakati mwingine naenda hebu nione, kwenye orodha nakuta, nakumbuka mmoja ambaye nilikuta amedai shilingi 250,000/= lakini malipo shilingi 660,000/=. Nikauliza kulikoni? Nikajibiwa, katika kulipa utaratibu ni kwamba, Mkaguzi wa Ndani na Mhasibu wanahakiki lile deni lenyewe kabla hata hawajatoa *cheque.* Sasa kuna baadhi ya Walimu hawakutumia viwango stahiki wakati wanaweka madeni yao, kwa hivyo wale hawakuwa *penalized.* Kama umetumia viwango sio

vya stahiki yako, kwa ngazi yako imerekebishwa, kwa hivyo, sio kipapaya cha Serikali mtu atakapokuta amepata hela zaidi kushinda zile alizodai lakini kwa sababu ya marekebeisho ya stahili yake kwa sababu hakuiandika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nilijibu hapa hoja moja ambayo ilisemwa tena na Mheshimiwa Mbunge mmoja, Mbunge huyo alisema nimeidanganya Kamati kwamba ikifika tarehe 30 Juni, nitakuwa nimekamilisha malipo haya. Kwa upande wa Wizara na upande wa TAMISEMI na hasa Wizara mimi nikishirikiana na TAMISEMI, kwa upande wangu wa Wizara, nilihakikisha usiku na mchana tunalifanya kazi suala hili na ilipofika tarehe 30, kama inavyoripotiwa katika kitabu hiki, malipo yote yalikuwa yamekamilishwa kulipwa. Kwa hivyo, Waswahili kule Bagamoyo wanasema, *"Ada ya Mja Hunena, Muungwana Vitendo"* na mimi ni muungwana sana katika tabia yangu, siwezi kuidanganya Kamati, kwa nini niidanganye kamati? Kwa nia gani? Wakati na-*deal* na Walimu? Haiwezekani hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilikiri kwamba linaweza likawa ni madhila na hili tutaendelea kulifanyia kazi ni kwamba wapo katika hawa ambao, katika orodha hii ya shilingi bilioni 52, waliokutwa kwamba, pamoja na uhakiki ule wa kwanza, ilipokuja katika malipo, Mkaguzi wa Ndani akagundua kwamba, mbona *cheque* hiyo kwenye *file* ipo katika orodha ya malipo TAMISEMI? Nyingine ilikuwa malipo ambayo ni ya mwaka 2009 ambayo yalisimamiwa na *CAG* na vidhibiti vipo kwamba,

imelipwa hizohizo ambazo zimedaiwa pamoja na kwamba sasa hivi imefika mpaka *stage* hii ya mwisho. Haya malipo yangekuwa sio halali kwa hivyo baadhi ya watu hawatolipwa kwa sababu ya matatizo haya ambayo yametokea katika malipo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ni wachache kwa sababu katika zile shilingi bilioni 22 kwa mfano, ambazo zimelipwa na Wizara pamoja na TAMISEMI, katika shilingi bilioni 22, zaidi ya shilingi bilioni 17 zimeweza kulipwa kwa Walimu hawa shilingi bilioni tano (5) ndio zimebaki kwamba ama ameshalipwa ama zingine hazina vithibitisho vile ambavyo vinamwezesha yule Mkaguzi wa Ndani aweze kuthibitisha kwamba haya malipo yafanywe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijibu hoja ya Kamati lakini pia niwaambie Walimu kwa ujumla kwamba tumejipanga Serikalini, Wizara ya Elimu pamoja na TAMISEMI kushughulikia kila ambaye atakuwa hakuridhika na kile kilichotokea. Kuhakikisha kwamba tunakishughulikia mapema ili tumalize kabisa, hela tunazo na hatuna roho za korosho za kukataa kumpa mtu hela yake ikiwa taratibu za malipo zote zimekaa vizuri na tunataka tusikae nazo zile hela kwa sababu tukikaa nazo sisi zinaweza zikapata mtu ambaye atapita pale na kipapaya akazichukua.

Mheshimiwa Spika, naomba Walimu waniamini kwamba hela hizi zipo na kwa kila ambaye atakuwa malipo yake hayakufanywa, barua zinaenda kwa kila ambaye madai yake yalikuwa yamehakikiwa humu, ataenda kuambiwa, ataambiwa ni kwa nini hakulipwa

lakini pia kwenye *Website* ya Wizara ya Elimu pamoja na ya TAMISEMI, orodha nzima itawekwa pale ili tuwapunguzie shida. Kama itahitajika, basi tutatumia gharama nyingine kuweka kwenye magazeti ili Walimu kila mahali walipo waweze kusoma nani amelipwa na nani hakulipwa; ndio muamini kwamba jambo hilo tutahakikisha kwamba tunalichukulia kwa umuhimu wake ili tuondoshe kabisa madhila ya Walimu. Hatukubali manung'uniko ya Walimu kuhusu madeni na tutayafanyia kazi kikamilifu ili kuhakikisha kwamba madeni haya yote tumeyamaliza kama ambavyo sasa yaliyobaki ni kidogo sana kwa yale ambayo hayana mgogoro wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la posho ya Walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu. Hili tumelitafakari sana. Mwanzoni tulidhani tuende nalo harakaharaka, ili tuweze kulipa lakini tukajikuta kulikuwa na *dispute* nyingi kwamba ni nani ambaye yuko kwenye mazingira magumu? Kwa hivyo, hatukupata muafaka wa harakaharaka. Lakini namba mbili ikaja hoja kwamba tunapowalipa hawa ambao wanaripoti sasa hivi katika maeneo yaliyokuwa ya mazingira magumu, je, wale ambao walikutwa palepale inakuwaje? Kwa sababu, kuna Walimu ambao walishatangulia wapo pale na tunawalipa wale ambao wanaripoti sasa hivi, je, waliotangulia itakuwaje? Lakini ikaja hoja pia kwamba hapohapo ambapo Mwalimu anakwenda kwenye mazingira magumu lakini pia kuna watumishi wengine wa umma, yuko Daktari, yuko Muuguzi, yuko Afisa Ugani na kadhalika. Serikali hii ni moja, hawa inawafikiria namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba hili jambo tunalichanganua kwa upana wake na kwa ukamilifu wake wa kujua umuhimu wa watumishi wa umma mbalimbali ili tuhakikishe kwamba kuondosha kero kwa kada moja, haitengenezi kero kwa kada nyingine. Tutaomba uvumilivu lakini hili tutalifanyia kazi kwa ukamilifu ili tuhakikishe kwamba tunapolitolea usuluhisho basi tunalitolea usuluhisho kwa watumishi wote wa umma, kwa umuhimu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine linahusu kuongeza mafunzo ya *VETA* kwa kuboresha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na Serikali itoe taarifa kuhusu hatua za awali zilizochukuliwa. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imeandaa mpango mkakati kuimarisha vyuo 55 vya *FDC* ili vyuo hivyo vitumike katika uendeshaji wa mafunzo ya ufundi stadi na uimarishaji huo utahusisha ukarabati, kuweka vifaa, mafunzo kwa Walimu katika kutekeleza mafunzo hayo. Aidha, utekelezaji wa mpango huu utafanyika kwa awamu tatu ambapo mwaka huu wa fedha, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 67.7 kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ili kuimarisha vyuo 25 katika hiyo awamu ya kwanza. Tutaenda awamu kwa awamu ili kuhakikisha kwamba tunapanua mafunzo hayo ya *VETA.* Lakini pia mpango ule ujenzi wa Vituo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa kila Wilaya, nayo pia kwa mwaka huu tutajitahidi kuanza na vyuo vinne na Mungu akijalia mkopo ule wa Benki ya Maendeleo ya Afrika ukitoka kwa wakati, pengine ndani ya mwaka huu wa fedha basi utaimarisha ujenzi sio tu vyuo hivyo ambavyo

tumevitaja bali kwa wingi zaidi kwa sababu tutakuwa na hela nyingi zaidi kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni matumizi ya fedha za Rada kwamba yafanyike mapema. Nataka kusema kwamba mchakato huo sasa unaendelea. Tumemaliza michakato ya awali na kwamba pesa tumeshazipata na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, imepewa dhamana ya kufanya manunuzi, kwa hivyo, inakamilisha taratibu zote zile za kimanunuzi kwa yote yale ambayo tumeyapanga au kukubaliana kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Uingereza, kupitia *DFID,* kwa ajili ya kazi hii ya manunuzi kwa pesa za chenji ya rada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la Kamati, ni kuhusu Serikali itoe mwongozo mahsusi wa utekelezaji wa Sera ya Uchangiaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari ili kuwezesha shule kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Niseme tu kwamba, ushauri huu wa Kamati tumeupokea. Najua kuna upungufu katika suala hili kwa hiyo, tutaufanyia kazi ya uhakika ili tutoe miongozo mahsusi, kamilifu kwa maeneo yote ya msingi na sekondari, tuondoshe madhila ambayo wazazi wanayapata wakati hakuna mwongozo kamilifu kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya ugatuaji bado inakabiliwa na changamoto nyingi, hivyo Serikali, iipe uwezo Halmashauri. Ugatuaji huu ndio sasa tumeanza kuutekeleza. Tumeanza kuutekeleza kwa shule za sekondari mwaka 2009 kwa hivyo tuko katika hatua za kwanza za ugatuaji na sasa tunapata *experience*

mbalimbali. Tutaendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI ili tuone yale ambayo yananyima fursa ya mafanikio kupitia ugatuaji ili tuweze kuyaimarisha. Kama ni kuimarisha Halmashauri, kama ni kuimaisha TAMISEMI yenyewe, tufanye hivyo ili tupate mafanikio zaidi. Cha muhimu hapa ni kwamba sasa Mwalimu hahitaji kutoka Mwanza kuja Dar-es-Salaam, Makao Makuu ya Wizara ya Elimu, kulekule Mkoani kwake, palepale katika Halmashauri yake, huduma zote zinazoendana na maslahi yake anaishia palepale badala ya kuhitaji kwenda safari ndefu kuja mpaka Dar-es-Salaam kwa ajili ya kupata ufafanuzi au kushughulikiwa matatizo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu Idara ya Ukaguzi wa Shule Nchini iwe Taasisi inayojitegemea. Hili Naibu Waziri, amelizungumzia...

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni…

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, *Order Please, Order Please!*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu mfumo wa madai ya Walimu nchini, Serikali na *CWT,* waendeleze majadiliano kwa kuzingatia Sheria za Kazi. Ushauri huu wa Kamati ya Huduma za Jamii tumeuzingatia. Nashukuru kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikal, ameutolea ufafanuzi na Mheshimiwa Naibu Waziri ametoa ufafanuzi. Niseme tu kwa nia thabiti kabisa, kwa ushauri huu wa Kamati na ushauri ambao umetolewa na Wabunge mbalimbali, tutaenda

kwenye majadiliano kwa nia thabiti na nia nzuri ili kuhakikisha kwamba mgogoro huu wa Walimu na Serikali unaondoka. Cha muhimu hapa kama ambavyo Mwanasheria Mkuu amesema, wote sisi twende katika majadiliano yale tukiwa na nia thabiti za moyoni, nia njema za kutaka kuumaliza mgogoro huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni hoja ambazo nilidhani bora nizitolee ufafanuzi wakati huu ili kuweza kujibu hoja zile muhimu za Kamati. Najua Kamati ilikuwa na hoja zingine lakini kwa sababu ya muda, basi bora nijaribu kutoa ufafanuzi katika hoja zile ambazo zimetolewa na Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani alihoji kuhusu wanafunzi waliofukuzwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, *UDOM* na *MUHAS* kwamba warudishwe vyuoni mara moja. Naomba nitoe jibu la pamoja kwamba suala hili la wanafunzi waliofukuzwa katika vyuo vikuu na vyote hivi vitatu ambavyo nimevitolea mfano na naomba nilikumbushe Bunge lako Tukufu kwamba Bunge hili ndilo ambalo linatunga sheria na ndilo ambalo limetunga Sheria ya Vyuo Vikuu na ndani ya Sheria ya Vyuo Vikuu, Sheria Na.7 ya mwaka 2005, imetoa maelekezo ya kila chuo kuandaa Hati Idhini yake ama *Charter* ya chuo.

Mheshimiwa Spika, *Charter* ya chuo ndiyo mwongozo wa kila chuo kikuu kwamba uendeshaji wa chuo utaendana na *charter* hiyo na ndani ya *charter* uongozi wa kiutawala umeainishwa, taratibu za kinidhamu zimeainishwa na taratibu nyingine zote ambazo zinahakikisha kwamba kuna utoaji wa elimu

bora katika vyuo hivi zinaainishwa. Sasa hili ni jambo ambalo linakwenda moja kwa moja chini ya taratibu za Hati Idhini ya vyuo na taratibu za kinidhamu. Kwa hiyo, wale ambao wameathirika katika tatizo hili ni kwamba wameathirika kwa sababu ya kuchukuliwa hatua na vyuo husika na wala hapa hakuna mwingiliano wa chombo chochote kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nisema kwamba hata pale iliposemwa kwamba taratibu za kuwachukulia nidhamu zimebagua makundi, hizi ni hisia tu lakini utaratibu ule na Kamati za Nidhamu ambazo zinaanza tangu ngazi ya Vitivo mpaka Kamati yenyewe ya Nidhamu mpaka mwisho Baraza la Chuo, majopo yote hayawezi kuwa kazi yao ni kuhakikisha kwamba wanakandamiza kundi fulani na hilo ni kundi gani basi si bora lingetajwa ikaeleweka kwamba kundi lipi hilo ambalo lilikuwa limenyongeshwa? Kwani si mnalifahamu, bora ulitaje ili Waheshimiwa Wabunge tuweze kulijua kama ni kundi gani katika kundi lile la wanafunzi ndiyo ambalo limebaguliwa. Naomba niseme kwamba kazi iliyofanywa ilifanywa kwa ukamilifu bila ubaguzi wowote lakini kwa kufuata Hati Idhini ya vyuo husika na hii imefuatana na sheria ambazo Bunge hili Tukufu imeziweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahisi kwamba muda hautanitosha kupitia hoja zote lakini naomba niende mpaka pale ambapo nitakuwa nimeishiwa na muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni wahitimu wa vyuo vikuu kunyimwa vyeti wakiwemo wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutokana na mikopo

kutowasilishwa vyuoni. Nitoe maelezo kwamba suala hili la wanafunzi kukosa vyeti vyao limewahusu Chuo Kikuu cha Dodoma lakini pengine ingeweza kuwahusu *MUCCOBS* na pia *IFM*. Lakini *IFM* na *MUCCOBS* halitawapata hilo kwa sababu siyo miongoni mwa wale ambao wamehitimu sasa na watakapohitimu mwakani suala lao limeshachukuliwa tayari na Serikali imelibeba na kwamba hatutaruhusu vyuo kuwanyima vyeti kwa sababu pesa zao Serikali imechukua jukumu kwamba italipa lakini hawa ambao wamehusika mwaka huu moja kwa moja ni wale ambao walikataa kusaini *form* zao za mikopo na hili tunalisema kwa uhakika, ni baadhi yao, kwa nini wasiwe wote sasa?

Mheshimiwa Spika, walipoambiwa wasaini *form* za mikopo wakakataa kwa kutegemea kwamba mikopo ile ni ruzuku na siyo mikopo na kama hawakusaini hakukuwa na haja yoyote au kithibitisho chochote cha kuweza kuwadai watakapokuwa wamemaliza masomo yao. Sasa utaratibu uliokuwepo ni kwamba kama fedha haikulipwa basi ni lazima irudi Bodi ya Mikopo na Bodi ya Mikopo hairuhusiwi kukaa nayo basi fedha ile inarudi Hazina kisha fedha ile inakuwa *allocated* kwa ajili ya wanafunzi wengine ili waweze kukopeshwa. Lakini pesa zile sasa hazipo na wanafunzi hao ambao wamefanya makusudi kutokulipa sasa itabidi wao wenyewe waweze kulipa fedha hizo ili waweze kugomboa vyeti vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni Serikali kufuta ubaguzi wa kutoa mikopo ya elimu ya juu kwa baadhi ya kozi bila kujali kozi za kipaumbele. Hii ni hoja ya Kambi ya Upinzani na ninaomba niitolee maelezo

yafuatayo. Wakati rasilimali ni pungufu basi ni lazima tutafute utaratibu wa kuweza kutumia rasilimali zile pungufu. Kwa hiyo ubaguzi huu wa mikopo siyo ubaguzi ambao kwanza umeathiri kwa kiasi kikubwa wale ambao wangeweza kupata mikopo kwa maana ya kwamba hata kwa mfano ungechukuliwa mwaka uliopita wa fedha shilingi bilioni 317 zote wakaambiwa wapewe wanafunzi, lazima kuna wanafunzi wangekosa. Kwa mfano, mwaka huu tuna bajeti ya shilingi bilioni 326 lakini ili kutoa mkopo kwa wanafunzi wote bila kujali kigezo tutahitaji jumla ya shilingi bilioni 500 kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya, Kama nilivyosema ni kwamba hoja ni nyingi na ni nzito lakini muda haukutosha. Kwa hiyo, naomba niishie hapa, lakini niseme tu kwamba yote haya ambayo yamehojiwa, tutahakikisha kwamba tunayatolea majibu ya maandishi ambayo tutayawasilisha kwa kila Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nakushukuru na hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, leo asubuhi kuna kikundi cha *VICOBA* ambacho ni wageni maalum wa Mheshimiwa Dkt. Makongoro Mahanga, Naibu Waziri, walitambulishwa lakini walikuwa hawapo. Wapo viongozi 12 wakiongozwa na Mratibu Mtendaji Bwana Aldo Mufinde, hii ni Kamati ya Maandalizi ya Maadhimisho ya miaka 10 ya *VICOBA* Tanzania. Naomba msimame ili Wabunge wawatambue. Nawashukuru sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna jambo lingine la haraka, leo kuna futari ambayo imeandaliwa na Mheshimiwa Spika lakini eneo lililoandaliwa kwa ajili ya futari kuna magari na sisi tunataka kula futari siyo magari, sasa naomba Wabunge, wageni na watumishi wenye magari yafuatayo wakayatoe sasa hivi kabla hayajavutwa na kupelekwa *depot*. Nayo ni gari namba T899BSR, T252BSX, T130BXJ, T311BSM. *(Kicheko)*

Katibu!

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 46 - Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi**

Kif. 1001 *Administration and HR. Management*... ... ... .... ..Tshs. 23,380,382,300/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Hamid Mgaya!

**MHE. NEEMA H. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Ninaomba kupata ufafanuzi wa kisera kuhusu matumizi ya fedha yatokanayo na *Skills Development Levy*, kwa nini fedha hizi hazipelekwi *NACTE* ili ziweze kutoa mafunzo bora kwa wataalamu wa ufundi nchini?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine kabla sijatoa ufafanuzi kwa Mheshimiwa Neema, kwa ruhusa yako naomba uniruhusu kwani kuna watu ambao nilikosa kuwatambua majina yao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, hapana, jibu tu hizo hoja kwanza.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la fedha za *Skills Development Levy* ni suala la kisheria na kwa bahati mbaya sana lililenga baadhi ya taasisi lakini siyo taaasisi zote kama vyuo vikuu, *NACTE* na kadhalika. Hivi sasa 2% zinakwenda *VETA* na asilimia zilizobaki sehemu

kubwa zinakwenda kwenye mikopo ya wanafunzi lakini kwa sababu hata *VETA* wenyewe wamewasilisha tayari maombi Serikalini ya Serikali kuangalia uwezekano wa kufanya marekebisho ili *VETA* kwa uhitaji mkubwa wa mafunzo ya ufundi stadi nchini kwetu waweze kupewa fedha nyingi zaidi kutoka kwenye *Skills Development Levy*. Kwa hiyo, tutalianglia jambo hili kwa ukamilifu ili tuone namna ya kuwezesha *VETA* lakini pia na mamlaka nyingine ambazo zinaendana na ufundi na ufundi stadi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza vituo vya uendelezaji yaani vya kujiendeleza Walimu *(Teachers Sources Centres)* vinapata wapi mafungu ya kujiendesha kwa sababu vituo hivyo havina kitu kabisa inavyoelekea ni Tanzania nzima.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Teachers Sources Centres* zote zinahudumiwa na Halmashauri zetu katika kila Halmashauri na kwa hiyo wajibu wa Halmashauri ni kuweka bajeti kupitia Idara ya Elimu ili kuwezesha vituo kufanya kazi zake ili Waratibu nao waweze kupata semina na Walimu wao pia waweze kupata semina kwa ajili ya kujiendeleza zaidi.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi na katika majibu ya Serikali, *AG* na Naibu Waziri TAMISEMI walisimama na kujibu hoja mtambuka. Nilitegemea wazo langu asimame Waziri wa Serikali ambaye siyo Waziri wa Elimu ili ajibu hoja yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nimeishauri Serikali kuwa ili kupunguza matatizo ya sekta ya elimu, sekta ya elimu itolewe TAMISEMI, isihusishe TAMISEMI bali isimame yenyewe. Matatizo yanayotokea ni kwa sababu leo uko TAMISEMI, ni kama mwanaume mwenye wake wengi, unaweza kufa njaa mwanamke huyu anadhani utakula huku na mwingine anadhani utakula kule. Nataka Serikali isimame na kutoa jibu, mtaitoa lini elimu kwenye TAMISEMI ili isimame yenyewe? *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** *Order please!*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Mwijage ingawa mfano alioutumia kidogo hauendani. Michango hii ya maandishi ilikuwa mingi na bahati mbaya sana hatukupata fursa ya kuitolea ufafanuzi hapa lakini kwa vile hili ni jambo la kero na limesemwa kwa hisia kali, tunalipokea pendekezo au wazo hili, tutalifanyia kazi kati ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Ofisi ya Waziri Mkuu ili tuone jambo ambalo tutaweza kulifanya liondoshe kadhia hii ambayo iko katika elimu. *(Makofi)*

**MHE. MARGRETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa kisera idara ya wanafunzi wenye ulemavu na masuala yao yako chini ya Kamishna wa Elimu ambayo ina shughuli nyingi, je, ni lini kisera Wizara itakubaliana nami kuifanya idara hii ndogo tu iliyomezwamezwa huko

chini iwe kurugenzi inayojitegemea kusudi masuala ya watu wenye ulemavu na wanafunzi yaweze kushughulikiwa kikamilifu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Kamishna wa Elimu ana kazi nyingi na kuna maeneo mengi ambayo anasimamia, anasimamia upande wa elimu ya msingi, elimu ya sekondari, kiubora na kiudhibiti na elimu ya ualimu. Lakini pamoja na kazi hizi ambazo Kamishna anazo na pia zinapokelewa na watendaji wengi kwenye idara yake na suala la walemavu kama tunapata matatizo ni yale ambayo siyo ya kisera au kisheria isipokuwa ya kiutendaji ndiyo ambayo yanatuathiri. Wakati mwingine hatuna fedha za kutosha kwa ajili ya vifaa ambavyo walemavu wanavihitaji. Kwa hiyo, kwa upande wa usimamizi kitengo hiki cha Kamishna wa Elimu hakina matatizo, lakini pale tutakapokuwa tumezidiwa ushauri huu tutauzingatia ili kuweza kuweka maboresho ambayo yatasaidia wananchi wenzetu walemavu wasiweze kuathiriwa na mfumo huu.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimekwazika sana na kauli ya Mheshimiwa Naibu Waziri wakati akisifia Baraza la Mitihani na kusema, kumbe wanawake wanaweza. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri atambue kwamba wanawake tunaweza sana na kama mpaka sasa hivi hajajua hilo ni tatizo lake binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo, nilikuwa naomba kujua katika hotuba ya Waziri na hotuba yetu nimeongea sana jana kuhusiana na suala zima la Walimu lakini mpaka sasa hivi sijaona mikakati yoyote ya kuweza kumsaidia Mwalimu. Kwa mfano, mpaka sasa hivi tafiti zinaonesha kwamba asilimia 60 ya Walimu wanaomaliza vyuo vikuu wanakaa shuleni katika kipindi cha chini ya miaka mitano. Sasa nilikuwa naomba kujua kuna mkakati gani wa kuhakikisha kwamba wanawa- *retain* Walimu?

*(Hapa Waziri alichelewa kuanza kujibu)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri muda!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI (ELIMU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Lyimo ambalo linataka kujua Serikali ina mpango gani ambao unaweza kumfanya Mwalimu aweze kuishi kwenye ajira yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia ni miundombinu, huduma zake, ndizo ambazo zinawafanya Walimu wengine kuacha sekta ya Serikali kwenda sekta binafsi. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa mpango tuliouweka wa kuboresha miundombinu, nyumba za Walimu, kupata vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na kuhakikisha kwamba malipo stahili ya Walimu wakiwa kwenye utumishi wao yanapatikana kama ambavyo tumeweza kupanga utaratibu, tuna

hakika kwamba sasa Walimu watakaa kwenye ajira zao.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Tangu kuundwa kwa Bodi ya Mikopo nchi hii imeonekana kumekuwa na migogoro mingi sana baina ya Bodi na wanafunzi wa vyuo vikuu. Hali hii ilipelekea Mheshimiwa Rais kuunda Tume ambayo iliongozwa na Profesa Makenya Maboko na lengo mojawapo lilikuwa ni kujaribu kutambua au kutafuta namna nzuri ya uendeshaji na utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu vya taifa hili. Lakini mpaka leo ripoti ya ile Tume haijawekwa wazi na hatujui ni nini yalikuwa mapendekezo yake na ni yapi ambayo yameshafanyiwa kazi ili kuondoa migogoro ambayo imekuwepo baina ya Bodi ya Mikopo na wanafunzi wa vyuo vikuu kwenye nchi hii? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, *short and clear.*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Tume imemaliza kazi na ni Tume ambayo Mheshimiwa Rais mwenyewe aliiteua, imefanya kazi nzuri, imewasilisha ripoti kwa Mheshimiwa Rais na kiutaratibu taarifa ile ni ya Mheshimiwa Rais.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, inatosha, ya Rais yamekwisha! (*Makofi*)

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi. Kwanza naomba niipongeze Serikali kwa jambo zuri la asubuhi hapa la

kuwatambua wanafunzi waliofanya vizuri katika mitihani yao ya kidato cha sita, lakini pia kuna suala la kuongeza katika hilo. Wapo watoto wetu wengine wa kitanzania ambao wanafanya mitihani kutoka *Cambridge* na wanafanya vizuri sana lakini bado taifa halijawatambua. Je, Serikali inasemaje kuhusu kutambua vijana hao nao?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mitihani ambayo Serikali tunahangaika nayo moja kwa moja ni ile ya mitaala yetu ya Serikali na ndiyo hii ambayo tunaweza tukachukua kila hatua tunayoipenda. Hii mingine tunaikubali na tunaziwezesha mamlaka za nchi za nje kuendesha mitihani yao hapa nchini, lakini siyo mitihani ambayo tunaweza tukaiingilia katika taratibu zozote.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kupata ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri. Mpango wa Serikali wa kudhibiti shule za watu binafsi ambazo ada za masomo zimekuwa kubwa na imebainika kwamba, kuna nyingine *form one to form four* ni shilingi milioni mbili (2), *five to six* shilingi milioni 3.5 na mwezi Novemba Waziri alikubali hapa kwamba utaunda Tume kufuatilia jambo hili. Je, amefikia wapi kudhibiti suala zima la mfumuko wa ada katika shule binafsi? *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli niliahidi kwamba tutaunda Tume na tumemudu kuifanikisha kuiunda kwa sababu kila Tume ili ifanye kazi inahitaji fedha. Tume ambayo tumefanikiwa kuiunda ni ile ya kwa ajili ya

vyuo vikuu na imeshafanya kazi, imekamilisha na kuwasilisha ripoti Serikalini. Hii ya shule za sekondari na msingi iko katika mchakato wa kuweza kuundwa hivi sasa.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwenye mchango wangu wa maandishi nilitaka kupata kauli ya Serikali kuhusu udahili wa wanafunzi katika vyuo vikuu ambapo vyuo vikuu vya umma udahili unakuwa na pointi 5.5 mpaka 6.0 wakati vile vya taasisi binafsi inakuwa ni tofauti na vile vya umma, wakati taifa ni moja na elimu tunayotoa ni ya aina moja na vyuo vyote vinapata mikopo kutoka Serikalini. Sasa kwenye *standard deviation, variation* inaruhusiwa kiasi gani kati ya vyuo vya umma na vile vya taasisi binafsi au *private universities*? Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Vyuo Vikuu ina mamlaka ya udhibiti wa vyuo vikuu hivi katika taaluma na imeweka utaratibu kwamba ili mwanafunzi ajiunge katika chuo kikuu kuna *minimum points* ambazo mwanafunzi huyu inabidi awe nazo. Sasa vyuo vinaweza vikachukua pointi zozote juu ya *minimum* ambazo kama ninakumbuka sasa kwa masomo yasiyokuwa ya sayansi ni points 2.5 na haya ya sayansi samahani sikuikariri, siikumbuki vizuri, lakini kila chuo sasa kinaweza kikaweka *standards* zake chenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, mtu halazimishwi. Kwa mfano Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama unataka kuchukua *Telecoms* unahitaji uwe na points 11

chini ya yapo hawakuchukui lakini vyuo vingine wanakuchukua kwa sababu hawa wamefaulu ila ni nafasi hazitoshi katika vyuo hivi. Kama nafasi zingekuwa zinatosha, wanafunzi wengi wa *points* hizi tano, sita, wangeweza kuchukuliwa. Kwa hivyo, vyuo viko huru kuamua wao wenyewe kufuatana na nafasi walizokuwa nazo na kumpa nafasi yule ambaye amefaulu kwa kiwango cha juu zaidi kuliko yule aliyefaulu kwa kiwango cha chini.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nasikitika sana kwamba Mheshimiwa Waziri amesema atatumia ile fedha ya chenji hata bila kulieleza Bunge hili na kupitisha kama *supplementary estimates*. Sijui huu ni utaratibu wa wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuuliza ni sera ya uwekezaji. Ukiangalia takwimu ambazo Mheshimiwa Waziri ametupa watoto ambao wako katika *primary* mpaka *secondary school* ni takribani watoto milioni 10. Watoto ambao wako katika *higher education* ni takribani 166,000 lakini fedha karibu shilingi bilioni 526 ziko kwenye *higher education* na unabakiwa na shilingi bilioni 100 kwa ajili ya watoto wengine ambao ni milioni 10. Mheshimiwa Waziri haoni kwamba, ndiyo maana elimu yetu iko chini kwa sababu msingi haujawekewa fedha ya kutosha? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ikiwa *short and clear* tunaweza tukaongeza watu wengi.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa siyo kwamba fedha hizi ambazo zinaonekana kwenye Wizara ya Elimu ndiyo ambazo pekee zinahudumia elimu ya msingi na sekondari. Wizara yangu inapitisha bajeti hapa ya shilingi bilioni 724 lakini imeshapitisha bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI katika eneo la elimu kuna shilingi trilioni moja na bilioni 700. Kwa hiyo, elimu ina fedha nyingi sana katika bajeti ya Serikali, tusiangalie hii tu ya Wizara ya Elimu. *(Makofi)*

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuuliza kwa nini Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inachelewa sana kutatua matatizo ya wananchi? Nakumbuka kule Moshi Vijijini Walimu walikuwa na malalamiko mengi sana, wananyanyasika, wananyanyaswa na Ofisi ya Elimu, ofisi ya fedha, ofisi ya utawala, wanacheleweshewa mishahara, wamelalamika kwa muda mrefu mpaka Mkuu wa Mkoa ameunda Tume, Tume imeona kweli Walimu walikuwa wananyanyasika na Mkuu wa Mkoa wetu akahamisha watumishi 32 ndani ya Mkoa ule. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu akahamisha wakuu wa idara saba (7).

Mheshimiwa Spika, swali ni kwamba, hawa Waheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake na wale walioko TAMISEMI, kwa nini wanachukua muda mrefu kufuatilia matatizo ya wananchi? Kama siyo Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro na Waziri Mkuu ina maana hata mgomo wa Walimu ungeanzia kule Moshi kutokana na matatizo makubwa wanayopata Walimu. Naomba

Waziri ajibu hapa, kwa nini hawasikilizi mapema matatizo ya Walimu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI (ELIMU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ngazi za utoaji huduma kwa elimu tuna ofisi ya Mkurugenzi kwenye ngazi ya Wilaya, Mkoa au Wizarani. Hatuwezi kujua lakini tumewakabidhi kazi ya kuhakikisha kwamba wanahudumia Walimu na kutatua matatizo yote ya Walimu. Tunaomba likitokea lingine Waheshimiwa Wabunge mtujulishe Wizarani mara moja tutakuja kwenye maeneo yenu tutatue matatizo ya Walimu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Na hawa Wabunge wote ni Madiwani.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri anajibu hoja nimemsikiliza kwa makini amesema kwamba, haja ya mja ni maneno na haja ya muungwana ni vitendo. (Ada ya mja ni maneno muungwana ni vitendo) (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo, nenda kwenye hoja.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa nakwenda kwenye hoja. Kwa hiyo, nitakachokifanya nitatembea na ile *Hansard* aliyoitumia Mheshimiwa Waziri na nitalala nayo kila ninapokwenda kwa sababu kwenye kitabu hiki cha hotuba ya Wizara yake ukurasa wa 98, nataka

nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya wananchi wa Ludewa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo, muda unakwenda nakuomba toa hoja ili ujibiwe.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe hoja, kwa niaba ya wananchi wa Ludewa tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri na tunaomba atekeleze huo uungwana wake kwenye ujenzi wa chuo cha *VETA* Ludewa. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Huo ni ushauri tu.

*(Hapa Waziri alisimama ili atoe ufafanuzi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kaa, huo ni ushauri tu. *(Kicheko)*

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika moja ya mchango wangu wa maandishi nilizungumzia suala zima la tatizo tulilonalo la vijana wetu ambao wako vyuo vikuu lakini hawapati nafasi nzuri kwa ajili ya kufanya *field*. Sasa ni kwa jinsi gani Wizara inajipanga kuhakikisha vijana walio vyuo vikuu wanapata nafasi kubwa ya ku- *attend field* ili wamalizapo masomo yao waweze kufanya kazi kwa umahiri wa hali ya juu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, *short and clear.*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo ya vitendo yanatolewa maelekezo na Tume ya Vyuo Vikuu baada ya kupitisha mitaala ya *program* husika. Kwa wale wote ambao katika *programs* zao kuna mafunzo ya vitendo, Serikali itahakikisha inajitahidi kuwapatia posho zao za mufunzo kwa wale ambao wana mikopo ya posho lakini pia tutajihidi kwa kila namna kuweza kushawishi viwanda na mashirika mbalimbali nchini watoe nafasi ili wanafunzi hao waweze kufanya mafunzo kwa vitendo katika viwanda hivyo.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Waziri. Kutokana na mamlaka niliyopewa na Kanuni ya 104 sasa tunaingia kwenye *guillotine*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na mabadiliko)*

**TAARIFA**

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa! Taarifa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cheyo sijakuruhusu!

**MHE. JOHN M. CHEYO:** *Okay*!

*Kif. 1002 Finance and Accounts……………………Tshs. 626,435,000/=*
*Kif. 1003 Policy and Planning……. Tshs.1,711,885,000/=*
*Kif. 1004 Internal Audit Unit ……… Tshs. 178,201,000/=*

*Kif. 1005 Procurement Management Unit……...………………………. Tshs.222,767,000/=*

*Kif. 1006 Government Communication Unit……………………………... Tshs. 77,747,000/=*

*Kif. 1007 Legal Unit…………………… Tshs. 87,050,000/=*

*Kif. 2001 Commissioner for Education…………………..Tshs. 7,133,693,000/=*

*Kif. 2002 Inspectorate ………………Tshs.15,242,470,000/=*

*Kif. 3001 Basic Education……………Tshs. 1,164,685,000/=*

*Kif. 3002 Adult Education & Non Formal Education .................Tshs.795,320,000/=*

*Kif. 4001 Secondary Education……Tshs. 1,045,045,000/=*

*Kif. 5001 Teacher Education……….Tshs. 47,101,818,000/=*

*Kif. 7001 Higher Education ……….Tshs. 526,397,669,000/=*

*Kif.7002 Tech. & Vocational Training Division................Tshs. 10,986,601,000/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 46 – Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi**

*Kif. 1001 Administration and HR Management......................Tshs. 600,000,000/=*

*Kif. 1003 Policy and Planning………………........Tshs.5,196,000,000/=*

*Kif. 2001Commissioner for Education ………….........................................Tshs. 0/=*

*Kif. 2002 Inspectorate ……………………..............Tshs. 0/=*

*Kif. 3001 Basic Education ……………Tshs.1,669,444,000/=*

*Kif. 4001 Secondary Education ……Tshs.11,773,040,000/=*

*Kif. 5001 Teacher Education …………Tshs.70,000,000/=*
*Kif.7001Higher Education ………..Tshs.67,472,833,000/=*
*Kif.7002 Tech. & Vocational*
*Training Division……….. Tshs. 3,800,000,000/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja!

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitangulize kuomba radhi kwa wale ambao sikuwataja na kwa sababu muda umekwisha niwaombe radhi sana kwamba makosa hayo yaliyotendeka ni makubwa. Nawaomba radhi watusamehe. Niwataje?

**MWENYEKITI:** Wataje!

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Afadhali, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuwashukuru wale ambao sikuwataja majina yao na ambao wamechangia kwa maandishi katika hoja ya Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Naomba niwataje kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Prof. Peter Msolla, Mheshimiwa Dkt. Abdulla Saadalla, Mheshimiwa Iddi Azzan, Mheshimiwa

Selemani Jafo, Mheshimiwa Deo Sanga, Mheshimiwa Mohamed Chomboh, Mheshimiwa Catherine Magige, Mheshimiwa Ramadhan Saleh, Mheshimiwa Amina Makilagi, Mheshimiwa Alhaji Mohamed Missanga, Mheshimiwa Kheri Ameir, Mheshimiwa Juma Nkamia, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Pauline Gekul, Mheshimiwa Dkt. Augustine Mrema na Mheshimiwa James Mbatia. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Dkt. Henry Shekifu, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Zarina Madabida, Mheshimiwa Magreth Mkanga, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Shaffin Sumar, Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mheshimiwa Kapt. George Mkuchika, Mheshimiwa Esther Bulaya, Mheshimiwa Donald Max, Mheshimiwa Zabein Mhita, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa Mch. Israel Natse, Mheshimiwa Vincent Nyerere, Mheshimiwa Kasim Majaliwa ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI (Elimu), Mheshimiwa Fredrick Werema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mheshimiwa Philipo Mulugo, Naibu Waziri wa Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mwingine ambaye amechangia kwa maandishi ni Dkt. Fenella Mukangara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tena, kama kuna watu ambao sikuwatambua, niombe radhi sana. Yale yaliyotokea nimeshindwa kuyadhibiti lakini nitajitahidi sana kutafuta njia za kuwatambua baada ya hapa. Naomba sasa nitoe taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Taarifa kuwa, Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Taasisi zake kwa Mwaka 2012/2013 mafungu kwa mafungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo basi naliomba Bunge lako Tukufu, liyakubali Makadirio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka 2012/2013 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Nachukua nafasi hii kukupongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wako.

Waheshimiwa Wabunge, *order please! Order please*! *You talk to the table not to anyone else here*. *(Kicheko/Makofi)*

Nawapongeza kwa kazi nzuri lakini nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu. Hili suala la Walimu mmelivamia njuga mwaka huu.

Mheshimiwa Waziri nazungumza na wewe na Naibu wako, mjaribu kumaliza matatizo ya Walimu. Hawa Walimu wana familia, wanafanyakazi katika mazingira magumu sana. Mjaribu kujikita na tuwapende na kuwajali wote wale waliotuweka kwenye madaraka. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nakumbusha tena kuhusu futari leo jioni ambayo imeandaliwa na Mheshimiwa Spika na itaanza Saa 12.30, wote mnaalikwa kuhudhuria futari hiyo muhimu na ndiyo siku ambayo Mheshimiwa Spika ataaga Wabunge kurudi Majimboni.

Waheshimiwa Wabunge, nilitaka ni-*draw attention* moja, muda wa kipindi cha Kamati ya Matumizi ni mdogo sana. Kwa mfano mimi huwa naenda kwa vyama, kwa upande wa CCM waliomba watu 41 wamepata watano, upande wa CHADEMA waliomba watu 18 wamepata wawili, Upande wa CUF waliomba sita wamepata wawili, NCCR Mageuzi waliomba wawili amepata mmoja, TLP mmoja na chama cha Mheshimiwa Cheyo (UDP) mmoja. Kwa hiyo, tunajaribu ku-*balance* ili kila chama na wao waweze kupata nafasi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno hayo, ninaahirisha Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 12.05 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano, Tarehe 15 Agosti, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*